**2 JUNI, 2023**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**Kikao cha Thelathini na Tisa – Tarehe 2 Juni, 2023**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. LAWRANCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**MHE. NEEMA W. MGAYA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2022/2023 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. LAWRANCE MAKIGI – KATIBU MEZANI**: Maswali.

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Maswali, Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 501

### Mwongozo wa kukopesha watu wenye ulemavu fedha za Halmashauri

**MHE. STELLA I. ALEX** aliuliza:-

Je, kuna mwongozo unaoruhusu watu wenye ulemavu mmoja mmoja kukopeshwa fedha za Halmashauri?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Deo Ndejembi, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa mtu mwenye ulemavu mmoja mmoja kuweza kupata mkopo ili kujikwamua kiuchumi na kuongeza mchango wake katika maendeleo ya Taifa.

Mwaka 2021 Serikali ilitoa mwongozo wa kumwezesha mtu mmoja mmoja kukopa kwa kufanya maboresho ya Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo kwa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu za mwaka 2019 za Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, ambapo maboresho hayo yalihusisha kuongeza Kifungu kipya cha 6A(i) na (a) ambacho kwa sasa kinatoa fursa kwa mtu mmoja mmoja mwenye Ulemavu kukopa kutoka katika mikopo inayotolewa na Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge kuendelea kutoa elimu juu ya uwepo wa fursa hii kwa watu wenye ulemavu nchini kwa lengo la kujikwamua kiuchumi na kujiongezea kipato.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, swali la nyongeza.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali. Serikali imetoa wito kwamba Wabunge tutoe elimu. Mimi kama Mbunge wa kundi hili, nimetoa elimu sana na kundi hili limekuwa likiitikia, lakini Halmashauri na Manispaa huwa hazitekelezi mwongozo huu na kanuni ambayo imeelezwa kwenye jibu la msingi: Nini kauli ya Serikali kwa Halmashauri na Manispaa zetu nchini? Kwa sababu kama mwongozo upo na kanuni zipo, kwa nini halitekelezeki? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natambua kwamba huenda kukawa kuna mabadiliko ya jinsi ya utolewaji wa mikopo hii. Niendelee kuiomba Serikali kwamba kwa kundi hili la watu wenye ulemavu, iendelee kufikiria kukopesheka mtu mmoja mmoja, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** La pili ni ombi Mheshimiwa. Swali la kwanza, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Ikupa kwa maana amekuwa *champion* hasa katika mabadiliko ya kanuni hizi za kuwezesha walemavu kuweza kupata mkopo kwa mtu mmoja mmoja.

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye swali lake kuhusu kwa nini kanuni hizi hazitekelezeki, nichukue nafasi hii mbele ya Bunge lako Tukufu kuwaelekeza Wakurugenzi wote wa Halmashauri nchini, kutekeleza mabadiliko haya ya sheria na kuhakikisha watu wenye ulemavu wanapata mkopo kwa mtu mmoja mmoja. Pia kama Mheshimiwa Ikupa alivyosema kwenye ushauri wake, katika mapitio mapya ambayo yanafanyika kwa maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tutaweka kipaumbele kwenye kundi hili la walemavu vilevile kuweza kuendelea kupata mkopo mtu mmoja mmoja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, Mbunge wa Msalala, sasa aulize swali lake.

Na. 502

**Mchakato wa kutangaza miradi ya barabara kupitia *TARURA***

**MHE. IDDI K. IDDI** aliuliza:-

Je, lini Sheria italetwa kupunguza michakato ya utangazaji wa Miradi ya *TARURA* na fedha kusimamiwa na Mameneja wa Wilaya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kassim Iddi Iddi, Mbunge wa Jimbo la Msalala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ununuzi wa Umma imetungwa ili kuweka uwiano mzuri wa haki na ushindani katika Ununuzi wa Umma na hutumika kwa Taasisi zote za Serikali na siyo *TARURA* pekee. Kwa mujibu wa muundo wa *TARURA,* fedha zote za miradi na utekelezaji wake umekasimiwa kwa Mameneja wa Wilaya. Malipo yote

huandaliwa na Meneja wa Wilaya na kutumwa kwa Meneja wa Mkoa kwa ajili ya uidhinishwaji na ulipwaji kupitia mfumo wa Malipo Serikalini *(MUSE)*. Aidha, Ofisi ya Mkoa kwa kushirikiana na Ofisi ya Meneja wa Wilaya, itaendelea kufanya tathmini kuhakikisha miradi inafanyika kwa kuzingatia thamani ya fedha ili iweze kukidhi uhitaji wake.

**SPIKA:** Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, swali la nyongeza.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa Serikali imeweka utaratibu wa kutangaza ajira ambazo zinatoka TAMISEMI na hivyo kukadiria watumishi kupelekwa *TARURA:* Kwa nini sasa Serikali isiruhusu *TARURA* wenyewe waweze kuajiri wakandarasi au wahandisi?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili. Kwa kuwa, Jimbo la Msalala liko katika mazingira magumu sana kwenye maeneo hayo kwa maana ardhi yake ni mbuga: Sasa Serikali haioni haja ya kuongeza bajeti ili iendane na uhalisia wa maeneo hayo kwenye Jimbo la Msalala? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, nikijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Iddi Kassim, la kwanza hili la kwa nini *TARURA* wasipewe vibali vya kuajiri wenyewe, ni kwamba ajira katika utumishi wa umma hutolewa kulingana na ukomo wa bajeti ambayo imepitishwa na Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *TARURA* wenyewe wanaomba vibali kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Utumishi na tutaendelea kutoa kipaumbele ajira za ma-*engineer* kwenye taasisi hii ya *TARURA* kadiri ya fedha ambavyo inapatikana na bajeti ya Serikali inaruhusu.

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye swali lake la pili la mgawanyo wa fedha, hasa kule Msalala kwa sababu ya mazingira magumu, kwa sasa tayari kuna *review* inayofanyika chini ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa maelekezo ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Angellah Kairuki, kuangalia ni namna gani mgawanyo wa fedha unakwenda katika maeneo mbalimbali hapa

nchini ikiwemo kule Msalala. Naomba Mheshimiwa Mbunge awe na Subira na muda siyo mrefu timu hii itawasilisha taarifa yake mbele ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI na baada ya timu hiyo kuwasilisha taarifa hiyo, tutaangalia upya *formula* inayotumika kwa ajili ya kupeleka fedha maeneo mbalimbali nchini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Timotheo Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa, kwenye nchi yetu majira yanatofautiana: Je, Serikali haioni umuhimu wa kuiruhusu na kuielekeza *TARURA* juu ya muda wa kutangaza na kutekeleza miradi kwa kuzingatia majira ya maeneo husika? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, *TARURA* inatangaza kazi zake hizi kote nchini mara baada tu ya bajeti yao kuidhinishwa. Ni kama hivi sasa bajeti ya Shilingi bilioni 776 imeidhinishwa na Bunge lako Tukufu, hivyo katika mwaka mpya wa fedha unaoanza mwezi Julai mwaka huu 2023, ndipo kazi zote zitaanza kutangazwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rehema Juma Migilla, Mbunge wa Ulyankulu, sasa aulize swali lake.

Na. 503

**Walimu walioajiriwa kwa muda kupata ajira ya kudumu – Ulyankulu**

**MHE. REHEMA J. MIGILLA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itawapa ajira za kudumu walimu walioajiriwa tangu mwaka 2002 kwa masharti ya ajira za muda Ulyankulu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rehema Juma Migilla, Mbunge wa Jimbo la Ulyankulu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2017 – 2021 Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua iliidhinishiwa na kuajiri walimu 13 ambao walitimiza sifa za kuajiriwa kwa masharti ya Ajira ya Kudumu na Malipo ya Uzeeni. Aidha, Walimu 29 wameajiriwa kwa masharti ya Ajira za Mkataba kwa kuwa walikuwa na umri wa zaidi ya miaka 45. Walimu hawa walikuwa ni wakimbizi waliopatiwa uraia wa Tanzania baada ya kupata sifa kwa mujibu wa sheria.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rehema Migilla, swali la Nyongeza.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kuishukuru Serikali kwa hatua iliyofikia kuhusu hawa walimu wangu, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na Serikali kutuambia kwamba hawa walimu 13 ambao walikuwa ni raia wa Burundi, wakimbizi, wamepatiwa ajira, lakini mpaka tunavyoongea hivi, hakuna barua waliyopewa inayoonesha kwamba wamepewa ajira za kudumu: Je, Serikali iko tayari kuiambia Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua na mamlaka zinazoshughulikia masuala ya walimu kuhakikisha hawa walimu wanapata barua zao za ajira na stahiki nyingine? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili. Kuna walimu hawa 29 ambao umri wao umevuka miaka 45 walikuwa wanajazishwa mikataba ya muda, lakini pamoja na kujazishwa mikataba ya muda walikuwa hawapewi *gratuity* yao.

Je, pamoja na kwamba wamejazishwa hii mikataba, lini watapewa stahiki zao kulingana na mikataba waliyokuwa wamejaza? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, nikijibu swali la kwanza la Mheshimiwa Migilla la hawa 13 kwamba bado hawajapata barua za ajira zao, tutakaa na Mheshimiwa Mbunge na kuwasiliana na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kaliua na kuona changamoto iko wapi kwa ajili ya hao walimu kupata barua zao kama ambavyo kibali kilitolewa na Ofisi ya Rais, Utumishi kwa ajili ya kuweza kuwaingiza katika ajira ya kudumu.

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye swali lake la pili, hili ni suala la kisheria. Ni sheria iliyopitishwa na Bunge hili Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwamba, mtumishi yeyote wa umma ni lazima anapoingia katika utumishi wa umma asiwe amevuka umri wa miaka 45 ili aweze kuwa amechangia katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa miaka isiyopungua 15. Ndiyo maana hawa baada ya kupata uraia wao na vibali kutoka Ofisi ya Rais, Utumishi walikuwa wameshavuka ule umri wa miaka 45.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, Katibu Mkuu Utumishi alitoa kibali kwa hawa 29 kuendelea kuwa na ajira ya mkataba, ambapo ni mikataba ya miaka mitano mitano, tofauti na mikataba mingine ya mwaka mmoja mmoja. Watapata kiinua mgongo chao pale watakapofikia umri wa kustaafu kwa mujibu wa sheria ilivyo ya kustaafu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. Mheshimiwa Zuena Athuman Bushiri, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 504

**Ujenzi wa Madaraja ya Kampimbi na Mgandu – Same**

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaboresha Madaraja ya Kampimbi na Mgandu Wilayani Same?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mhandisi Godfrey Kasekenya Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Madaraja ya Kampimbi yapo kwenye Barabara ya Same – Kisiwani hadi Mkomazi yenye urefu wa Kilometa 98. Mkataba kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Same – Kisiwani hadi Mkomazi yenye urefu wa Kilometa 98 umepangwa kusainiwa kabla ya mwisho wa mwezi Juni, 2023. Ujenzi utajumuisha barabara na madaraja hayo na utaanza katika mwaka wa fedha 2023/2024, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri, swali la nyongeza.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi kuuliza maswali ya nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, kwanza naishukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi ya Awamu ya Sita kwa kuiona barabara ile kwa kuwa imekuwa na changamoto kubwa sana. Naishukuru Serikali kwa kuingia mkataba wa kutengeneza barabara ile ya Mkomazi – Kisiwani – Same. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina swali moja tu la nyongeza. Kuna maeneo ambayo yalitengenezwa kwa kiwango cha lami,

kilometa tano, tatu na tano tena; katika Kata ya Ndungu zimetengenezwa kilometa tano, katika Kata ya Maore zimetengenezwa kilometa tano na katika Kata ya Kihurio zimetengenezwa pia kilometa tano…

**SPIKA:** Swali lako Mheshimiwa.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Je, Serikali sasa kupitia mkataba huu itabomoa ile lami ambayo imetengenezwa ambayo imeanza kuchakaa au itaendelea na ile ile? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Zuena Bushiri, Mbunge, Viti Maalum, Mkoa wa Kilimanjaro, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza napokea hizo pongezi kwa niaba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kuhusu suala lake la maeneo ambayo tumeyajenga, wakati hizi barabara zinajengwa kwa vipande vipande yalikuwa ni maelekezo kutokana na wananchi wa maeneo hayo yalivyokuwa korofi, lakini pia kwenye miji midogo waliomba viongozi na wakatoa maelekezo barabara hizo ziweze kujengwa kwa kiwango cha lami kwa vipande vipande.

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba pamoja na wananchi ambao wanahusika na hiyo barabara, usanifu uliofanyika, hayo maeneo yameshakuwa yamechakaa na hayaendani na usanifu wa sasa. Kwa hiyo, maeneo yote yale yatafumuliwa na yatajengwa upya, isipokuwa kuna kilometa tano na kitu ambayo inaendela kujengwa, hiyo ndiyo ianendana na usanifu wa sasa, lakini maeneo yote ya zamani yatafumuliwa na kujengwa upya, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, maswali ya nyongeza mafupi na moja kwa moja kwenye swali.

Mheshimiwa Priscus Tarimo, swali la nyongeza.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ni lini Barabara ya Tengeru – Holili itaanza kupanuliwa ikiwa ni pamoja na kujenga daraja jipya la Kikavu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja pamoja na daraja hilo, tayari yapo mazungumzo, na *JICA* wameshakubali kufadhili ujenzi wa barabara hiyo na daraja hilo la Kikavu ikiwa ni pamoja na barabara kama kilometa 10 katika Mji wa Moshi. Kwa hiyo, sasa hivi suala linaloendelea ni mazungumzo kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na *JICA* ili tuanze kujenga hayo maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, swali la nyongeza.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Barabara ya Mkomazi – Kisiwani – Same ni kweli ina madaraja mengi sana: Je, Mheshimiwa Waziri, Daraja la Saseni na Daraja la Mpirani, nayo mtayarudisha yawe mapya kama ambavyo barabara itakuwa mpya? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Same Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, usanifu huu ni mpya tofauti na uliokuwepo zamani. Kwa hiyo kila kitakachofanyika ni kujenga barabara yote, hizo kilometa 98 ikiwa ni pamoja na hayo madaraja, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, Mbunge wa Lupa, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo.

Na. 505

**Ujenzi wa Barabara ya Makongolosi – Mkiwa – Chunya**

**MHE. SUMA I. FYANDOMO K.n.y. MHE. MASACHE N. KASAKA** aliuliza: -

Je, lini barabara ya Makongolosi – Mkiwa – Chunya itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, Mbunge wa Lupa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inajenga kwa kiwango cha lami barabara ya Mbeya – Chunya – Makongolosi – Rungwa – Mkiwa (km 503.36) kwa awamu, ambapo sehemu ya Mbeya – Chunya – Makongolosi (kilometa 111) ujenzi umekamilika. Ujenzi wa sehemu ya Noranga – Itigi – Mkiwa (kilometa 56.9) sehemu ya Noranga – Itigi

(Mlongaji) (kilometa 25) umefikia asilimia 12 na kwa sehemu ya Noranga – Doroto (kilometa 6) na Itigi – Mkiwa (kilometa 25.6) mkataba wa ujenzi tayari umesainiwa. Kwa sehemu iliyobaki ya barabara za Makongolosi – Rungwa – Noranga (kilometa 356) na Mbalizi – Makongolosi (kilometa 50) Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Suma Fyandomo, swali la nyongeza.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Mbalizi – Shigamba, ile barabara ni muhimu sana, ambayo inaunganisha na Mkoa wa Songwe;

Je, ni lini Serikali itaanza kujenga barabara hiyo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; hili swali linajirudiarudia lakini halijapata majibu sahihi ya Serikali; barabara ya kutoka Katumba – Suma – Mwakaleli – Luangwa – Mbambo na Tukuyu Mjini, hii ni ahadi ya tangu awamu ya nne;

Je, ni lini Serikali itaanza kuijenga barabara hiyo? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mbalizi – Shigamba tayari tulishapata maelekezo na tunaifanyia kazi. Hivi sasa tunakamilisha usanifu wa kina na mhandisi mshauri yupo kazini. Akishakamilisha barabara hii ambayo ni ya Mbalizi – Shigamba na inaunganisha Itumba na Malawi, sasa Serikali itaanza kuijenga kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, na barabara ya pili aliyoitaja, kimsingi tumeshaitengea fedha kwa kipande kuanza kuijenga kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema William Mgaya, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Je, ni lini Serikali itajenga barabara ya kutoka Njombe – Mdandu – Iyai kutokea Mbeya kwa kuwa barabara hii ni muhimu ndani ya Jimbo la Wanging'ombe na hatuna barabara ya lami yoyote zaidi ya hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Neema William Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, barabara inayoanzia Njombe – Ramadhani – Iyai, Serikali imekuwa inajenga kwa awamu. Na katika mwaka huu wa fedha nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tumetenga fedha kwa ajili ya kuendelea kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami kuunganisha Makao Makuu ya Wanging'ombe na Makao Makuu ya Mkoa wa Njombe.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Napenda kuuliza Serikali ina mpango gani wa kuifanyia matengenezo barabara ya ulinzi ya Kusini sehemu ya Kivava – Kitaya baada ya mafuriko yaliyotokea hivi karibuni?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Nanyamba, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, moja ya vipaumbele vya Serikali ni kuhakikisha kwamba barabara zote za ulinzi zinapitika. Barabara aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge bado ni barabara ya changarawe, na kutokana na mvua iliyonyesha kama alivyosema, kuna maeneo ambayo hayapitiki.

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali tayari imeshaanza kufanya mipango ya kurudisha mawasiliano maeneo yote yaliyokatika ili iweze kupitika, hasa tukizingatia umuhimu wa barabara yenyewe, barabara ya ulinzi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Furaha Matondo, swali la nyongeza.

**MHE. FURAHA N. MATONDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

Je, ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami barabara ya kutoka Bukonyo – Bukongo – Masonga yenye kilometa 32 kwa sababu upembuzi yakinifu ulikwisha fanyika? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Furaha Ntengo Matondo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, barabara hii aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge itajengwa baada ya kufanya usanifu wa kina wa mwisho ambapo ile barabara bado hatujafanya usanifu. Kwa hiyo tukishafanya usanifu tutajua gharama na ndipo Serikali sasa itatafuta fedha kujenga hiyo barabara kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenani, swali la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Namanyere – *Kipili Port* ni barabara muhimu sana kwa uchumi wa Wilaya ya Nkasi na Mkoa wa Rukwa kwa ujumla;

Je, ni lini barabara hii itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mbunge wa Nkasi Kaskazini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kama alivyosema Mbunge barabara hii inakwenda kwenye Bandari ya Kipili. Tumetenga fedha kiasi kwa ajili ya kuifanyia ukarabati mkubwa ili iweze kupitika. Lakini lengo la Serikali ni kuijenga hii barabara kwa kiwango cha lami, hasa tukizingatia umuhimu wenyewe, kwamba inakwenda kwenye bandari ambayo inahusisha biashara kati ya Tanzania na *DR Congo.* Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Kilimo; Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo.

Na. 506

**Wafanyabiashara wazawa kuruhusiwa kununua kahawa kwa wakulima**

**MHE. FLORENT L. KYOMBO K.n.y. MHE. OSCAR I. KIKOYO** aliuliza: -

Je, kwa nini Serikali isiruhusu wafanyabiashara wazawa wa kusindika kahawa Mkoa wa Kagera kununua kutoka kwa wakulima?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mbunge wa Jimbo la Muleba Kusini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka utaratibu wa uuzaji na ununuzi wa kahawa za wakulima kupitia vyama ya ushirika ili kuondoa uuzaji wa kahawa katika mifumo isiyo rasmi na kuimarisha biashara ya mazao nchini. Aidha, kupitia mfumo huo wafanyabiashara wazawa waliowekeza kwenye viwanda vya kuongeza thamani na kusindika kahawa Mkoani Kagera wanaruhusiwa kununua kahawa kwenye minada ghafi inayoendeshwa na Bodi ya Kahawa. Kupitia utaratibu huo wanunuzi wazawa wanapata nafasi ya kushindana kununua kahawa moja kwa moja kwa wakulima kama ilivyowasilishwa na vyama vyao vya msingi *(AMCOS)*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, swali la nyongeza.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Dkt. Ishengoma Kikoyo, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza: -

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa kuwa malengo ya Serikali ni kuhamasisha uchumi ambao ni shindani katika ununuzi wa kahawa;

Je, Serikali haioni sasa itoe kibali cha wanunuzi binafsi kushindana na *AMCOS* kununua kahawa moja kwa moja kutoka kwa wakulima?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa kahawa inaendeshwa kwa Bodi ya Kahawa;

Je, Serikali haioni kwamba ni muda mwafaka kuleta Sheria ya Bodi ya Kahawa hapa Bungeni ikafanyiwa marejeo ili kuendana na uchumi wa sasa? Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika majibu yangu ya msingi, Serikali imeweka utaratibu ambao unaruhusu pia wawekezaji binafsi kununua kupitia katika *AMCOS*, ambapo wao wanakusanya. Na ninaomba tu niliweke wazi hapa lieleweke vizuri; *AMCOS* hanunui kahawa, anachokifanya yeye ni ku-*aggregate* na baadaye ndipo wanunuzi binafsi wanakwenda kununua kupitia kahawa iliyokusanywa. Kwa hiyo tutakachokifanya ni kuboresha mazingira zaidi ili wakulima wanufaike na bei lakini vilevile na waagizaji binafsi wapate uhakika wa kahawa yao.

Mheshimiwa Spika, la pili, kuhusu marejeo ya sheria; kutokana na kuwa na Agenda Maalum ya 10/30, hivi sasa tunafanya marejeo katika sheria zetu zote ili kuhakikisha kwamba zinaendana na mipango tuliyonayo ya kukuza sekta ya kilimo kwa asilimia 10 ifikapo mwaka 2030, ikiwemo sheria ambayo pia inaongoza zao la kahawa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari; Mheshimiwa Katani Ahmadi Katani, Mbunge wa Tandahimba, swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, naona ananiangalia. Haya, amesimama Mheshimiwa Mussa Sima.

Na. 507

**Tatizo la mawasiliano Kata za Litehu, Ngoja na Mkwiti – Tandahimba**

**MHE. MUSSA R. SIMA K.n.y. MHE. KATANI A. KATANI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itapeleka mawasiliano ya simu yenye usikivu katika Kata za Litehu, Ngonja na Mkwiti Wilayani Tandahimba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhandisi Kundo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Katani Ahmadi Katani, Mbunge wa Jimbo la Tandahimba, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, vijiji vilivyopo katika Kata za Mkwiti, Litehu na Ngonja vitafanyiwa tathmini kujua mahitaji halisi ya huduma ya mawasiliano na hatimaye kuingizwa katika orodha ya miradi ya Serikali itakayotekelezwa na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF)* kulingana na upatikanaji wa fedha, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mussa Sima, swali la nyongeza.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ninataka kujua tu, kwanza ni lini vijiji hivyo vitafanyiwa tathmini?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; pale Singida Mjini, Kata ya Unyamikumbi ndiyo kata pekee ambayo mawasiliano yanasumbua sana: -

Je, ni lini Serikali itatuletea mnara kwa ajili ya kutatua tatizo la mawasiliano katika kata ile?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima kwa niaba ya Mheshimiwa Katani, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, tathmini tayari imeshaanza kufanyika na awamu ya kwanza tumekamilisha vijiji 2,116. Kwa hiyo naamini

kwamba katika awamu ijayo vijiji na kata za Litehu, Ngonja na Mkwiti zitaingizwa katika utekelezaji huo, na baada ya hapo, fedha zitakapopatikana tutafikisha huduma ya mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, kipengele cha pili kuhusu Kata ya Singida Mjini pale, tutatuma wataalam wetu wakaangalie tatizo ni lipi hasa. Kama ni kuongeza nguvu tutafanya hivyo, na kama itahitaji kupeleka mnara tutafanya hivyo. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Phillipo Mulugo, swali la nyongeza.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ninataka niulize swali moja la nyongeza kwa Serikali: -

Jimbo la Songwe ni jimbo ambalo liko kijijini sana, na Kata za Magamba, Mpona, Ifwenkenya, Manda, Mkukwe, Ngwara na Gua hazina mawasiliano kabisa;

Je, ni lini Serikali itapeleka mawasiliano katika kata hizo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Phillipo Augustino Mulugo, Mbunge wa Jimbo la Songwe, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimesema, ili vijiji viingizwe katika utekelezaji ni lazima kwanza vifanyiwe tathmini, na tayari katika vile vijiji 2,116, vijiji vya Mkoa wote wa Songwe vipo. Na juzi tumesaini mikataba ya kupeleka minara 758 lakini Mheshimiwa Rais ametafuta fedha kwa ajili ya minara mingine 600. Kwa hiyo naamini kwamba katika vijiji ambavyo tayari vimeshafanyiwa tathmini, tutapeleka minara hiyo 600 ili kuhakikisha kwamba huduma ya mawasiliano inaimarika kwa wananchi.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Deus Sangu, swali la nyongeza.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Vijiji vya Kapewa na Mtetezi vilivyopo Kata ya Mpui vina changamoto kubwa ya mawasiliano. Nataka kujua ni lini Serikali mtapeleka minara katika vijiji hivyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, vijiji ambavyo Mheshimiwa Mbunge amevitaja vipo katika utekelezaji wa Mradi wa Tanzania Kidigitali. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza; je, ni lini Serikali itapeleka mtandao katika Vijiji vya Hunyali, Kihumbu na Sarakwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge tayari ameshafika ofisini kwetu na mimi nimekuwa nikiwasiliana naye mara kwa mara na tayari vijiji ambavyo ameshavileta ofisini viko kwenye mchakato wa kuingizwa katika utekelezaji. Pindi fedha zitakapopatikana tutafikisha huduma ya mawasiliano katika vijiji ambavyo Mheshimiwa Getere amevitaja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Almas Maige, swali la nyongeza.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu niulize swali la nyongeza. Je, ni lini Serikali itapeleka mawasiliano katika Kata ambazo Jimbo la Tabora Kaskazini hakuna mawasiliano; Igulungu, Chitage, Bukumbi na Chese?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Athuman Almas Maige, Mbunge wa Tabora Kaskazini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa, tunakiri kwamba Tabora Kaskazini ina changamoto kubwa sana ya mawasiliano; na katika mradi wetu huu kwa bahati mbaya sana haikuwezekana. Hata hivyo, tayari tumeshachukua kata tano za Tabora Kaskazini ambazo tunakwenda kuzifikishia huduma ya mawasiliano ndani ya mwaka huu wa fedha, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Issa Mtemvu, na wewe Dar es Salaam kuna mahali simu hazisikiki? Haya, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Ni kweli kabisa Dar es Salaam, hasa Dar es Salaam Vijijini, Kibamba kule, mawasiliano ni shida. Maeneo ya Mabwepande eneo la Kibesa na maeneo ya Kata ya Saranga, maeneo ya mpakani na Ilala hakuna kabisa mawasiliano: -

Je, Serikali mko tayari kwa minara 600 hii kupeleka na maeneo hayo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, Mbunge wa Kibamba, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge wiki jana alinifikishia changamoto hii, na tayari Serikali tumeshaipokea na tunaifanyia kazi. Tutamjulisha Mheshimiwa Mbunge hatua ambayo tutakuwa tumefikia kulingana na upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cosato David Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 508

**Gharama za mawasiliano**

**MHE. COSATO D. CHUMI** aliuliza: -

Je, kwa kiasi gani Mkongo wa Taifa umesaidia kuboresha na kupunguza gharama za mawasiliano?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Cosato David Chumi, Mbunge wa Jimbo la Mafinga Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano nchi nzima ambao unafanyika kwa awamu mbalimbali kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, ni kweli uwepo wa muundombinu huu umeboresha huduma za mawasiliano na kusaidia kupunguza gharama za mawasiliano kwa kupunguza gharama za uwekezaji kwa watoa huduma za mawasiliano ambao wangepaswa kujenga muundombinu kama huu kuboresha miundombinu na huduma zao. Hii imesaidia kupunguza gharama za mawasiliano *(cost of backhaul transport bandwidth)* kwa asilimia 99 na kufanya gharama za maunganisho kwa watoa huduma kupungua kutoka shilingi 157 mwaka 2015 hadi kufikia shilingi mbili mwaka 2022.

Mheshimiwa Spika, kupungua kwa gharama hizi kumesaidia kushuka kwa gharama za huduma kwa mtumiaji wa mwisho kutoka shilingi 147 kwa dakika mwaka 2009 hadi shilingi 30 kwa dakika mwaka 2022, sawa na asilimia 79.6; hii ni pasipo kutumia vifurushi.

Mheshimiwa Spika, matokeo makuu ya kushuka kwa gharama hizi kupitia miundombinu wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ni kuongezeka kwa matumizi ya huduma za mawasiliano kwa wananchi na Serikali kwa ujumla. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cosato David Chumi, swali la nyongeza.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, ili upitishe miundombinu ya mawasiliano kwa kila kilometa moja watu wa mawasiliano wanachajiwa dola 1,000, lakini ukipitisha miundombinu kama ya maji au umeme kando ya barabara kuu za *TANROADS* au za *TARURA, charge* yake ni kama dola 50 kwa kilometa moja.

Je, Serikali haioni ni wakati sasa wa kuzungumza ndani kwa ndani ya Serikali ili kupunguza hiyo gharama ya dola 1,000 ili kupunguza hizo gharama za mawasiliano?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; maeneo ya Mtula, Kisada na Kata nzima ya Bumilayinga, kuna masiliano ya kusuasua: -

Je, ni lini Serikali itaboresha na kuimarisha mawasiliano katika kata hizo za Mji wa Mafinga?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Cosato David Chumi, Mbunge wa Jimbo la Mafinga Mjini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kuna gharama za kupitisha mkongo wa Taifa ambazo ni dola 1,000 ambazo tunaziita *right of ways* na Mheshimiwa Rais tayari ameshaelekeza tuhakikishe kwamba tunalifanyia kazi kwa sababu gharama hizi mwisho wa siku zinaingia kwenye *capex* na mwisho wa siku zinaenda kwa mtumiaji wa mwisho.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ili tuhakikishe kwamba mtumiaji wa mwisho anapata huduma ya mawasiliano kwa gharama nafuu ni kuhakikisha kwamba gharama ambazo zilizopo katikati hapa ambazo zitamsababishia mtumiaji wa mwisho kuwa na gharama kubwa ya kutumia huduma ya mawasiliano tumeshaanza kazi nzuri ya kushirikiana na wenzetu *TANROADS*, *TARURA* na kadhalika ili kuhakikisha kwamba hizi gharama tumezitazama kwa namna ambayo zitasaidia zaidi wananchi badala ya kuwaumiza wananchi, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Martha Festo Mariki Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 509

**Kuanzisha matawi ya Vyuo Vikuu Katavi**

**MHE. MARTHA F. MARIKI** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha matawi ya Vyuo Vikuu vya Umma katika Mkoa wa Katavi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Juma Kipanga majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia napenda kujibu swali la Mheshimwa Martha Festo Mariki, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Sita imelenga kupanua na kuboresha huduma za jamii ikiwemo Elimu ya Juu ili kufikia maeneo yote ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kutokana na azma hiyo, Serikali kupitia Mradi wa *Higher Education for Economic Transformation*

– *HEET* wa miaka mitano kuanzia mwaka 2021-2026 inatarajia kujenga kampasi mpya 14 za Vyuo Vikuu katika mikoa ambayo haina Taasisi ya Elimu ya Juu ukiwemo Mkoa wa Katavi.

Mheshimiwa Spika, Kupitia Mradi wa *HEET,* Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo *(SUA)* kimetengewa jumla ya shilingi bilioni 18.4 kwa ajili ya ujenzi wa kampasi mpya katika Mkoa wa Katavi Wilaya ya Mlele, Halmashauri ya Mpimbwe. Kwa sasa kazi zinazoendelea katika kampasi hiyo ni tathmini ya athari za kimazingira na Jamii yaani *environmental and social impact assessment* na mchakato wa kumpata mshauri elekezi unatarajia kukamilika mwishoni mwa mwezi Juni 2023 na baadaye mkandarasi wa ujenzi, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Martha Mariki swali la nyongeza.

**MHE. MARTHA F. MARIKI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa ni azma ya Serikali kukuza kilimo nchini. Je, Serikali haioni sasa kuna umuhimu wa kuwapa kipaumbele kwenye mikopo wanafunzi ambao wanachaguliwa kwenda kusomea masomo ya kilimo hususan katika kampasi zilizopo pembezoni mfano kampasi ya Mizengopinda ya sasa hivi ina zaidi ya miaka mitatu ambayo imejikita zaidi katika kutoa elimu ya nyuki?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa sasa katika Mkoa wa Katavi tuna hiyo kampasi moja. Serikali haioni kuna umuhimu wa kuongeza kamapasi nyingine ili kupanua wigo wa elimu katika Mkoa wetu wa Katavi kwa kuongeza kampasi kama vyuo vya afya pamoja na vyuo vya uhasibu? Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Martha Mariki Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwenye swali lake la kwanza anataka kufahamu mkakati wa Serikali juu ya mikopo. Naomba kumfahamisha

Mheshimiwa Mbunge Serikali imekuwa ikiongeza kiwango au kiasi cha mikopo kwa wananfunzi wa elimu ya juu. Kwa takwimu zilizopo kwa mwaka 2021/2022 tulitenga na kupeleka jumla ya bilioni 570 kwa ajili ya wanafunzi hao. Mwaka 2022/2023 tulipeleka zaidi ya bilioni 554 hela ya kawaida lakini tulikuwa na vile vile bilioni tatu kwa ajili ya *Samia Scholarship* lakini katika bajeti yetu vile vile tumeweza kutenga jumla ya bilioni 738 kwa ajili ya mikopo katika mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wote kwamba Serikali imejipanga na kujizatiti kuhakikisha kwamba wanafunzi wetu wanapata mikopo kwa wakati wake.

Mheshimiwa Spika, tuna kozi za vipaumbele ikiwemo na hiyo aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge kozi za sayansi lakini zile za uhandishi, kozi za udaktari na kozi hizi za kilimo pamoja na masuala ya nyuki kwa ujumla wake ndizo ambazo tunazizingatia katika utoaji wa mikopo katika kipindi kijacho.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la pili anataka kufahamu utaratibu gani Serikali itatumia kuongeza idadi ya vyuo. Nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge. Uwepo wa kampasi hii unaweza ukasaidia katika kuongeza aidha ndaki au shule nyingine katika kampasi hii. Kwa sababu tukumbuke hata hiyo *University of* Dar es Salaam wakati inaanzishwa ilianza na kozi moja lakini imeweza kupanuka mpaka hivi sasa ina kozi mbalimbali. Kwa hiyo, hata kozi hizi hapo baadae tutaangalia uhitaji na namna gani ya kuweza kuangalia kozi nyingine za kuanzishwa katika kampasi hii, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Juliana Shonza swali fupi.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuzingatia kwamba Mkoa wa Songwe ni mpya naomba kufahamu Serikali ina mkakati gani wa kutujengea angalau kampasi moja tu ya chuo kikuu cha umma, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shonza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwisha eleza katika majibu ya swali la msingi kwamba tunakwenda kujenga kampasi 14 katika mikoa kumi na nne nchini. Moja ya Mikoa ambayo tunaweza kujenga ni katika Mkoa wa Songwe ambapo Chuo chetu cha *DIT* ndicho ambacho kitakwenda kujengwa katika eneo hili la Songwe.

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako labda ningeweza kusema na mikoa mingine ambayo inaweza kujengewa ili Waheshimiwa Wabunge waweze kujua. Naanza na Mkoa wa Manyara Chuo chetu cha *TIA* kitakwenda kujenga tawi pale. Singida ni *TIA*, Kagera *University of* Dar es Salaam, Lindi *University of* Dar es Salaam, Ruvuma ni *TIA*, Shinyanga ni *MAMCU*, Simiyu ni *IFM,* Rukwa ni *MUST*, Tabora ni Julius Nyerere, Kigoma ni *MUHAS*, Zanzibar ni *University of* Dar es Salaam, Mwanza ni *ARU*, Tanga ni Mzumbe na Songwe ni *DIT*, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Hapa nimesikia Songwe imetajwa au umesharidhika.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Mheshimiwa Spika, swali langu lilikuwa linafanana na la Mheshimiwa Shonza.

**SPIKA:** Haya Ahsante sana. Mheshimiwa Omar Ali Omar Mbunge wa Wete sasa aulize swali lake.

Na. 510

**Kupanga kusahihisha mitihani ya kidato cha nne Zanzibar**

**MHE. OMAR ALI OMAR** aliuliza: -

Je, kwa nini Serikali haipangi kusahihishia mitihani ya kidato cha nne Zanzibar?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Omari Ali Omari, Mbunge wa Wete, kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2021 na 2022 Serikali ilisahihisha mitihani ya Taifa, kidato cha nne *(CSEE)* katika kituo cha Shule ya Sekondari Hasnuu Makame, Kusini Unguja. Aidha, Serikali itaendelea kusahihisha mitihani Zanzibar kwa vituo vya mitihani vyenye sifa za kulaza watahini wasiopungua 500 kwa wakati mmoja, kuwa na vyumba visivyopungua ishirini vya kazi, na miundombinu ya maji na umeme kwa wakati wote wa kazi ya kusahihisha, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Omar Ali Omar swali la nyongeza.

**MHE. OMAR ALI OMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Ni masomo gani ambayo yalisahihishwa katika kipindi hicho alichokitaja Mheshimiwa Waziri 2021/ 2022?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; je, Wizara imejipanga kusahihisha mitihani mingapi katika mwaka 2023?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ali Omar kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika utaratibu wa usahihishaji wa mitihani kila kituo kawaida huwa kina sahihisha mtihani mmoja na kwa miaka hiyo niliyoitaja ya 2021/2022 katika kituo hiki cha Zanzibar ni somo la *civics* ndilo ambalo lilisahihishwa katika kituo hicho.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la pili anataka kufahamu ni mitihani gani ambayo itasahihishwa. Masuala ya mitihani na masomo gani yatasahihishwa ni jambo la siri. Kwa hiyo, hatuwezi ku-*disclose* hatuwezi kufungua hapa sasa hivi ni mitihani gani utakwenda kusahihishwa kwenye kituo hiki na ni mapema Sana.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tarehe 26 Juni, tutaanza kufanya ukaguzi wa vile vituo ambavyo tunalenga sasa mitihani itakwenda kusahihishwa lakini somo gani kwamba linapelekwa katika kituo hicho litaendelea kuwa siri mpaka baada ya kazi hiyo kumalizika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 511

**Kuwatengea maeneo mengine wakulima pindi Serikali inapotwaa maeneo yao**

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA** aliuliza:-

Je, ni ni kwa nini Serikali pindi inapotwaa maeneo ya wakulima isiwatengee maeneo mengine mbali ya kulipa fidia?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Pinda majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI,** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Naghenjwa Livingston Kaboyoka Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi, Sura 113 kifungu cha 3 Kifungu kidogo cha (1)(g), malipo ya fidia ni takwa la kisheria pindi Serikali inapotwaa ardhi kutoka kwa wananchi. Kimsingi, fidia kwa mujibu wa Sheria inajumuisha thamani ya ardhi na maendelezo yaliyopo juu ya ardhi. Fidia yaweza kulipwa kwa fedha au kupewa ardhi mbadala au vyote kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitekeleza fidia ya ardhi mbadala au fedha au vyote kwa pamoja kutokana na mazingira ya eneo la mradi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka swali la nyongeza.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nina maswali mawili ya nyongeza, kwa vile kumekuwa na malamaiko ya wananchi ambao wananyang'anywa mashamba yao halafu wanapewa hela. Katika harakati za kuhangaika kutafuta mashamba mpaka ile hela inaisha. Je, Serikali haioni kuna umuhimu wa kuelimisha wananchi kuhusu Sheria hii ili pale wanapopewa fedha waombe pia wapewe na shamba?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; kutokana na kwamba ardhi kubwa ya Tanzania haijapimwa. Je, Serikali itakapowapa mashamba mbadala hawa wananchi walionyang'anywa itawahahikishiaje kwamba hawatahamishwa tena maana haya yameshatokea na wananchi wanahangaika sana katika kuji-*establish* mara ya tatu. Naomba nipate majibu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa swali lake la kwanza kwamba tutoe elimu ya hii Sheria kwa wananchi ili waweze kupata fidia zote mbili kwa pamoja au kwa namna yoyote ile.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye swali la msingi, suala la fidia linazingatia sana mazingira ya eneo ambapo mtu anafidiwa. Kwa hao wenzetu wa kulima kimsingi mamlaka za Mkoa huwa zinashirikishwa kwa karibu sana katika suala zima la namna ya kuwapa fidia ya maeneo mengine wale wananchi na kumekuwa hakuna matatizo makubwa sana. Usalama wa mashamba pale wanapofidiwa yale mashamba kwa vyovyote kama ni mkono wa Serikali umekwenda kuwaondoa pale. Yale mashamba mapya watakayopewa lazima yatolewe kwa utaratibu wa kupimwa na wapewe zile hati ambazo zitawasaidia kuwaweka kwenye usalama wa maeneo mapya waliyopewa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Waitara swali la nyongeza.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwenye Jimbo langu eneo la Mgodi wa *Barrick North Mara*, Serikali ilipeleka Mthamini Mkuu wa Serikali ikafanye *evaluation* eneo la kiwanja na *Mkomalela North* tangu mwaka jana. Mwaka huu wanasema hawana mpango wa kutoa hilo eneo.

Je, nini kauli ya Serikali kwa wananchi wale katika maeneo ya kiwanja na Mkomalela?

**SPIKA:** Swali hilo nadhani limeshawahi kujibiwa na Wizara ya Madini ama sio swali hilo. Mheshimiwa Waitara ni swali hilo hilo au sio.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, ule mgogoro upo huu wamezua mwingine juzi tena hili ni jipya. Ni jipya kabisa.

**SPIKA:** Ambaye hana mpango wa kuchukua ni nani? Mgodi.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, yaani Mgodi ili ulipe fidia Wizara ya Ardhi inatuma Mtathmini anafanya tathmini walifanya

hivyo na wakatoa *notice* kuzuia wanainchi wasiendeleze maeneo yale kwa sababu mgodi unachukua. Baada ya mwaka mmoja. Juzi madiwani na wenyeviti wa vijiji wakaitwa eneo hilo wakaambiwa sasa mgodi hauna mpango wa kutwaa hilo eneo, shida inabaki hapo.

**SPIKA:** Nataka kuelewa ni swali hilo hilo ambalo limewahi kujibiwa na Madini kwa sababu Serikali ni moja asije huyu wa ardhi hapa akajibu tofauti na wale wa madini halafu tukatekeleza mgogoro mwingine. Wewe niambie ni swali hilo hilo ambalo umeshawahi kuuliza kwa Wizara ya Madini au hapana.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, ni swali jipya kama hana majibu anaweza akajipanga. Mimi nitali...

**SPIKA:** Hapana, yeye sijampa nafasi ya kujibu bado nataka tuelewani mimi na wewe kwanza ili nijue nimpe nafasi yupi maana Serikali ni moja. Swali ni hilo hilo au ni tofauti.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, ni swali jipya, ahsante.

**SPIKA:** Kuhusu jambo hilo hilo.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Ndio, jambo hilo hilo.

**SPIKA:** Swali jipya kuhusu jambo hilo hilo.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, ndio.

**SPIKA:** Watu wa Madini, Waziri.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, swali alilozungumza Mheshimiwa Waitara na hata tulivyojibu wakati ule, tulikuwa tunazungumzia eneo la Mrwambe na Nyamichune. Maeneo ambayo yalifanyiwa uthamini baadae mgodi ukaonesha kwamba hauyahitaji ukawarudishia wananchi. Sasa kwa sababu wananchi walikuwa wamesubiri kwa muda na kwa mujibu wa Sheria ikabidi walipwe kitu kinachoitwa fedha ya usumbufu au *excrasher*. Kwa hiyo, mwezi wa

sita huu mgodi umeshakubali kulipa hizo fedha na Mheshimiwa Waitara tulishazungumza. Namuomba tu avumilie kidogo kwa sababu mwezi wa sita ndio huu tumeuanza watalipwa wakamilishe.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waitara majibu hayo ni ya mgogoro huo yanavyotoka huko Madini. Kwa hiyo, tusimweke mazingira Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kujibu swali ambalo tayari limeshajibiwa na watu wa Madini.

Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata swali la nyongeza.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Nilitaka kujua ni lini Serikali itamaliza mgogoro wa shamba la *EFATHA* ambalo unavikumba vijiji vya Msanda, Muungano, Kaungu, Sandulula, Malonje, Ulinzi na Mawenzusi. Ni lini sasa mgogoro huu utaisha wananchi wanapata tabu sana sana hawana pa kulima. Tunaomba Serikali imalize mgogoro huu. Ni lini sasa Serikali itamaliza mgogoro huu? Ahsante.*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza Waheshimiwa Wabunge ni wape angalizo. Vyanzo vingi vya migogoro ni matumizi ya nguvu yasiyozingatia utaratibu. Tunapotoa shamba kwa mwekezaji, mwananchi mwingine yeyote haruhusiwi kwenda kulivamia lile shamba bila kuzingatia taratibu. Kama unaona kabisa kwamba zile taratibu za umiliki wa yule mmiliki zimekiukwa fuata taratibu tulishatoa maelekezo. Halmashauri zianzishe ule mchakato wa kumjadili huyu muhusika wa shamba hilo ambaye ameliteIekeza.

Mheshimiwa Spika, wananchi kuanza kuvamia maeneo haya kwa kweli sio kitu cha busara sana. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge sisi ni viongozi wote tushirikiane kwenye hili kuwaelimisha wananchi juu ya taratibu zinazoweza zikafatwa ili kupata kile ambacho tunakihitaji kwa matumizi yetu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri anataka kujua mgogoro utamalizwa lini maana yake mgogoro upo wewe umeelezea kuzalishwa kwa mgogoro sasa kwa kuwa mgogoro tayari upo utakwisha lini ndio swali la Mbunge.*(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyotangulia kusema maelezo haya tayari tumekwishaanza na tumeunda timu ya ufatiliaji ili makundi ya pande mbili zote yakutane ili kuona uwekezekano wa kulimaliza hili tatizo.

Mheshimiwa Spika, kama mninavyosema vyanzo vikubwa vya migogoro hii ni matumizi ya nguvu zisizozingatia taratibu.

**SPIKA:** Hilo umeshaeleweka, hoja ni kwamba mgogoro ukisha kuwepo lazima umalizwe, lazima umalizwe. Ukishakuwepo mgogoro umeshatengenezwa lazima umalizwe sasa aliyepelekea huko. Naona Waziri amesimama.

Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa fursa kwa ajili ya kujibu suala hili na nimshukuru pia Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri.

Mheshimiwa Spika, mgogoro huu wa *EFATHA* na wananchi wa Sumbawanga kama alivyosema. Mgogoro huu ni wa siku nyingi na mgogoro ulisha wahi kufika mahakamani lakini ulitokana pia na mgawanyo wa maeneo katika lile eneo ambapo mwekezaji alipewa. Mwekezaji alifata taratibu zote katika kupewa yale maeneo. Changamoto inapokuja ni kwamba kadri mahitaji ya wananchi yanavyozidi kuwa makubwa basi wanaona kama vile mwekezaji pengine amekiuka taratibu katika kupewa, lakini taratibu zote zifuatwa.

Mheshimiwa Spika, naomba niwahakikishie wananchi wa Jimbo la Sumbawanga ambako ndiko kuna mgogoro huo, nitakwenda mwenyewe kule kwa ajili ya kuzungumza nao ili tuweze kuumaliza kwa sababu umekuwa ni wa muda mrefu. Tutapanga na Mbunge kwenda kuumaliza mgogoro huo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Askofu Josephat Mathias Gwajima, Mbunge wa Kawe, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Mariam Kisangi.

Na. 512

**Kumaliza Migogoro ya Ardhi – Kawe**

**MHE. MARIAM N. KISANGI K.n.y. MHE ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itamaliza migogoro ya ardhi maeneo ya Chasimba, Chatembo, Chachui, Nkasangwe na Mabwepande – Kawe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante na kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Askofu Josephat Mathias Gwajima, Mbunge wa Kawe, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, migogoro ya ardhi katika Jimbo la Kawe kwa ujumla inahusu wananchi wa Chasimba, Chatembo na Chachui kuvamia eneo la Kiwanda cha Wazo, wananchi kuvamia mashamba ya wananchi wengine katika eneo la Nkasangwe na wananchi kufanya maendelezo katika mashamba yenye miliki likiwemo Shamba la Shirika la *DDC* katika eneo la Mabwepande.

Mheshimiwa Spika, kwa nyakati tofauti Serikali imekuwa ikishughulikia migogoro hii kwa kuwashawishi wamiliki wa maeneo yaliyovamiwa kuyaachia maeneo hayo ambapo wananchi tayari wameshavamia na kufanya maendelezo na wanapaswa kulipa fidia kwa wamiliki. Hata hivyo, pamoja na jitihada hizo za Serikali kutatua migogoro hiyo kiutawala, kumekuwa na mwitikio mdogo kwa wananchi kulipa fidia kwa maeneo waliyovamia na hivyo kuchelewesha upatikanaji wa suluhisho la kudumu la migogoro hii.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Kisangi, swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri, kwanza naipongeza Serikali kwa niaba ya Mheshimiwa Askofu Gwajima, kwa kweli alikuwa huko na amelishughulikia suala hili na Serikali imelipokea na imelifanyia kazi. Pongezi sana kwa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, je, Serikali imejipanga vipi sasa kuhakikisha inadhibiti migogoro yote iliyopo katika jimbo hilo ili isijirudie tena? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha Mgogoro wa Shamba la Malolo upande wa Jimbo la Kibamba Halmashauri ya Ubungo nao unaumaliza kama vile walivyomaliza kwenye Wilaya ya Kinondoni? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza udhibiti wa migogoro isiweze kujitokeza, ni juhudi za Serikali na tumekuwa tukishirikiana na taasisi mbalimbali katika kuhamasisha migogoro hii isiendelee kujitokeza. Hata hivyo, suala la Malolo, Kibaha nimwahidi tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kwamba baada ya Bunge lako Tukufu kumalizika, tutaanza

ziara za kutembelea maeneo haya na kukutana na wananchi na taasisi zile ambazo zinagongana kwenye migongano hii ili kuitafutia suluhisho la kudumu, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Afya. Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga, Mbunge wa Viti Maalumu, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete.

Na. 513

**Kumaliza tatizo la uviaji mimba**

**MHE. SALMA R. KIKWETE K.n.y. MHE. JUDITH S. KAPINGA** aliuliza:-

Je, Serikali inafanya nini kuhakikisha uviaji mimba usio salama unakwisha?

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka mikakati mbalimbali ya kuhakikisha uavyaji mimba usio salama unakwisha kama ifuatavyo: -

(i) Kutoa elimu juu ya afya ya uzazi kwa watoto wa kike ambao wapo chini ya umri wa kuzaa, klabu za vijana na vijana balehe kutojihusisha na ngono zembe ili kuepuka kupata mimba zisizotarajiwa.

(ii) Kusimamia utoaji wa huduma za uzazi wa mpango katika vituo vya huduma bila malipo ili kuwawezesha wanawake na wanaume kuzuia mimba zisizotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwaasa vijana, akina mama na wanaume wote kwa pamoja wachukue hatua za kuhakikisha kuwa mimba zinazopatikana zinakuwa zimepangwa na wawe wanahudhuria katika kliniki zetu za uzazi wa mpango ili waweze kupatiwa elimu ya afya ya uzazi ikiwemo jinsi ya kuepukana na mimba zisizotarajiwa ili kuondokana na uavyaji wa mimba usio salama, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, swali la nyongeza.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa majibu ya Serikali. Nina swali la nyongeza. Kwa kuwa utoaji wa Mimba siyo kitu kizuri na kinahatarisha maisha ya wasichana: Je, elimu hiyo ambayo mmeitoa, imetolewa kwa kiwango gani au katika mikoa mingapi ya nchi yetu ya Tanzania? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba elimu ni mchakato endelevu na ni mchakato ambao watoto wanapata mashuleni, lakini kila akina mama wanapohudhuria kliniki tunawapa elimu na vile vile, kuna vipindi mbalimbali vinavyotolewa kwenye *tv* ambavyo vinawafikia wananchi. Kwa hiyo, kimsingi hakuna Mkoa wala wilaya ambayo elimu hiyo haijatolewa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, Mbunge wa Same Magharibi, sasa aulize swali lake.

Na. 514

**Usambazaji wa umeme wa *REA* - Same Magharibi**

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID** aliuliza:-

Je, ahadi ya Serikali ya kusambaza umeme wa *REA III* katika vijiji 48 vya Jimbo la Same Magharibi na vitongoji vyake imefikia wapi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Stephen Byabato, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, Mbunge wa Same Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Same, Vijiji 91 kati ya 100 tayari vimepelekewa umeme na vijiji tisa vilivyobaki vitapelekewa umeme ifikapo mwezi Desemba, 2023.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali imepanga kuanza ujenzi wa miundombinu ya kusambaza umeme katika vitongoji 2,034 nchini kwa gharama ya shilingi bilioni 377.05 ambapo vitongoji 15 katika Jimbo la Same Magharibi vitapelekewa umeme. Serikali itaendelea kupeleka umeme kwenye vitongoji 162 vilivyobaki kulingana na upatikanaji wa rasilimali fedha, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, tuna vijiji zaidi ya hivyo ambavyo amevitaja Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa mfano vijiji vya Gundusini, Mabilioni,

Gavao, Saweni, Rwinndini, Ruvu, Jiungeni, Mferejini, Duma, Emugule na Endevesi vyote hivi havina umeme. Sasa Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari tutembelee vijiji hivi ili aone hali halisi kuliko kwamba zinawekwa nyumba mbili halafu tunaambiwa Kijiji kimewekewa umeme? Hilo halitakubalika.

Mheshimiwa Spika, la pili. Je, Serikali iko tayari kutoa kwa Wabunge orodha ya Wakandarasi wale wanaokwenda kuweka umeme katika maeneo yao ili nao waweze kufuatilia? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nishukuru Waheshimiwa Wabunge jana wametupitishia bajeti kwa ajili ya kwenda kutekeleza miradi na ahadi ambazo tumezitoa. Pia nimwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba niko tayari kuambatana naye kwenda jimboni kwake baada ya Bunge kuisha ili kuona vijiji hivyo ambavyo havijafikiwa na umeme. Kama tulivyosema viko tisa na ni kweli hata jana tumesoma kwenye bajeti, tunatambua kwamba sio wananchi wote na vitongoji vyote vimepata umeme, lakini jitihada na hatua zimeanza na tunaamini tutakamilisha. Ifikapo Desemba, 2023 hatutarajii kuwa na kijiji ambacho hakijafikiwa na miundombinu ya umeme.

Mheshimiwa Spika, katika eneo lingine, tuko tayari na tulishafanya hivyo na tutafanya tena kuhakikisha kila Mbunge anamfahamu Mkandarasi wake na *scope* yake na wale wanaosaidia katika usimamizi. Nikitoka hapa nitapitia kwa Mheshimiwa Mbunge nimpatie pia wale wa kwake wanaofanya kazi kwenye maeneo yake ili aweze kuwa na nafasi nzuri ya kufanya ufuatiliaji yeye mwenyewe.

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo, Mbunge wa Kishapu, sasa aulize swali lake.

Na. 515

**Kupeleka umeme katika kata ambazo hazina umeme – Kishapu**

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka umeme katika Kata za Lagana, Itilima na Bunambiyu Wilayani Kishapu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

**NAIBU WAZIRI NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo, Mbunge wa Kishapu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mkandarasi M/S SUMA JKT anayetekeleza mradi wa *REA III Round II* katika Wilaya ya Kishapu ana jumla ya vijiji 51 katika mkataba wake, vikiwemo vijiji vya Kata za Lagana, Itilima na Bunambiyu Wilayani. Mkandarasi kwa sasa anaendelea na utekelezaji wa mradi ambapo ameshawasha umeme katika vijiji 13 kati ya 51 sawa na asilimia 25.5. Aidha, kati ya vijiji 13 vilivyowashwa, vijiji vitano ni vya Kata ya Itilima. Mkandarasi anaendelea na ujenzi katika vijiji 38 vilivyobakia vikiwemo vijiji vitano vya Kata ya Lagana, vijiji vitatu vya Kata ya Itilima na vijiji viwili vya Kata ya Bunambiyu ambavyo vinatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Desemba, 2023.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha mradi unakamilika kwa wakati, Serikali imemfungulia Mkandarasi Hati ya Muamana *(LC)* ili aweze kuhakikisha anaongeza kasi ya kufanya kazi na kuimaliza mwezi Desemba, 2023, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Spika, naomba niishukuru sana Serikali kwa majibu mazuri, lakini bado kasi ya

utekelezaji wa miradi inakwenda taratibu sana. Swali la kwanza: Je, Mheshimiwa Waziri, uko tayari kuambatana nami ili twende jimboni ili tukasukume kwa pamoja utekelezaji wa miradi hii katika jimbo langu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Kata ya Bunambiyu pamoja na Mwasubi ni maeneo ambayo zikinyesha mvua huwa hayapitiki ni maeneo ambayo yanapata maji kwa wingi sana. Sasa, mko tayari kuhakikisha kwamba mnaweka msukumo mkubwa ili maeneo hayo yapewe kipaumbele, wakati huo huo maeneo hayo niliyoyataja na yenyewe yaweze kufanyiwa kazi kwa haraka?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Boniphace, amekuwa akifuatilia sana haya maeneo na mradi ule mkubwa wa umeme wa kutumia *solar* ambao tumeufanikisha juzi kuusaini, na katika Jimbo lake, mkoa wote wa Shinyanga na nchi nzima itakuwa ni faraja kubwa.

Mheshimiwa Spika, namuahidi kwamba niko tayari kuambatana naye kwenda kuhakikisha tunaendelea kumsimamia mkandarasi huyu kama tulivyoahidi katika bajeti. Vile vile, mbinu za kufungua *LC*, kuongeza wasimamizi na kuwawezesha, zitatusaidia kuhakikisha kwamba ndani ya muda tunakamilisha kazi hii. Hilo jambo la maeneo ambayo yana changamoto, tutalichukua kwa ukubwa wake ili kuhakikisha tunamaliza kazi hii mapema kwa mujibu wa mkataba. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwenu na Serikali kutoa majibu. Waheshimiwa Mawaziri mnaozungumza tusikilizane. Tutaanza na tangazo la wageni. Tutaanza na wageni walioko Jukwaa la Spika.

Kwanza ni wageni wangu kutoka Benki ya CRDB na hawa ni Ndugu Jane Maganga ambaye ni Meneja Biashara CRDB Benki

Kanda ya Kati Dodoma; Ndugu Benedicta Mshana, Meneja Biashara *CRDB Bank* Kanda ya Kusini Mtwara; Ndugu Japhary Katula, Meneja Biashara *CRDB Bank*, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Mbeya; Ndugu George Yatera, Meneja Biashara *CRDB Bank*, Kanda ya Mashariki Dar es Salaam; Ndugu David Peter, Meneja Biashara *CRDB Bank,* Kanda ya Kaskazini, Arusha; Ndugu Ferooz Korongo, Meneja Biashara, *CRDB Bank,* Kanda ya Ziwa, Mwanza; Ndugu Jumanne Wagama, Kaimu Meneja, Kanda ya Magharibi; na Ndugu Grace Kisole, Meneja Tawi la Bunge, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana. Leo kuna orodha ndefu ya wageni hapa mbele, sijui hayo makofi tutaenda nayo kwa sura gani, lakini siku ya leo wageni ni wengi hapa ndani.

Wageni wangu wengine 56 ambao ni Wanakwaya, Kwaya ya Mtakatifu Yohane Paul wa II wa Kanisa Katoliki la Mbeya Mjini, karibuni sana. Kipekee kabisa, namwona mmoja amebeba na mtoto pale kuonesha kwamba kazi inaendelea. Pia kwaya hii inalelewa na Mheshimiwa Phillipo Mulugo, Mbunge wa Songwe. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wangu wengine wawili kutoka *Serena Hotel* ya Jijini Dar es Salaam, na hawa ni Ndugu Seraphin Lusala - Mkurugenzi wa Mauzo na yupo pia Ndugu Alex Kulwa, Mhasibu Mkuu, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni wa Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, anao wageni wake walioko Jukwaa la Spika ambao tutaanza kuwatangaza.

Kwanza ni Dkt. Hassan Abbas, Katibu Mkuu; Ndugu Anderson Mutatembwa, Naibu Katibu Mkuu; Ndugu Cyrus Kapinga, Mkurugenzi wa Sera na Mipango; Ndugu Prisca Lwangili, Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimaliwatu; Dkt. Maurus Msuha, Mkurugenzi wa Wanyamapori; Ndugu Deusdedith Bwoyo, Mkurugenzi wa Misitu na Nyuki; Dkt. Teresa Mugobi, Kaimu Mkurugenzi wa Utalii; Dkt. Christowaja Ntandu, Mkurugenzi wa Mambo ya Kale; Jenerali Mstaafu George Marwa Waitara ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi *TANAPA;* Meja Jenerali Mstaafu Hamis Semfuko ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi

ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania *(TAWA);* na yupo pia Jenerali Mstaafu Venance Salvatory Mabeyo ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, haya ahsanteni sana. *(Makofi)*

Yupo pia Dkt. Siima Bakengesa ambaye ni Mwakilishi wa Mwenyekiti wa Bodi Tendaji ya Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania *(TFS);* Dkt. Oswald Masebo ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Makumbusho ya Taifa; Ndugu William Mwakilema, Kamshina wa Uhifadhi *(TANAPA);* Ndugu Mabula Misungwi Nyanda, Kamshina wa Uhifadhi Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori *(TAWA);* Ndugu Elibariki Bajuta, Naibu Kamishna wa Uhifadhi Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro; Profesa Dos Santos Silayo, Kamshina wa Uhifadhi Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania *(TFS);* Ndugu Damas Mfugale, Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Utalii Tanzania *(TTB);* Dkt. Noel Lwoga, Mkurugenzi Mkuu Shirika la Makumbusho ya Taifa Tanzania; na Dkt. Ernest Mjingo, Mkurugenzi Mkuu, Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania *(TAWIRI)*. *(Makofi)*

Pia yupo Dkt. Revocatus Mushumbusi ambaye ni Mkurugenzi Mkuu Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzani (*TAFORI);* Yupo Profesa Jafari Kidegesho ambaye ni Mkuu wa Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori – MWEKA; yupo Dkt. Florian Mtei ambaye ni Kaimu Mkuu wa Chuo cha Taifa cha Utalii; yupo pia Dkt. Edward Kohi ambaye ni Mkurugenzi wa Utafiti na Mafunzo; yupo pia Ndugu Lucy Saleko, Mkurugenzi wa Sheria. Karibuni sana. *(Makofi)*

Sasa hawa Wameambatana na hawa wafuatao ambao tutawatambulisha kwa makundi; wapo wafanyabiashara na wawakilishi wa vyama vya utalii; wapo wadau wa sekta ndogo ya misitu na nyuki, *NABAC*, *TABEDO NA EAMCEF*; wapo wadau wa sekta ndogo ya wanyamapori, *TWEA* na *TNRF;* wapo viongozi wa CCM kutoka mikoa yenye migogoro kati ya wanyamapori na binadamu. Karibuni sana. *(Makofi)*

Utambulisho huu naamini Mheshimiwa Waziri kwa namna kazi inavyofanywa huu utambulisho hatutaurejea mwakani ya migogoro kati ya wanyama pori na binadamu naamini tutakuwa tumekaa vizuri

kwa hiyo watakuja wawakilishi wa maeneo yenye hali nzuri, nawatakia kila lakheri kwenye hili. Wapo pia Naibu Makamishna na Makamanda wa Kanda wa Jeshi la Uhifadhi kutoka *TANAPA, TAWA, NCAA* na *TFS,* karibuni sana. *(Makofi)*

Sasa ili mpigwe picha vizuri simameni halafu mpige wote saluti kwa pamoja ili picha iitoke vizuri. Haya ahsanteni sana wahifadhi wetu. *(Makofi)*

Pia wapo wadau kutoka vyombo vya habari ambao wamelikwa na Mheshimiwa Waziri. Haya, pengine hawajapata nafasi ya kuingia sasa wataingia baadaye wapo. *(Makofi)*

Wapo wadau kutoka Benki ya *NMB*, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunao wageni wetu Wabunge, tutaanza na Wageni 11 wa Mheshimiwa Ummy Mwalimu ambaye ni Waziri wa Afya na hawa ni walimu na wanafunzi wa Tanga *Girl Guide* kutoka Mkoa wa Tanga, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo Wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko, Waziri wa Madini kutoka Mkoa wa Geita, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo Wageni 32 wa Mheshimiwa Angela Kairuki, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, na hawa ni watumishi 32 Waadventista Wasabato kutoka Jimbo la Mara wakiongozwa na Askofu Mkuu Jimbo la Mara Mchungaji Joseph Matongo; karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Vita Kawawa ambaye ni mtoto wake kutoka Jijini Dodoma, karibu sana.

Wapo wageni watano wa Mheshimiwa Catherine Magige ambao wanatoka *TAWTO Members Safari* ya Jijini Arusha, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Florent Kyombo ambao ni wananchi kutoka Nkenge Mkoa wa Kagera, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Mwita Waitara kutoka Tarime Mkoa wa Mara wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Tarime, Mheshimiwa Simon Samuel, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Kenneth Nollo ambao ni Chama cha Wakandarasi Wanawake Tanzania kutoka Mikoa mbalimbali, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 30 wa Mheshimiwa Ally Kassinge, ambao ni walimu na viongozi wa Chama cha Walimu kutoka mikoa na wilaya mbalmbali nchini, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Luhaga Mpina kutoka Denmark na Jimboni Kisesa, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni tisa wa Mheshimiwa Japhet Hasunga ambao ni Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Vwawa na Wafanyakazi wa Shule kutoka Mkoa wa Songwe, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni sita wa Mheshimiwa Cosato David Chumi ambao ni wazalishaji wa bidhaa za mazao ya misitu wakiongozwa na Afisa Biashara na Uwekezaji wa Halmashauri ya Mji wa Mafinga Ndg. Kassim Mohamed Said, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 40 wa Mheshimiwa Mohamed Monni ambao ni wanafunzi 30 na walimu 10 wa Shule ya Msingi Kuu kutoka Chemba Mkoani Dodoma, nadhani hawajapata nafasi hapa, wameshasimama? Naam? Aanh! wako upande huu. Haya, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 72 ambao ni Timu ya Michezo ya Mwanza Vetenari *Sport Club* waliokuja kujifunza namna Bunge linavyofanya kazi, na hawa wanatoka Mkoa wa Mwanza, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge kuna jambo moja tulizungumza jana kuhusu Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, kwamba leo wangetoa kauli kuhusu likizo ya wanafunzi na kambi, lakini wameomba watoe

kauli hiyo siku ya jumatatu na mimi nimewaruhusu. Kwa hiyo siku ya jumatatu watatoa kauli kuhusu kambi za wanafunzi walio kwenye madarasa yale ambayo yanafanya mitihani mwakahu watatoa maelezo haya jumatatu halafu tutaona baada ya wao kutoa tuchukue hatua gani kama zipo za kuchukua.

Waheshimiwa Wabunge ninayo matangazo mawili moja linatoka kwa Mwenyekiti wa *Bunge Sport Club* ambapo anawatangazia kuhusu hawa wageni wetu waliotoka Mwanza; kwamba Waheshimiwa Wabunge wote kesho siku ya jumamosi tarehe 03 juni, 2023 kutakuwa na mechi ya kirafiki ya mpira wa miguu na pete kati ya timu ya Waheshimiwa Wabunge na timu ya *Mwanza Veteran* ambayo mechi hiyo itachezwa katika uwanja wa Jamhuri saa tisa na nusu alasiri.

Vilevile timu ya Mwanza Veteran wapo humu ndani ya Ukumbi wa Bunge sasa hivi nimeshawatangaza kwa hiyo waheshmiwa Wabunge wote mnakaribishwa kwenda kuwashangilia Wabunge wakati wakiwafunga magoli mengi Mwanza Veteran; ina maana timu za Bunge, ya pete na miguu wanacheza vizuri sana kama Yanga. *(Makofi na Kicheko)*

Haya ahsanteni sana, jamani sasa Yanga ndio wawakilishi wetu kimataifa kwa hiyo maana yake ndio wao wanafanya vizuri.

Tangazo lingine linatoka kwa Katibu wa Bunge; Waheshimiwa Wabunge mnatangaziwa kuwa Wizara ya Fedha na Mipango itaendesha semina kuhusu matumizi ya matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 pamoja na Sensa ya Majengo, Semina hii itafanyika siku ya jumatatu tarehe 5 Juni, 2023 mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge saa saba kamili mchana, itafanyika Ukumbi wa Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa kuhudhuria semina hii muhimu hasa ukizingatia namna mnavyofuatilia miradi ya maendeleo katika maeneo yenu na ni vizuri kwa sababu mmeshafahamu wako watu wangapi huko mkijua na majengo basi inakuwa rahisi zaidi kutoa michango yenu hapa ndani.

Waheshimiwa Wabunge hayo ndiyo matangazo niliyokuwa nayo hapa mbele tunaendelea na ratiba yetu.

Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tuko kwenye hoja za Serikali sasa nimwite Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, aje awasilishe hoja ya Wizara yake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, leo katika Bunge lako tukufu, ninaomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Aidha, ninaomba Bunge lako tukufu lijadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa bashrafu ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kunipa afya na uzima na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako hili tukufu leo kutoa taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Serikali kupitia Sekta ya Maliasili na Utalii. Aidha, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kuwajalia afya njema viongozi wetu wakuu wa kitaifa, Waheshimiwa Mawaziri wenzangu, Waheshimiwa Wabunge, viongozi wengine wa Serikali na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee kabisa na kwa unyenyekevu mkubwa sana nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Amiri Jeshi Mkuu, kwa kuendelea kuniamini na kuniteua kusimamia Wizara

hii leo ikiwa natimiza miezi mitatu na siku 19 tangu tarehe 14 Februari, 2023, aliponihamisha kutoka sekta michezo. Hii ni Wizara yangu ya tatu katika kipindi cha mika mitatu. Naomba nichukue fursa hii kumwahidi Mheshimiwa Rais na Bunge lako kwamba mimi na watendaji wenzangu tutaendeleza kwa nguvu zetu zote na maarifa, kujitoa na kujitolea na zaidi ubunifu mkubwa wote pale ambapo wenzetu walipoanza sisi tutaendeleza, na kwamba Bunge hili na mihimili mingine ya dola itarajie ushirikiano wa dhati kutoka kwetu.

Mheshimiwa Spika, usuli wa yote, Wizara hii imepewa dhamana ya kusimamia, kulinda na kuendeleza maeneo ya hifadhi za wanyamapori, misitu, nyuki na malikale yenye mchango mkubwa katika uhifadhi wa mazingira, ustawi wa wananchi lakini pia ukuaji wa uchumi. Aidha, Wizara hii ina jukumu la kuendeleza utalii ambao pia ni chanzo cha mapato ya fedha za kigeni na fursa za ajira kwa Watanzania. Ni kwa muktadha huo wa mtawanyiko wa majukumu ya Wizara hii, tulipoingia, mimi na wenzangu tulifanya uchambuzi wa kina na kuja na falsafa mbili zinazojengwa katika nguzo kubwa mbili kuu zinazofupisha muktadha wa malengo na majukumu adhimu ya Wizara hii kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, mosi, nguzo inayojenga jukumu kubwa la kwanza la Wizara hii ni uhifadhi *(conservation)*. Uhai wetu sisi wanadamu unategemea maji na pia viumbe hai wengine kama vile wanyama na mimea. Takriban vyote hivi viko kwenye maeneo yanayolindwa au kupaswa kuangaliwa na Wizara hii. Takriban vyanzo vyetu vyote vya maji hapa nchini vinatokana na misitu inayolindwa. Misitu hiyo inayotupa leo kivuli, nishati, chakula isingelindwa isingekuwepo. Nchi yetu inasifika kwa wanyamapori waliotapakaa sehemu mbalimbali wanaosaidia utalii wetu, kitoweo na uchumi wa mwananchi mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla. Vyote hivi bila uhifadhi, havipo.

Mheshimiwa Spika, kwa minajili ya kufupisha umuhimu wa sekta ya uhifadhi kwa uhai wa taifa yatosha kumnukuu Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, mwaka 1961; alitoa tamko kwenye Kongamano la Kimataifa la Uhifadhi Kuhusu Mustakabali wa

Wanyamapori katika Afrika huru. Tamko hili maarufu kama Arusha *Manifesto* alisema naomba nimnukuu Baba wa Taifa: -

Mheshimiwa Spika, Baba wa Taifa alisema; "Uhai wa wanyamapori ni jambo linalotuhusu sote katika Afrika. Viumbe hawa wa porini, wakiwa katika mapori wanamoishi, siyo muhimu tu kwa ajili ya kuajabiwa na kuvutia lakini pia ni sehemu ya maliasili yetu na pia ndio mustakabali wa maisha yetu ya baadaye. Kwa kukubali dhamana ya wanyamapori wetu tunatamka kwa dhati kwamba tutafanya kila tuwezalo kuhakikisha kwamba wajukuu wa watoto wetu wataweza kufurahia urithi huu mkubwa na wa thamani adhimu. Uhifadhi wa wanyamapori na maeneo yote yenye mapori huhitajia maarifa ya kitaalamu, wafanyakazi waliopata mafunzo maalumu, na fedha; na hivyo tunaomba mataifa mengine yashirikiane nasi katika kazi hii muhimu, ambayo kufanikiwa au kutofanikiwa kwake hakuathiri tu Bara la Afrika bali ulimwengu mzima kwa ujumla". Mwisho wa kumnukuu Mwalimu Julius Kambarge Nyerere mwaka1961.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana tunasema tumeamua na wakati ni sasa. Juhudi nguvu maarifa na rasilimali zetu nyingi tuendaka na katika siku chache zinaelekezwa kwa nguvu zaidi katika kuendeleza uhifadhi.

Mheshimiwa Spika, nguzo yetu ya pili inayounda jukumu jingine kuu la Wizara hii ni kujitangaza (*promotion*). Hii inatokana na muktadha wa nguzo ya kwanza kwamba nchi yetu imejaaliwa rasilimali nyingi za misitu, wanyamapori na malikale. Ili rasilimali hizi zilete faida za kiutalii na uwekezaji mwingine mkubwa lazima zitangazwe kwa nguvu na ubunifu mkubwa *(aggressiveness and creativeness)*. Tunatambua kwambawahenga walipata kunena kuwa "*chema chajiuza, kibaya chajitangaza,*" tunawashukuru sana. Lakini katika zama hizi za ushindani, kila mtu akivutia alichonacho, sisi, tumeamua kwenda na kauli nyingine ya wahenga isemayo "*Mgaagaa na upwa hali wali mkavu*"

Mheshimiwa Spika, mwelekeo mpya sasa wa Wizara ni kuhakikisha "Tunagaagaa na Upwa" kwa kuwekeza nguvu zaidi na kwa njia za kisasa na ubunifu zaidi kutangaza rasilimali zetu na utalii

wetu ili kuliingizia Taifa letu mapato zaidi katika sekta hii ambayo hata bila kuwekeza sana katika kujitangaza tayari inachangia asilimia 25 ya fedha za kigeni na asilimia 21 ya Pato la Taifa. Tunaweza na inawezekana kwenda maradufu ya sasa; na hapa tulipo na kwa vyovyote vile hatutakula wali mkavu.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kumpongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwani yeye ndiye mwana maono, mkuu wa falsafa na misingi niliyoieleza hapo juu, kwani amekuwa mhifadhi namba moja aliyehakikisha wanyamapori, misitu na vyote vilivyomo ndani yake vinalindwa kwa faida ya leo na vizazi vijavyo. Na yeye na Serikali zilizopita wameruhusu takribani asilimia 32 ya ardhi ya nchi yetu kuwa maeneo maalum yaliyohifadhiwa. Akiwa muumini pia wa nguzo kuu ya pili ya sekta hizi, ni yeye pia aliyetoka ofisini na kwenda milimani, mabondeni, alikwenda baharini, alihifadhi na hata majukwaani katika kushiriki filamu ya "*Tanzania; The Royal Tour*," hivyo kusaidia kuutangaza utalii wetu katika namna ambayo haijapata kutokeakutokea na kuleta faida lukuki ambazo nitazieleza punde.

Mheshimiwa Spika, halikadhalika, napenda pia kutumia fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; kwa jinsi nao, kwa nyakati tofauti ambavyo wamekuwa wakijipambanua kuwa waumini na watekelezaji wakubwa wa maono ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika uhifadhi na utangazaji wa Utalii.

Mheshimiwa Spika, sisi waumini wa uhifadhi, uendelezaji na utangazaji wa utalii, tunaamini kwa dhati kuwa kwa namna moja au nyingine, kila Mtanzania ni mdau wetu na kila anachokifanya au kukitenda kilicho chema kinasaidia kufikia azma ya nchi yetu kufikia watalii milioni tano na mapato yanayofikia Dola za Marekani bilioni sita ifikapo mwaka 2025. Hivyo basi, kwa niaba ya wadau wa uhifadhi na utalii na Watanzania wote kwa ujumla natumia fursa hii kulipongeza Bunge lako Tukufu kupitia wewe Mheshimiwa Dkt. Tulia

Ackson Mwansasu, Mbunge, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge, Naibu Spika, pamoja na Wenyeviti wa Bunge, Wenyeviti wa Kamati na Wabunge wote kwa miongozo yenu ya mara kwa mara, ushauri wenu na mapendekezo ya kuhakikisha uhifadhi na utangazaji wa utalii vinaendelea vyema.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, naungana na Waheshimiwa Mawaziri wenzangu walionitangulia kumpongeza Mheshimiwa Abdul Yussuf Maalim kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Amani, Zanzibar na kuungana nasi katika Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, "*Figa moja haliinjiki chungu*" kwa dhati, na kwa nia yako ya kutusaidia kwa karibu, ulitupa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii yenye wabunge wabobezi na watopezi wa sekta hii na wenye mapenzi na uhifadhi na utangazaji wa utalii chini ya Mwenyekiti mahiri kabisa Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava (Mb) Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Najma Murtaza Giga (Mb) Mheshimiwa Simai Mohamed Waziri wa utalii wa mambo ya kale kule zanzibara kwa ushirikano mzuri alionipa.

Mheshimiwa Spika, na Waheshimiwa Wanakamati. Wabobezi hawa, wametuthibitishia kuwa "*Penye wengi pana mengi*," wamejadili nasi, wametoa ushauri na mapendekezo na vyote sasa vimekuwa msingi wa mapendekezo ya makadirio haya ya mapato na matumizi na bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Tunawashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, "chanda chema huvikwa pete" naomba kutumia fursa hii pia kuwashukuru viongozi na Watendaji wenzangu wa wizara na katika taasisi zetu kwa ushirikiano, ubunifu, usimamizi na utekelezaji makini wa yale ambayo tunaelekezwa au yapo kwenye mkakati ya Serikali na Wizara.

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Mary Francis Masanja, Mbunge, Naibu Waziri mbobezi wa sekta hizi; Dkt. Hassan Abbasi Said, Katibu Mkuu mbunifu asiyechoka; Ndugu Anderson Gukwi Mutatembwa, Naibu Katibu Mkuu mwanamikakati makini;

wenyeviti wa bodi wote kwa uchache, Jenerali Mstaafu George Marwa Waitara, *TANAPA,* Jenerali Mstaafu Venance Salvatory Mabeyo, Ngorongoro, Meja Jenerali Hamis Rajab Semfuko, *TAWA*, Brigedia Jenerali Baraka Naziadi Mkeremi, *TFS*, Wakurugenzi wa Idara na Vitengo na Wakuu wa Taasisi, wanataaluma mahiri na wafanyakazi wa kada za kati mpaka wa chini wanaojituma sana, wote nawashukuru kwa kujitoa sana katika kutekeleza majukumu yao. Hakika nyie ni nguzo muhimu ya wizara na mjue kwamba mnanisaidia sana na mnaliheshimisha Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee pia, nitambue na kushukuru, kwa umaalum wake na kwa unyenyekevu wa juu kabisa, askari na maafisa wa Jeshi la Uhifadhi wanaokesha kila uchao maporini, wanakesha vilimani, mabondeni, kwenye maji au misitu minene, kwenye jua, kwenye mvua usiku na mchana kulinda na kuhifadhi rasilimali zetu na wanyamapori, malikale na misitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kutimiza wajibu wao huo kwa Taifa, askari hao vijana ni watoto wetu wazalendo, wapo ambao kwa kujitoa kwao huko wamejeruhiwa kunusurika kupoteza maisha, kama askari wetu hodari waliotaka kuzamishwa majini na majingili kule Manyara hivi karibuni na hata wengine wamepoteza maisha wakiwemo askari Deus Mwakajegela aliyefariki kwa kuchomwa mkuki mwaka jana akilinda mpaka wa Hifadhi ya Taifa Serengeti. Askari Theonas Nota aliyefariki kwa ajali ya ndege aina ya Cesna siku chache zilizopita ndege 192-5HFZS wiki mbili zilizopita akienda doria kule Pori la Akiba Selous na askari Taiko Olesalei Marau ambaye akiwa mstari wa mbele akiongoza doria na wenzake watano katikati ya eneo la misitu minene ya Hifadhi ya Ngorongoro Mei 18, 2023, aliyevamiwa na kuuawa na wanyama hatari aina ya mbogo. Wapo askari 13 na Wakala wa Huduma za Misitu *(TFS)* waliouawa na wananchi au majangili wa misitu katika maeneo mbalimbali nchini. Akiwemo mmojawapo ambaye ametoweshwa na mpaka sasa haijulikani alipo na familia yake imebaki kuishi na majonzi makubwa. Jitihada za kumtafuta mtumishi huyo bado zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, aidha, Bunge lako Tukufu pia litambue kuwa Taifa limewapoteza Askari wa *TAWA*, James Chacha Karomba,

aliyeuwawa na wafugaji akitekeleza majukumu yake katika Pori la Akiba la Inyonga, Askari Mwita Msabi aliyeuawa na majangili wakati wa Doria ya ushirikiano na TFS katika Hifadhi ya Msitu wa Uzungwa, Askari Chacha Mwita Magoro, Nkwabi Daudi na Mathias Mgongolwa waliofariki katika ajali ya maji wakati wakipambana na majangili katika Mapori ya Igombe, Lukwika Lusekelo na Kilombero.

Mheshimiwa Spika, hakuna namna ya kuwalipa mashujaa hawa, zaidi ya kuwaombea, kuendelea kuwatambua na kuwathamini daima milele na sisi sote kuazimia kuendeleza walipoishia katika kuzilinda rasilimali zetu. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. Amen. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni vyema kusisitiza hapa kwa wananchi wetu kutii sheria bila shuruti na pia kuwaona askari hawa kuwa wazalendo wa Taifa na kushirikiana nao. Naendelea kuwasihi askari wetu wa Jeshi la Uhifadhi, licha ya mafunzo ya kijeshi mliyoyapata, waliyonayo na silaha mlizonazo mnazozibeba, kuendelea kujifunza na kutumia busara kila inapobidi, kama ambavyo wamefanya mara nyingi, katika kuendelea kukabiliana na wananchi wasiotaka kutii sheria na wanapokabiliana na wahalifu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natambua katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita, Bunge lako Tukufu pia limeondokewa na baadhi ya Wabunge wenzetu akiwemo Mheshimiwa Mussa Hassan Mussa, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Amani Zanzibar. Aidha, nitoe pole pia kwa Bunge lako na Serikali kuondokewa na Wabunge wenzetu wa zamani, Waziri wa zamani wa Mambo ya Nje, Mheshimiwa Bernard Kamilius Membe; Mheshimiwa Herman Kiligini Waziri wa zamani wa Kilimo na Mifugo na Mheshimiwa Wakili Nimrod Mkono aliyekuwa Mbunge wa zamani wa Jimbo la Musoma Vijijini ambalo sasa ni Butiama. Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi, Amen.

Mheshimiwa Spika, "Kibuzi na Kibuzi Hununua Jahazi", katika kuelekea mwisho lakini si kwa umuhimu na wa bashrafu hii ya hotuba yangu, nikiri nguvu, ari na kujituma kwangu katika kuwahudumia wadau wa maliasili na utalii licha ya watendaji wenzangu wizarani kunachangiwa kwa kiasi kikubwa na makundi haya mawili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mosi na kipekee naishukuru sana familia yangu, kila mmoja ana mchango wake katika familia yangu lakini kipekee nimshukuru sana Mke wangu Mheshimiwa Wanu Hafidh Ameir, Mbunge ambaye hayupo hapa leo yupo safarini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yupo kijana wetu hapa leo Nassir Mohamed Mchengerwa anayewakilisha familia aliyeambatana na wanafunzi wenzie. Ambaye ambatana na wanafunzi wenzake kuja Bungeni kujifunza, mtoto wenu huyu. Napenda kuwashukuru kwa upendo wao, uvumilivu wao na maombi yao kwangu wakati wote katika utekelezaji wa majukumu yangu ya Kitaifa. Sina cha kuwalipa zaidi ya kuwaahidi utendaji bora, kuwaheshimisha na zaidi kuendelea kuwa baba bora wa familia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili; nawashakuru sana wananchi wangu wa Jimbo langu la Rufiji wakiongozwa na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Pwani, Mwishehe Mlaho na Mwenyeketi wa Chama cha Mapinduzi Wilaya ya Rufiji Kasokala Mbonde. Pili nawashukuru sana kila mmoja kule Rufiji kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika kutekeleza majukumu ya Kitaifa na Jimbo na kuniombea kila siku. Ninaahidi sitawaangusha na nitaendelea kushirikiana nao kila hatua katika kuleta maendeleo ya jimbo letu na Taifa kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hotuba yangu imegawanyika katika sehemu kuu sita ambazo ni; Utangulizi; Majukumu; Mwelekeo na Vipaumbele vya Wizara; Mchango wa Maliasili na Utalii katika kukuza Uchumi na Maendeleo Endelevu; Maoni na Ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii; Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na haya yote yameelezwa kwa kina katika Kitabu cha Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mwaka 2023/2024 ambacho kimewasilishwa mezani kwako na naomba kiwe sehemu ya Kumbukumbu Rasmi ya Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Spika, kwa muhtsari naomba sasa kuwasilisha utekelezaji wa mikakati ya makadirio ya mapato na matumizi kwa bajeti ya mwaka ujao wa fedha kwa Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mchango wa Sekta ya Maliasili na Utalii katika kukuza uchumi na maendeleo endelevu; umuhimu wa Sekta ya Maliasili na Utalii kwa Taifa unaweza kuelezwa kwa namna nyingi, mifano mingi na takwimu nyingi, lakini vyakutosha kujitangaza sana ili kuvuna matunda ya sekta hizi, tayari mchango wa sekta hizi ni mkubwa ambapo Sekta ya Utalii pekee inachangia asilimia 25 ya fedha za kigeni, huku Sekta ya Misitu ikichangia asilimia 5.9 ya mapato yote ya nje. Kwa upande wa Pato la Taifa, Sekta ya Utalii inachangia takriban asilimia 17.5 na Sekta ya Misitu na Nyuki inachangia asilimia 3.3 ya Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mpango wa Bajeti kwa mwaka wa 2022/2023, ukusanyaji wa maduhuli; katika mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara ilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 670.86. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 469.36 zinakusanywa kupitia mfumo ya TEHAMA wa Wizara kwenda Mamlaka ya Mapato Tanzania kutokana na vyanzo vya mapato kutoka *TANAPA*, *NCAA* na *TAWA* na shilingi bilioni 201.49 zinakusanywa na Wizara kutokana na vyanzo vya mapato kutoka Idara, Mifuko na baadhi ya taasisi zake kupitia Mfumo wa *MNRT Portal*. Hadi kufikia mwezi Aprili 2023, Wizara imekusanya jumla ya shilingi bilioni 616.34 sawa na asilimia 92 ya lengo la makusanyo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 485.70 zimekusanywa na Wizara kutokana na vyanzo vya taasisi za *TANAPA, NCAA* pamoja na *TAWA* na shilingi bilioni 130.64 zimekusanywa na wizara kutokana na idara, mifuko na baadhi ya taasisi zake.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya kawaida na maendeleo; katika mwaka wa fedha 2022/2023; Wizara iliidhinishiwa kutumia jumla ya shilingi bilioni 624.14 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 443.71 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 180.44 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi kufikia mwezi Aprili 2023, Wizara na taasisi zake ilipokea jumla ya shilingi bilioni 449.17 sawa na asilimia 72 ya fedha iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 353.80 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 95.37 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Fedha za matumizi ya kawaida zinajumuisha shilingi bilioni 144.71, fedha za matumizi mengineyo na shilingi bilioni 209.09

fedha za mishahara. Fedha zilizopokelewa zimewezesha kufanikisha utekelezaji na kuleta mafanikio mbalimbali katika Sekta ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, mafanikio 10 muhimu katika utekelezaji wa majukumu muhimu ya Sekta ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Wizara katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imepata mafanikio mbalimbali makubwa ambayo tumeyaainisha kwa kina katika kitabu cha bajeti ya Wizara kuanzia ukurasa wa 19 hadi 29 na ukurasa wa 39 hadi ukurasa wa 89 lakini kwa upekee wake haya 10 ya kimkakati ni ya muhimu kwa wananchi wetu kuyafahamu ili Waheshimiwa Wabunge pia watupe maoni yao ya ziada.

Mheshimiwa Spika, watalii wamiminika waongezeka mara dufu nchini. Kufuatia juhudi zilizofanywa za pamoja na wadau kutangaza vivutio vya utalii, kuimarika kwa miundombinu ya utalii ndani ya hifadhi na kuzinduliwa kwa filamu aliyoshiriki Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan yaani *Tanzania the Royal Tour* kwa ujumla watalii Nchini wa ndani na nje wameongezeka mara dufu kutoka jumla ya watalii 1,711,625 mwaka 2021 hadi kufikia jumla ya watalii 3,818,180 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 123. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mafanikio haya idadi ya watalii wa kimataifa imeongezeka kutoka 922,692 mwaka 2021 hadi kufikia watalii 1,454,920 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 57.7. Aidha, idadi ya watalii wa ndani imeongezeka kutoka watalii 788,933 mwaka 2021 hadi 2,363,260 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 199.5. Hongera sana kwa Mheshimiwa Rais na wadau wote wa utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mapato ya jumla ya utalii yaongezeka mara dufu. Katika kipindi hiki mapato yatokanayo na watalii yameongezeka kutoka dola za Kimarekani milioni 1,310 mwaka 2021 hadi kufikia dola za Kimarekani milioni 2,527.72 kwa mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 93 na makadirio ya mwelekeo wa sasa ni kuwa mwaka huu tunaweza kuvuka nusu ya malengo tuliyojiwekea, kufikisha mapato ya

sekta hizi ya dola bilioni sita kwa mwaka, tunaweza na wakati ni sasa, tunaweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Taasisi za Wizara za vunja rekodi ya idadi ya watalii tangu zianzishwe. Pamoja na kuongezeka kwa ujumla kwa idadi ya watalii Kitaifa katika kipindi hiko cha utekelezaji taasisi kubwa za utalii nchini zimeshudia kuvunjwa kwa rekodi ya idadi ya watalii katika maeneo yao kwa mujibu wa taarifa za miaka 10 yaani kuanzia Julai mwaka jana hadi Aprili mwaka huu. Kwa mfano wakati wa mwaka mzima 2021/2022 miezi 12 *TANAPA* ilipokea jumla ya watalii wa ndani na nje 734,847 na katika kipindi cha miezi 10 tu Julai mpaka Aprili 2023 tayari watalii wamefikia milioni 1,438,399.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Wakala wa Huduma za Misitu *(TFS)* watalii wameongezeka kutoka 152,002 kwa mwaka mzima wa 2021/2022 hadi kufikia watalii 220,826 kwa miezi 10 tu ya mwaka 2022/2023. Aidha, kwa upande wa *TAWA* watalii na wawindaji wameongezeka kutoka 531,000 kwa mwaka 2021/2022 hadi kufikia watalii wawindaji 692,000 kwa kipindi cha miezi 10 tu ya Mwaka wa Fedha 2022/2023 kwa *record* hii taasisi hizi zimepokea watalii wengi kuliko wakati wowote katika historia ya kuanzishwa kwa taasisi hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mapato ya utalii kwa taasisi nayo yaongezeka mara dufu. Kama ilivyo kwa idadi ya watalii karibu taasisi zote za utalii nchini zimevunja rekodi ya mapato katika maeneo yao. Kwa mfano watalii wakati *TANAPA* kwa mwaka mzima 2021/2022 walikusanya jumla ya shilingi bilioni 174 kwa miezi kumi tu kwa mwaka wa fedha wamekusanya zaidi ya bilioni 291. Kwa upande wa Mamlaka ya Ngorongoro, mapato kwa mwaka 2021/2022 yalikuwa ni shilingi bilioni 91, wakati mwaka huu kwa miezi 10 tu yamevuka hadi kufikia bilioni 141.6. Mapato yote haya kwa taasisi hizi mbili ni makubwa kiukweli hayajawahi kutokea wala hayajawahi kukusanywa Taifa hili, tutaendelea kusimamia mapato haya na niko hapa kuwathibitishia Waheshimiwa Wabunge tunaweza na tunaweza kufika malengo na ndoto za Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Hifadhi za Tanzania zapata tuzo Duniani. Mafanikio ya tano makubwa yaliyotekelezwa na wizara yetu ni pamoja na matokeo ya utunzaji wa usimimamizi wa vivutio vyetu vya utalii kiasi cha kutambulika Kimataifa na kuongoza au kupata tuzo kubwa ikiwemo Hifadhi ya Taifa Serengeti kutangazwa kuwa ni hifadhi bora Afrika *(African's Leading National Park Attraction)* kwa kipindi cha miaka minne mfululizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika *World Travel Awards,* Tanzania kutajwa kuwa ni moja ya maeneo 24 ya kutembelewa Duniani kiutalii kwa mwaka 2022, *CNN Travel where to travel in 2023 the best destination to visit* na pia Hifadhi ya Taifa ya Serengeti imetajwa kuwa ni miongoni mwa vivutio sita vikubwa vinavyopendekezwa kutembelewa duniani kwa mwezi Juni, 2023, *trip advisor, May 2023* lakini kwa mujibu wa Shirika la Habari la Kiutalii la Nchini Marekani la *U.S. News Travel* katika habari yake iliyokuwa na anwani ya *best places to visit ni June 2023* Hifadhi ya Taifa Serengeti na hasa tukio la uhamiaji wa wanyama *wildebeest migration* limetajwa kuwa ni tukio namba moja katika vivutio vikubwa 15 duniani. Tukio la wanyama *wildebeest migration* limetajwa kuwa ni tukio kubwa duniani katika vivutio 15 ambapo walimwengu wamesisitizwa kutembelea mwezi Juni 2023. Nawapongeza wahifadhi wanautalii wote nchini na nje ya nchi kwa mafanikio hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuongezeka kwa idadi ya mapori ya akiba. Katika jitihada za kuendeleza uhifadhi wa rasilimali muhimu katika kipindi hiki pia Wizara imefanikiwa kupandisha mapori tengefu mawili yaani Kilombero na Pololeti, kuwa mapori ya akiba. Hatua hii imeongeza idadi ya mapori ya akiba kutoka 27 hadi 29. Lengo la jitihada hizi ni kuimarisha ulinzi na matumizi endelevu ya rasilimali na utunzaji wa vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, ulinzi wa rasilimali waimarika Tanzania sasa ni rekodi za dunia tu. Wizara imeendelea kuongeza jitihada na kuimairisha ulinzi wa uhifadhi wa rasilimali za maliasili kwa kudhibiti ujangili, biashara haramu ya nyara, uvunaji haramu wa mazao ya misitu na nyuki na uvamizi wa maeneo yaliyohifadhiwa. Mafanikio haya yamechangiwa na juhudi mbalimbali za Serikali ikiwa ni pamoja

na kufanya siku ya doria 479,242 zilizowezesha kukamatwa kwa watuhumiwa 12,058 pamoja na nyara mbalimbali za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jitihada hizi pamoja na mambo mengine zimewezesha kuongezeka kwa idadi ya tembo kutoka 43,330 mwaka 2014 hadi 60,000 kwa mwaka 2023 na kufanya Tanzania kuwa ni Nchi ya tatu Afrika kwa tembo wengi. Idadi ya faru weusi imeongezeka kutoka 163 mwaka 2019 hadi 238 mwaka 2022 na hivyo kuvuka lengo kwa Mkakati wa Kitaifa wa Kuhifadhi Faru 205 ifikapo Desemba 2023. Aidha kwa sasa idadi ya samba nchini imefikia zaidi ya 14,912 na kuifanya Tanzania kuongoza duniani kwa kuwa na simba wengi kuliko Taifa lolote duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuendeleza kampeni za upandaji miti na mashamba ya miti. Katika kuhakikisha upatikanaji wa malighafi itokanayo na misitu nchini inazidi kuwa ya kutosha, wizara kupitia Taasisi ya Utafiti wa Misitu Nchini *(TAFORI)* imezalisha miche 26,900,353 ambayo ilipandwa katika mashamba ya Serikali yenye ukubwa wa hekta 7,475 na miche mingine kugawiwa kwa jamii na kupandwa katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hatua hizo, wizara kwa kushirikiana na Benki za *NMB* imeanzisha kampeni ya kupanda miti Kitaifa ambayo ilizinduliwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, mwezi Machi, 2023. Kampeni hii ina lengo la kupanda takriban miti 1,000,000 kwa mwaka katika maeneo ya shule za msingi na sekondari.

Mheshimiwa Spika, aidha, mafanikio mengine makubwa yaliyopatikana kwenye sekta ya misitu ni pamoja na kufunguka kwa biashara ya hewa ya ukaa nchini. Tayari Tasisi za *TFS* na *TAWA* zimeshaingia makubaliano ya awali na Kampuni ya *Blue Carbon* kutoka Falme za Kiarabu na *Green Cop* ya nchini Singapore. Makubaliano haya yanalenga kuhakikisha kuwa Tanzania inaendelea kunufaika na biashara ya hewa ya ukaa huku ikisaidia kudhibiti athari za tabianchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuongezeka kwa masoko ya kiwango cha mazao ya nyuki yanayouzwa nje ya nchi. Moja ya mazao bora ya misitu ambayo nchi yetu imejaaliwa ni zao la asali. Kwa sasa nchi yetu ni miongoni mwa nchi zinazozalisha asali bora kabisa duniani. Katika kuhakikisha asali inayozalishwa nchini inaendelea kuwa ni ya viwango vya ubora vinavyohitajika katika masoko ya kimataifa, Wizara imeanzisha mfumo unaoitwa *Honey Traceability System* ambao unafuatilia ubora wa asali kuanzia kwa mfugaji nyuki hadi pale inapoingia sokoni.

Mheshimiwa Spika, aidha, kupitia mashindano ya ubora wa asali inayozalishwa Barani Afrika, asali kutoka Mkoa wa Tabora ilishika nafasi ya pili kwa ubora Afrika. Kutokana na juhudi hizi, asali ya Tanzania imeendelea kukuzwa na masoko ya nje na kupendwa kabisa katika masoko ya Umoja wa Ulaya, Uarabuni na kwenye masoko mapya Poland na nchini China.

Mheshimiwa Spika, kufuatia mafanikio haya, nitumie fursa hii kuwaomba Watanzania kuchangamkia fursa hii ya kuzalisha asali ili kunufaika na masoko haya yaweze kuiingizia nchi yetu fedha za kigeni kwani asali nayo ni dawa, ni chakula na ni kipato, kwani mwaka 2021/2022 mauzo ya fedha za kigeni kutokana na asali na nta nje ya nchi yalifikia jumla ya shilingi bilioni 30.58 iliyotokana na tani 1,562.93 na asali ya tani 747.56 ya nta. Vilevile mazao ya misitu ya nje ya nchi yalikuwa shilingi bilioni 234.5 mwaka 2022. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, linginie ni kuhusu kufunguka kwa mazao mapya ya utalii wa ikolojia na historia. Katika kutanua wigo wa mazao ya utalii na kuongeza idadi ya watalii na mapato, Wizara imeendelea kujenga na kukarabati miundombinu ya utalii katika hifadhi za misitu ya mazingira asilia na maeneo ya malikale ili kuachana na utegemezi kuwa utalii ni wanyamapori pekee. Hii imehusisha ukarabati wa kilometa 178 za njia, kutembelea watalii na kilometa 258 za barabara za hifadhini na kutangaza maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kupitia juhudi hizo, jumla ya watalii 1,108,111 walitembelea vivutio hivyo wakiwemo watalii wa makumbusho na malikale 887,285 na watalii wa ikolojia 220,826 mwaka 2022/2023

ikilinganishwa na jumla ya watalii 734,082 wakiwemo malikale na makumbusho 582,080 na watalii wa ikolojia 152,002 mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii kuwapongeza watendaji wetu wa malikale na makumbusho za Taifa kwa maboresho na mageuzi haya. Nawahimiza Watanzania kuendelea kutembelea maeneo yetu haya ya utamaduni na maeneo yetu mengine ya asili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu masuala mahususi ya kisekta na mikakati maalum, mwelekeo wa utalii wetu na sakata la migogoro ya wanyamapori na binadamu. Kama tulivyoeleza awali, katika Wizara sasa ikiwa inaelekea kuongeza juhudi katika nguzo kuu mbili, uhifadhi na utangazaji wa vivutio vyetu, naomba kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa kumekuwa na masuala ya msingi yanayohitaji nguvu zaidi na juhudi zaidi kuyaendea iwapo tunataka mafanikio zaidi katika Sekta hizi za Maliasili na Utalii. Hivyo kabla ya kueleza makadirio ya mwelekeo wa bajeti kwa mwaka ujao, naomba kuzungumzia masuala mawili changamoto ya migogoro baina ya binadamu na wanyamapori wakali na waharibifu pamoja na mipaka kati ya vijiji na hifadhi; na pili, nje kidogo ya migogoro nidokeze kuhusu mwelekeo mpya wa Wizara katika kutangaza utalii.

Mheshimiwa Spika, nikianza na suala la migogoro, ninakiri kwamba pamoja na nchi yetu kwa sasa kusifika duniani kutokana na mafanikio ya uhifadhi, kero kubwa ambayo kamati na Wabunge wetu wengi wamekuwa wakitoa ushauri hapa Bungeni ni migogoro inayoikumba sekta hii baina ya binadamu na wanyamapori wakali na waharibifu, pamoja na migogoro ya mipaka kati ya wananchi na maeneo kadhaa yaliyohifadhiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, migogoro hii imekuwa ikisababisha madhara kwa pande zote mbili. Serikali kamwe hairidhishwi na hali hii. Niko hapa leo kuwahakikishia kuwa kwa kutumia wataalamu mbalimbali na maoni ya wananchi na hata Waheshimiwa Wabunge, tumeendelea kuchukua hatua madhubuti kukabiliana na changamoto hizi. Naomba sasa niwashirikishe mikakati 10 tunayoendelea nayo inayohusishwa katika kudhibiti changamoto hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mkakati wa kwanza ni kukamilisha maelekezo ya Baraza la Mawaziri juu ya mipaka kati ya vijiji 975 vilivyokuwa na migogoro ya hifadhi. Bunge lako Tukufu litakumbuka kuwa katika kutatua changamoto ya mipaka kati ya vijiji na mapori ya akiba ya hifadhi zetu, Serikali iliunda Kamati ya Mawaziri nane na kupita nchi nzima kuchambua na kutoa mapendekezo ambayo yalipata baraka zote za Baraza la Mawaziri. Uamuzi wa Baraza la Mawaziri umeshafikishwa kwa wakuu wote wa mikoa ili washirikishe wananchi katika zoezi la kuweka mipaka mipya katika maeneo yanayotenganisha vijiji na maeneo ya hifadhi ambayo katika maeneo mengi Serikali imeamua kuwaachia wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maeneo makubwa yaliyokuwa ya awali ni ya hifadhi kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na baadhi kubaki kwenye hifadhi ili kulinda rasiliamli nyingine zikiwemo vyanzo vya maji. Utekelezaji huu unaendelea vizuri na ninaomba kutumia fursa hii kusisitiza na kuwakumbusha wakuu wote wa mikoa nchini ambao bado hawajatoa matamko kama inavyotakiwa, wafanye hivyo kabla ya tarehe 30 Juni, 2023. Naomba kuwakumbusha Wakuu wa Mikoa kutoa matamko katika maeneo yao kabla ya tarehe 30 mwezi Juni, 2023 ili wataalam waendelee kuweka vigingi vya mipaka na Wizara iweze kutoa ramani mpya na wananchi washirikishwe kwenye hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuendelea kutekeleza mikakati ya kitaifa wa utatuzi wa migogoro baina ya binadamu na wanyamapori wakali na waharibifu 2020/2024. Katika eneo hili hasa tunapoangalia tatizo la wanyama wakali na waharibifu, tumehuisha mkakati huu ambao pamoja na mambo mengine, umezingatia kuchukua hatua za kukabiliana na changamoto ya migongano baina ya binadamu na wanyamapori wakali na waharibifu ikiwa ni pamoja na kujenga vituo 16 maalum vya askari vyenye maeneo yenye matukio mengi ya wanyamapori wakali na waharibifu kwa ajili ya kuimarisha doria za udhibiti wa matukio ya wanyamapori hao.

Mheshimiwa Spika, vituo hivyo vimejengwa katika Wilaya ya Meatu (Malwilo), Itilima (Longalambogo), Busega (Mwabayanda), Mchinga (Milola), Rufiji (Ngarambe), Liwale (Ngumbu), Tunduru

(Chingulungulu), Nachingwea (Nditi), Mwanga (Kwakoa), Songwe (Gua), Iringa (Mbolimboli), Nzega (Ndala), Mvomero (Sangasanga), Chamwino (Ilangali), Mpwapwa (Mtera) na Kondoa (Idindiri). Hatua hizi zimefanya idadi ya vituo maalum vya Askari kwa ajili ya kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu kufikia 154. Katika mwaka huu wa fedha vituo vingine 16 vinaendelea kujengwa kwenye maeneo yenye changamoto kwa kuzingatia jiografia ya migogoro hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu kutoa elimu kuhusu namna ya kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu, katika mwaka 2022/2023 Wizara imetoa elimu kwa wananchi wa Halmashauri za Wilaya 28 ikiwemo kugawa orodha ya namba za simu za makamanda wa *TAWA, TANAPA* na *TFS* katika maeneo husika ili kutoa taarifa. Orodha hiyo ni kama ilivyo kwenye jedwali namba 13 katika Kitabu cha Hotuba ya Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2023/2024 kwa ajili ya rejea ya Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kutoa vifaa kwa wananchi vya kupambana na kufukuza wanyamapori wakali na waharibifu, Wizara imeshatoa mizinga ya nyuki 176, tochi zenye mwanga mkali 221, vuvuzela 125, *roman candles* 107, ving'ora 20, fataki 170, honi 70, baruti pakiti 124, filimbi 210, pilipili ya unga na mbegu ambavyo husaidia kuwafukuza tembo na wanyama wakali wengine. Vile vile Wizara imejenga vizimba vinne vya kuzuia na madhara yatokanayo na mamba katika Wilaya ya Songwe viwili na Buchosa viwili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu kutoa kifuta jasho na machozi kwa wanaoathirika na wanyamapori wakali na waharibifu, pamoja na kuwa nchi nyingi duniani zimefuta dhana ya kifuta jasho na machozi kunapotokea madhara ya binadamu na wanyamapori, Serikali ya Tanzania walau bado inatoa kifuta jasho na machozi kwa wananchi inapobainika sababu na madhara husika ya wanyamapori hao hazikuchangiwa na waathirika wenyewe. Katika mwaka huu wa fedha kiasi cha shilingi bilioni 1.13 zimelipwa kama kifuta jasho na machozi kwa wananchi 4,869 walioathiriwa katika wilaya 36 na kiasi kingine cha shilingi milioni 884 kitalipwa wakati wowote kwa wananchi walioathirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, tayari kiasi cha Shilingi bilioni 1.5 kimeshapokelewa Wizarani kwa ajili ya kuwalipa wananchi walioathirika. Naomba Waheshimiwa Wabunge pelekeni salamu hizi kwa wananchi wetu, fedha tumeshapokea. Aidha, Wizara inaendelea kushirikiana na wadau kufanya mapitio ya kanuni ya kifuta jasho na kifuta machozi za mwaka 2011 kwa lengo la kuboresha kanuni hizo na kuimarisha mifumo ya ukusanyaji na utunzaji wa taarifa za matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu ili kupunguza mlolongo na kushughulikia changamoto zitokanazo na athari za wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, kufanya utafiti wa kuwafunga mikanda ya mawasiliano viongozi wa makundi ya wanyamapori wakali na waharibifu ili kubaini mienendo yao. Katika kutekeleza hilo, jumla ya tembo 156 wamefungwa mikanda hiyo kurahisisha ufuatiliaji wa mienendo yao katika mifumo ya ekolojia ya Tarangire, Manyara, Serengeti, Nyerere Selous, Mikumi Selous, Nyasa na *Lake Natron Western Kilimanjaro*. Aidha, simba 32 walifungwa vifaa hivyo katika mifumo ya ikolojia ya Serengeti na Ruaha, Rungwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kutumia ndege maalum kuondoa wanyamapori kwenye makazi, Wizara imekuwa ikitumia ndege maalum *(drones)* na wakati mwingine *helicopter* katika kupambana na wanyamapori wakali na waharibifu hasa tembo. Mfano katika mwaka 2022/2023 makundi matatu yenye jumla ya tembo 270 yaliondolewa kwenye makazi ya watu katika Wilaya za Nachingwea na Liwale kwa kutumia *helicopter* kwa kushirikiana na wadau wa uhifadhi. Wizara pia inalitaarifu Bunge lako Tukufu inatarajia kununua *helicopter* tatu nyingine ili kukabiliana na wanyamapori hao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *TAWA* pamoja na *TANAPA* kuongeza vitendeakazi vya kupambana na wanyamapori wakali na waharibifu; Wizara imenunua magari 247, pikipiki 50 na kuajiri askari wapya zaidi ya 136 kwa ajili ya kuimarisha shughuli za doria ikiwa ni pamoja na kukabiliana na matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu. Aidha, katika jitihada za kupambana na wanyamapori hao, Wizara imejenga jumla ya mabwawa nane na kukarabati mengine 17 katika hifadhi mbalimbali ikiwa ni jitihada za kuzuia wanyamapori kutoka nje ya hifadhi wakati wa ukame.

Mheshimiwa Spika, vilevile Wizara imeendelea kutekeleza mpangokazi wa kuondoa shoroba za wanyamapori ili kufungua mapito ya wanyamapori. Tunawaomba na kuwasihi sana wananchi kutojenga au kufanya shughuli za kijamii kwenye maeneo ambayo shoroba au njia ya mapito yao ya wanyamapori ili kupunguza tatizo hili la wanyamapori wakali na waharibifu.

Mheshimiwa Spika, sambamba na kuongeza Askari wa Doria na kutumia Askari wa Wanyamapori wa vijiji, Wizara kupitia taasisi zake za uhifadhi, inaendelea kushirikiana na kutoa mafunzo kwa Askari Wanyamapori wa vijiji kudhibiti matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 jumla ya Askari Wanyamapori 410 wa vijiji wamepewa Mafunzo ya Uhifadhi na Mbinu za Kukabiliana na Matukio ya Wanyamapori Wakali na Waharibifu.

Mheshimiwa Spika, aidha, jumla ya askari 231 wa Jeshi la Uhifadhi walipata mafunzo maalum ya kijeshi na ya namna ya kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu na wamesambazwa katika maeneo mbalimbali nchini ili kuongeza nguvu katika doria za udhibiti wa wanyama hawa.

Mheshimiwa Spika, ili kuwa na namna ya kisayansi zaidi ya kutatua changamoto za migogoro kati ya wanyamapori na binadamu ninakusudia kuunda kamati maalum itakayopita kwenye maeneo mbalimbali yenye changamoto husika na kufanya tathmini ya chanzo na sababu mahususi ya mgogoro wa wanyamapori kwa kila eneo na kunishauri juu ya hatua zaidi za haraka kutokana na upekee wa kila eneo. Kamati hii nitaitangaza na itaanza kazi mwezi Julai mwaka 2023 na nitaomba uridhie baadhi ya Wabunge niwateue ambao maeneo yao yana migogoro ili wafanye kazi hii kwa pamoja na kamati hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati Wizara ikiendelea kupambana na changamoto za wanyamapori wakali na waharibifu, kwa sasa ni vyema wananchi wakaendelea kuchukua tahadhari mbalimbali kwa mujibu wa maelekezo ya wataalamu ikiwemo kutoingia kwenye maeneo ya hifadhi, kutofanya shughuli za kibinadamu kwenye mapito ya wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, aidha, nimeagiza Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori *(TAWA)* na wataalamu wengine wa wanyamapori waende kwa ndani katika vijiji vyote nchini vyenye changamoto hii ili kuendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu namna ya kujikinga na wanyamapori hao na kuwafundisha Askari wa Vijiji mbinu zaidi za medani, nami mwenyewe nitakwenda huko kila Jimbo ambako kwenye malalamiko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, ni muhimu kwa wananchi kutoa taarifa haraka wanapoona makundi ya wanyamapori wakali na waharibifu kwenye maeneo yao, kupitia namba za simu za bure zilizoambatanishwa katika Kitabu cha Hotuba ya Bajeti ya Wizara. Pia niahidi kushirikiana na taasisi nyingine za Serikali kuondoa changamoto ya kupanga matumizi ya ardhi, ama kwenye maeneo ya hifadhi au mapito (shoroba) za wanyamapori, moja ya sababu kubwa ya changamoto ya sasa ya wanyamapori wakali na waharibifu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mikakati maalum ya kutangaza na kuinua sekta ya utalii nchini. Pamoja na jukumu la uhifadhi, Wizara hii inasimamia pia Sekta ya Utalii ambayo ni eneo muhimu katika uchumi wa nchi yetu. Kwa mujibu wa tathmini za ndani na hata ripoti ya Kimataifa ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Utalii Duniani *(UNWTO)* 2022 kupitia taarifa yake iitwayo, *Tourism Doing Business Investing in The United Republic of Tanzania* pamoja na Tanzania kutajwa kuongoza Afrika kwa hazina ya utalii wa maliasili *(nature based tourism)* imeonekana pia kuwa Sekta ya Utalii ina fursa ya kuchangia zaidi katika Pato la Taifa, lakini inakumbwa na changamoto mbalimbali ikiwemo kutojitangaza vya kutosha na uwekezaji mdogo, kuwa wanyonge kwa muda mrefu. Tumekuwa wanyonge kwa muda mrefu sana. Tuendako na katika mwaka mmoja ujao Wizara inakwenda kutekeleza mikakati 10 ya kina katika kuutangaza zaidi utalii wetu ndani na nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza, kushirikiana na Kamati ya Kitaifa ya Kutangaza Tanzania kuendeleza filamu ya *Tanzania The Royal Tour*. Filamu ya *Tanzania The Royal Tour* imeendelea kuwa johari muhimu nchini katika kuendelea kuutangaza utalii wetu kwa miaka mingi sana.

Hivyo Wizara itashirikiana na Kamati ya Kitaifa iliyoundwa na Mheshimiwa Rais kuendelea kusambaza filamu hii hasa kwenye mashirika mbalimbali ya ndege, mitandao mikubwa ya utalii duniani na kuendelea kuwasisitiza wadau kuendelea kuionesha katika mikutano ya matukio makubwa hasa tunapokuwa na wageni ili wazidi kuiona nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, pili, kuwekeza katika misafara ya kujifunza kuwaongoza watalii na kuyafikia masoko ya kimkakati *(FAM trips)*. Mwelekeo wa dunia na biashara ya utalii kwa sasa ni kwamba wanaoamua kwa kiasi kikubwa mtalii aende wapi ni mawakala wa biashara za utalii *(tour agents)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara imeanza mkakati wa kuwaalika mawakala wa utalii kutoka nchi mbalimbali duniani kuja nchini kuviona vivutio vyetu na kisha kwenda kuvitangaza. Tayari mawakala 65 kutoka nchi za China, Mexico, Marekani, Argentina, Brazil, Ureno, Ubelgiji, Ufaransa na Canada wametembelea nchini na kujifunza na kujionea vivutio mbalimbali vya utalii kwa lengo la kuvitangaza katika nchi zao na kuanza kuleta watalii nchini. Tatu, ni kuandaa makala nyingine ya Kimataifa kuitangaza Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara itawekeza kwenye uzalishaji wa makala zaidi ya *video* na picha za Kimataifa *(photos, films)* na *documentaries* hasa kwa kushirikiana na wazalishaji wa Kimataifa hususan kutoka *Hollywood* kwa lengo la kuendelea kuitangaza Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kushirikiana na mashirika makubwa ya utalii duniani, kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara tayari imeanza mazungumzo na ushirikiano ili kujitangaza kimkakati zaidi kupitia mashirika makubwa ya utalii ikiwemo *TripAdvisor* wanaohudumu watalii takribani milioni 400 duniani kwa mwezi, *Expedia* wanaohudumu zaidi ya watalii milioni 350 duniani kwa mwezi na *Safari Club International* yenye wanachama zaidi ya 50,000 na makampuni ya mawakala ya uwindaji wa kitalii.

Mheshimiwa Spika, kutangaza utalii kupitai ligi kubwa za michezo duniani. Wizara inajipanga kuwekeza katika kutangaza vivutio vya utalii kwenye ligi kubwa za michezo mbalimbali duniani ikiwemo soka na kikapu katika nchi za Uingereza, Hispania na Marekani. Katika hatua za awali, mwezi Mei, 2023 Bodi ya Utalii ya Tanzania ilisaini hati ya makubaliano ya awali *(MOU)* na Klabu za *Seattle Sounder (soccer), Seahawks* (Mpira wa Miguu wa Marekani) na *Portland Trailbraizers* (kikapu) za nchini Marekani ili kuitangaza Tanzania na mazungumzo yanaendelea. Pia kufungua utalii wa historia, ikolojia na kanda mpya za utalii kusini mwa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mkakati mwingine ni kuongeza mazao ya utalii kwa kufungua maeneo mengine ya kitalii ikiwemo utalii wa ikolojia, historia na pia kufungua maeneo ya kusini mwa nchi ambako kuna vivutio vingi lakini juhudi zaidi kuvitangaza vinahitajika. Kuitangazwa Tanzania kama vivutio vya fukwe na utalii wa meli na visiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka ujao Wizara inakusudia kuandaa mpango mkakati kuhusu utalii wa bahari, utalii wa visiwa, meli na fukwe. Mkakati huo pamoja na mambo mengine utawezesha kuwa na namna bora ya kuratibu, kusimamia fukwe kutoka Tanga hadi Mtwara na kuwa na tija itakayowezesha kuvutia wawekezaji kuwekeza katika hoteli za nyota tano katika bahari, maziwa na visiwa. Aidha mkakati huo utaainisha namna bora ya kuratibu fukwe ili ziratibiwe na Wizara ya Maliasili na Utalii na kwa nia ya kuongeza mapato, idadi ya watalii. Hata hivyo kwa sasa tayari utalii wa fukwe umeonyesha matunda makubwa Visiwani Zanzibar na Tanzania Bara. Huu umeonesha kuzidi kushamiri ambapo kwa mwaka wa fedha 2023 jumla ya watalii 2,020 wamewasali nchini kupitia utalii wa meli *(Cruise Ship)* kutoka masoko makubwa ya utalii yakiwemo Marekani, Ufaransa, Uholanzi, Italia, Brazil na Afrika ya Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuwekeza na kuitangaza Tanzania na utalii wa mikutano na matukio. Utalii wa mikutano na matukio kwa sasa ni mkakati mwingine na mkubwa sana wa kuongeza utalii kuitangaza nchi yetu. Amani na utulivu wa nchi hii na baadhi ya miundombinu tuliyonayo kwa sasa vinavutia wengi kupenda kuja

Tanzania kwa ajili ya mikutano na matukio. Wizara itaendelea kuongeza nguvu ili ikiwemo kuongeza nguvu, rasilimali na miundombinu ya mikutano na matukio ikiwemo kuanza kujenga ukumbi mkubwa wa kisasa na hoteli ya kitalii ya kisasa eneo la Kigamboni Jijini Dar es salaam.

Aidha, Wizara itafanyia kazi suala la kuwa na vivutio mahususi vya utalii wa mikutano iwapo nchi au taasisi itaamua kufanya matukio yao hapa nchini. Kuanzisha tamasha kubwa la kimataifa la utalii wa utamaduni.

Mheshimiwa Spika, matamasha makubwa duniani yawe ya vyakula, mavazi ya utamaduni na utalii hutumika kimkakati sana kuzitangaza nchi kuvutia watalii wengi. Matamasha hayo ni kama *rial carnival* Brazil, *tommorrow land* Ubeligiji, *October first* Ujerumani na *Coachella* inchini Marekani; huvutia zaidi ya watu milioni tatu kwa kila moja kwa siku chache zifanyikazo. Tanzania imesheheni urithi wa utamaduni na sasa unaweza kutumika vyema kuvutia watalii kushiriki katika matamasha hayo. Hivyo tutaendelea kushirikiana na sekta ya utamaduni sanaa na michezo kuyaingia haya masoko, kuanzisha tuzo ya kimataifa za utalii nchini.

Mheshimiwa Spika, wahenga walisema mcheza kwao hutuzwa. Nitumie fursa hii kusisitiza kuwa kwa kazi kubwa inayofanywa na wadau wote wa utalii nchini ni vyema kuweka mfumo wa wazi na kutoa tuzo kwa ajili ya kuwapongeza wale waliofanya vizuri zaidi na kuwahamasisha waliyokuwa nyuma kuongeza bidii. Hivi karibuni nitateua kamati ya kitaifa ya kuratibu jambo hili litakalotangaza zaidi nchi yetu. Tuzo hizi zitatumika au zitatumia kwa jina moja la kivutio cha utalii kama Ngorongoro au Serengeti au Kilimanjaro. Wadau watapewa nafasi ya kutoa maoni. Sisi tunaamini mikakati hii ikiwezeshewa ipasavyo Wizara hii itaendelea kuwa chachu na kuongeza mapato ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini ukweli ni kwamba kutekeleza mikakati hasa ya kutangaza Taifa katika dunia ya ushindani ni suala linalohitaji rasilimali fedha za kutosha. Ni kwa ajili hiyo Wizara imeanza na inaendelea kujenga hoja kuhusu kurejesha tozo ya maendeleo ya

utalii *(tourism development levy)* lakini pia kama ilivyokuwa zamani, taasisi za uhifadhi utalii zinapaswa kurejeshewa uwezo wa kubaki na sehemu ya fedha wanazokusanya *(retention)*. Wizara itahakikisha iwapo maono haya mapya yatafikiwa fedha zote zitasimamiwa kikamilifu ili ziweze kutumika katika kusukuma maendeleo ya sekta ya maliasili na utalii ikiwa ni pamoja na kuendeleza utalii nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tamko langu kuhusu zoezi la kuhamisha wananchi Ngorongoro. Kuhusu zoezi la kuhamisha wananchi kwa hiari kutoka Eneo la Urithi wa Dunia Ngorongoro kwanza nawapongeza wananchi wote ambao kwa hiari yao walijiandikisha na hata kuhamia eneo la Msomela Wilayani Handeni. Huko wanaendelea maisha yao salama wakiwa wamepewa nyumba na maeneo ya kulisha mifugo yao na mashamba, huku pia wakipata haki zao nyingine za kibinadamu kama shule na kufanya biashara tofuati na walivyokuwa wakiishi kwa mashaka. Ninawaahidi wananchi waliosalia na ambao wamekuwa wakijiandikisha kwa wingi na kwa shauku kutaka kuhama kwamba zoezi hili bado halijasimamishwa na Serikali tofauti na yanavyosemwa na baadhi wanao jaribu kukwamisha hasa majirani zetu. *(Makofi)*

Aidha, naomba kuliharifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imejiandaa na ina rasilimali za kutosha kwa ajili ya kukamilisha zoezi hilo, na kwamba hatutarudi nyuma wala hakutakuwa na kusalimu amri katika kukamilisha zoezi hili ambalo litaendelea kufanyika kwa weledi na kasi kubwa. Tukutane Msomela *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tamkao maalum kwa wadau wa sekta ya utalii kati ya Mei, 25 na 26 mwaka huu Wizara ilikutana na wadau wa kisekta wakiwemo wanyamapori, misitu na nyuki na utalii kwa lengo la kupitia changamoto na kuweka mikakati ya pamoja ya kutatua changamoto zilizopo katika sekta hizo. Ninawaahidi wadau wetu kuwa Wizara itaendelea kuwa nao, itakuwa karibu nao, itawalinda; Wizara itawatetea, itatetea maslahi yao na zaidi watimize wajibu wao kwa kutii kulipa kodi na kufanya biashara zao kwa njia za halali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara inaahidi kuunda kamati itakayo washirikisha na itakayoongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii Dkt. Hassan Abbas kupitia changamoto zao na kutoa mapendekezo kwa Serikali. Vilevile nitoe wito kwa taasisi mbalimbali na Serikali kutuachia kwa sasa tuitengeneze sekta hii ya utalii badala ya kuleta kodi mpya na tozo mpya bila ya kuwa tumeshauriana au kushirikisha wadau wetu hawa ipasavyo. Niwaombe wenzetu tunaoshirikiana nao wawashirikishe wadau wa utalii, watushirikishe na sisi kabla hawajatangaza tozo mpya zinazowavuruga wadau wetu wa utalii.

Mheshimiwa Spika, mpango na bajeti ya wizara kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024. Wahenga walisema *"Mwenda tezi na omo marejeo ngamani."* Baada ya maelezo hayo kuhusu utekelezaji wa mikakati ijayo na tamko maalum kuhusu wenzetu hao wanaohama Ngorongoro sasa nihitmishe kwa kurejea ngamani kwa kufanya jambo la muhimu kwa kujielekeza sasa kutoa hoja ya kuomba fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwab Spika, mpango wa bajeti kwa mwaka fedha 2023 umezingatia miongozo mbalimbali ikiwemo mwongozo wa maandalizi ya mpango wa bajeti (2023/2024, 2025/2026). Mpango wa Taifa wa Maendeleo ya Taifa kwa Miaka Mitano (2021/2022, 2025/2026), Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi 2020/2025. Na ninawashukuru Wenyeviti wa Mikoa wote ambao mmefika hapa na Makatibu na Mikoa kushuhudia hili. Nawashukuru sana Wenyeviti wa Mikoa mliopo hapa; Sera na Sheria mbalimbali, mipango mkakati ya Wizara 2021/2022, 2022/2025, 2025/2026. Maagizo mbalimbali ya Viongozi Wakuu wa Serikali na mikataba ya kikanda na kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukusanyaji wa maduhuli, katika mwaka 2023/2024 makadirio ya maduhuli yaliyokusanywa kutokana na Sekta ya Maliasili na Utalii ni jumla ya shilingi bilioni 771.88. Kati ya fedha hizo bilioni 572.91 zitakusanywa na Mifumo ya TEHAMA ya Wizara kwenda Mamlaka ya Mapato Tanzania kutoka Vyanzo vya *TANAPA, NCAA* na *TAWA*. Aidha shilingi bilioni 198.97 zitakusanywa kupitia mfumo wa *MRT Portal* kutoka vyanzo vya idara na taasisi nyingine za Wizara.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Katika mwaka 2023/2024 Wizara inakadiria kutumia jumla ya shilingi bilioni 658.67. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 486.50 zitagharamia matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 168.17 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Fedha za matumizi ya kawaida zinajumuisha mishahara na Maendelo. Fedha za matumizi ya kawaida zinajumuisha *(PE)* shilingi bilioni 184.29.

Mheshimiwa Spika, maombi ya fedha kwa mwaka 2023/2024. Ninaomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 654,668,208,000 kwa matumizi ya Fungu 69 Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Kati ya fedha hizo shilingi 486,501,449,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingili 168,166,759,000 ni za miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, fedha za matumizi ya kawaida zinajumuisha shilingi 184,288,496,000 za mishahara na shilingi 302,212,953,000 za matumizi mengineyo. Fedha za miradi ya maendeleo zinajumuisha shilingi 109,879,593,000 fedha za ndani na shilingi 58,287,166,000 ni fedha za nje…

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kabla ujatoa hoja hebu hii sehemu ya kwanza. Fedha za matumizi ya kawaida ni sawa, hebu nenda hapa juu kwenye fedha za matumizi…

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, fedha za matumizi ya kawaida zinajumuisha shilingi bilioni 184,288…

**SPIKA:** Ngoja, ngoja, ile kwenye shilingi bilioni 654, sehemu hiyo.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ninaomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 658,668,208,000…

**SPIKA:** Umesema bilioni 658 hapa inasomeka… Haya tusomee.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Bilioni 654,668,208,000 kwa matumizi ya Fungu 69 ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Kati ya fedha hizo shilingi 486,501,449,000… *(Makofi)*

**SPIKA:** Ngoja, ngoja Mheshimiwa, kati ya fedha hizo...

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Shilingi 486,501,449,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, na shilingi 168,166,759,000 ni za miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, fedha za matumizi ya kawaida zinajumlisha shilingi 184,288,000,449 za mishahara na shilingi milioni 302…

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, milioni 288 umesema laki mbili. Bilioni 184, anzia hapo. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Bilioni 184, …

**SPIKA:** Mheshimiwa ngoja, nyinyi. Mheshimiwa Waziri ngoja, Waheshimiwa Wabunge msizungumze na Waziri, mwacheni Waziri asome.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, fedha…

**SPIKA:** Bilioni…

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, fedha za matumizi ya kawaida zina jumlisha shilingi 184,288,496,000 za mishahara na shilingi 302,212,953,000 ni za matumizi mengineyo. Fedha za miradi ya maendeleo zinajumuisha shilingi 109,879,593,000, fedha za ndani shilingi 58,287,166,000 fedha za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Kwa minajiri ya tanbin ya hotuba yangu niseme kwamba mafanikio ya Wizara hii ni matokeo ya kazi kubwa na ya pamoja inayofanywa wadau wa ndani nan je ya nchi. Nazishukuru nchi marafiki, washirika wa maendeleo, jumuiya za kikanda, mashirika ya kimataifa, taasisi za kiserikali pamoja na wadau wengine wakiwemo sekta binafsi, makampuni ya utalii, makampuni ya

uwindaji, hoteli, waongoza utalii, wanahabari na kila mmoja anayetimiza wajibu wake katika sekta kwa ushirikiano wao katika kuendelea/kuendeleza sekta ya maliasili, malikale na utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa naona ni fahari kuwataja baadhi ya wadau hawa ambao ni Serikali ya Canada, China, Falme za Kiarabu, Korea Kusini, Marekani, Morroco, Namibia, Norway, Ubeligiji, Ufaransa, Rufin, Ujerumani, Uswiss na Jumuiya ya Umoja wa Nchi za Ulaya. Mashirika na taasisi za kimataifa ni pamoja na *AfDB, AWF, AWHF, ENABEL, FAO, FZS, GEF, GIZ, ICCROM, ICOM, MIKOMOZI, ILO, IMF, ITC, IUCN*, *KfW, NORAD, PAMS Foundation, Trade Aid, UNDP, UNESCO, UNWTO, USAID, WCS, WHS, WTTC*, *World Bank, World Aid, WMF, WWF*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wadau wa sekta ya utalii nchini, *TCT, TATO, TAHOA, TAHA,* HATI, TAOTO, *TWEA* na wadau wote wanaoshiriki kikamilifu katika shughuli za uhifadhi na maliasili, malikalikale na uendelezaji utalii. Wote tunawashukuru sana, sana, sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Hotuba hii inapatikana pia katika Tovuti ya Wizara ya Maliasili na Utalii www.maliasili.go.tz

Mheshimiwa Spika, naomba Hotuba yangu yote iingie kwenye *Hansard* za Bunge kwa ajili ya kumbukumbu za kizazi cha leo na vizazi vya kesho.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 – KAMA ILIVYOWALISHWA MEZANI**

## 1.0 UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** kufuatia taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, leo katika Bunge lako Tukufu, ninaomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti

ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Aidha, ninaomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**2. Mheshimiwa Spika,** nianze kwa bashrafu ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kunipa afya na uzima na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu leo kutoa taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Serikali kupitia Sekta ya Maliasili na Utalii. Aidha, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kuwajalia afya njema Viongozi wetu Wakuu wa Kitaifa, Waheshimiwa Mawaziri wenzangu, Waheshimiwa Wabunge, Viongozi wengine wa Serikali na wananchi kwa ujumla.

**3. Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee kabisa na kwa unyenyekevu mkubwa nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Amiri Jeshi Mkuu, kwa kuendelea kuniamini na kuniteua kusimamia Wizara hii takriban miezi mitatu na siku 19 tangu Februari 14, 2023, aliponihamisha kutoka Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo. Namuahidi Mhe. Rais na Bunge lako kuwa mimi na watendaji wenzangu tutaendeleza kwa nguvu, maarifa, kujitoa, kujitolea na zaidi ubunifu mkubwa pale walipoishia wenzetu waliotutangulia na kwamba Bunge hili na mihimili mingine ya Dola itarajie ushirikiano wa dhati kutoka kwetu.

**4. Mheshimiwa Spika**, usuli wa yote, Wizara hii imepewa dhamana ya kusimamia, kulinda na kuendeleza maeneo ya hifadhi za wanyamapori, misitu, nyuki na malikale yenye mchango mkubwa katika uhifadhi wa mazingira, ustawi wa wananchi lakini pia ukuaji wa uchumi. Aidha, Wizara ina jukumu la kuendeleza utalii ambao pia ni chanzo cha mapato ya fedha za kigeni na fursa za ajira kwa Watanzania. Ni kwa muktadha huo wa mtawanyiko wa majukumu ya Wizara hii, tulipoingia, mimi na wenzangu, tulifanya uchambuzi wa kina na kuja na falsafa mbili zinazojengwa katika nguzo kubwa mbili zinazofupisha muktadha wa malengo na majukumu adhimu ya Wizara hii kama ifuatavyo:

Mosi, nguzo inayojenga jukumu kubwa la kwanza la Wizara hii ni **UHIFADHI** (**yaani Conservation**): Mheshimiwa Spika uhai wetu sisi wanadamu unategemea maji na pia viumbe hai wengine kama vile wanyama na mimea: karibu vyote hivi viko kwenye maeneo yanayolindwa au kupaswa kuangaliwa na Wizara hii. Karibu vyanzo vyetu vingi vya maji hapa nchini vinatokana na misitu iliyolindwa, misitu hiyo inayotupa leo kivuli, nishati, chakula isingelindwa isingekuwepo. Nchi yetu pia inasifika kwa wanyamapori waliotapakaa sehemu mbalimbali wanaosaidia utalii wetu, kitoweo na uchumi wa mwananchi mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla. Vyote hivi bila uhifadhi, havitakuwepo. Ni vivutio hivi ambavyo kwa mujibu wa Ripoti ya Baraza la Utalii na Masuala ya Safari Duniani (World Travel and Tourism Council, WTTC) ya Mwezi Mei, 2022, imeitaja Tanzania kuwa nchi ya kwanza Afrika kwa kuwa na vivutio vya asili na kuwa miongoni mwa 10 Bora Duniani kwa uhimilivu wa maeneo yake kupokea watalii (sustainability). Hii ni heshima kubwa kwa nchi yetu.

Pili, Mheshimiwa Spika, nguzo yetu ya pili inayounda jukumu jingine kuu la Wizara ni **KUJITANGAZA** (**yaani PROMOTION**). Hii inatokana na muktadha wa nguzo ya kwanza kwamba nchi yetu imejaaliwa rasilimali nyingi za misitu, wanyamapori na malikale, ili rasilimali hizi zilete faida za kiutalii na uwekezaji mwingine mkubwa lazima zitangazwe kwa nguvu na ubunifu mkubwa. Tunatambua kwamba wahenga walipata kunena kuwa "**Chema Chajiuza, Kibaya Chajitangaza**" tunawashukuru sana lakini katika zama hizi za ushindani, kila mtu akivutia alichonacho, sisi, TUMEAMUA NA WAKATI NI SASA, kwenda na kauli yao nyingine isemayo: "**Mgaagaa na Upwa Hali Wali Mkavu"**

Mwelekeo mpya sasa wa Wizara ni kuhakikisha "Tunagaagaa na Upwa" kwa kuwekeza nguvu zaidi na kwa njia za kisasa na kiubunifu zaidi kutangaza rasilimali zetu na utalii wetu ili kuliingizia Taifa letu mapato zaidi katika sekta hii ambayo hata bila kuwekeza sana katika kujitangaza tayari inachangia asilimia 25 ya fedha za kigeni na asilimia 21 ya Pato la Taifa. Tunaweza na inawezekana kwenda maradufu ya sasa na hapa tulipo.

**5. Mheshimiwa Spika,** nitumie fursa hii kumpongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwani yeye ndiye mwana maono mkuu wa falsafa na misingi niliyoieleza hapo juu kwani amekuwa MHIFADHI namba moja anayehakikisha wanyamapori, misitu na vyote vilivyyomo ndani yake vinalindwa kwa faida ya leo na vizazi vijavyo na yeye na Serikali zilizopita wameruhusu takriban asilimia 32 ya ardhi ya nchi yetu kuwa maeneo maalum yaliyohifadhiwa. Akiwa muumini pia wa nguzo kuu ya pili ya sekta hizi, ni yeye pia aliyetoka ofisini na kwenda milimani, mabondeni, baharini, hifadhini na hata majukwaani kushiriki filamu ya "**TANZANIA; THE ROYAL TOUR,**" hivyo kusaidia kuutangaza utalii wetu katika namna ambayo haijapata kutokea na kuleta faida lukuki ambazo tutazieleza punde.

**6. Mheshimiwa Spika,** Halikadhalika, napenda pia kutumia fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; kwa jinsi nao, kwa nyakati tofauti ambavyo wamekuwa wakijipambanua kuwa waumini na watekelezaji wakubwa wa maono ya Mhe. Rais katika uhifadhi na Utangazaji wa Utalii.

**7. Mheshimiwa Spika,** sisi waumini wa uhifadhi, uendelezaji na utangazaji wa utalii, tunaamini kwa dhati kuwa kwa namna moja au nyingine, kila Mtanzania ni mdau wetu na kila anachokifanya au kukitenda kilicho chema kinasaidia kufikia azma kuu ya nchi yetu kufikia watalii milioni 5 na mapato yanayofikia Dola za Marekani Bilioni 6 ifikapo mwaka 2025. Hivyo basi, kwa niaba ya wadau wa uhifadhi na utalii na Watanzania wote kwa ujumla natumia fursa hii kulipongeza Bunge lako Tukufu kupitia wewe Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu (Mb.), Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb.), Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge, Wenyeviti wa Kamati mbalimbali na wabunge wote kwa miongozo yenu ya mara kwa mara, ushauri na mapendekezo ya kuhakikisha **uhifadhi** na **utangazaji** wa utalii vinaendelea vyema. Kwa upande mwingine, naungana na

Waheshimiwa Mawaziri wenzangu walionitangulia kumpongeza Mheshimiwa Abdul Yussuf Maalim kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Amani, Zanzibar na kuungana nasi katika Bunge hili.

**8. Mheshimiwa Spika, "Figa Moja Haliinjiki Chungu"** kwa dhati, na nia yako ya kutusaidia kwa karibu, ulitupa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii yenye wabunge wabobezi na watopezi wa sekta hii na wenye mapenzi na uhifadhi na utangazaji wa utalii chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava (Mb.); Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Najma Murtaza Giga (Mb.); na Waheshimiwa Wanakamati. Wabobezi hawa, wametuthibitishia kuwa "**Penye wengi pana mengi,"** wamejadili nasi, wametoa ushauri na mapendekezo na vyote sasa vimekuwa msingi wa mapendekezo ya makadirio haya ya mapato na matumizi na bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Tunawashukuru sana.

**9. Mheshimiwa Spika,** "**Chanda Chema Huvikwa Pete**" naomba kutumia fursa hii pia kuwashukuru viongozi na Watendaji wenzangu Wizarani na katika taasisi zetu kwa ushirikiano, ubunifu, usimamizi na utekelezaji makini wa yale ambayo tunaelekezwa au yapo kwenye mikakati ya Serikali na Wizara. Nawashukuru: Mheshimiwa Mary Francis Masanja (Mb.), Naibu Waziri mbobezi wa sekta hizi; Dkt. Hassan Abbasi Said, Katibu Mkuu mbunifu asiyechoka; Ndugu Anderson Gukwi Mutatembwa, Naibu Katibu Mkuu mwanamikakati makini; Wakurugenzi wa Idara na Vitengo na Wakuu wa Taasisi, wanataaluma mahiri; na wafanyakazi wa kada za kati mpaka wa chini wanaojituma sana, wote nawashukuru kwa kujitoa sana katika kutekeleza majukumu yao. Hakika nyie ni nguzo muhimu ya Wizara.

**10. Mheshimiwa Spika**, kipekee pia, nitambue na kushukuru, kwa umaalum wake na kwa unyenyekevu wa juu kabisa, askari na maafisa wa jeshi la uhifadhi wanaokesha kila uchao maporini, vilimani, mabondeni, kwenye maji au misitu minene, kwenye jua, kwenye mvua usiku au mchana kulinda na kuhifadhi rasilimali zetu za wanyamapori, malikale, misitu na nyuki.

**11. Mheshimiwa Spika,** katika kutimiza wajibu wao kwa Taifa, wapo vijana wetu wazalendo, watoto wetu na wajukuu zetu waliojitoa kuishi

misituni na maporini kulinda raslimali zetu ambao kwa kujitoa kwao huko, wamejeruhiwa na hata wengine wamepoteza maisha wakiwemo askari Deus Mwakajegela aliyefariki kwa kuchomwa mkuki mwaka jana na mwananchi wakati akilinda mpaka wa Hifadhi ya Taifa Serengeti; askari Theonas Nota aliyefariki kwa ajali ya ndege aina ya Cesna 192-5HFZS wiki mbili zilizopita akienda doria kule Pori la Akiba Selous; na askari Taiko Olesalei Marau ambaye alikuwa mstari wa mbele akiongoza doria na wenzake watano (5) katikati ya Eneo la misitu minene ya Hifadhi ya Ngorongoro Mei 18, 2023, aliyevamiwa na kuuawa na mnyama hatari aina ya mbogo na wapo jumla ya askari 13 wa Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) waliouawa na wananchi au majangili wa misitu katika maeneo mbalimbali nchini akiwemo mmojawapo ambaye ametoweshwa na mpaka sasa hajulikani alipo na familia yake imebaki kuishi na majonzi makubwa. Jitihada za kumtafuta mtumishi huyo bado zinaendelea.

**12. Mheshimiwa Spika,** Aidha, Bunge lako Tukufu pia litambue kuwa Taifa liliwapoteza askari wa TAWA, James Chacha Karomba, aliyeuwawa na wafugaji akitekeleza majukumu yake katika Pori la Akiba Inyonga, askari Mwita Msabi aliyeuawa na majangili wakati wa Doria ya ushirikiano na TFS katika hifadhi ya msitu wa Uzungwa, askari Chacha Mwita Magoro, Nkwabi Daudi na Mathias Mgongolwa waliofariki katika ajali ya maji wakati wakipambana na majangili katika Mapori ya Igombe, Lukwika Lumesule na Kilombero.

**13. Mheshimiwa Spika,** Hakuna namna ya kuwalipa mashujaa hawa, zaidi ya kuwaombea, kuendelea kuwatambua na kuwathamini daima milele na sisi sote kuazimia kuendeleza walipoishia katika kuzilinda rasilimali zetu. Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi. Amen. Lakini ni vyema kusisitiza hapa kwa wananchi wetu kutii sheria bila shuruti na pia kuwaona askari hawa kuwa wazalendo wa Taifa na kushirikiana nao. Naendelea kuwasihi askari wetu wa Jeshi la Uhifadhi, licha ya mafunzo ya kijeshi waliyonayo na silaha walizokabidhiwa, kuendelea kujizuia na kutumia busara kila inapobidi, kama ambavyo wamefanya mara nyingi, katika kuendelea kukabiliana na wananchi wasiotaka kutii sheria na wanapokabiliana na wahalifu wengine.

**14. Mheshimiwa Spika,** natambua katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita, Bunge lako Tukufu pia limeondokewa na baadhi ya Wabunge wenzetu akiwemo Mhe. Mussa Hassan Mussa, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Amani Zanzibar. Aidha, nitoe pole pia kwa Bunge lako na Serikali kwa kuondokewa na Wabunge wenzetu wa zamani: Waziri wa zamani wa Mambo ya Nje, Mhe. Bernard Kamilius Membe; Mhe. Herman Kiligini Waziri wa zamani wa Kilimo na Mifugo; na Mhe. Nimrod Mkono aliyekuwa Mbunge wa zamani wa Jimbo la Butiama. Mungu aziweke roho za marehemu mahala pema peponi, Amen.

**15. Mheshimiwa Spika, "Kibuzi na Kibuzi Hununua Jahazi"**, katika kuelekea mwisho lakini si kwa umuhimu wa bashrafu ya hotuba yangu, nikiri nguvu, ari na kujituma kwangu katika kuwahudumia wadau wa maliasili na utalii kunachangiwa kwa kiasi kikubwa na makundi haya mawili: mosi nawashakuru sana wananchi wa Jimbo langu la Rufiji kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika kutekeleza majukumu ya kitaifa na Jimbo na kuniombea kila siku. Ninaahidi sitawaangusha na nitaendelea kushirikiana nao kila hatua katika kuleta maendeleo ya Jimbo letu na Taifa kwa ujumla. Pili na kipekee, naishukuru sana na kwa dhati ya kipekee familia yangu kwa upendo wao, uvumilivu na maombi yao wakati wote wa utekelezaji wa majukumu yangu ya kitaifa. Sina cha kuwalipa zaidi ya kuwaahidi utendaji bora na kuwaheshimisha.

**16. Mheshimiwa Spika,** hotuba yangu imegawanyika katika sehemu sita (6) ambazo ni: Utangulizi; Majukumu, Mwelekeo na Vipaumbele vya Wizara; Mchango wa Maliasili na Utalii katika kukuza Uchumi na Maendeleo Endelevu; Maoni na Ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii; Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2022/2023; na Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

## 2.0 MAJUKUMU, MWELEKEO NA VIPAUMBELE VYA WIZARA

**17. Mheshimiwa Spika**, jukumu kuu la Wizara ni kuhifadhi na kusimamia matumizi endelevu ya maliasili, malikale na maendeleo ya utalii. Jukumu hilo linajumuisha uendelezaji wa Sekta ya Utalii kwa

kupanua wigo wa mazao ya utalii, kuimarisha utangazaji na kuboresha huduma za utalii ili kuongeza mchango wake katika pato la Taifa; kusimamia uhifadhi wa rasilimali za wanyamapori na misitu kwa kufanya doria ndani na nje ya maeneo yaliyohifadhiwa; kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu; na kusimamia ukusanyaji wa maduhuli yatokanayo na rasilimali, matumizi endelevu ya rasilimali za maliasili na malikale. Katika kutekeleza jukumu hilo, Wizara huandaa Sera, Sheria, Kanuni, Mikakati na Miongozo mbalimbali inayolenga kuboresha uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za wanyamapori, misitu, nyuki na malikale; na maendeleo ya utalii. Sambamba na hilo, Wizara inaongozwa na misingi ya Uwazi na Uwajibikaji, Utaalam, Ushirikishwaji na Uhifadhi Endelevu.

**18. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha miaka mitatu (2022/2023 – 2024/2025) Wizara itatekeleza mikakati mbalimbali iliyojikita katika dhana za uhifadhi na utangazaji utalii. Hatua hii inalenga kuinua mchango wa sekta ya utalii kiuchumi na kuleta mageuzi ya haraka yenye lengo la kufikia na hata kuvuka idadi ya watalii milioni tano na mapato ya Dola za Marekani bilioni sita ifikapo mwaka 2025, kama ilivyoainishwa kwenye Ilani ya CCM ya mwaka 2020. Mikakati hiyo inajumuisha: kutekeleza njia mbalimbali za uhifadhi na ujenzi wa miundombinu ya kuvutia watalii; kuratibu uzalishaji wa filamu 4 za kimataifa; kutangaza kaulimbiu ya "Tanzania Unforgettable" katika ligi kubwa za michezo za Marekani, Uingereza na Hispania; kutangaza utalii wa Tanzania kwa njia za kidijitali; kuwekeza utangazaji wa utalii kwa kulipia makala na filamu za Tanzania katika mashirika ya ndege; kuandaa na kutumia majukwaa ya matamasha ya kimataifa kutangaza utalii; kutumia vyombo vya habari vya kimataifa vyenye ushawishi; kutumia fursa za masoko ya ndani na kikanda kutangaza utalii; kutumia ofisi za balozi, mabalozi wa hiari wa utalii na watu mashuhuri; kutumia mitandao ya kijamii ikiwemo YouTube, Amazon, Google, Facebook, TripAdvisor, IMDb na WeChat ambayo inafikiwa na watu wengi zaidi; na ziara za mafunzo (FAM Trips) kwa makundi mbalimbali ikiwemo wakala wa biashara za utalii, waandishi wa habari na wawekezaji katika masoko ya utalii.

**19. Mheshimiwa Spika,** Wizara pia inalenga kutangaza kaulimbiu ya "Tanzania Unforgettable" katika ligi kubwa za michezo hasa soka,

kikapu na riadha Marekani na Ulaya kwenye masoko yetu makuu na yale mapya ya kimkakati na tayari mazungumzo na vilabu husika yanaendelea. Aidha, katika kuendeleza utalii wa utamaduni na matukio, Wizara itaendelea kushirikiana na waandaaji wa matamasha mengine duniani kama vile BET, Superbowl, Afrima, MTV Mama, Coechella na Tommorrow Land ili kujitangaza. Lakini pia Wizara inakamilisha mikakati ya kuendelea kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuboresha zaidi Tamasha la SAUTI ZA BUSARA vilevile kubuni Tamasha kubwa lingine kwa Tanzania Bara litakaloileta dunia Tanzania na hasa katika miji kitovu cha Utalii kama Arusha, Kilimanjaro, Mwanza, Mara na Manyara.

## 3.0 MCHANGO WA SEKTA ZA MALIASILI NA UTALII KATIKA KUKUZA UCHUMI NA MAENDELEO ENDELEVU

**20. Mheshimiwa Spika,** umuhimu wa sekta ya maliasili na utalii kwa Taifa unaweza kuelezwa kwa namna nyingi, mifano mingi na takwimu nyingi, lakini itoshe tu kuonesha kuwa, hata wakati huu ambapo hatujawekeza vya kutosha ili kuvuna matunda ya sekta hizi, tayari mchango wa sekta hizi ni mkubwa kama ifuatavyo: wakati sekta ya utalii pekee inachangia asilimia 25 ya fedha za kigeni, sekta ya misitu inachangia kwa asilimia 5.9 mapato yote ya nje; mchango wa sekta ya utalii ni takriban asilimia 17.5 na sekta ya misitu na nyuki asilimia 3.3 ya pato la taifa. Aidha, kwa sasa, hapa nchini, asilimia 85 ya nishati yote inayotumika nchini hutokana na matumizi ya miti (mkaa na kuni). Vilevile, asilimia 90 ya vifaa vya ujenzi na samani vinavyotumika majumbani hutokana na rasilimali za misitu.

**21. Mheshimiwa Spika,** fauka ya hayo, umuhimu wa sekta hii kiuchumi ni UHAI WA MWANADAMU: pamoja na uhifadhi wa vyanzo vya maji ambavyo vingi viko katika maeneo yaliyohifadhiwa na yanayoendelea kulindwa kupitia Sekta ya Maliasili na Utalii, asilimia 90 ya umeme unaozalishwa kwa nguvu ya maji nchini unatokana na vyanzo vya maji vilivyopo ndani ya maeneo yaliyohifadhiwa. Aidha, vituo vya uzalishaji umeme vya Mtera, Kihansi na Kidatu vinategemea maji yanayotoka katika hifadhi za Taifa za Kitulo, Ruaha na Udzungwa pamoja na mapori ya akiba ya Rungwa,

Mpanga Kipengere na Kilombero; na hifadhi za misitu za Iyovi, Nanganje, Masagati, Makombe na Shamba la Miti Sao Hill.

**22. Mheshimiwa Spika,** vilevile, vyanzo hivyo vinaendelea kuchangia maji kwenye mradi wa Bwawa la kuzalisha umeme la Mwl. Nyerere vikiungana na vyanzo vya maji vinavyotoka katika hifadhi za misitu za Magombera, Uluguru, Nanganje, Iwonde, Masagati, Sali, Mzelezi, Nawenge, Muyowe, Mhulu, Ligamba, Ukwiva na Palaulanga. Kwa upande mwingine, kituo cha kuzalisha umeme cha Hale kinategemea maji kutoka kwenye vyanzo vya maji vilivyopo katika hifadhi za Taifa Mlima Kilimanjaro, Arusha na misitu ya Milima ya Tao la Mashariki. Pia, vyanzo hivyo huchangia katika mito mbalimbali ambayo hutumika kwa shughuli za kilimo, ufugaji na matumizi ya nyumbani. Sambamba na hilo, hifadhi za Taifa, misitu ya Lindimaji, mapori ya akiba, mapori tengefu na maeneo ya ardhioevu hutoa huduma za kiikolojia.

**23. Mheshimiwa Spika,** vilevile, mazao ya nyuki hutumika kwa chakula na malighafi za viwanda vya kutengeneza vipodozi, madawa na vyakula. Pia, nyuki ni rafiki wa mazingira na mchavushaji mkuu wa mimea, hivyo husaidia kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo. Takriban asilimia 80 ya mimea yote ya chakula huchavushwa na nyuki. Kwa upande mwingine, maeneo ya hifadhi ni muhimu katika uhifadhi wa udongo na ufyonzaji wa hewa ukaa, hali inayopunguza athari za mabadiliko ya tabianchi. Vilevile, malikale zinatumika kuhifadhi historia, tamaduni zetu na huvutia watalii.

**24. Mheshimiwa Spika,** kwa minajili ya kufupisha umuhimu wa sekta za uhifadhi kwa uhai wa Taifa yatosha kumnukuu Baba wa Taifa, Mwalimu Julius K. Nyerere, mwaka 1961, alitoa tamko kwenye Kongamano la Kimataifa la Uhifadhi kuhusu mustakabali wa wanyamapori katika Afrika huru. Tamko hili maarufu kama Arusha Manifesto lilisema, nanukuu:

"Uhai wa wanyamapori ni jambo linalotuhusu sote katika Afrika. Viumbe hawa wa porini, wakiwa katika mapori wanamoishi, siyo muhimu tu kwa ajili ya kuajabiwa na kuvutia lakini pia ni sehemu ya maliasili yetu na pia ndio mustakabali wa maisha yetu ya baadaye. Kwa kukubali dhamana ya wanyamapori wetu tunatamka kwa dhati

kwamba tutafanya kila tuwezalo kuhakikisha kwamba wajukuu wa watoto wetu wataweza kufurahia urithi huu mkubwa na wa thamani adhimu. Uhifadhi wa wanyamapori na maeneo yote yenye mapori huhitajia maarifa ya kitaalamu, wafanyakazi waliopata mafunzo maalumu, na fedha; na hivyo tunaomba mataifa mengine yashirikiane nasi katika kazi hii muhimu, ambayo kufanikiwa au kutofanikiwa kwake hakuathiri tu Bara la Afrika bali ulimwengu mzima kwa ujumla". (Mwalimu J.K. Nyerere 1961).

Tamko hili limekuwa ni msingi wa uhifadhi na matumizi endelevu ya wanyamapori nchini na hivyo ninawaomba wadau wote kuendelea kushirikiana kikamilifu na Wizara katika kufanikisha azma hiyo ya Baba wa Taifa na kwetu sisi katika mwaka mmoja uliopita na katika miaka mingi ijayo maono haya yameendelea na yataendelea kuwa mwelekeo wetu.

**4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI**
***NA UTALII***

**25. Mheshimiwa Spika,** mnamo tarehe 03 Juni 2022, Wizara iliwasilisha katika Bunge lako Tukufu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023, na kupokea maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii pamoja na michango ya Waheshimiwa Wabunge, kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Vilevile, imepokea maoni ya Kamati wakati ikiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**26. Mheshimiwa Spika,** ushauri na maoni ya Kamati yalikuwa ni pamoja na: kuendelea kuweka mikakati madhubuti ya kuongeza nguvu katika utambuzi na utangazaji wa vivutio vya utalii; kufanya tathmini ya utekelezaji wa Mradi wa Usimamizi wa Maliasili na Kuendeleza Utalii Kanda ya Kusini (REGROW) ili maeneo mengine yanufaike na mradi huo katika awamu ya pili; na kutatua migogoro ya mipaka kwenye maeneo ya hifadhi kwa wakati ili kuepusha madhara yanayoendelea kujitokeza. Ushauri mwingine uliotolewa ni

pamoja na Wizara kuchukua hatua madhubuti za haraka katika kukabiliana na changamoto za migongano ya binadamu na wanyamapori wakali na waharibifu; kuharakisha mchakato wa kupandisha hadhi Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) kuwa Mamlaka; kuharakisha mapitio ya Sera na Sheria ambazo zimepitwa na wakati; na kuharakisha mchakato wa kuleta Bungeni Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA).

**27. Mheshimiwa Spika,** naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara imezingatia maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na maandalizi ya mpango na bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

## 5.0 UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2022/2023

**28. Mheshimiwa Spika,** Wizara inasimamia maeneo yaliyohifadhiwa kisheria yenye ukubwa wa kilomita za mraba takriban 307,800 sawa na asilimia 32.5 ya eneo lote la nchi. Maeneo hayo yanajumuisha hifadhi za Taifa 22, Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, Mapori ya Akiba 29, Mapori Tengefu 23, Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi za Wanyamapori (WMAs) 22, maeneo matatu (3) ya ardhioevu chini ya mkataba wa Ramsar, Hifadhi za Misitu ya asili 416, Hifadhi za Misitu ya Mazingira Asilia 23, Mashamba ya Miti ya Serikali 24, Hifadhi za Nyuki 14, Maeneo ya Malikale 132 na Vituo Saba (7) vya Makumbusho ya Taifa.

**29. Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umezingatia miongozo mbalimbali ikiwemo Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2022/2023 - 2024/2025, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022 - 2025/2026), Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020 - 2025, Sheria na Sera mbalimbali, Mpango Mkakati wa Wizara (2021/2022 - 2025/2026), maagizo mbalimbali ya viongozi wa Serikali na Mikataba ya Kikanda na Kimataifa.

**30. Mheshimiwa Spika,** ninaomba sasa nitoe taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

### 5.1 Ukusanyaji wa Maduhuli

**31. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara ilipangiwa kukusanya jumla ya **Shilingi 670,856,583,921.00.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 469,364,418,596.00** zinakusanywa kupitia mifumo ya TEHAMA ya Wizara kwenda Mamlaka ya Mapato Tanzania kutokana na vyanzo vya mapato kutoka TANAPA, NCAA na TAWA; na **Shilingi 201,492,165,325.00** zinakusanywa na Wizara kutokana na vyanzo vya mapato kutoka Idara, Mifuko na baadhi ya Taasisi zake kupitia mfumo wa MNRT Portal.

**32. Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Aprili 2023, Wizara imekusanya jumla ya **Shilingi 616,339,998,496.49** sawa na **asilimia 92** ya lengo la makusanyo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 485,701,521,769.48** zimekusanywa na Wizara kutokana na vyanzo vya taasisi za TANAPA, NCAA na TAWA; na **Shilingi 130,638,476,727.01** zimekusanywa na Wizara kutokana na Idara, mifuko na taasisi zake nyingine.

### 5.2 Matumizi ya Kawaida na Maendeleo

**33. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara iliidhinishiwa kutumia jumla ya **Shilingi 624,142,732,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo **Shilingi 443,706,567,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 180,436,165,000** kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Aprili 2023, Wizara na taasisi zake ilipokea jumla ya **Shilingi 449,172,169,458.11** sawa na asilimia 72 ya fedha iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 353,800,483,601** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 95,371,685,857.11** kwa ajili ya miradi ya maendeleo (Dev). Fedha za matumizi ya kawaida zinajumuisha jumla ya **Shilingi 144,708,217,720.46** fedha za matumizi mengineyo (OC) na **Shilingi 209,092,265,880.56** fedha za mishahara (PE). Fedha zilizopokelewa

zimewezesha kufanikisha utekelezaji na kuleta mafanikio mbalimbali katika Sekta ya Maliasili na Utalii.

### 5.3 Mafanikio

**34. Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara imepata mafanikio mbalimbali yakiwemo:

### (i) Kuongezeka kwa Idadi ya Watalii na Mapato

**35. Mheshimiwa Spika,** kufuatia juhudi zilizofanyika za kutangaza vivutio vya utalii, kuimarika kwa miundombinu ya utalii ndani ya hifadhi na kuanzishwa kwa Programu maalum ya kutangaza nchi ijulikanayo kama Tanzania – the Royal Tour pamoja na mikakati mingine ya kutangaza utalii, idadi ya watalii wa ndani na kimataifa waliotembelea maeneo ya hifadhi na Makumbusho ya Taifa imeongezeka kutoka watalii 1,711,625 mwaka 2021 hadi kufikia watalii 3,818,180 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 123. Katika ongezeko hilo idadi ya watalii wa kimataifa imeongezeka kutoka watalii 922,692 mwaka 2021 hadi kufikia watalii 1,454,920 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 57.7. Aidha, idadi ya watalii wa ndani imeongezeka kutoka watalii 788,933 mwaka 2021 hadi 2,363,260 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 199.5. Napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza Watanzania kwa mwamko wao kutembelea vivutio vya utalii na ninawahamasisha waendelee kutembelea vivutio hivyo zaidi. Vilevile, ni vyema wananchi wakashiriki kunufaika na utalii unaoongezeka nchini ikiwemo hasa katika maeneo ya hifadhi na miji ya kitalii kuhakikisha wanaboresha makazi yao (home stays) na hata kujenga makazi maalum (BnB) kwa ajili ya watalii wanaopenda kuishi wenyewe au na jamii kufikia huko.

### (ii) Tanzania Kuendelea Kutambulika Kimataifa

**36. Mheshimiwa Spika**, kufuatia mikakati mbalimbali ya utangazaji utalii ikiwemo uendelezaji wa Programu ya Tanzania – the Royal Tour, Tanzania imeendelea kutambulika Kimataifa na kupata Tuzo mbalimbali zikiwemo: Hifadhi ya Taifa Serengeti kuwa hifadhi bora

Afrika (African's Leading National Park Attraction) kwa kipindi cha miaka minne (4) mfululizo kuanzia mwaka 2019 hadi 2022; Tanzania kuwa nchi ya saba (7) miongoni mwa nchi 18 za Afrika zilizo bora kutembelewa kiutalii kwa mwaka 2022; Hifadhi ya Taifa ya Serengeti kuwa miongoni mwa vivutio sita (6) vikubwa vinavyopendekezwa kutembelewa mwezi Juni, 2023. Taarifa hizo ni kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na taasisi kubwa duniani ya masuala ya utalii ya Tripadvisor ya nchini Marekani. Sambamba na hilo, Hifadhi ya Taifa Serengeti imeorodheshwa kuwa eneo la kwanza kati ya maeneo 15 maridhawa kutembelewa mwezi Juni, 2023 kulingana na taarifa iliyotolewa na U.S. News & World Report. Vilevile, Bodi ya Utalii Tanzania imefanikiwa kuwa Mshindi wa Kwanza kwa Taasisi zinazotangaza Utalii Afrika (African's Leading Tourist Board) kupitia mashindano yaliyoratibiwa na World Travel Awards.

**37. Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwingine, hifadhi tatu (3) za Tanzania zimeingizwa kwenye orodha ya hifadhi 25 bora duniani kupitia Travelers' Choice Destination – National Parks of the World ambapo Hifadhi ya Taifa ya Serengeti imekuwa ya kwanza ikifuatiwa na Hifadhi za Taifa Kilimanjaro (12) na Tarangire (14) kwa ripoti ya mwaka 2022. Katika hatua nyingine, asali inayozalishwa nchini kutoka katika miti jamii ya miombo imeshika nafasi ya pili (2) kwa ubora katika ukanda wa Afrika kupitia mashindano yaliyofanyika kwenye Kongamano la Wafugaji Nyuki Kanda ya Afrika (African Symposium) nchini Afrika ya Kusini mwezi Machi, 2023.

**(iii) Kupandishwa Hadhi Maeneo ya Hifadhi na Misitu**

**38. Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanikiwa kupandisha mapori tengefu mawili (2), Kilombero na Pololeti, kuwa mapori ya akiba. Hatua hii imeongeza idadi ya mapori ya akiba kutoka 27 hadi 29. Lengo la jitihada hizi ni kuimarisha ulinzi na matumizi endelevu ya rasilimali zilizopo katika mapori hayo. Vilevile, upandishwaji hadhi wa mapori hayo unalenga kuchochea uhifadhi, utunzaji wa vyanzo vya maji na uwekezaji katika shughuli za utalii wa picha na uwindaji. Katika kuimarisha ushiriki wa jamii kwenye uhifadhi wa rasilimali za wanyamapori, Wizara imewezesha uanzishwaji wa Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori ya Mpimbwe katika Mkoa wa Katavi. Kwa upande

mwingine, Wizara imewezesha uanzishwaji wa Msitu wa Halmashauri ya Ulanga wenye ukubwa wa hekta 57,370 na misitu 17 ya vijiji yenye ukubwa wa hekta 104,185 kutoka katika vijiji 17 vya wilaya za Kilwa, Tunduru, Liwale na Kilindi. Sambamba na hilo, ushirikishwaji wa wananchi kutumia rasilimali za samaki na nyuki katika Mapori ya Akiba Kilombero, Uwanda, Ugalla na Moyowosi umeimarika.

**(iv) Kuimarika kwa Ulinzi wa Rasilimali za Wanyamapori na Misitu**

**39. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuongeza jitihada za kuimairisha ulinzi na uhifadhi wa rasilimali za maliasili kwa kudhibiti ujangili, biashara haramu ya nyara, uvunaji haramu wa mazao ya misitu na nyuki na uvamizi wa maeneo yaliyohifadhiwa. Jitihada hizi pamoja na mambo mengine zimewezesha kuongezeka kwa idadi ya tembo kutoka 43,330 mwaka 2014 hadi 60,000 mwaka 2023 na kuifanya Tanzania kuendelea kuwa nchi ya tatu (3) barani Afrika kwa kuwa na tembo wengi. Kwa upande mwingine, idadi ya faru weusi imeendelea kuongezeka kutoka 163 mwaka 2019 hadi 238 mwaka 2022 na hivyo kuvuka lengo la Mkakati wa Kitaifa wa Kuhifadhi Faru 205 ifikapo Desemba 2023. Sambamba na hilo, taarifa za hali ya usalama zinaonesha katika kipindi cha mwezi Julai 2022 hadi Aprili 2023 hakuna vifo vya wanyamapori vilivyotokana na ujangili vilivyoripotiwa. Vilevile, Tanzania imeendelea kuongoza Duniani kwa kuwa na simba wengi wapatao 14,912 na twiga 24,000. Ongezeko hili linathibitisha kupungua kwa ujangili wa wanyamapori nchini. Haya ni matokeo ya mipango bora na ushirikiano katika uhifadhi.

**40. Mheshimiwa Spika,** mafanikio hayo yamechangiwa na juhudi mbalimbali za Serikali ikiwa ni pamoja na kufanya siku doria 479,242 zilizowezesha kukamatwa kwa watuhumiwa 12,058 pamoja na nyara mbalimbali za Serikali. Vilevile, Wizara imefanya operesheni maalumu za kiintelejensia zilizowezesha kuzuiwa kwa matukio ya ujangili na uvunaji haramu wa mazao ya misitu; kukamata silaha mbalimbali zikiwemo bunduki 214 (riffle 12, bastola 2, shotgun 45 na gobore 155), risasi 1,427 na kuvunjwa kwa mitandao saba (7) ya ujangili. Sambamba na hilo, Wizara imeendelea kuimarisha Jeshi la Uhifadhi la Wanyamapori na Misitu kwa kutoa mafunzo ya ndani na nje ya kijeshi, upelelezi, uchunguzi na usimamizi wa kesi kwa askari wake kwa lengo

la kuimarisha uhifadhi. Katika mafuzo hayo, jumla ya Askari 54 walishiriki.

### (v) Kuendeleza Programu za Upandaji Miti na Mashamba ya Miti

**41. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha upatikanaji wa malighafi itokanayo na misitu, Wizara ilikusanya tani 14.7 za mbegu za miti na kuzalisha miche 26,900,353 ambayo ilipandwa katika mashamba ya Serikali yenye ukubwa wa hekta 7,475 na miche mingine kugawiwa kwa jamii na kupandwa katika maeneo yao. Sambamba na hatua hizo, Wizara kwa kushirikiana na Benki ya NMB imeanzisha kampeni ya kupanda miti kitaifa ambayo ilizinduliwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, mwezi Machi, 2023. Kampeni hii ina lengo la kupanda takriban miti 1,000,000 kwa mwaka katika maeneo ya shule za msingi na sekondari. Hadi sasa miti iliyopandwa na TFS kwa kushirikiana na Benki ya NMB ni 334,000 katika lengo la miti 500,000 ifikapo Juni, 2023. Vilevile, Wizara inaendelea na kampeni ya Kijanisha Dodoma na kampeni ya kupanda Miti 1,000,000 kwa kila mkoa.

**42. Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwingine, Wizara imeendelea na kazi ya kuhudumia mashamba ya miti kwa kupalilia hekta 19,186, kupogoa miti hekta 7,831 na kupunguza miti katika hekta 1,287.03. Lengo ni kuhakikisha upatikanaji wa malighafi kwa ajili ya viwanda vya misitu. Juhudi hizi zimewezesha Wizara kutenga takriban mita za ujazo 1,133,825 na vipande 12,000 vya nguzo kutoka kwenye mashamba ya miti kwa ajili ya viwanda vya mazao ya misitu na wafanyabiashara wengine wa mazao ya misitu.

### (vi) Kuongezeka kwa Masoko na Kiwango cha Mazao ya Nyuki yanayouzwa Nje ya Nchi

**43. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha kuwa soko la mazao ya nyuki hususan asali inayozalishwa nchini inapenya katika masoko ya kimataifa, Wizara imewekeza katika eneo la kuongeza uzalishaji wa asali bora ambapo kwa mwaka 2022 jumla ya tani 31,695 za asali na tani 1,907 za nta zimezalishwa kulinganisha na tani 31,442 za asali na tani 1,901 za nta zilizozalishwa 2021. Kiwango hiki kimetokana na utoaji

wa elimu ya mbinu bora za ufugaji nyuki kwa wafugaji nyuki 1,998; mizinga ya kisasa 1,025; pamoja na vifaa vingine vya kuvunia mazao hayo.

**44. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha asali inayozalishwa nchini inakuwa na viwango vya ubora vinavyohitajika katika masoko ya kimataifa, Wizara imeanzisha mfumo unaoitwa Honey Traceability System ambao unafuatilia ubora wa asali kuanzia kwa mfugaji nyuki hadi pale inapoingia sokoni. Aidha, kupitia mashindano ya ubora wa asali zinazozalishwa barani Afrika, asali kutoka Mkoa wa Tabora ilishika nafasi ya pili (2) kwa ubora. Hivyo, kutokana na juhudi hizi, asali ya Tanzania imeendelea kuuzwa katika masoko ya nchi za Umoja wa Ulaya, Uarabuni na kwenye masoko mapya ya Poland na China. Sambamba na hilo, mazao ya nyuki nje ya nchi kwa mwaka 2021/2022 yalikuwa tani 1,562.93 za asali na tani 747.56 za nta ambayo yalileta jumla ya Shilingi bilioni 30.58. Vilevile, mazao ya misitu nje ya nchi yalikuwa Shilingi bilioni 234.5 mwaka 2022. Kufuatia mafanikio haya, nitumie fursa hii kuwaomba Watanzania kuchangamkia fursa ya masoko haya ili tuweze kuingizia nchi yetu fedha za kigeni.

**(vii) Kuendeleza Utalii Ikolojia katika Hifadhi za Misitu ya Mazingira Asilia na Maeneo ya Malikale**

**45. Mheshimiwa Spika,** katika kutanua wigo wa mazao ya utalii na kuongeza idadi ya watalii na mapato, Wizara imeendelea kujenga na kukarabati miundombinu ya utalii katika hifadhi za misitu ya mazingira asilia na maeneo ya malikale. Uendelezaji huo umehusisha ukarabati wa kilomita 178 za njia za kutembea watalii na kilomita 258 za barabara za hifadhini. Hatua hiyo imeenda sambamba na kuandaliwa kwa vipindi na kutangaza vivutio vilivyopo katika maeneo hayo na programu za utalii wa ndani. Mathalan, kwa mwaka fedha 2022/2023 jumla ya vipindi 48 vya redio na 48 vya televisheni viliandaliwa na kurushwa katika vyombo mbalimbali vya habari. Aidha, Wizara iliandaa na kusambaza vipeperushi 2,300 na nakala za miongozo ya waongoza utalii kwa lengo la kutangaza vivutio vilivyopo katika maeneo ya hifadhi za misitu ya mazingira asilia na maeneo ya malikale. Kupitia juhudi hizo, kwa mwaka wa fedha

2022/2023 kufikia mwezi Aprili 2023 jumla ya watalii 220,826 walitembelea vivutio hivyo wakiwemo watalii wa ndani 193,194 na watalii wa nje 27,632 ikilinganishwa na jumla ya watalii 152,002 ambapo watalii wa ndani walikuwa 134,861 na nje 17,141 kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Vilevile, mapato kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kufikia Aprili 2023 yalikuwa Shilingi 1,144,023,420 ikilinganishwa na mapato ya Shilingi 606,553,290 kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**46. Mheshimiwa Spika,** ongezeko la utalii katika maeneo ya hifadhi za misitu ya mazingira asilia na maeneo ya malikale, limechangiwa na kampeni mbalimbali ikiwemo Bata Msituni iliyofanyika hifadhi ya msitu Vikindu; Mbio za nyika msituni na mashindano ya pikipiki na baiskeli yaliyofanyika katika shamba la miti West Kilimanjaro (West Kili tour challenge); Kampeni ya majaribio ya mashindano ya magari katika shamba la miti Sao Hill; mbio za Marathon zilizofanyika katika hifadhi ya msitu Rongai; shamba la miti Rubare; na hifadhi ya Mji Mkongwe Bagamoyo. Vilevile, Wizara imeendelea kutumia vyombo vya habari kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo katika maeneo ya misitu ya Pugu, Vikindu, Ziwa Duluti na Meru.

**(viii) Kufunguka kwa Biashara ya Hewa ya Ukaa**

**47. Mheshimiwa Spika,** nchi yetu inayo rasilimali kubwa ya misitu ambayo inaweza kutumika katika kukuza uchumi kupitia biashara ya hewa ya ukaa. Wizara kupitia Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania kwa mara ya kwanza imesaini Hati ya Makubaliano (MoU) na Kampuni ya Blue Carbon kutoka Falme za Kiarabu kwa ajili ya biashara ya hewa ya ukaa katika misitu. Kwa upande mwingine, Wizara kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania imesaini pia makubaliano ya awali na kampuni ya GreenCop ya nchini Singapore yenye thamani ya Shilingi bilioni 8.4 kama malipo ya awali katika misitu. Makubaliano hayo yanalenga kuhakikisha kuwa Tanzania inaendelea kunufaika na biashara ya hewa ya ukaa. Kwa sasa, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais inaendelea kufanya tathmini ya kubaini uwezo wa misitu yetu kufyonza hewa ya ukaa. Matokeo ya tathmini hiyo yatawezesha nchi kujua kiwango cha

hewa ya ukaa kilichopo katika maeneo ya misitu na hivyo kufanya biashara hiyo kwa mafanikio.

**(ix) Kuimarika kwa Maeneo ya Malikale na Makumbusho**

**48. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuboresha miundombinu katika maeneo ya malikale na makumbusho. Maboresho hayo yamechangia kuongezeka kwa wageni wanaotembelea vivutio hivyo kutoka 582,080 kwa mwaka 2021/2022 hadi kufikia 887,285 mwaka 2022/2023 sawa na ongezeko la asilimia 52. Aidha, mwitikio huu umechochewa na juhudi mbalimbali zikiwemo: kuwekwa kwa maonesho 13 ya kudumu katika vituo sita (6) vya Makumbusho ya Mwl. Nyerere-Butiama; Makumbusho ya Majimaji; Azimio la Arusha; Makumbusho ya Elimu Viumbe; Kijiji cha Makumbusho na Nyumba ya Utamaduni. Vilevile, Wizara imeweka maonesho ya kudumu ya mijusi ya Dinasoria katika eneo la Lindi Mjini na Mkwajuni - Tendaguru mkoani Lindi. Katika hatua nyingine, Wizara imewezesha jamii kuona maonesho kwa kutumia gari la kimaonesho linalotembea ambapo wananchi wanafikiwa na kupatiwa elimu ikiwa ni pamoja na kuona vivutio vya urithi wa asili vinavyohamishika wakiwa katika maeneo yao. Sambamba na hilo, Wizara imefanikiwa kujenga vituo vitatu (3) vipya katika maeneo ya malikale ya Mbuamaji – Kigamboni; Mkwajuni Tendaguru – Lindi na Mikumbi – Lindi Mjini. Kwa kujenga vituo hivyo, Wizara itaboresha utalii wa utamaduni pamoja na matarajio ya kupata jumla ya watalii 63,519 na mapato ya wastani wa Shilingi 265,560,000 kwa mwaka.

**(x) Kufanya Marekebisho ya Sheria ya Sekta ya Mambo ya Kale**

**49. Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanya marekebisho ya Sheria ya Mambo ya Kale, Sura 333 ambayo imewezesha kuhamisha majukumu ya kiutendaji kutoka Idara ya Mambo ya Kale kwenda Shirika la Makumbusho ya Taifa. Aidha, Sheria hiyo iliyohuishwa imetoa fursa ya kuanzishwa kwa Makumbusho binafsi. Hatua hii, itasaidia kuongeza idadi ya watalii na mapato yatokanayo na sekta ya Mambo ya Kale.

## 5.4 Utekelezaji wa Masuala Mtambuka

### (i) Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Katika Maeneo ya Hifadhi

**50. Mheshimiwa Spika,** katika hatua za kutatua changamoto ya mipaka kati ya vijiji na maeneo yaliyohifadhiwa, Serikali iliunda Kamati ya Mawaziri Nane na kupita nchi nzima kuchambua na kutoa mapendekezo ambayo yalipata baraka za Baraza la Mawaziri. Uamuzi wa Baraza la Mawaziri umeshafikishwa kwa Wakuu wote wa Mikoa ili washirikishe wananchi katika zoezi la kuweka mipaka mipya katika maeneo yanayotenganisha vijjiji na maeneo ya hifadhi ili kupunguza migogoro.

**51. Mheshimiwa Spika,** naomba kutumia fursa hii kusisitiza na kuwakumbusha Wakuu wa mikoa wote ambao bado hawajatoa matamko kama inavyotakiwa wafanye hivyo kabla ya Juni 30, 2023 ili wataalamu waendelee kuweka vigingi vya mipaka na Wizara iweze kutoa ramani mpya.

**52. Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla katika utekelezaji wa zoezi la utatuzi wa migogoro ya mipaka vijiji 249 vimenufaika na umegaji wa maeneo ya hifadhi. Aidha, jumla ya ekari 1,728,057.91 zimeondolewa kwenye maeneo ya hifadhi na kupewa wananchi kwa mchanganuo ufuatao: ekari 707,962 zimetokana na kufuta mapori tengefu 12; ekari 46,715 zimetokana na kufuta misitu saba (7); na ekari 973,380.91 zimetokana na kumegwa kwa maeneo yaliyohifadhiwa ya Hifadhi za Taifa, Mapori ya Akiba, Hifadhi za Misitu na maeneo ya Malikale. Hatua hii imewezesha wananchi kupata maeneo makubwa kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na baadhi kubaki kwenye hifadhi ili kulinda rasilimali nyingine zikiwemo vyanzo vya maji na hivyo kupunguza migogoro baina ya wananchi na maeneo yaliyohifadhiwa.

**53. Mheshimiwa Spika,** sambamba na utekelezaji wa maamuzi ya Kamati hiyo, Wizara imeendelea kuimarisha mipaka ya maeneo ya hifadhi kwa kuweka vigingi 2,473; mabango 247; na kusafisha barabara za mpaka (mkuza) zenye jumla ya urefu wa kilomita 583.6. Aidha, Wizara inaendelea kutoa elimu ya uhifadhi na usimamizi wa

maeneo yaliyohifadhiwa kwa jamii hasusan inayopakana na maeneo ya hifadhi.

**(ii) Ushirikishaji wa Wadau katika Uhifadhi, Utalii na Elimu kwa Umma**

**54. Mheshimiwa Spika**, kwa kutambua mchango wa wadau katika uhifadhi na uendelezaji utalii, Wizara imeendelea kushirikiana na wananchi, sekta binafsi, washirika wa maendeleo na wadau wengine katika kutekeleza majukumu yake. Katika kuendelea kuitangaza nchi kimataifa Wizara imeendelea kushirikiana na Kamati ya Rais ya Kuitangaza Tanzania Kimataifa kwa kuendelea kufanya maonesho mbalimbali ya filamu ya Tanzania-The Royal Tour.

**55. Mheshimiwa Spika,** Tamko Maalum kwa Wadau wa Sekta ya Utalii: kati ya Mei 25 na 26 mwaka huu, Wizara ilikutana na wadau wa kisekta wakiwemo wa wanyamapori, misitu, nyuki na utalii kwa lengo la kupitia changamoto na kuweka mikakati ya pamoja ya kutatua changamoto zilizopo katika sekta hizo. Nawaahidi wadau wetu kuwa Wizara itaendelea kuwa nao karibu, itawalinda, itatetea maslahi yao na zaidi nao watimize wajibu wao kwa Taifa kwa kulipa kodi na kufanya biashara zao kwa njia za halali.

**56. Mheshimiwa Spika,** kutokana na maoni na ushuhuda wa wadau katika vikao hivyo, ni wazi kuwa ipo haja kwa Serikali yetu kuendelea kuilea sekta ya utalii kwa namna mbalimbali, hivyo nitumie fusa hii pia kuzikumbusha taasisi nyingine za umma na sekta binafsi kushirikiana na Wizara mama ya Utalii wanapotaka kuibua kodi mpya, tozo mpya na kanuni nyingine zinazoweza kuathiri biashara hii yenye ushindani duniani na kuibua kelele zinazoweza kuathiri biashara hiyo. Kwa namna hii tunaweza kwa pamoja kuinua biashara ya utalii nchini.

**57. Mheshimiwa Spika,** halikadhalika, Wizara imeweza kuwafikia wadau wakubwa wa kimataifa kama TripAdvisor, CNN, Expedia na kufikia makubaliano ya awali na timu ya michezo za nchini Marekani za Sounders FC (Soka na ndio mabingwa wa mabara), Seahawks (mpira wa miguu wa Marekani na imeshashiriki Superbowl mara kadhaa) na Portland Trailbraizers inayoshiriki ligi ya kikapu ya NBA.

**58. Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea na mazungumzo na klabu mbili kubwa za Ligi Kuu ya Uingereza na Hispania kwa ajili ya kutangaza vivutio vya utalii. Vilevile, Wizara na wadau wake ilishiriki maonesho ya kimataifa ya utalii kama: TOPRESA nchini Ufaransa; World Travel Market – (WTM) nchini Uingereza; International Tourism & Travel Show (IMTM) nchini Canada; FITUR nchini Hispania; Matka Nordic Travel Fair nchini Finland; na Tourism Expo nchini Japan.

**59. Mheshimiwa Spika**, katika kutangaza utalii ndani ya nchi, Wizara iliandaa vipindi vya radio 80, televisheni 128, magazeti 13, kuchapisha na kurusha maudhui 181 kwenye mitandao ya kijamii kwa lengo la kuelimisha umma. Aidha, programu 62 za kielimu ziliandaliwa ambapo wanafunzi 19,641 walipata elimu kuhusu uhifadhi wa malikale, urithi wa utamaduni na shughuli za utalii. Vilevile, warsha 11 na makongamano matano (5) yaliyoshirikisha wadau 2,170 kwenye mikoa ya Lindi, Mtwara, Arusha, Tanga, Ruvuma na Pwani yalifanyika kwa ajili ya kuhamasisha uhifadhi, uendelezaji na matumizi endelevu ya malikale zilizopo katika maeneo yao. Kwa upande mwingine, Wizara ilishiriki katika kampeni za utangazaji wa vivutio vya utalii ambapo jumla ya wanafunzi 13,150 walifikiwa.

**60. Mheshimiwa Spika**, kwa upande mwingine, Wizara imeendelea kutoa elimu ya upandaji miti, ufugaji nyuki na namna ya kupambana na moto usio na mpango kwa kutengeneza na kusambaza makala 57, kuandaa vipindi 48 vya Misitu ni Uhai na vipindi 48 vya Tanzania ya Kijani ambavyo vilirushwa kupitia TBC. Vilevile, Wizara imeandaa na kusambaza vipeperushi 3,800, majarida 160, mabango sita (6) na vipeperushi 910 zenye maudhui ya uhifadhi wa misitu na nyuki. Katika mwaka mmoja ujao na kwa kuzingatia kuwa taarifa za utafiti zinaonesha kuwa Watanzania wengi wanaogopa gharama na hawana taarifa za kutosha kuhusu wanafikaje katika vivutio vya nchi yetu, mikakati zaidi hasa kwa kutumia kampeni mbalimbali za Radio, TV, watu mashuhuri na viongozi wenye ushawishi zitafanyika ikiwemo pia TTB na wadau wa utalii kuhakikisha wananchi wanapata taarifa sahihi za gharama na namna ya kutembelea vivutio mbalimbali vya utalii vilivyopo katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

**61. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kutoa mafunzo kwa jamii ambapo vikundi 12 vya wafugaji nyuki vyenye jumla ya watu 184 vimepata mafunzo ya mbinu bora za ufugaji nyuki kwa ajili ya kuanzisha utalii wa nyuki (Api-tourism) katika wilaya za Iringa, Chamwino, Mvomero na Kilombero. Aidha, elimu na ushauri wa mbinu bora za ufugaji nyuki na uchakataji wa mazao yake ilitolewa kwa wananchi 559 katika wilaya za Arumeru, Arusha, Hai, Karatu, Meatu na Monduli. Sambamba na hilo, jumla ya mizinga 200 ilitolewa bure kwa jamii ya Wahadzabe wilayani Karatu na mizinga 80 kwa wafugaji nyuki kwenye Wilaya za Iringa, Kilolo na Manyoni ili kuboresha maisha ya wananchi pamoja na kupunguza migongano baina ya binadamu na wanyamapori wakali na waharibifu.

**(iii) Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa**

**62. Mheshimiwa Spika,** Tanzania imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wa kikanda na kimataifa katika kuhifadhi maliasili, malikale na kuendeleza utalii. Aidha, kwa lengo la kuendelea kutangaza vivutio vilivyopo nchini, Wizara iliandaa Mkutano wa 65 wa Shirika la Utalii Duniani Kamisheni ya Afrika (65th UNWTO-CAF Meeting) ambao ulifanyika tarehe 05 hadi 07 Oktoba, 2022 Jijini Arusha. Washiriki wa Mkutano huo walikuwa ni Mawaziri wa Utalii 39 kutoka nchi wanachama pamoja na wadau 695 ikijumuisha 430 wa ndani na 265 wa nje. Kwa upande mwingine, Mawaziri hao walifanya ziara ya mafunzo kwa kutembelea vivutio vya utalii vikiwemo Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro; WMA ya Burunge; Coffee Tour; Cultural Arts Gallery; Tanzanite Museum; Arusha Museum; Maporomoko ya Napuru na kikundi cha sanaa za kitamaduni Arusha. Vilevile, mwongozo wa uwekezaji katika Sekta ya Utalii nchini ulizinduliwa. Hatua hii imewezesha kuendeleza zao la Utalii wa Mikutano na Matukio (MICE) ikiwemo kujenga kumbi mbalimbali hapa nchini ikiwemo Kigamboni, Dar es Salaam.

**63. Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyingine, Wizara iliandaa Mkutano wa Wataalam wa Malikale uliohudhuriwa na watafiti 98 kutoka Bara la Afrika, Ulaya na Amerika. Lengo la mkutano huo lilikuwa kushirikishana matokeo ya tafiti zinazohusiana na masuala ya malikale. Kupitia mkutano huo, Wizara imeandaa mikakati mbalimbali

ya kuhifadhi, kutafiti na kuendeleza rasilimali za malikale. Vilevile, Wizara imeshiriki mikutano mbalimbali inayohusu Sekta ya Maliasili na Utalii ikiwemo: Mkutano wa 22 wa Kimataifa wa Baraza la Usafiri na Utalii Duniani uliofanyika mwezi Novemba, 2022 jijini Riyadh, Saudi Arabia; Mkutano wa 19 wa Mkataba wa Kimataifa wa Biashara ya Wanyamapori na Mimea iliyo hatarini kutoweka (CITES CoP19) uliofanyika mwezi Novemba, 2022 nchini Panama. Katika mkutano huo, Tanzania ilichaguliwa kuwa mjumbe wa Kamati muhimu za uendeshaji wa Mkataba huo.

**64. Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwingine, Tanzania ilishiriki katika Mkutano wa 27 wa nchi wanachama wa Mkataba wa Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi (CoP27) uliofanyika mwezi Novemba, 2022 jijini Sharm-El-Sheikh, Misri; Kongamano la Wafugaji Nyuki Duniani (APIMONDIA) lililofanyika Jijini Instanbul, Uturuki mwezi Septemba, 2022; Kongamano la Wafugaji Nyuki Kanda ya Afrika lililofanyika jijini Durban, Afrika ya Kusini mwezi Machi, 2023; Mkutano wa Jukwaa la Uhifadhi wa Wanyamapori Afrika uliofanyika mwezi Novemba, 2022 jijini Gaborone, Botswana. Pia, kwa lengo la kuendelea kutunza na kuhifadhi miti jamii ya mikoko, Wizara imeshiriki Mkutano wa tano wa Umoja wa Sayansi za Bahari kwa nchi zilizoko Magharibi mwa Bahari ya Hindi (WIOMSA) ulifanyika mwezi Oktoba, 2022 Afrika ya Kusini. Kupitia mikutano hii Tanzania imeimarisha mahusiano ya kikanda ikiwa ni pamoja na kuhamasisha uwekezaji katika nchi yetu.

**65. Mheshimiwa Spika,** Wizara ilishiriki Kongamano la Biashara na Uwekezaji nchini Afrika Kusini mjini Pretoria mwezi Machi, 2023 na kufanikiwa kutangaza vivutio vya Utalii kidijitali kwa kutumia QR Coded collateral; kujenga ushirikiano baina ya Bodi ya Utalii Tanzania na Taasisi ya Umoja wa Huduma za Utalii ya Afrika Kusini (SATSA) kwa lengo la kutangaza vivutio vya nchi mbili kwa pamoja (Joint Destination Promotion); na kusaini Hati ya Makubaliano (MoU) baina ya Chuo cha Taifa cha Utalii na na Chuo Kikuu cha Teknolojia cha Tshwane ili kuimarisha ushirikiano.

**66. Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwingine, Wizara imeendelea kutekeleza mikataba mbalimbali ya uhifadhi wa mazingira, maliasili,

malikale na utalii. Mikataba hiyo ni pamoja na: Mkataba wa Kimataifa wa Biashara ya Wanyamapori na Mimea iliyo hatarini kutoweka (CITES); Mkataba wa Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi (UNFCCC); Mkataba wa Kupambana na Hali ya Kuenea kwa Jangwa na Ukame (UNCCD); Mkataba wa UNESCO unaohusu Uhifadhi na Ulinzi wa Maeneo ya Urithi wa Dunia ya Asili na Utamaduni; Mkataba wa Wanyamapori Wahamao (CMS); na Mkataba wa Uhifadhi wa Bioanuai (CBD). Kwa kutekeleza mikataba hiyo, Tanzania imeendelea kushirikiana na nchi nyingine duniani katika uhifadhi wa maliasili, malikale na ulinzi wa urithi wa Dunia.

**(iv) Kuimarisha Utendaji wa Wizara na Rasilimaliwatu**

**67. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha utendaji kazi, Wizara imeendelea kuboresha mazingira ya kazi ambapo nyumba na ofisi 39 zimejengwa katika vituo vya Wizara pamoja na ununuzi wa mitambo 56, magari 247, pikipiki 50, samani na vitendea kazi vya ofisi. Wizara inaendelea na jitihada za ukamilishaji wa ujenzi wa Jengo la Makao Makuu ya Wizara awamu ya pili katika eneo la Mji wa Serikali – Mtumba, jijini Dodoma ambapo kwa sasa ujenzi umefikia asilimia 92.
Vilevile, jumla ya watumishi 1,126 walipata mafunzo ambapo watumishi 575 walipewa mafunzo ya muda mrefu na watumishi 551 walipewa mafunzo ya muda mfupi kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kufanya kazi kwa ufanisi. Pia, Wizara ilipokea watumishi wapya 428 wa kada mbalimbali ikiwemo askari 314 ili kuimarisha uhifadhi, kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu pamoja na biashara haramu ya nyara na mazao ya misitu na nyuki. Sambamba na hilo, Wizara imepandisha vyeo watumishi 1,899 kwa lengo la kuongeza ufanisi na kuboresha maslahi ya watumishi.

**68. Mheshimiwa Spika,** kwa lengo la kuimarisha Jeshi la Uhifadhi, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora imeandaa Mwongozo wa pamoja wa Miundo ya Taasisi zinazounda Jeshi la Uhifadhi ili kuweka usawa kwenye maeneo ya msingi kama vile mishahara na ngazi za vyeo vya maafisa kuendana na matakwa ya Amri za Jumla. Vilevile, Wizara imewapatia mafunzo maafisa na Askari 449 katika maeneo ya Upelelezi 107 na Intelijensia 342. Sambamba na hilo, Wizara

imeendelea na mafunzo ya mabadiliko ya muundo wa utendaji, mafunzo ya awali ya kijeshi na mafunzo ya uongozi kwa Maafisa 55 na Askari 545.

**69. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kutoa stahili za watumishi kwa mujibu wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo na kusimamia masuala ya maadili na mapambano dhidi ya rushwa mahala pa kazi ili kuimarisha uadilifu katika utekelezaji wa majukumu kwa kuzingatia Mkataba wa Huduma kwa Mteja. Kwa upande mwingine, Wizara imeendelea kuimarisha afya za watumishi kwa kuhamasisha na kuwawezesha kushiriki mazoezi baada ya saa za kazi na siku za mapumziko. Aidha, Wizara imeshiriki mashindano ya SHIMUTA yaliyofanyika mwezi Novemba, 2022 mkoani Tanga; SHIMIWI yaliyofanyika mkoani Tanga mwezi Oktoba, 2022; na maadhimisho ya Mei Mosi yaliyofanyika Kitaifa mwezi Aprili, 2023 mkoani Morogoro. Kwa upande mwingine, Wizara imeendelea kusimamia maslahi, ustawi na afya za watumishi ikiwa ni pamoja na kuwawezesha watumishi waliojitokeza wanaoishi na VVU na UKIMWI kupata lishe bora. Aidha, watumishi wenye ulemavu wameendelea kupatiwa huduma kulingana na mahitaji yao.

**70. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha uwajibikaji na utawala bora, Wizara imekamilisha uteuzi kwa Wakuu wa Taasisi za: Bodi ya Utalii Tanzania; Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania; uteuzi wa bodi tisa (9) za taasisi; na kujaza nafasi wazi sita (6) za uongozi katika Menejimenti ya Wizara.

## 5.5 Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara Kisekta

### 5.5.1 Sekta ya Wanyamapori

**71. Mheshimiwa Spika**, Sekta ya Wanyamapori ina jukumu la kulinda na kuhifadhi rasilimali za wanyamapori ndani na nje ya maeneo yaliyohifadhiwa kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho. Sekta hii inasimamia hifadhi za Taifa 22, Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, mapori ya akiba 29, mapori tengefu 23, maeneo matatu (3) ya ardhioevu na bustani tano (5) za wanyamapori za Serikali. Aidha, sekta inasimamia shughuli za uhifadhi katika maeneo 22 ya Jumuiya za Hifadhi za

Wanyamapori, ufugaji wa wanyamapori katika mashamba matano (5) ya watu binafsi, bustani za wanyamapori 24, maeneo ya mazalia ya wanyamapori 29 na ranchi tano (5) za sekta binafsi. Sambamba na hilo, utekelezaji wa majukumu ya sekta ya wanyamapori hufanywa na Idara ya Wanyamapori, Shirika la Hifadhi za Taifa, Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro, Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania, Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania, Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori, Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori– Mweka, Taasisi ya Taaluma ya Wanyamapori - Pasiansi na Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii - Likuyu Sekamaganga. Utekelezaji wa jukumu hili unaongozwa na Sera ya Taifa ya Wanyamapori ya mwaka 2007 na kusimamiwa na Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori Sura 283; Sheria ya Hifadhi za Taifa Sura 282; Sheria ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro Sura 284; na Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania Sura 260.

### 5.5.1.1 Masuala Mahsusi ya Sekta ya Wanyamapori

**Utatuzi wa Migogoro inayotokana na migongano baina ya Binadamu na Wanyamapori Wakali na Waharibifu**

**72. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kukabiliana na changamoto ya wanyamapori wakali na waharibifu kwa kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Utatuzi wa Migogoro baina ya Wanyamapori na Binadamu (2020 – 2024). Migongano hiyo kwa kiasi kikubwa husababishwa na kuwepo kwa matumizi ya ardhi yasiyozingatia mpango bora wa matumizi ya ardhi hasa baadhi ya watendaji wetu wanaohusika na kugawa ardhi kutotimiza wajibu wao kwa kuzingatia miongozo iliyopo; kuongezeka kwa shughuli za kibinadamu hususan katika maeneo yanayopakana na hifadhi za wanyamapori, shoroba za wanyamapori na maeneo ya mtawanyiko ya wanyamapori kuvamiwa na wananchi; uchungaji wa mifugo kwenye maeneo yaliyohifadhiwa; na mabadiliko ya tabia nchi yanayosababisha ukame wa muda mrefu na hivyo kusababisha baadhi ya wanyamapori kutoka nje ya hifadhi kwa lengo la kupata mahitaji nje ya hifadhi.

**73. Mheshimiwa Spika,** hatua zilizochukuliwa katika kukabiliana na changamoto ya migongano baina ya binadamu na wanyamapori

wakali na waharibifu ni pamoja na kujenga vituo 16 maalum vya askari kwenye maeneo yenye matukio mengi ya wanyamapori wakali na waharibifu kwa ajili ya kuimarisha doria za udhibiti wa matukio ya wanyamapori hao. Vituo hivyo vimejengwa katika wilaya za Meatu (Malwilo), Itilima (Longalombogo), Busega (Mwabayanda), Mchinga (Milola), Rufiji (Ngarambe), Liwale (Ngumbu), Tunduru (Chingulungulu), Nachingwea (Nditi), Mwanga (Kwakoa), Songwe (Gua), Iringa (Mbolimboli), Nzega (Ndala), Mvomero (Sangasanga), Chamwino (Ilangali), Mpwapwa (Mtera) na Kondoa (Idindiri). Hatua hii imefanya idadi ya vituo maalum vya askari kwa ajili ya kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu kufikia 154. Katika mwaka huu wa fedha vituo vingine vipya 16 vinaendelea kujengwa kwenye maeneo yenye changamoto kwa kuzingatia jiografia ya migogoro hiyo.

**74. Mheshimiwa Spika,** hatua nyingine zilizochukuliwa ni kuendelea kutoa elimu kuhusu namna ya kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu na utaratibu au vigezo vinavyotumika katika kulipa kifuta machozi na kifuta jasho kwa jamii zinazoishi karibu na maeneo yaliyohifadhiwa. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara imetoa elimu hiyo kwa wananchi wa Halmashauri za wilaya 28 na kutoa vifaa mbalimbali vya kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu kama vile mizinga ya nyuki 176, tochi zenye mwanga mkali 221, vuvuzela 125, Roman candles 107, ving'ora 20, fataki 170, honi 70, baruti pakiti 124, filimbi 210, pilipili ya unga na mbegu. Sambamba na hilo, Wizara imeimarisha vizimba vinne (4) vya kuzuia madhara yatokanayo na mamba katika wilaya za Songwe viwili (2) na Buchosa viwili (2). Katika hatua nyingine, Wizara inaendelea kushirikiana na wadau kufanya mapitio ya Kanuni za kifuta jasho na kifuta machozi za mwaka 2011 kwa lengo la kuboresha kanuni hizo na kuimarisha mifumo ya ukusanyaji na utunzaji wa taarifa za matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu ili kupunguza mlolongo wa kushughulikia changamoto zinazotokana na athari za wanyamapori.

**75. Mheshimiwa Spika**, hatua nyingine ni kufanya utafiti kwa kuwafunga mikanda ya mawasiliano viongozi wa makundi ya wanyamapori wakali na waharibifu ili kubaini mienendo yao. Katika kutekeleza hilo, jumla ya tembo 156 wamefungwa mikanda hiyo kurahisisha ufuatiliaji wa mienendo yao katika mifumo ikolojia

Tarangire-Manyara, Serengeti, Nyerere Selous-Mikumi; Selous-Niassa na Lake NatronWestern Kilimanjaro na simba 32 katika Mifumo Ikolojia ya Serengeti na Ruaha-Rungwa. Kwa upande mwingine, Wizara imekuwa ikiondoa wanyamapori kama vile tembo kwenye makazi ya watu kwa kutumia helikopta na ndege maalum (drones). Mfano, katika mwaka wa fedha 2022/2023 makundi matatu (3) yenye jumla ya tembo 270 yaliondolewa kwenye makazi ya watu katika wilaya za Nachingwea na Liwale. Katika hatua nyingine, Wizara imenunua magari 247, pikipiki 50 na kuajiri askari 136 kwa ajili ya kuimarisha shughuli za doria ikiwa ni pamoja na kukabiliana na matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu. Sambamba na hilo, Wizara kupitia taasisi zake za uhifadhi inaendelea kushirikiana na askari wanyamapori wa vijiji kudhibiti matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu.

**76. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023 jumla ya askari wanyamapori 410 wa vijiji wamepewa mafunzo ya uhifadhi na mbinu za kukabiliana na matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu. Aidha, jumla ya askari 231 wa jeshi la uhifadhi walipata mafunzo maalum ya kijeshi ya namna ya kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu na wamesambazwa katika maeneo mbalimbali nchini ili kuongeza nguvu katika doria za kuwadhibiti wanyamapori hao. Sambamba na hilo, Wizara imetoa orodha ya namba za simu za kupiga bure pamoja na orodha ya namba za simu za Wakuu wa Kanda kwa lengo la kurahisisha mawasiliano inapotokea changamoto ya wanyamapori wakali na waharibifu.

**77. Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyingine Wizara imejenga mabwawa nane (8) na kukarabati mabwawa 17 katika hifadhi mbalimbali ikiwa ni jitihada za kuzuia wanyamapori kutoka nje ya hifadhi wakati wa ukame. Aidha, Wizara inaendelea kutekeleza Mpango Kazi wa kuongoa shoroba za wanyamapori ili kufungua mapito ya wanyamapori. Pamoja na kwamba, nchi nyingi duniani zimefuta dhana ya malipo ya kifuta jasho na machozi kwa wananchi walioathirika wanyamapori wakali na waharibifu, Wizara imeendelea kulipa kifuta jasho na machozi kwa waathirika. Katika kipindi mwaka 2022/2023 jumla ya Shilingi 1,133,356,300 zimelipwa kama kifuta jasho

na machozi kwa wananchi 4,869 walioathiriwa katika wilaya 36 na kiasi kingine cha Shilingi milioni 884 kitalipwa wakati wowote kwa wananchi walioathirika.

Vilevile, Wizara itaendelea kutekeleza mikakati ya muda mrefu na mfupi ya kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu kwa kushirikiana na wananchi na wadau mbalimbali wa uhifadhi hii ni pamoja na kuimarisha mahusiano ya ujirani mwema kwa kuchangia shughuli za kijamii na maendeleo kwa ustawi wa jamii zinazoishi karibu na maeneo ya hifadhi.

**78. Mheshimiwa Spika**, ili kuwa na namna ya kisayansi zaidi ya kutatua changamoto za migogoro kati ya wanyamapori na binadamu, Wizara inakusudia kuunda Kamati Maalum itakayopita kwenye maeneo mbalimbali yenye changamoto husika na kutathmini chanzo na sababu mahsusi za mgogoro wa wanyamapori kwa kila eneo na kushauri hatua za haraka kutokana na upekee wa kila eneo. Aidha, wakati Wizara ikiendelea kupambana na changamoto za wanyamapori wakali na waharibifu, ni vema wananchi wakaendelea kuchukua tahadhari mbalimbali kwa mujibu wa maelekezo ya wataalam ikiwemo kutoingia kwenye maeneo ya hifadhi na kutofanya shughuli za kibinadamu kwenye mapito ya wanyamapori. Lakini pia, maafisa wenye dhamana ya kugawa maeneo ya ardhi kwa ajili ya matumizi mbalimbali wahakikishe kunakuwa na ushirikishaji wa wataalam wa maliasili kuliko kupanga matumizi ya eneo ambalo baadaye wanyamapori wanaanza kusumbua wananchi.

### 5.5.1.2 Idara ya Wanyamapori

**79. Mheshimiwa Spika,** Wizara katika kuimarisha uhifadhi na ulinzi wa rasilimali wanyamapori imepandisha hadhi mapori tengefu ya Kilombero na Pololeti kuwa mapori ya akiba. Sambamba na hilo, Wizara imefanya tathmini ya maeneo 61 ya shoroba ambapo maeneo 18 ya kipaumbele yamebainishwa na Mpango Mkakati wa Kitaifa wa Kuongoa Shoroba hizo umeandaliwa na kuzinduliwa. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI pamoja na wadau wengine imeendelea na zoezi la uhakiki wa shoroba za Kwakuchinja

ili kubaini maeneo ambayo yamesalia na ambayo bado yanatumiwa na wanyamapori kwa ajili ya kuyawekea alama za mipaka na kuyahifadhi. Uhifadhi wa shoroba hii utawezesha wanyamapori wanaohama katika majira mbalimbali ya mwaka kuendelea kutumia ushoroba huu kuhama kutoka Hifadhi ya Tarangire kwenda Hifadhi ya Ziwa Manyara.

**80. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha jitihada za kudhibiti ujangili Wizara imefanya mapitio ya Mkakati wa Kupambana na Ujangili na Biashara Haramu ya Wanyamapori wa mwaka 2014 - 2019 uliomaliza muda wake na kuandaa mkakati mpya wa miaka kumi (2022 - 2032). Katika hatua nyingine, Wizara imeandaa kanuni za ufifilishaji za mwaka 2023 na kufanya mapitio ya Kanuni za uwindaji wa wenyeji na wageni wakazi ya mwaka 2021; Kanuni za Uwekezaji Mahiri ya mwaka 2021; Kanuni ya Uwindaji wa Kitalii ya mwaka 2015; Kanuni ya Mashamba ya Wanyamapori ya mwaka 2020; na Kanuni za WMA za mwaka 2018. Kanuni hizi zitaimarisha uhifadhi, kuboresha mazingira ya uwekezaji na utoaji huduma kwa wateja. Vilevile, Wizara imefanya maboresho ya Kanuni na Amri za Jumla za Jeshi la Uhifadhi ili kuimarisha nidhamu, upelelelezi na uendeshaji wa mashtaka.

### 5.5.1.3 Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania – TANAPA

**81. Mheshimiwa Spika,** Shirika limeendelea na jitihada za kuimarisha na kuendeleza miundombinu ya utalii kwa lengo la kuongeza idadi ya watalii na mapato. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kufikia mwezi Aprili, 2023 Shirika limepokea jumla ya watalii 1,438,399 na kukusanya mapato ya Shilingi 291,107,634,419 ikilinganishwa na watalii 858,900 na mapato ya Shilingi 140,231,422,143.61 kwa kipindi kama hicho mwaka 2021/2022. Ongezeko la watalii ni sawa na asilimia 67.5 na mapato ni asilimia 107.6.

**82. Mheshimiwa Spika,** katika kuongeza huduma za malazi kwa watalii, Shirika limetangaza na kupata wawekezaji 17 ambao wako katika hatua mbalimbali za ujenzi wa nyumba za malazi ya watalii zenye jumla ya vitanda 796 katika hifadhi sita (6). Kwa upande mwingine, shughuli za ujenzi wa huduma za kitalii za gharama nafuu katika hifadhi za Mikumi (nyumba ndogo mbili (2) na ukumbi mmoja

wa chakula); Kitulo (nyumba 3); Burigi-Chato (nyumba sita (6); Milima ya Udzungwa (ukumbi mmoja wa kijamii) na Ruaha (upanuzi wa ukumbi wa chakula uliopo) zinaendelea. Miradi hii iko katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Pia, Shirika limeboresha huduma za utalii ikiwa ni pamoja na; ukarabati wa hosteli mbili (2), mabanda 23, mahema tisa (9), vyoo vya watalii vitatu (3), Lango moja (1), gati mbili (2) na hoteli moja (1). Vilevile, Shirika limekarabati barabara zenye urefu wa kilomita 3,677.5; vivuko 44; daraja moja (1); viwanja vya ndege 20; njia za kupanda milimani (nature trails) zenye urefu wa kilomita 296.2 katika hifadhi za Taifa. Sambamba na hilo, Shirika limenunua magari madogo tisa (9) na lilipokea jumla ya mitambo na malori 74, kupitia miradi ya REGROW na Mpango wa Maendeleo wa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya Athari za UVIKO-19 kwa ajili ya kutengeneza na kuboresha barabara.

**83. Mheshimiwa Spika,** Shirika limeendelea kutekeleza miradi ya ujirani mwema katika vijiji vinavyopakana na hifadhi za Taifa. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Aprili 2023 jumla ya miradi 29 yenye thamani ya Shilingi bilioni 2.6 imetekelezwa kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya 10; miradi ya elimu 14; vituo vya polisi viwili (2); na visima vitatu (3) vya maji. Aidha, Shirika limeendelea kushirikiana na Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) kutekeleza miradi nane (8) ya kielimu ya ujirani mwema katika vijiji vinvyopakana na Hifadhi za Taifa Katavi (1), Mikumi (2), Mkomazi (3) na Serengeti (2). Vilevile, jumla ya vikundi 293 vya jamii inayozunguka hifadhi za Taifa Ruaha, Udzungwa na Mikumi vilipewa mafunzo ya COCOBA na vikundi 168 vilipewa fedha mbegu chini ya mradi wa REGROW. Kwa upande mwingine, Shirika limeendelea kuimarisha mahusiano na jamii kwa kufanya mikutano 2,986 katika vijiji 653 kuhusu elimu ya uhifadhi ambapo jumla ya wananchi 283,659 walifikiwa.

**84. Mheshimiwa Spika,** katika kudhibiti majanga ya moto hifadhini, Shirika limeendelea na juhudi mbalimbali za kudhibiti matukio ya moto katika hifadhi za Taifa. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Aprili 2023 jumla ya matukio ya moto 58 yalitokea na kudhibitiwa katika Hifadhi za Taifa 10 ambazo ni: Arusha (2), Kilimanjaro (14), Ziwa Manyara (4), Milima ya Mahale

(2), Mkomazi (9), Nyerere (17), Ruaha (3), Tarangire (2), Milima ya Udzungwa (2) na Mto Ugalla (3). Aidha, kwa kufuata miongozo ya usimamizi wa moto kwa kila hifadhi, zoezi la kuchoma moto mpango limefanyika katika eneo lenye ukubwa wa hekta 1,437,655.

**85. Mheshimiwa Spika,** Shirika limeendelea kutoa semina mbalimbali za udhibiti wa moto kwa jamii zinazozunguka hifadhi za Taifa ambapo jumla ya semina 24 zilifanyika katika vijiji 19 vinavyopakana na hifadhi za Taifa Tarangire, Kilimanjaro na Mto Ugalla. Kwa upande mwingine, Shirika limeendelea kuimarisha mipaka na kuweka alama ili kuzuia moto usio na mpango kuingia ndani ya hifadhi na kuondoa migogoro ya mipaka kati ya hifadhi na wananchi. Katika hatua nyingine shirika limeandaa na kufanya mapitio ya Mipango ya Jumla ya Usimamizi (GMP) wa hifadhi za Taifa za Nyerere, Mkomazi na Ruaha.

**5.5.1.4 Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania – TAWA**

**86. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka imeendelea kuimarisha ulinzi wa rasilimali za wanyamapori, kudhibiti ujangili na uvamizi wa maeneo yaliyohifadhiwa. Hadi kufikia mwezi Aprili 2023, jumla ya siku doria 195,912 sawa na asilimia 69 ya lengo la siku doria 284,460 zimefanyika. Doria hizo zimefanikisha kukamatwa kwa watuhumiwa 2,786; bunduki 108; risasi 1,334; kutegua mitego 3,080 ya nyaya za kutegea wanyamapori. Aidha, Mamlaka imeendelea kutumia mifumo ya kiteknolojia kuimarisha ulinzi ambapo jumla ya faru tisa (9) walikamatwa ambapo saba (7) waliwekewa visukuma mawimbi na wawili (2) waliwekewa alama za utambuzi kwenye masikio katika mapori ya akiba Maswa na IkorongoGrumeti. Vilevile, Mamlaka imekarabati kilomita 1,649 za barabara katika mapori ya akiba ya Inyonga, Igombe, Moyowosi na Lukwati Piti. Katika hatua nyingine, Mamlaka imejenga karakana katika Pori la Akiba Rukwa na Kanda ya Kaskazini, kituo cha Askari Swagaswaga, nyumba tatu (3) za watumishi, minara mitatu (3) pamoja na majengo mawili (2) ya mawasiliano kwa ajili ya kuratibu mawasiliano ya doria katika mapori ya akiba Selous na Maswa. Aidha, jumla ya Askari 150 wamepatiwa mafunzo ya ukakamavu na utayari ya jeshi.

**87. Mheshimiwa Spika**, Mamlaka imekamilisha ujenzi wa vituo 16 vya Askari katika maeneo yenye changamoto kubwa ya wanyamapori wakali na waharibifu. Katika hatua nyingine, Mamlaka imenunua pikipiki 50 kwa ajili ya doria za mwitikio wa haraka kudhibiti matukio hayo pamoja na kutoa elimu kwa wananchi. Sambamba na hilo, Mamlaka imeanzisha utaratibu wa kutumia askari wa wanyamapori wa vijiji kudhibiti matukio ya wanyamapori ambapo jumla ya askari 37 kutoka wilaya tisa (9) za Tunduru (4); Nachingwea (4); Liwale (4); Lindi vijijini (4); Rufiji (4); Meatu (4); Itilima (4); Busega (4); na Bunda (5) wamepatiwa mafunzo na kuanza kutekeleza majukumu yao katika vituo tisa (9). Vilevile, Mamlaka imeongeza matumizi ya teknolojia ikiwa ni pamoja na kutumia helkopta kufukuza wanyamapori kwenye maeneo rasmi ya wananchi, ndege nyuki (drone) na visukuma mawimbi kwa lengo la kufuatilia mienendo ya wanyamapori wakali na waharibifu hususan tembo.

**88. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha miundombinu ya ulinzi wa rasilimali za wanyamapori, na kudhibiti ujangili, Mamlaka imejenga karakana moja (1), kununua mitambo minne (4); boza mbili (2) za kubebea mafuta; na mbili (2) za kubebea maji kwa ajili ya ujenzi barabara ndani ya mapori ya akiba. Katika hatua nyingine, Mamlaka imeendelea kuboresha miundombinu ya utalii kwa kujenga barabara zenye urefu wa kilomita 157 katika mapori ya akiba ya Kijereshi na Maswa. Sambamba na hilo, Mamlaka imejenga makasha tisa (9) ya kutunzia wanyamapori katika bustani za Ruhila na Tabora. Aidha, Mamlaka imeandaa mipango ya jumla ya usimamizi ya mapori ya Rungwa, Kizigo na Muhesi ili kuimarisha usimamizi wa rasilimali za wanyamapori zilizopo kwenye mapori hayo.

**89. Mheshimiwa Spika,** Sambamba na hilo, Mamlaka imeendelea kushiriki katika matukio ya Kitaifa na Kimataifa kwa lengo la kutangaza vivutio vya utalii na fursa za uwekezaji katika maeneo yake. Miongoni mwa matukio hayo ni pamoja na: Mkutano wa 19 wa nchi wanachama wa CITES; onesho la the Abu Dhabi International Hunting and Equestrian Exhibition (ADIHEX 2022); na fainali za Kombe la Dunia nchini Qatar. Kufuatia juhudi hizo idadi ya watalii wa uwindaji wameongezeka kutoka 531 kwa mwaka 2021/2022 hadi kufikia watalii wa uwindaji 692 kwa kipindi cha miezi 10 tu ya mwaka wa fedha

2022/2023. Sambamba na hilo, Mamlaka imeendelea kutekeleza Mpango wa uwekezaji mahiri (SWICA).

**90. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka imeendelea kushirikiana na wananchi kutatua na kupunguza migogoro katika maeneo ya hifadhi kwa kutambua na kuweka alama za mipaka katika mapori ya akiba Mkungunero, Swagaswaga, Igombe, Mpanga Kipengere, Wamimbiki na Kilombero ambapo jumla ya vigingi 1,479 vimewekwa katika maeneo hayo sawa na asilimia 55 ya lengo la vigingi 2,678. Kwa upande mwingine, Mamlaka imesafisha mkuza wenye urefu wa kilomita 33 na kufyeka mpaka wenye urefu wa kilomita 332 katika mapori ya akiba.

**91. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha mahusiano kati ya hifadhi na jamii na kuhakikisha kuwa wananchi wananufaika na uwepo wa Hifadhi katika maeneo yao, TAWA imechangia miradi ya maendeleo iliyoibuliwa na jamii kwenye maeneo yanayozunguka mapori ya akiba ambapo jumla ya miradi sita (6) yenye thamani ya Shilingi 177,000,000 imetekelezwa. Miongoni mwa miradi hiyo ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa soko la samaki Kilombero, darasa na ofisi ya walimu katika Shule ya Msingi Usinge wilaya ya Kaliua na mradi wa maji Kijiji cha Kwa Mtoro-Swagaswaga. Aidha, Mamlaka imeendelea kutekeleza Mwongozo wa Kusimamia Shughuli za Uvuvi na Ufugaji Nyuki katika mapori ya akiba ya Ugalla, Uwanda, Moyowosi na Kilombero. Vilevile, Mamlaka imefanya mikutano 1,067 ya kutoa elimu ya uhifadhi kwa jamii ambapo wananchi 317,409 kutoka wilaya 112 walishiriki. Jitihada hizi zimeimarisha mahusiano na kuwezesha Mamlaka kukusanya Shilingi bilioni 1.04 kutokana na ada ya shughuli za uvuvi na ufugaji nyuki katika mapori ya akiba.

**92. Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha utendaji wa Mamlaka ya Usimamazi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), Wizara inaendelea na taratibu za kutunga Sheria ya Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania na kazi hii inatarajia kukamilika katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024.

### 5.5.1.5 Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro – NCAA

**93. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Mamlaka imefanya jumla ya siku doria 38,843 na operesheni maalum sita (6) zilizowezesha kukamatwa kwa wahalifu 423 wa makosa mbalimbali. Kwa upande mwingine, Mamlaka imeendelea kutoa elimu ya uhifadhi kwa jamii kwa kufanya vikao 10 na mikutano 20 katika vijiji vinavyozunguka hifadhi. Aidha, Mamlaka imesafisha mpaka wenye jumla ya kilomita 200 na kuweka jumla ya vigingi 50 kwa ajili ya kuepusha migororo ya mipaka.

**94. Mheshimiwa Spika,** katika jitihada za kupambana na mimea vamizi, Mamlaka imeendelea kutekeleza Mpango Mkakati wa kitaifa wa Kutokomeza Mimea Vamizi (2019 - 2024). Aidha, magugu vamizi yalifyekwa na kung'olewa katika eneo lenye ukubwa wa hekta 900 ndani ya bonde la Kreta. Vilevile, hekta 2,150 zilichomwa moto ili kuondoa magugu vamizi na kuboresha nyanda za malisho katika eneo hilo. Katika hatua nyingine, Mamlaka imeotesha jumla ya miche ya miti 317,889 na kugawa miche 66,442 katika maeneo ya wilaya za Karatu, Ngorongoro na Monduli.

**95. Mheshimiwa Spika,** katika kuboresha shughuli za uhifadhi na utalii ndani ya Hifadhi, Mamlaka imeimarisha miundombinu kwa kujenga barabara zenye jumla ya kilomita 90 kwa kiwango cha changarawe kwenye maeneo ya Enduleni hadi Ndutu kilomita 19.5; Viewpoint hadi Alaililai kilomita 39; na Alaililai hadi Nayobi kilomita 30; na barabara ya Ngoitoktok kilomita 1.5. Aidha, Mamlaka imeendelea kufanya ukarabati wa mara kwa mara kwenye mtandao wa barabara wenye jumla ya Kilomita 606. Vilevile, Mamlaka imenunua malori 14, mitambo mitano (5) na maboza mawili (2) ya maji kwa ajili ya matengenezo ya barabara.

**96. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka imeendelea na juhudi za kuboresha huduma za utalii kwa kuhakikisha upatikanaji wa maji safi na salama ambapo jumla ya visima vitatu (3) vyenye uwezo wa kuzalisha lita 22,400 kwa saa vimechimbwa katika maeneo ya Laetoli, Ndutu na Olduvai. Sambamba na hilo, Mamlaka inakamilisha mradi wa ujenzi wa mtambo wa kutibu maji ujulikanao kama Mama Hhawu

Water Treatment Plant ambao kwa sasa umefikia asilimia 95 na umeanza kutumika. Mradi huu unahusisha ujenzi wa mtambo wa kutibu maji, ujenzi wa maabara ya ubora wa maji na ujenzi wa tenki la maji la ujazo wa lita 135,000 katika geti la Loduare. Mradi huu una uwezo wa kuzalisha maji ujazo wa lita 1,500,000 kwa siku na utanufaisha watalii wanaoingia Ngorongoro kupitia lango la Loduare, huduma za malazi zinazozunguka eneo la Hifadhi, Ofisi za Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro pamoja na jamii inayozunguka Hifadhi ikiwemo Hospitali Teule ya Lutheran na Magereza ya Karatu.

**97. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea na zoezi la kuhamisha wananchi waliojitokeza kuhama kwa hiari kutoka ndani ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro. Hadi mwezi Aprili 2023, jumla ya nyumba 503 zimejengwa katika Kijiji cha Msomera-Handeni ambapo kaya 551 zenye watu 3,010 na mifugo 15,321 zimehamia kwa ajili ya kupisha shughuli za uhifadhi. Wananchi waliohama kwa hiari wamenufaika kwa kupewa fidia, motisha, nyumba, kiwanja cha makazi chenye ukubwa wa ekari 2.5 na eneo la shamba lenye ukubwa wa ekari tano (5). Sambamba na hatua hii, Serikali imeboresha miundombinu mbalimbali ya kijamii ikiwemo ujenzi wa shule, zahanati, visima vya maji, mawasiliano, malambo, majosho, barabara, umeme, soko na kituo cha polisi. Aidha, Wizara imekamilisha zoezi la kufuta Pori Tengefu Handeni ili kuwezesha wananchi waliohamia kwa hiari kumilikishwa maeneo hayo. Wizara inawapongeza wananchi waliohamia na inawaahidi waliosalia na ambao wamekuwa wakijiandikisha kwa wingi kutaka kuhama kuwa zoezi hili, bado halijasimamishwa na Serikali, tofauti na inavyosemekana kwa baadhi ya wanaojaribu kukwamisha. Aidha, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali imejiandaa na haitarudi nyuma wala hakutakuwa na kusalimu amri katika kukamilisha zoezi hili ambalo litaendelea kufanyika kwa weledi na kasi kubwa. Tukutane Msomera.

**98. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha watumishi wanatekeleza majukumu yao kwa weledi, Mamlaka imewezesha jumla ya watumishi 216 kupata mafunzo ya muda mrefu (36) na mfupi (180). Aidha, watumishi 76 wapya wamehudhuria mafunzo ya Jeshi la Uhifadhi katika Kituo cha Mlele kwa lengo la kuimarisha nidhamu na ukakamavu. Kwa upande mwingine, Mamlaka imenunua magari 14

kwa ajili ya shughuli za uhifadhi na utalii. Katika hatua nyingine, Mamlaka inaendelea na ujenzi wa ofisi ya Makao Makuu katika eneo la Kemyn, wilayani Karatu.

**99. Mheshimiwa Spika,** kufuatia uamuzi waSerikali wa kuliweka Pori la Akiba Pololeti chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kwa lengo la kuimarisha ulinzi, uhifadhi na utalii, Mamlaka imepeleka jumla ya Askari 43 kwa ajili ya kuimarisha ulinzi. Aidha, Mamlaka kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi imekamilisha zoezi la kupima vijiji 14 vinavyopakana na Pori la Akiba Pololeti na kutatua migogoro ya mipaka katika vijiji saba (7) vinavyozunguka eneo hilo. Sambamba na hilo, Mamlaka imewezesha zoezi la uandaaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi katika vijiji 36 na kufungua barabara ya mkuza yenye urefu wa kilomita 112.63 itakayotumika kwa shughuli za ulinzi na uendelezaji wa pori hilo.

### 5.5.1.6 Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania – TAWIRI

**100. Mheshimiwa Spika,** Taasisi ina jukumu la kufanya, kuratibu na kusimamia tafiti za wanyamapori nchini. Katika kutekeleza jukumu hilo, Taasisi imefanya tafiti za kimkakati hususan zinazohusu migongano baina ya binadamu na wanyamapori wakali na waharibifu katika kanda za: Kaskazini (mikoa ya Kilimanjaro na Arusha); Kaskazini- Magharibi (mikoa ya Kagera na Mara); Magharibi (mikoa ya Katavi, Rukwa, Kigoma na Tabora); na Kusini-Mashariki (mikoa ya Morogoro, Lindi na Ruvuma). Tafiti zimebaini visababishi vikuu vitatu vya migongano baina ya binadamu na wanyamapori ni kuongezeka kwa shughuli za kibinadamu karibu na hifadhi; katika maeneo ya shoroba na mitawanyiko ya wanyamapori; mabadiliko ya tabia za wanyamapori kwa upande wa malisho na kupelekea kula mazao na uvamizi wa mifugo kwenye maeneo yao; na mabadiliko ya tabia nchi yanayosababisha ukame katika maeneo mengi na kufanya wanyamapori kuongeza wigo wa kutafuta mahitaji na kutoka nje ya maeneo yaliyohifadhiwa.

**101. Mheshimiwa Spika,** katika jitihada za kutatua migongano baina ya binadamu na wanyamapori, simba watano (5) wamehamishwa

kutoka vijiji vya Mdori na Magara wilayani Babati na kupelekwa Hifadhi ya Taifa Tarangire na simba wawili (2) walihamishwa kutoka eneo la Chumo – Kilwa kwenda kwenye maeneo ya hifadhi ili kuepusha madhara kwa jamii. Sambamba na hili, tembo wapatao 270 waliondolewa kutoka maeneo ya makazi rasmi ya wananchi katika wilaya za Nachingwea na Liwale na kuelekezwa hifadhini kwa kutumia helikopta. Aidha, Taasisi imefunga visukuma mawimbi 62 kwa wanyamapori kama ifuatavyo: tembo makundi 13 katika wilaya za Serengeti, Nachingwea, Liwale, Tunduru na Mvomero na makundi 26 yanatarajiwa kufungwa kabla ya mwaka wa fedha kuisha; mbwa mwitu makundi matatu (3) katika Mfumo Ikolojia wa Serengeti, Ruaha-Rungwa na Nyerere-Selous; simba 15 (Mfumo Ikolojia wa Serengeti, Nyerere-Selous na Tarangire-Manyara); na nyumbu 10 (Mfumo Ikolojia wa Tarangire-ManyaraNatron na Serengeti).

**102. Mheshimiwa Spika,** katika kukabiliana na mimea vamizi katika maeneo yaliyohifadhiwa, Taasisi imevumbua namna ya kutumia mimea vamizi (mfano magugu aina ya Makutian, Eleusine jaegerii yaliyovamia eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro) kama nishati mbadala kwa kutengeneza mkaa banifu (briquettes). Uvumbuzi huu utaongeza uhitaji wa mimea vamizi na hivyo kupunguza tatizo na kiwango cha utegemezi wa matumizi ya miti kama kuni au mkaa na badala yake kutumia mkaa huu mpya kama nishati mbadala.

**103. Mheshimiwa Spika,** Taasisi imeidadi wanyamapori katika mifumo ikolojia ya NyerereSelous-Mikumi-Liparamba na Saadani–Wamimbiki. Matokeo ya sensa ya wanyamapori katika mfumo ikolojia Nyerere-Selous-Mikumi-Liparamba yameonesha kuwa idadi ya tembo ni 20,006; viboko 29,071; twiga 1,679 na nyumbu 19,060. Matokeo haya yakilinganishwa na sensa ya mwaka 2018, yanaonyesha kuongezeka kwa idadi ya tembo kwa asilimia 22, palahala kwa asilimia 34, kuro kwa asilimia 34 jambo linaloashiria kuimarika kwa hali ya uhifadhi katika mfumo ikolojia huo. Kwa upande mwingine, utafiti umeonesha kupungua kwa nyati kwa asilimia 11 na kongoni kwa asilimia 26.6 katika mfumo huo wa ikolojia. Hali hii imesabishwa na ongezeko la shughuli za binadamu kama vile makazi, kilimo na mifugo katika maeneo hayo.

**104. Mheshimiwa Spika**, katika kuimairisha afya za wanyamapori, Taasisi imeendelea kufanya uchunguzi wa magonjwa na vifo vya wanyamapori. Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Taasisi ilitibu faru mmoja (1) aliyeonyesha dalili za kupooza (Pori la Akiba Ikorongo), pofu 20 waliokuwa na ugonjwa wa macho (Hifadhi za Ngorongoro na Serengeti), simba wawili (2) waliogundulika kuwa na kansa (Hifadhi ya Taifa Serengeti) na matibabu ya wanyamapori (mbuni, simba, chui, duma na tembo) kwenye bustani za Serikali za Mlimwa – Dodoma na Tabora. Aidha, makundi ya nyani manne (4) yenye takriban nyani 120 yanayotumika kwa utalii katika Hifadhi ya Taifa Gombe walipatiwa matibabu maalum ili kuwaponya na kuzuia uwezekano wa kusambaa kwa ugonjwa wa kaswende (Baboon Genetal Infection) kwa sokwe na binadamu.

**105. Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwingine, twiga 18 walifanyiwa uchunguzi na kupatiwa matibabu kwa ajili ya ugonjwa mpya wa ngozi unaoathiri wanyamapori hawa. Utafiti wa ugonjwa wa ngozi kwa twiga umeonesha kuwa ugonjwa huu upo katika hifadhi za Taifa za Ruaha, Tarangire na Mikumi. Majaribio ya awali yameonesha kuwa ugonjwa huu unaweza kutibiwa kwa kutumia kwa pamoja dawa za antibiotic na ivermectin. Hata hivyo, changamoto kubwa ipo katika kuwakamata twiga wote kwa ajili ya kuwapatia matibabu kutokana na ikolojia ya wanyamapori. Vilevile, Taasisi imeendelea kufuatilia na kudhibiti mlipuko wa ugonjwa wa kimeta ambao uliwakumba wanyamapori aina ya twiga, tembo, pundamilia na swala pala katika maeneo ya Hifadhi ya Taifa Tarangire, Mamlaka ya Hifadhi Ngorongoro na Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori Enduimeti.

### 5.5.1.7 Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori MWEKA – CAWM

**106. Mheshimiwa Spika**, Chuo kina jukumu la kutoa mafunzo, kufanya utafiti na kutoa ushauri katika nyanja za uhifadhi wa wanyamapori na uendeshaji utalii. Katika mwaka 2022/2023, Chuo kimedahili jumla ya wanafunzi 854 katika ngazi za Astashahada, Stashahada, Shahada na Shahada ya Uzamili. Aidha, Chuo kimetoa mafunzo ya muda mfupi kwa washiriki 299 kati ya hao: 251 mafunzo ya waongoza watalii wa kupanda mlima; 13 mafunzo ya utalii wa

kutembea kwa miguu; na 35 mafunzo ya kukamata na kuhamisha nyoka.

**107. Mheshimiwa Spika**, kazi nyingine zilizofanyika ni pamoja na kuandaa Mpango kamambe kwa kampasi ya Mweka (Mweka Campus Master Plan), kujenga ukuta wenye urefu wa mita 370 katika kampasi ya Mweka na kuendelea na ujenzi wa jengo la kutolea mafunzo lenye ghorofa mbili (2). Jengo hilo litakapokamilika litakuwa na vyumba vya mihadhara vyenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000 kwa wakati mmoja pamoja na ofisi za wanataaluma. Katika kuboresha utoaji wa mafunzo, Chuo kimejenga miundombinu wezeshi yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 294. Hali kadhalika, Chuo kinakamilisha ununuzi wa magari manne (4).

**5.5.1.8 Taasisi ya Taaluma ya Usimamizi wa Wanyamapori Pasiansi – PWTI**

**108. Mheshimiwa Spika,** Taasisi ya Taaluma ya Usimamizi wa Wanyamapori Pasiansi ina jukumu la kutoa mafunzo ya uhifadhi wa wanyamapori na himasheria katika ngazi ya Astashahada. Katika kutekeleza jukumu hilo, Taasisi imedahili wanafunzi 418 wa kozi ndefu katika fani za uhifadhi wanyamapori na himasheria, uongozaji watalii na usalama kwa ngazi ya Astashahada na Astashahada ya awali; na kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa washiriki 56. Katika hatua nyingine, Taasisi imetoa mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi wote yaliyofanyika katika Hifadhi ya Taifa Serengeti, mapori ya akiba ya Ikorongo na Grumet, eneo la hifadhi ya wanyamapori ya Ikona na maeneo ya wazi ya Wilaya ya Serengeti.

**109. Mheshimiwa Spika,** Taasisi imekamilisha taratibu za kuhuisha usajili wake NACTVET na kuandaa mtaala kwa ajili ya uanzishwaji wa kozi ya Stashahada katika fani ya Uhifadhi wa Wanyamapori, Uongozaji Watalii na Usalama. Katika hatua nyingine, Taasisi imeendelea kuimarisha mazingira ya kufanyia kazi kwa kuchimba kisima cha maji; kukamilisha ujenzi wa uzio wa chuo wenye urefu wa mita 180; kukarabati mabweni na madarasa ya wanafunzi; kukarabati mifumo ya maji na umeme; kuchimba na kuweka matanki ya kutunzia maji katika kambi za mafunzo Fort Ikoma. Sambamba na hilo, chuo

kimefanikisha kumilikishwa eneo lililopo katika Kijiji cha Makundusi lenye ukubwa wa hekta 76 kwa ajili ya mafunzo ya vitendo.

**5.5.1.9 Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii, Likuyu - Sekamaganga – CBCTC**

**110. Mheshimiwa Spika,** Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii, Likuyu - Sekamaganga kina jukumu la kuzijengea uwezo jamii zinazoishi jirani na maeneo yenye wanyamapori ili ziweze kushiriki katika uhifadhi na matumizi endelevu ya maliasili. Katika kutekeleza jukumu hilo, kituo kimetoa mafunzo ya muda mrefu kwa wanafunzi 105 kwa ngazi ya Astashahada ya utalii na Uongozaji Watalii. Kwa upande mwingine kituo kimetoa mafunzo ya muda mfupi kwa askari wa vijiji 320; kituo kimefanya mapitio ya mitaala ya Kozi ya Astashahada ya awali ya Utalii na Uongozaji Watalii; Askari Wanyamapori wa Vijiji (VGS); na Mtaala wa Viongozi na Wajumbe wa Kamati za Maliasili za Vijiji. Sambamba na hilo, kituo kimeandaa mtaala wa Kozi za Astashahada na Stashahada ya Utalii na Uongozaji Watalii. Katika kuboresha miundombinu, kituo kimefanya ukarabati wa bweni la wanafunzi wa kike ambao uko katika hatua za umaliziaji.

**5.5.1.10 Mfuko wa Uhifadhi wa Wanyamapori Tanzania - TWPF**

**111. Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Uhifadhi wa Wanyamapori Tanzania una jukumu la kuwezesha uhifadhi wa wanyamapori ndani na nje ya maeneo yaliyohifadhiwa. Katika kutekeleza jukumu hilo, Mfuko umewezesha utekelezaji wa kazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na: Operesheni za uzuiaji ujangili na kuwezesha kukamatwa kwa watuhumiwa 39, meno 51 ya tembo, vipande 122 vya meno ya tembo pamoja na nyara na vielelezo vingine. Hata hivyo, meno ya tembo yaliyokamatwa siyo meno ya tembo waliouawa na majangili katika mwaka 2022/2023. Kwa upande mwingine, Mfuko umelipa jumla ya Shilingi 1,118,731,300 kama kifuta jasho na machozi kwa wananchi 4,710 walioathiriwa na wanyamapori wakali na waharibifu; umewezesha utoaji wa elimu kwa wananchi kuhusu namna ya kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu; utatuzi wa migogoro kati ya hifadhi na wananchi na kupandisha hadhi maeneo yaliyohifadhiwa. Vilevile, Mfuko umewezesha mapitio ya kanuni

mbalimbali za Sekta ya Wanyamapori; kufuatilia utendaji wa jumuiya ya hifadhi ya wanyamapori (WMAs); uratibu wa uhifadhi wa faru nchini; na utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa inayohusu wanyamapori ambayo Tanzania imeridhia.

### 5.5.2 Sekta ya Misitu na Nyuki

**112. Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Misitu na Nyuki ina jukumu la kusimamia uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu na nyuki. Utekelezaji wa jukumu hilo unaongozwa na Sera ya Taifa ya Misitu (1998) na Sera ya Taifa ya Ufugaji Nyuki (1998). Aidha, utekelezaji wa shughuli mbalimbali katika sekta hizi unasimamiwa na Sheria ya Misitu Sura 323, Sheria ya Ufugaji Nyuki Sura 224 na Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania Sura 270. Vilevile, uhifadhi na usimamizi wa rasilimali za misitu na nyuki hutekelezwa kupitia Idara ya Misitu na Nyuki, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania, Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania, Chuo cha Misitu Olmotonyi, Chuo cha Viwanda vya Misitu Moshi, Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki - Tabora na Mfuko wa Misitu Tanzania.

**113. Mheshimiwa Spika,** Tanzania ina misitu yenye hekta milioni 48.1 ambapo asilimia 93 ni misitu ya mataji wazi (woodland), na asilimia saba (7) ni misitu iliyofunga. Usimamizi wa misitu hii umegawanyika katika makundi mbalimbali ikiwemo: Serikali Kuu hekta milioni 19.2 sawa na asilimia 40; Serikali za Mitaa hekta milioni 3.4 sawa na asilimia saba (7); Serikali za vijiji hekta milioni 21.6 sawa na asilimia 45 na watu binafsi hekta milioni 3.4 sawa na asilimia saba (7) na eneo lililobaki la hekta 500,000 sawa na asilimia 1. Aidha, sehemu kubwa ya eneo la misitu iliyopo inafaa kwa ufugaji nyuki ambapo vijiji vimetenga takriban hekta 143,936.78 kwa ajili ya ufugaji nyuki. Kwa upande mwingine, jumla ya hekta 36,640.43 za hifadhi za nyuki zilizo chini ya Wakala wa Huduma za misitu hutumika kwa ajili ya ufugaji nyuki pamoja na tafiti mbalimbali.

### 5.5.2.1 Masuala mahsusi ya Sekta ya Misitu na Nyuki

### (i) Utatuzi wa Changamoto ya Moto katika Mashamba ya Miti na Hifadhi za Misitu ya Asili

**114. Mheshimiwa Spika,** ongezeko la shughuli za kibinadamu ikiwemo usafishaji wa mashamba kwa ajili ya shughuli za kilimo, ufugaji, makazi, uwindaji haramu wa wanyamapori na uvunaji haramu wa asali umekuwa ni chanzo kikubwa cha moto ndani ya hifadhi za misitu. Uchomaji moto holela umekuwa na athari kubwa katika maeneo ya hifadhi ikiwemo kupoteza bioanuai, kuathiri ubora wa miti pamoja na upotevu wa mapato ya Serikali. Mathalan, katika kipindi cha mwaka 2021/2022 takriban hekta 3,172 ziliungua moto katika mashamba ya miti ya Sao hill, Wino na Buhigwe. Tathmini zilizofanyika zilibaini kuwa chanzo cha moto katika mashamba hayo kilikuwa ni uchomaji holela wa moto wakati wa maandalizi ya mashamba ya wananchi yaliyopakana na mashamba hayo.

**115. Mheshimiwa Spika,** katika kukabiliana na changamoto ya matukio ya moto katika maeneo ya hifadhi na mashamba ya miti, Wizara imefanya juhudi mbalimbali zikiwemo: kutoa elimu ya kuzuia moto kwa wananchi zaidi ya 13,000 katika vijiji 311; kuandaa mwongozo wa kukabiliana na moto; kukarabati minara 21 ya kufuatilia matukio ya moto na kuimarisha vikosi vya kukabiliana na matukio ya moto vyenye jumla ya watu 345. Katika hatua nyingine, Wizara imenunua mitambo maalumu yenye uwezo wa kuzima moto hadi umbali wa mita mia moja, kuimarisha njia za kuzuia moto katika hifadhi za misitu ambapo takriban mipaka yenye urefu wa kilomita 1,812 na njia za kuzuia moto zenye urefu wa kilomita 1,446 zimesafishwa. Kutokana na juhudi hizo, matukio ya moto katika mashamba ya miti ya Serikali yameendelea kupungua mwaka hadi mwaka ambapo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 sehemu ya eneo la hekta 290 za mashamba ya miti ya Serikali ziliungua na moto.

**(ii) Kuimarika kwa Kiwango cha Ubora wa Mazao ya Nyuki Yanayozalishwa Nchini**

**116. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuwanufaisha wananchi wanaoishi jirani na maeneo ya hifadhi kupitia miradi ya ufugaji nyuki. Katika kutekeleza hilo, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo inatekeleza programu za ufugaji nyuki katika mikoa mbalimbali hapa nchini kwa lengo la kuongeza uzalishaji na ubora wa mazao ya nyuki. Katika kipindi cha mwaka 2022/2023, Wizara imetoa mafunzo ya udhibiti na ubora wa mazao ya nyuki kwa maafisa ufugaji nyuki 23 kutoka katika wilaya 19. Vilevile, wananchi 1,998 na vikundi 64 vya ufugaji nyuki vilipewa mafunzo ya mbinu bora za ufugaji nyuki pamoja na kugawa mizinga 1,025 ya kufugia nyuki.

**117. Mheshimiwa Spika,** kutokana na jitihada hizo, kiwango cha uzalishaji wa asali nchini kimeongezeka kutoka tani 30,400 mwaka 2021/2022 hadi kufikia tani 31,695 mwaka 2022/2023. Katika hatua nyingine, Wizara imeendelea kukusanya sampuli za asali kutoka katika maeneo mbalimbali hapa nchini kwa lengo la kutambua ubora wa asali inayozalishwa katika maeneo hayo. Kwa mwaka 2022/2023, jumla ya sampuli 70 zilikusanywa na kupelekwa maabara nchini Ujerumani. Matokeo ya sampuli hizo yameonesha kuwa asilimia 96 ya asali hiyo imekidhi viwango vya kimataifa na hivyo kuendelea kuchochea wananchi kufuga nyuki kwa lengo la kuuza katika soko la ndani na kimataifa.

**5.5.2.2 Idara ya Misitu na Nyuki**

**118. Mheshimiwa Spika,** kwa lengo la kuweka mazingira wezeshi ya kufanya biashara ya mazao ya misitu, Wizara imefanya mapitio ya Kanuni za Usimamizi na Matumizi Endelevu ya Rasilimali za Misitu ya mwaka 2019. Kwa upande mwingine, Wizara imeandaa: Mkakati wa Kitaifa wa Mkaa; Mkakati wa Kitaifa wa Miti ya Mianzi; na Mkakati wa Kitaifa wa Kilimo Msitu. Aidha, Wizara imeandaa Mwongozo wa Uandaaji wa Mpango wa Usimamizi wa Hifadhi na Mashamba ya Nyuki; Mwongozo wa uandaaji wa Mpango wa Usimamizi katika Hifadhi za Misitu ya Asili ya Serikali Kuu na Mamlaka za Serikali za Mitaa; na Mwongozo wa Uwekezaji katika Viwanda vya Misitu.

**119. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha ushirikishwaji wa wadau katika usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za misitu na nyuki, Wizara ilifanya mikutano miwili (2) ya wadau wa Sekta ya Misitu na Ufugaji Nyuki ambapo mikakati mbalimbali ya kukabiliana na changamoto zilizopo iliandaliwa. Katika hatua nyingine, Wizara imeratibu mikutano miwili (2) ya Kamati ya Kitaifa ya Ushauri wa Misitu – NAFAC; mikutano mitatu (3) ya Kamati ya Kitaifa ya Ushauri wa Ufugaji Nyuki – NABAC; vikao vitatu (3) vya wadau wa misitu kupitia Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) pamoja na vikao viwili (2) vya Kamati Endeshi ya Mazao ya Misitu Yaliyohandisiwa.

**120. Mheshimiwa Spika,** kwa lengo la kuendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu uhifadhi wa rasilimali za misitu, Wizara imeandaa na kuchapisha nakala 2,800 za Jarida la Misitu ni Mali zilizotolewa kwa jamii ili kuwajengea uelewa kuhusu umuhimu wa uhifadhi wa rasilimali za misitu na nyuki. Pia, Wizara imeendelea na zoezi la kufanya tathmini ya mchango wa Sekta ya Misitu kwenye pato la Taifa kwa kutumia Mfumo wa Green Accounting. Katika hatua nyingine, Wizara imeshiriki Kongamano la 47 la Kimataifa la Wafugaji Nyuki (APIMONDIA) lililofanyika Uturuki mwezi Machi, 2023; Kongamano la Wafugaji Nyuki Kanda ya Afrika (Symposium) lililofanyika Afrika ya Kusini ambapo kupitia makongamano hayo, Tanzania imefanikiwa kufungua masoko mapya ya asali na nta nchini Poland na China. Kwa mantiki hiyo, nitumie fursa hii kuwahimiza Watanzania kuchangamkia fursa hii ili tuweze kuiongezea nchi yetu fedha za kigeni.

**121. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha misitu inahifadhiwa, inalindwa na kuwa endelevu kwa kizazi cha sasa na kijacho, Wizara inakamilisha maandalizi ya kuipandisha hadhi Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) kuwa Mamlaka. Kazi hii inatarajia kukamilika katika mwaka wa fedha 2023/2024.

### 5.5.2.3 Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania – TFS

**122. Mheshimiwa Spika,** jukumu la Wakala ni kusimamia, kuhifadhi na kuendeleza rasilimali za misitu na nyuki zilizo chini ya Serikali Kuu. Wakala unasimamia jumla ya hifadhi za misitu 463 inayojumuisha

misitu ya asili 416, misitu ya mazingira asilia 23, mashamba ya miti 24 na hekta 158,100 za mikoko. Vilevile, Wakala unasimamia na kuendeleza hifadhi za nyuki (14) na vituo vya malikale sita (6). Aidha, usimamizi wa hifadhi hizo hufanywa kwa kushirikiana na mamlaka nyingine za Serikali zikiwemo Serikali za Mitaa.

**123. Mheshimiwa Spika,** Wakala umezalisha jumla ya tani 14.7 za mbegu za miti na kuotesha miche 26,860,353 ya aina mbalimbali ambayo itapandwa katika mashamba 24 ya Serikali na mingine kugawiwa kwa watu binafsi, taasisi na mashirika mbalimbali kwa ajili ya kupandwa katika maeneo yao. Hadi mwezi Aprili, 2023 Wakala umepanda miti katika hekta 7,475 na kurudishia miti iliyokufa kwenye hekta 1,948.7. Vilevile, Wakala umeendeleza mashamba ya miti kwa kupalilia hekta 19,186, kupogolea hekta 8,963 na kupunguzia miti kwenye hekta 1,359. Katika hatua nyingine, Wakala umeanza kutekeleza Mkakati wa Usimamizi na Uendelezaji wa Mashamba ya Miti ya Serikali wa miaka 30 (2021 - 2050) kwa kuotesha miche 11,000 ya miti aina ya mpira (rubber) itakayopandwa kwa majaribio katika eneo la hekta nane (8) ndani ya Shamba la Miti Rondo. Kwa upande mwingine, Wakala umeanza majaribio ya upandaji wa mti aina ya Prunus africana inayotumika kutengeneza madawa ya kutibu saratani na magonjwa mengine katika mashamba ya Mbizi, Wino, Rongai, Sao Hill, Iyondo Mswima, Meru na Shume. Sambamba na hilo, Wakala umeendelea kuhifadhi maeneo ya mikoko kwa kupanda miche 70,346 kwenye eneo la hekta 31 katika delta ya Rufiji na mwambao wa Wilaya ya Kinondoni.

**124. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha kuwa rasilimali za misitu na nyuki zinasimamiwa ipasavyo, Wakala umeandaa mipango ya usimamizi wa misitu 42 yenye ukubwa wa hekta 1,031,293 ambayo ipo katika hatua mbalimbali za ukamilishwaji. Aidha, Wakala umeendesha operesheni za kiintelijensia 183 na siku doria 95,800 ambazo zililenga kukabiliana na uharibifu wa misitu. Kutokana na juhudi hizi, Wakala ulikamata na kutaifisha; magunia ya mkaa 20,027, vipande vya mbao 34,730, kuni zenye mita za ujazo 161 na magogo yenye mita za ujazo 3,359.

**125. Mheshimiwa Spika,** katika jitihada za kukabiliana na majanga ya moto kwenye hifadhi za misitu, Wakala umesafisha mipaka yenye urefu wa kilomita 1,812 na njia za kuzuia moto zenye urefu wa kilomita 1,446. Vilevile, wananchi zaidi ya 13,000 kutoka vijiji 311 walipatiwa elimu ya athari za moto na mbinu za kukabiliana na matukio ya moto. Katika hatua nyingine, vikosi vya kukabiliana na matukio ya moto vyenye jumla ya watu 345 viliimarishwa kwa kupewa mafunzo sambamba na kukarabati minara 21 ya kuangalizia moto.

**126. Mheshimiwa Spika,** kufuatia juhudi mbalimbali za kuendeleza utalii ikolojia sambamba na muendelezo wa Programu ya Tanzania the Royal Tour, Wakala umeendeleza vivutio vya utalii wa kiikolojia na kupandisha hadhi misitu mitatu (3) yenye ukubwa wa hekta 25,224 kuwa hifadhi za misitu ya mazingira asilia ya Uvinza, Matogoro Mashariki na Vilima vya Hassama. Vilevile, Wakala umeendelea kuimarisha miundombinu ya utalii katika misitu ya hifadhi kwa kukarabati kilomita 236.7 za njia za watalii na kilomita 643.54 za barabara za msituni.

**127. Mheshimiwa Spika,** Wakala umejenga malango manne (4) katika hifadhi za mazingira asilia za Matogoro, Mlima Hanang, Amani na Pugu kazimzumbwi; ofisi moja katika Hifadhi ya Ziwa Duluti na vyoo saba (7) katika Hifadhi ya Mazingira Asilia Amani, Vikindu, kituo cha Malikale cha Kolo; na kukarabati hosteli moja (1) katika hifadhi ya Mazingira Asilia Amani. Vilevile, Wakala umekarabati kambi sita (6) za watalii katika Hifadhi ya Mazingira Asilia Kilombero; kutengeneza benchi nane (8) na meza tatu (3) katika Shamba la Miti West Kilimanjaro. Pia, Wakala umeimarisha miundombinu ya vituo vya Michoro ya Miambani Kolo – Kondoa na Magofu ya Tongoni – Tanga kwa kukarabati kilomita tano (5) ya njia za kutembea kwa miguu, ujenzi wa banda moja (1) la kupumzika watalii, mageti matatu (3) na mabango nane (8). Uboreshwaji wa miundombinu hiyo umechangia kuleta hamasa katika utalii ikolojia.

**128. Mheshimiwa Spika,** Wakala umeendelea kutangaza vivutio vya utalii ikolojia, utamaduni pamoja na uhifadhi wa rasilimali za misitu kupitia matukio mbalimbali ya ndani na nje ya nchi ikiwemo: Tanga Trade Fair; West Kili Forest Tour Challenge; Bata Msituni Festival;

APIMONDIA na Mkutano wa 27 wa nchi wanachama wa mkataba wa kuhimili athari za mabadiliko ya Tabianchi (CoP27). Pia, Wakala umetengeneza na kusambaza vitabu (booklets) 1,000, vipeperushi 2,350, mabango (banner) 12, na majarida 200 yenye jumbe mbalimbali zinazohusiana na utalii ikolojia. Aidha, juhudi hizi zimechangia kuongezeka kwa idadi ya watalii waliotembelea vivutio vya kiikolojia kutoka watalii 117,330 mwezi Machi, mwaka 2021 hadi kufikia 210,987 mwezi Machi, mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 79.8.

**129. Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwingine, Wakala umeendelea kuimarisha shughuli za ufugaji nyuki kwa kutengeneza na kutundika mizinga 921 katika manzuki zilizopo kwenye mashamba ya miti Buhigwe, Makere na Silayo. Vilevile, Wakala umeendelea kusimamia mashamba ya nyuki mawili (2) ambayo ni Mwambao (Kilindi na Handeni); Kanda ya Kati (Kondoa na Manyoni); na kusimamia manzuki 182 na kuzalisha tani 10.3 za asali na kilo 588 za nta zenye thamani ya jumla ya Shilingi bilioni 1.24. Kwa upande mwingine, Wakala umetoa elimu ya ufugaji bora wa nyuki kwa wafugaji nyuki 1,998 kutoka katika vijiji 40 katika mikoa ya Manyara, Dodoma, Pwani, Simiyu, Lindi, Ruvuma, Kigoma, Tabora na Shinyanga. Katika hatua nyingine, Wakala umeanzisha shamba jipya la nyuki la Kipembawe wilayani Chunya lenye ukubwa wa hekta 20,728 na kusaidia uanzishwaji na usimamizi wa shamba la nyuki la jamii mkoani Ruvuma.

**130. Mheshimiwa Spika,** kwa lengo la kutoa elimu na kuhamasisha jamii kushiriki katika uhifadhi wa rasilimali za misitu na nyuki, Wakala uliandaa makala 57, vipindi 48 vya Misitu ni Uhai na vipindi 48 vya Tanzania ya Kijani na kurushwa katika vyombo mbalimbali vya habari nchini. Vilevile, Wakala uliandaa na kusambaza vipeperushi 3,800, majarida 160, mabango makubwa sita (6) na madogo 916 yenye jumbe mbalimbali za uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu na nyuki.

**131. Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwingine, Wakala umeendelea kuimarisha na kuendeleza mikakati ya kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi kwa kununua magari 11, mtambo

mmoja (1) na pikipiki 43. Aidha, watumishi 97 wamewezeshwa kupata mafunzo ya muda mrefu na watumishi 203 mafunzo ya muda mfupi katika vyuo mbalimbali. Vilevile, Wakala umeendelea kuimarisha ulinzi wa hifadhi za misitu kwa kutoa mafunzo ya utayari kwa askari 289; mafunzo ya uongozi kwa maafisa 47. Kwa upande mwingine, Wakala umekamilisha ujenzi wa ofisi ya kanda ya kati na ujenzi wa vituo viwili (2) vya askari katika mashamba ya miti ya Kiwira na Kawetire. Kwa hatua nyingine, ujenzi wa majengo sita (6) ya ofisi; vituo vya askari sita (6); na maghala nane (8) ya kuhifadhia silaha unaendelea.

### 5.5.2.4 Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania – TAFORI

**132. Mheshimiwa Spika,** Taasisi ina jukumu la kufanya, kuratibu utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu katika nyanja za misitu na ufugaji nyuki. Katika kutekeleza majukumu yake, Taasisi imefanya tathmini ya rasilimali za misitu kutoka kwenye mashamba ya Serikali na watu binafsi kwa kutumia masalia ya mazao ya misitu kwa lengo la kuongeza tija katika viwanda vya mazao ya misitu. Matokeo ya tathmini hiyo yamebaini uwepo wa jumla ya viwanda vya misitu 592 katika mikoa ya Iringa, Njombe, Mbeya, Songwe na Rukwa. Viwanda hivyo vimegawanyika katika makundi saba (7) ikiwemo viwanda vya kuchakata mbao 555; viwanda 17 vya kutibu nguzo; viwanda 17 vya uhandisi wa mazao ya misitu (veneer, plywood and marine boards); kiwanda kimoja (1) cha tetefya na karatasi; viwanda viwili (2) vya mkaa mbadala; kiwanda kimoja (1) cha kuzalisha umeme kwa kutumia mabaki ya mazao ya misitu; na kiwanda kimoja (1) cha miwati. Takriban asilimia 95 ya viwanda vilivyopo vinapata malighafi kutoka katika mashamba ya miti ya Serikali Kuu. Aidha, tathmini imebaini kuwa takriban hekta 207,320 za mashamba ya miti zinapatikana katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ambapo takriban asilimia 74 ya miti iliyopo katika mashamba hayo ni miti jamii ya misindano.

**133. Mheshimiwa Spika,** tafiti zinaonesha kuwa mahitaji ya malighafi kwa viwanda vya misitu vilivyopo nchini ni takriban mita za ujazo 4,446,526 kwa mwaka na kiasi kinachopatikana kwa mwaka ni mita za ujazo 1,495,519 sawa na asilimia 34 ya mahitaji. Tathmini hii inaonesha kuwa viwanda vingi vinafanya kazi chini ya uwezo

kutokana na kukosekana kwa upatikanaji wa malighafi ya kutosha. Aidha, hali hii inachochea na kuhamasisha uwekezaji zaidi katika kuanzisha mashamba mapya ya miti. Hivyo, nitumie nafasi hii kuziomba taasisi mbalimbali za Serikali na sekta binafsi kuwekeza kwenye kuanzisha mashamba mapya ya miti hasa ile yenye uhitaji mkubwa kwenye viwanda vyetu.

**134. Mheshimiwa Spika,** kwa lengo la kuhakikisha kuwa jamii inapata taarifa za tafiti za misitu na ufugaji nyuki, Taasisi imefanya maboresho ya mfumo wa kielektroniki wa taarifa za usimamizi wa misitu na ufugaji nyuki. Mfumo huu unatumika kuhifadhi taarifa za miradi na programu za utafiti wa misitu na ufugaji nyuki zilizofanyika nchini. Aidha, kwa sasa taarifa za miradi mbalimbali zimekusanywa na kuhifadhiwa kwenye mfumo huo. Kazi inayoendelea ni kuunganisha mfumo huu na mifumo mingine inayofanya kazi zinazoendana kutoka katika taasisi nyingine za Serikali.

**135. Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwingine, Taasisi imefanya tathmini ya idadi ya miti, hali ya masoko na mchango wa aina tatu (3) za miti ya Mkurungu (Pterocarpus tinctorius), Msekeseke (Swartzia madagascariensis) na Msandali (Osyris lanceolata) ambayo iko hatarini kutoweka lakini ina mchango mkubwa kibiashara. Matokeo yameonesha kuwa miti hii imesambaa katika eneo kubwa hapa nchini ikipatikana zaidi katika misitu iliyohifadhiwa na kiwango cha upatikanaji kinatofautiana kati ya aina moja ya mti na nyingine. Aidha, mti wa mkurungu unapatikana kwa wastani wa mashina 25 kwa hekta hususan katika mikoa ya Tabora, Katavi, Kigoma na Songwe, Msekeseke kwa wastani wa mashina 17 kwa hekta hususan katika mikoa ya Lindi, Ruvuma, Katavi na Kigoma na Msandali kwa wastani wa mashina 33 kwa hekta hususan kwa mikoa ya Dodoma, Manyara, Arusha, Tanga na Iringa. Pia, tathmini imeonesha kuwa mahitaji ya miti jamii ya Mkurungu kwenye soko la Kimataifa kwa mwaka ni takriban mita za ujazo 188,440 zenye thamani ya Shilingi bilioni 65.9 ila Tanzania inachangia asilimia 7.4 tu (mita za ujazo 13,883) kwenye soko hilo. Kwa upande mwingine, imebainika kuwa miti hii ina soko kubwa nje ya nchi hususan China ingawa hilo soko linaathiriwa na kiwango kidogo cha upatikanaji wake. Katika kuhakikisha upatikanaji endelevu wa miti ya aina hii, Taasisi

inaendelea na utafiti wa namna ya kuzalisha vipando vya miti aina ya Mkurungu, Msekeseke na Msandali na kuhamasisha iweze kupandwa kibiashara.

**136. Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha kuwa rasilimali za nyuki zinatumika na kuendelezwa ipasavyo, Taasisi imefanya utafiti kwa lengo la kutatua changamoto zinazoikabili Sekta ya Ufugaji Nyuki. Utafiti huu unafanyika kwa awamu mbili (2) ambapo katika awamu ya kwanza utafiti umefanyika katika mikoa ya Dodoma, Geita, Iringa, Kagera, Katavi, Kigoma, Kilimanjaro, Lindi, Mbeya, Morogoro, Mtwara, Njombe, Pwani, Ruvuma, Simiyu, Singida, Songwe, Tabora na Tanga. Matokeo ya awali yanaonesha kuwa asilimia 46.6 ya wafugaji nyuki bado wanatumia mizinga ya jadi na pia uzalishaji wa asali unatofautiana kati ya eneo moja na lingine. Hata hivyo, asali inayozalishwa kutoka kwenye mzinga ya jadi inaweza kuwa na ubora mdogo ikilinganishwa na ile inayozalishwa kwenye mizinga ya kisasa. Hivyo, Taasisi bado inaendelea na utafiti kuhusu aina na ukubwa wa mizinga inayofaa kwa kila ukanda ikiwemo kuona namna bora ya kuboresha mizinga ili iweze kuzalisha asali bora itakayokubalika katika masoko ya kimataifa.

**137. Mheshimiwa Spika**, utafiti umebaini kuwa kiwango kidogo cha uzalishaji wa asali kwa mzinga kinasababishwa na ukataji wa miti kwa ajili ya shughuli za kilimo; kuingiza mifugo kwenye maeneo ya kufugia nyuki; kutokuwa na wataalam wa kutosha wa kutoa elimu ya ufugaji nyuki hasa kwenye Halmashauri za Wilaya; uwepo wa visumbufu vya nyuki na uharibifu wa mizinga.

**138. Mheshimiwa Spika**, kwa upande mwingine, Taasisi imeendelea kutekeleza Mpango Mkakati wa Kitaifa wa Kudhibiti Viumbe Vamizi. Katika kutekeleza hilo, Taasisi imefanya tafiti katika mikoa ya kaskazini na kubaini uwepo wa aina 10 ya mimea vamizi yenye athari kimazingira na kiuchumi. Matokeo ya tafiti yanaonesha uwepo wa mmea vamizi aina ya Mrashia (Prosopis juliflora) katika maeneo kame ya mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Tanga. Pamoja na madhara mengine ya kimazingira, aina hii ya mmea inapunguza na kuharibu nyanda za malisho na kufyonza maji mengi ardhini (takriban lita 36 kwa mti kwa siku), hivyo kupunguza thamani ya ardhi kwa ajili ya

shughuli za kiuchumi hasa ufugaji na kilimo. Katika kudhibiti ueneaji wa mmea huo, Taasisi imetoa elimu kwa wananchi wa wilaya za Longido, Ngorongoro na Monduli. Vilevile, Taasisi imeanzisha mashamba darasa mawili (2) kwenye kijiji cha Mawasiliano, Wilaya ya Siha; na Kijiji cha Tingatinga, Wilaya ya Longido kwa lengo la kufundisha namna bora ya kuongoa ardhi kwa kutumia mimea ya asili.

**139. Mheshimiwa Spika**, Taasisi imefanya utafiti kuhusu faida na athari za biashara ya zao la utomvu litokanalo na miti aina ya misindano. Matokeo ya awali yameonesha kuwa ugemaji wa utomvu hufanyika hasa kwenye Shamba la Miti Sao Hill; mashamba ya miti ya Kampuni ya Green Resources; na mashamba ya miti ya watu binafsi katika wilaya za Kilolo, Mufindi, Njombe, Wanging'ombe na Makete. Kwa upande mwingine, ugemaji wa utomvu hufanyika katika wilaya za Geita, Sengerema na Bukoba. Vilevile, utafiti umebaini kuwa biashara ya utomvu huchangia mapato kwenye Taasisi za Serikali na Sekta binafsi. Mathalan, kwa kipindi cha miaka minne (2017/2018 hadi 2020/2021) Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania ulikusanya takriban Shilingi bilioni 2.4 na halmashauri za wilaya za Mufindi na Mafinga Mji zilikusanya Shilingi milioni 112; na mwaka 2020/2021 Kampuni ya Green resources ilipata kiasi cha Shilingi milioni 230. Pamoja na faida inayopatikana, Taasisi imebaini kuwa, ugemaji wa utomvu una athari katika ukuaji na ubora wa miti kwa asilimia 16. Hivyo, umri sahihi wa miti inayofaa kugemwa utomvu ni kuanzia miaka 18. Kutokana na uwepo wa mahitaji ya utomvu hasa kwenye soko la kimataifa, wadau mbalimbali wanashauriwa kuanzisha mashamba ya miti ya misindano itakayotumika kwa ajili ya kuzalisha utomvu.

### 5.5.2.5 Mfuko wa Misitu Tanzania – TaFF

**140. Mheshimiwa Spika**, Mfuko una jukumu la kuwezesha shughuli za uhifadhi, usimamizi na uendelezaji wa rasilimali misitu. Katika kutekeleza jukumu hilo, Mfuko umetoa ruzuku kwa miradi 149 yenye thamani ya Shilingi 1,215,000,000 inayoendelea na miradi mipya 137 yenye thamani ya Shilingi 1,718,375,000 ya uanzishaji wa vitalu vya miti na upandaji miti shuleni, uanzishwaji wa mashamba ya miti na kuboresha uhifadhi kupitia ufugaji nyuki. Miradi hiyo imetekelezwa

katika wilaya 75 za mikoa 24. Aidha, Mfuko umewezesha TAFORI kufanya na kuratibu tafiti sita (6) za kimkakati zenye lengo la kuendeleza sekta za Misitu na Ufugaji Nyuki. Kwa upande mwingine, Mfuko umenunua magari matatu (3) yanayotumika kwa ajili ya kuimarisha ulinzi katika maeneo ya hifadhi za misitu pamoja na kuboresha ukusanyaji wa maduhuli ya misitu.

**141. Mheshimiwa Spika**, Mfuko umegharamia mapitio ya Sheria ya Misitu Sura 323 na Kanuni za utoaji wa ruzuku kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi wake. Mapitio hayo yamejumuisha kuongeza majukumu ya ufugaji nyuki ili kuendelea kuboresha sekta ya ufugaji nyuki. Kwa upande mwingine, Mfuko umegharamia vikao vitatu (3) vya Kamati ya Kitaifa ya Ushauri ya Misitu (NAFAC), vikao vitatu (3) vya Kamati ya Kitaifa ya Ushauri ya Ufugaji Nyuki (NABAC) na vikao viwili (2) vya Kamati Endeshi ya Mazao ya Misitu yaliyohandisiwa. Aidha, Mfuko umeendelea kuwezesha elimu ya uhifadhi, usimamizi, uendelezaji na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu kwa kugharamia uandaaji na urushaji wa vipindi 40 vya redio kupitia kipindi cha Misitu ni Uhai kinachorushwa kupitia kituo cha TBC Taifa. Vilevile, Mfuko umefanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa jumla ya miradi 209 kwa lengo la kuhakikisha kuwa miradi inatekelezwa kwa ufanisi.

### 5.5.2.6 Vyuo vya Taaluma ya Misitu na Nyuki

**142. Mheshimiwa Spika**, Vyuo vya taaluma ya misitu na nyuki vinajumuisha Chuo cha Misitu Olmotonyi; Chuo cha Viwanda vya Misitu; na Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki. Vyuo hivi vimepewa jukumu la kutoa mafunzo ya uhifadhi, usimamizi na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu na nyuki katika ngazi ya Astashahada na Stashahada. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Chuo cha Viwanda vya Misitu kimedahili wanafunzi 319 pamoja na kutoa mafunzo kwa mafundi seremala 56 kutoka katika vijiji vitano (5) vya wilaya za Tunduru na Namtumbo kuhusu namna ya kuanzisha karakana ya mafundi seremala. Vilevile, Chuo kimetoa ushauri elekezi wa namna ya matumizi ya teknolojia mpya ya matumizi ya mashine za kuchakata magogo zijulikanazo kama Slidetech na Norwood ambapo wataalam kutoka kampuni ya New Forest, Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine na Chuo cha Misitu Olmotonyi walishiriki.

Sambamba na hilo, Chuo kimetengeneza samani mbalimbali za maofisini kwa ajili ya Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori (MWEKA) na Chuo cha Misitu Olmotonyi.

**143. Mheshimiwa Spika**, Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki kimedahili wanafunzi 394 na kufanya mapitio ya mtaala wa mafunzo ya ufugaji nyuki kwa ngazi ya Astashahada na Stashahada. Aidha, Chuo kimetoa mafunzo ya mbinu bora za ufugaji nyuki kwa maafisa ufugaji nyuki 24 kutoka katika wilaya 19 za Tanzania Bara na Zanzibar. Vilevile, Chuo kimezalisha asali kutoka katika manzuki zake zilizopo wilayani Sikonge ambapo asali hiyo ilishindanishwa katika Kongamano la Ufugaji Nyuki Kanda ya Afrika lililofanyika jijini Durban nchini Afrika ya Kusini ambapo asali hiyo ilishika nafasi ya pili kwa ubora Barani Afrika. Kwa upande mwingine, Chuo cha Mafunzo ya Misitu Olmotonyi kimedahili wanafunzi 880 wa ngazi ya Astashahada na Stashahada; kutoa mafunzo ya kuanzisha vitalu vya miti, kuotesha na kukuza miche ya miti kwa wananchi wa vijiji vya Terat, Mkono, Dosoito, Kwaugulu na Mikandiri vilivyoko wilaya ya Arumeru; na kukuza miche 50,000 ya miti aina ya Pinus, Casuarina, Cypress na Grevillea ambapo miche 32,776 imeoteshwa katika Shamba la Miti la Chuo. Vilevile, chuo kimewezesha wakufunzi tisa (9) kupata mafunzo ya kuandaa vipindi na kufundisha kwa njia ya masafa.

### 5.5.3 Sekta ya Utalii

**144. Mheshimiwa Spika**, Sekta ya Utalii ina jukumu la kusimamia, kuendeleza na kutangaza utalii ndani na nje ya nchi. Utekelezaji wa jukumu hilo unaongozwa na Sera ya Taifa ya Utalii ya mwaka 1999, Sheria ya Utalii Na. 29 ya mwaka 2008 na Sheria ya Bodi ya Utalii Tanzania Sura 364. Aidha, jukumu hilo hutekelezwa kupitia Idara ya Utalii, Bodi ya Utalii Tanzania na Wakala wa Chuo cha Taifa cha Utalii.

### 5.5.3.1 Masuala Mahsusi katika Sekta ya Utalii

### Uendelezaji wa Programu ya Tanzania - the Royal Tour katika Kutangaza Utalii

**145. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kutangaza utalii kwa kutumia mikakati mbalimbali ikiwemo kuisambaza filamu ya Tanzania - the Royal Tour ambayo imesikika, imetazamwa na kufuatiliwa na watu takriban bilioni 1.2 duniani ikijumuisha masoko ya kimkakati ya Marekani, Ufaransa, Uingereza, Italia na China. Mikakati inayoendelea kutekelezwa ni pamoja na kutangaza utalii na fursa za uwekezaji kupitia Kituo cha Utangazaji Utalii Kidijitali - Digital Marketing Command Centre (DMCC); ziara za mafunzo (FAM Trips); misafara ya utangazaji utalii (Roadshows); kutangaza utalii kwa kulipia makala na filamu za Tanzania katika mashirika ya ndege; kurusha maudhui ya filamu hizo katika vyombo vya habari, mitandao ya kijamii, matukio na maonesho mbalimbali ya utalii kitaifa na kimataifa na mashirika ya ndege. Sambamba na hilo, kauli mbiu ya Tanzania Unforgettable itaendelea kutangazwa katika ligi kubwa za michezo Marekani, Uingereza na Hispania.

**146. Mheshimiwa Spika,** uendelezaji wa Programu hii, umewezesha kuleta matokeo chanya kwa kuongeza idadi ya watalii wanaotembelea nchini. Mathalan, idadi ya watalii imeongezeka kutoka 922,692 mwaka 2021 hadi kufikia 1,454,920 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asimilia 57.7 na mapato yatokanayo na watalii yameongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 1,310 mwaka 2021 hadi kufikia Dola za Marekani Milioni 2,527.72 kwa mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 93. Vilevile, idadi ya watalii wa ndani katika robo ya kwanza ya mwaka 2023 imeongezeka hadi kufikia watalii 409,092 sawa na ongezeko la asilimia 41.4 ikilinganishwa na watalii 289,372 katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2022.

**147. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2022/2023 jumla ya watalii 2,020 wamewasili nchini kupitia usafiri wa meli (Cruise Ship) kutoka masoko ya utalii yakiwemo Marekani, Ufaransa, Uholanzi, Italia, Brazil na Afrika Kusini. Aidha, watalii 107 walikuja nchini kwa njia ya treni maarufu ya kitalii ijulikanayo kwa jina la Rovos kutoka mji wa

Cape Town nchini Afrika ya Kusini hadi jijini Dar es Salaam. Sambamba na hilo, mawakala wa utalii zaidi ya 65 kutoka nchi za China, Mexico, Marekani, Argentina, Brazil, Ureno, Ubelgiji, Ufaransa na Canada wametembelea nchini ili kujifunza na kujionea vivutio mbalimbali vya utalii kwa lengo la kuvitangaza katika nchi zao. Kwa upande mwingine, uwekezaji katika sekta ya utalii umeongezeka kutoka miradi 16 mwaka 2020 hadi kufikia 26 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 62.5.

**5.5.3.2 Idara ya Utalii**

**148. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuboresha mazingira ya biashara za utalii nchini ili kuvutia uwekezaji. Hatua hii imewezesha ongezeko la idadi ya wakala wa biashara za utalii kutoka 2,051 mwaka 2020/2021 hadi 2,950 mwaka 2022/2023 sawa na ongezeko la asilimia 43.8. Kwa upande mwingine, Wizara imeendelea kuboresha na kuimarisha mfumo wa kielektroniki wa MNRT Portal ili kusimamia vema ukusanyaji wa maduhuli yatokanayo na shughuli za utalii nchini. Mathalan, katika kutekeleza hilo, Wizara imefanya kaguzi za wakala wa biashara za utalii katika mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Dodoma na kwenye malango ya kuingilia wageni katika hifadhi za Taifa za Manyara, Mikumi, Tarangire, Ruaha pamoja na Mamlaka ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro ambapo jumla ya Shilingi bilioni 1.01 zimekusanywa kutokana na kaguzi hizo.

**149. Mheshimiwa Spika,** katika kuendeleza mazao ya utalii ya kimkakati, Wizara imeendelea kushirikiana na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi pamoja na Mamlaka ya Bandari Tanzania katika maandalizi ya ujenzi wa miundombinu ya utalii wa meli (Cruiseship Terminal) kwenye Bandari kuu ya Dar es Salaam. Ujenzi huo utajumuisha gati la kupokea meli za kitalii pamoja na jengo la kupokea wageni.

**150. Mheshimiwa Spika,** katika jitihada za kuongeza wigo wa mazao mengine ya utalii, Wizara imeendelea kubaini vivutio vya utalii katika mikoa ya Iringa na Njombe. Hatua hiyo inalenga kuongeza na kuibua mazao ya utalii ambayo ni pamoja na historia na malikale; utalii wa jiolojia; utalii wa utamaduni; utalii wa ikolojia na utalii wa nyuki; pamoja na utalii wa kilimo ikiwemo maua na viungo. Sambamba na

hilo, Wizara imeendelea kuimarisha ushirikiano na wadau wa utalii nchini ambapo katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara ilifanya vikao viwili (2) Jijini Arusha. Vikao hivyo vilihusisha wadau wa Sekta za Umma na Binafsi kupitia vyama mbalimbali vya wadau wa Sekta ya Utalii vikiwemo TCT, TATO, HAT, TLTO, TTGA na TPSF. Vikao hivyo pamoja na mambo mengine, vimesaidia kujadili fursa za uwekezaji, uendelezaji na utangazaji utalii pamoja na utatuzi wa changamoto mbalimbali zinazoikabili sekta ya utalii nchini.

**5.5.3.3 Bodi ya Utalii Tanzania – TTB**

**151. Mheshimiwa Spika,** Bodi ina jukumu la kutangaza utalii wa Tanzania ndani na nje ya nchi. Katika kutekeleza jukumu hilo, Bodi imeratibu ushiriki wa Tanzania katika maonesho mbalimbali ya kitaifa, kikanda na kimataifa, maonesho hayo ni pamoja na: TOPRESA nchini Ufaransa; East Africa Regional Tourism Expo – (EARTE) nchini Burundi; Magical Kenya nchini Kenya; World Travel Market – (WTM) nchini Uingereza; International Tourism & Travel Show (IMTM) nchini Canada; FITUR nchini Hispania; Matka Nordic Travel Fair nchini Finland; Malawi International Tourism Expo nchini Malawi; Pearl of Africa Tourism Expo nchini Uganda; na Tourism Expo nchini Japan. Sambamba na hilo, Wizara imeshiriki misafara ya utangazaji utalii maarufu kwa jina la My Tanzania Roadshow katika miji ya Warsaw na Krakow - Poland, Budapest-Hungary, Prague-Czech, FrankfurtUjerumani, Amsterdam-Uholanzi, Brussels-Ubelgiji na Paris-Ufaransa. Aidha, Bodi imeendelea kutangaza vivutio vya utalii kupitia matukio yanayoangaliwa na kufuatiliwa na watu wengi Duniani hususan FIFA World Cup Qatar 2022. Kwa ujumla juhudi hizi zimechangia katika kuongezeka kwa idadi ya watalii na wakala wakubwa wa utalii wanaotembelea nchini.

**152. Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwingine Bodi imeandaa Onesho la Sita la Kimataifa la Utalii Swahili International Tourism Expo – S!TE, 2022 lililofanyika tarehe 21 hadi 23 Oktoba, 2022 Jijini Dar es Salaam. Katika onesho hilo, wanunuzi wa huduma za utalii wa kimataifa 43 walishiriki kutoka nchi 15 za kimkakati zikiwemo Marekani, Afrika Kusini, Ufaransa, Brazil, Israel, Urusi, Poland, Jamhuri ya watu wa Czech, Japan, Bulgaria, Oman, Nchi za Umoja za Falme za Kiarabu, Uholanzi, Hispania, India, Sweden na Slovakia. Aidha, waoneshaji 77

kutoka kampuni mbalimbali za utalii pamoja na wageni zaidi ya 800 walihudhuria onesho hilo. Katika hatua nyingine, onesho hilo lilijumuisha ziara za mafunzo za wakala wa utalii hao kwenye maeneo ya utalii yafuatayo: Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro na Hifadhi za Taifa za: Serengeti, Mkomazi, Nyerere, Ruaha, Milima ya Udzungwa na Mikumi. Vilevile, wakala hao walitembelea eneo la Kilwa Kisiwani, Kituo cha utalii wa utamaduni Mto wa Mbu na vivutio vya utalii vilivyopo mikoa ya Iringa na Kilimanjaro kwa lengo la kujifunza na kujionea vivutio mbalimbali vya utalii ili kuvitangaza katika nchi zao.

**153. Mheshimiwa Spika,** Bodi imeendelea kushirikiana na Balozi za Tanzania zilizopo katika nchi mbalimbali kuratibu maonesho ya kimataifa na misafara ya utalii pamoja na kutoa nyenzo za utangazaji na filamu zenye maudhui ya Utalii. Nchi hizo ni pamoja na Uingereza, Japani, Canada, Ufaransa, Hispania, Qatar, Marekani, Afrika Kusini, China, Ujerumani, Saudi Arabia, Israel, Sweden, India, Uganda na Burundi. Vilevile, Wizara inaendelea kutumia mabalozi wa Hiari wa Utalii na watu mashuhuri katika kutangaza vivutio vya utalii kupitia matukio mbalimbali kwa lengo la kuongeza idadi ya watalii.

**154. Mheshimiwa Spika,** Bodi imeendelea kuhamasisha utalii wa ndani kwa kutekeleza mikakati mbalimbali ya kutangaza utalii ikiwemo kutoa elimu ya utalii kwa wanafunzi, kushiriki matamasha na matukio, kufanya ziara za mafunzo kwa wadau mbalimbali na kutumia vyombo vya habari. Kupitia juhudi hizo, Bodi imeratibu ziara ya mafunzo kwa waandishi wa habari 12 kutoka vyombo mbalimbali vya habari nchini. Waandishi hao walitembelea vivutio vilivyopo kusini mwa Tanzania ikiwemo Hifadhi ya Taifa Kitulo, Ziwa Nyasa, mapori ya akiba ya Mpanga Kipengere na Liparamba pamoja na vituo vya Zana za Mawe Isimila na Magofu ya Kilwa. Ziara hiyo imesaidia kutengeneza vipindi 16 vya televisheni, 10 vya redio, 88 vya blogu na makala za magazeti 13 zenye maudhui ya kutambulisha vivutio vilivyopo katika maeneo hayo. Katika hatua nyingine, Bodi imeendelea kuratibu na kushiriki maonesho, matamasha na matukio mbalimbali yakiwemo: Maonesho ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (Sabasaba); Nanenane; Karibu Kusini; Tamasha la Kumbukizi ya Vita ya Majimaji; Zanzibar Tourism Summit; East Africa Trade Fair; Kilimanjaro Marathon (Moshi-Kilimanjaro), Serengeti Safari Marathon,

Burigi Utalii Marathon, Arusha Wildlife Marathon na Mwalimu Nyerere Marathon.

**5.5.3.4 Wakala wa Chuo cha Taifa cha Utalii – NCT**

**155. Mheshimiwa Spika**, Chuo kina jukumu la kutoa mafunzo katika fani ya utalii, ukarimu na uratibu wa matukio katika ngazi ya Astashahada na Stashahada; kutoa ushauri wa kitalaam; na kufanya tafiti katika fani hizo. Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Chuo kimedahili jumla ya wanafunzi 1,045 katika ngazi ya Astashahada na Stashahada. Aidha, Chuo kimetoa mafunzo kwa wadau katika mnyororo wa utalii ambapo maafisa uhamiaji 412 walishiriki mafunzo hayo. Katika hatua nyingine, Chuo kupitia Mradi wa Ajira kwa Vijana unaosimamiwa na Forum for International Cooperation (FIC) kimetoa mafunzo ya muda mfupi ya Uanagenzi (Modular Apprenticeship) kwa washiriki 150. Vilevile, Chuo kupitia Mradi wa Education and Skills for Productive Jobs (ESPJ) kimetoa mafunzo ya utarajali kwa wahitimu 1,000 kutoka NCT na VETA katika fani za Utalii na Ukarimu.

**156. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha kuwa mafunzo yanayotolewa yanakidhi vigezo vya kitaifa na kimataifa, Chuo kimeingia makubaliano ya kujengeana uwezo na kuimarisha mafunzo na Chuo Kikuu cha Teknolojia cha Tshwane nchini Afrika Kusini. Chuo hicho kimebobea katika utoaji wa mafunzo kwa vitendo kwenye fani za Utalii na Ukarimu. Vilevile, Chuo kimesaini Hati ya Makubaliano (MoU) na Chuo cha Bahari cha Dar es Salaam (DMI) kwa lengo la kuongeza wigo wa ajira kwa wahitimu kutoka NCT katika meli za kitalii zinazosafirisha watalii Duniani. Kwa upande mwingine, Chuo kimefanya kongamano la Pili la Kimataifa lililofanyika mwezi Oktoba, 2022 Jijini Dar es Salaam ambapo wadau mbalimbali wakiwemo wanataaluma katika Sekta ya Utalii na ukarimu kutoka nchi zinazoendelea walishiriki. Lengo la kongamano hilo lilikuwa ni kujadili Mkakati wa Ustahimilivu wa Athari za UVIKO-19 na Urejeshaji wa Biashara za Utalii katika nchi zinazoendelea. Katika kutanua wigo wa utoaji wa huduma za mafunzo, Chuo kimepata eneo la ekari 26 kwa ajili ya ujenzi wa Kampasi mpya mkoani Njombe.

### 5.5.4 Sekta ya Mambo ya Kale

**157. Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Mambo ya Kale ina jukumu la kusimamia uhifadhi, kutafiti na kuendeleza rasilimali za malikale. Utekelezaji wa jukumu hilo unazingatia Sera ya Malikale ya mwaka 2008; Sheria ya Mambo ya Kale Sura 333 na Sheria ya Makumbusho ya Taifa Sura 281. Sekta ya Mambo ya Kale inajumuisha Idara ya Mambo ya Kale na Shirika la Makumbusho ya Taifa.

#### 5.5.4.1 Masuala Mahsusi katika Sekta ya Mambo ya Kale Kufungua Fursa za Utalii wa Malikale katika Ukanda wa Pwani na Kusini-Mashariki mwa Tanzania

**158. Mheshimiwa Spika,** katika kuendelea kukuza utalii wa malikale, Wizara imeandaa mkakati wa kufungua na kutangaza fursa za utalii zilizopo Ukanda wa Pwani na Kusini-Mashariki mwa Tanzania katika maeneo ya malikale. Mkakati huu unalenga kuhamasisha utalii wa malikale, kuainisha fursa za kiuchumi zilizopo na kutoa elimu ya uhifadhi endelevu kwa jamii pasipo kuharibu ama kuondoa uhalisia wa majenzi ya kale na masalia ya akiolojia na paleontolojia yaliyopo chini ya ardhi katika maeneo hayo. Katika kutekeleza mkakati huo, Wizara imefanya ukarabati wa majenzi ya kale 33 yakiwemo: gereza na gati la kale – Mikindani – Mtwara; mnara wa kale – Lindi; visima vya kale vitatu (3), msikiti mmoja (1) na makaburi 26 yaliyopo Mbuamaji na Kimbiji –Kigamboni, Dar es Salaam.

**159. Mheshimiwa Spika,** sambamba na hilo, Wizara imeingia makubaliano na Mfuko wa Malikale Duniani (World Heritage Monument Fund) kwa ajili ya ukarabati wa majenzi ya kale yaliyopo Kisiwa cha Kua, Mafia. Vilevile, Wizara, imeshirikisha wadau mbalimbali kupitia vikao, warsha, makongamano na semina kuhusu uhifadhi, usimamizi na uendelezaji wa malikale katika maeneo ya Tendaguru - Lindi, mji Mkongwe Mikindani-Mtwara na Mafia-Pwani. Pia, Wizara imefungua maonesho mawili (2) ya Dinasoria mkoani Lindi; kujenga Kituo cha Makumbusho ya ukombozi wa nchi zilizo kusini mwa Bara la Afrika kilichopo Lindi Mjini; Kituo cha Taarifa na Makumbusho ya Historia ya Miji ya Kale Kigamboni; na Kituo cha Makumbusho ya Dinasoria – Lindi. Juhudi hizi zitaendelea kufungua

fursa za uhifadhi na utalii wa malikale katika Ukanda wa Pwani na Kusini-Mashariki mwa Tanzania.

### 5.5.4.2 Idara ya Mambo ya Kale

**160. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2022/2023 Wizara imefanya tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Malikale ya mwaka 2008; kufanya mapitio ya Sheria ya Mambo ya Kale Sura 333 na Sheria ya Makumbusho ya Taifa Sura 281 kwa lengo la kuhamisha majukumu ya kiutendaji kutoka Idara ya Mambo ya Kale kwenda Shirika la Makumbusho ya Taifa. Vilevile, Mpango wa Miaka mitano wa Usimamizi wa Mji Mkongwe wa Mikindani (Mikindani Heritage Management Plan 2022/2023 -2026/2027) na Mpango wa Usimamizi wa Hifadhi ya Paleontolojia Tendaguru (Tendaguru Palaentological Site Management Plan) imeandaliwa. Aidha, Wizara imeratibu tafiti tisa (9) za akiolojia na paleontolojia ili kuibua maeneo mapya ya malikale katika kanda za Kaskazini (Olduvai, Engaresero, Mumba); Kanda ya Kati (Kondoa, Singida na Tabora); Kanda ya Ziwa (Butiama); na Kanda ya Pwani (Kilwa).

**161. Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwingine, Wizara imefanya ufuatiliaji wa hali ya uhifadhi katika vituo na maeneo sita (6) ya malikale na kubaini yanakidhi vigezo vya kuwa Urithi wa Taifa. Maeneo hayo ni: Handaki la Mireshe lililopo Chuo cha Mafunzo ya Wanyamapori Mweka – Kilimanjaro; eneo la Lugalo, eneo la kihistoria Kikongoma, mapango ya Mlambalasi, Pango la Magubike na michoro ya miambani Igeleke – Iringa ambapo taratibu za kuyatangaza kwenye Gazeti la Serikali zinaendelea. Aidha, Wizara imefanya tathmini ya vivutio na mazao ya utalii katika njia ya kati ya biashara ya utumwa na vipusa kutoka Ujiji hadi Bagamoyo ambapo vituo 14 vyenye vivutio 112 vya kihistoria na asili vimebainishwa ili kukuza utalii katika maeneo ya Zanzibar, Bagamoyo, Manispaa ya Morogoro, Rubeho, Mamboya, Mpwapwa, Kongwa, Dodoma, Kondoa, Kilimatinde, Manispaa ya Tabora, Ulyankulu na Ujiji-Kigoma.

**162. Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyingine Wizara imekamilisha upimaji wa maeneo manne (4) ya malikale kwa lengo la kupunguza migogoro, kutambua mipaka na kuimarisha uhifadhi katika eneo la

Isimila Iringa, Magofu ya Kaole–Bagamoyo, Magofu ya Tongoni-Tanga na Makumbusho ya Dkt. David Livingstone Ujiji-Kigoma. Sambamba na hilo, Wizara imekamilisha ukusanyaji wa mahitaji ya ujenzi wa mfumo wa kidijitali ili kurahisisha mchakato wa utoaji wa leseni za kufanya tafiti za kisayansi, utafutaji tunu na filamu katika maeneo ya malikale nchini.

#### 5.5.4.3 Shirika la Makumbusho ya Taifa – NMT

**163. Mheshimiwa Spika,** Shirika lina jukumu ya kukusanya, kuhifadhi, kutafiti na kutoa elimu kwa umma kuhusu mikusanyo ya kisayansi na kiutamaduni yenye hadhi ya urithi wa Taifa. Aidha, Shirika linasimamia na kuendeleza vituo vya Makumbusho saba (7) na maeneo 91 ya malikale yaliyopo katika maeneo mbalimbali nchini. Vilevile, katika kuimarisha utekelezaji wa shughuli za Makumbusho, Shirika limejenga maonesho ya kudumu tisa (9) na kuboresha matano (5) yakiwemo Onesho la Dinasoria, Lindi; Onesho la Reptilia katika Makumbusho ya Elimu Viumbe Arusha; Onesho la Mwl. Nyerere; Onesho la Mila za Wazanaki katika Makumbusho ya Mwl. Nyerere, Butiama; na Onesho la Kumbukizi ya Vita vya Majimaji Songea. Sambamba na hilo, Shirika limeboresha miundombinu ya kuvutia watalii ikiwemo kujenga mabanda ya maduka ya zawadi katika Makumbusho ya Majimaji; na Onesho la Historia ya Tanzania kabla na baada ya Uhuru katika Makumbusho ya Azimio la Arusha.

**164. Mheshimiwa Spika,** Shirika limeendelea kutangaza vivutio vya urithi wa kiutamaduni na kuhamasisha utalii wa ndani kidijitali kupitia maudhui 97 kwenye mitandao ya kijamii, vipindi vya televisheni 112, vipindi vya radio 70 na matamasha 14. Matamasha hayo ni pamoja na Tamasha la Utamaduni wa Mtanzania katika Kijiji cha Makumbusho lililoshirikisha jamii ya Wasafwa; Tamasha la Majimaji lililoanzia Nandete, Kilwa mkoani Lindi na kuhitimishwa Songea mkoani Ruvuma; Tamasha la malezi ya watoto kiutamaduni; na Tamasha la Watoto wenye mahitaji maalum yaliyofanyika Kijiji cha Makumbusho Dar es Salaam.

**165. Mheshimiwa Spika,** Shirika limeendelea kutoa elimu ya urithi wa asili na malikale kwa kuhamasisha jamii na wanafunzi kuanzisha klabu

27 za makumbusho mashuleni ambapo jumla ya walimu na wanafunzi 19,255 walipata elimu hiyo. Aidha, Shirika limeendelea kutumia mifumo ya TEHAMA kuhifadhi mikusanyo na kuandaa maonesho ya kidijitali. Hadi sasa, maonesho sita (6) yametayarishwa likiwemo Onesho la Bibi Titi Mohamed, Onesho la Nyumba za Asili, Onesho la Vivutio vya Mji Mkongwe wa Mikindani. Vilevile, Onesho la Matumaini baada ya Huzuni limeandaliwa kidijitali katika Makumbusho ya Taifa Dar es Salaam ili kuwakumbuka wahanga wa mlipuko wa bomu katika Ubalozi wa Marekani mwaka 1998 lililotembelewa na Mheshimiwa Kamala Harris, Makamu wa Rais wa Marekani.

**166. Mheshimiwa Spika,** Shirika limefanya tafiti tano (5) za masuala ya uhifadhi ukiwemo; Utafiti kuhusu umuhimu wa mashirikiano ya Taasisi za Utamaduni kutangaza urithi wa asili na kiutamaduni uliopo nchini Tanzania na Utafiti kuhusu uhifadhi wa Mnara wa Kihistoria wa Mwenge wa Uhuru uliopo jijini Arusha. Aidha, Shirika limetoa machapisho ya kitafiti mawili (2) yakiwemo: Chapisho kuhusu uhifadhi wa malikale nchini, na Chapisho la mtawanyo wa aina za nondo wachavushao katika misitu na makazi, Milima ya Usambara Mashariki. Vilevile, Shirika limekusanya na kuhifadhi jumla ya mikusanyo 12,470 ya akiolojia, paleontolojia, mila, biolojia, historia na sanaa ikiwemo: mchoro wa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar na kitabu cha wageni kilichosainiwa na Mwl. Julius Kambarage Nyerere alipotembelea Shule ya Sekondari Old Moshi mwaka 1967.

**167. Mheshimiwa Spika,** Shirika limefanya tathmini ya uhifadhi na kuainisha thamani za kitamaduni katika hifadhi ya eneo la DinasoriaTendaguru, eneo la Mbuamaji na Kimbiji-Kigamboni, Dar es Salaam na Jengo la Boma lililopo Liwale mkoani Lindi. Matokeo ya tathmini hiyo yamebaini kuwa, eneo la Paleontolojia la Tendaguru, Lindi lina sifa ya kipekee na limewekwa kwenye orodha ya matazamio kuwa Urithi wa Dunia. Aidha, Shirika limeshirikiana na jamii ya Wabena mkoani Njombe katika uhifadhi wa Msitu wa Nyumbanitu ili kuendeleza utalii katika maeneo ya urithi usioshikika.

**168. Mheshimiwa Spika,** Shirika limekamilisha ujenzi wa nyumba za asili kwa kaya tano (5) za jamii za: Wasafwa, Wahehe, Wairaq,

Wasukuma na Wazanaki katika Kijiji cha Makumbusho, Dar es Salaam kwa kuzingatia ramani ya Tanzania. Aidha, Shirika linaendelea kushauri, kuhamasisha na kushirikisha jamii kuhusu uhifadhi na uanzishwaji wa makumbusho binafsi ambapo makumbusho binafsi nne (4) zimeanzishwa katika jamii ya Wameru - Arusha, Jamii za watu wa Tanga, Makumbusho ya Chifu Ndasikoi wa Kimaasai - Arusha na Makumbusho ya Mtemi KimweriTabora. Katika hatua nyingine, Shirika limeendelea kutoa ushauri wa kitaalamu wa namna bora ya kuanzisha makumbusho za Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Bunge, Benki Kuu ya Tanzania na Mamlaka ya Bandari Tanzania. Vilevile, Shirika linaendelea na utekelezaji wa Mpango wa Miaka 10 wa Kuenzi, Kutangaza na Kuhifadhi Urithi wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ambapo programu mbalimbali zimefanyika zikiwemo, Nyerere Marathon, Mbio za Baiskeli kuanzia Dar es Salaam hadi Butiama; makongamano na warsha za kumuenzi Mwl. Julius Kambarage Nyerere.

### 5.5.4.4 Mfuko wa Mambo ya Kale

**169. Mheshimiwa Spika,** Mfuko huu ulianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Mambo ya Kale Sura 333 kwa lengo la kutekeleza majukumu ya uhifadhi na utafiti wa malikale. Katika mwaka 2022/2023, Mfuko umewezesha uandaaji wa andiko la kushauri namna ya urejeshaji wa malikale zilizopo nje ya nchi; uandaaji wa andiko la maeneo 13 ya malikale yakiwemo ya harakati za wapigania uhuru wa nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara ambayo yatatangazwa kwenye Gazeti la Serikali kuwa Urithi wa Taifa; uhakiki wa mipaka ya Kituo cha Miambamakazi Mumba-Karatu; na kufanyika kwa tathmini ya hali ya uhifadhi wa vituo vya Mapango ya Amboni-Tanga, Isimila na KalengaIringa kabla na baada ya kukasimishwa kwa taasisi za Wizara. Vilevile, mfuko umewezesha vikao vya utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi katika vituo vya Makumbusho ya Kalenga-Iringa na magofu ya Kunduchi, Dar es Salaam.

### 5.6 Miradi ya Maendeleo

**170. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara ilitengewa **Shilingi 180,436,165,000** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya

maendeleo ya Wizara na Taasisi. Fedha hizo zinajumuisha **Shilingi 109,879,593,000** fedha za ndani; na **Shilingi 70,556,572,000** fedha za nje. Aidha, fedha hizo za maendeleo zinajumuisha **Shilingi 71,684,572,000** kwa ajili ya kutekeleza miradi tisa (9) chini ya Wizara na **Shilingi 108,751,593,000** za Miradi inayotekelezwa na Taasisi (TANAPA, NCAA, TAWA na NCT). Hadi kufikia Aprili 2023, Wizara ilipokea jumla ya **Shilingi 154,644,316,852.95** sawa na **asilimia 86** ya fedha zilizoidhinishwa kwa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 119,461,591,502** ni fedha za ndani na **Shilingi 35,182,725,351.03** ni fedha za nje. Aidha, miradi ya maendeleo iliyotekelezwa ni kama ifuatavyo:-

**(i) Mradi wa Kuboresha Usimamizi wa Maliasili na Kukuza Utalii Kanda ya Kusini (Resilient Natural Resources Management for Tourism and Growth - REGROW)**

**171. Mheshimiwa Spika,** mradi huu unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Benki ya Dunia. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 mradi uliidhinishiwa kiasi cha Shilingi 61,325,930,496. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na ukamilishaji na utiaji saini mikataba nane (8) ya ujenzi wa miundombinu mbalimbali ikiwemo ujenzi wa viwanja vya ndege sita (6) katika hifadhi za Taifa za Ruaha (3), Nyerere (2) na Mikumi (1) na ujenzi wa malango (3), vituo vya kutolea taarifa (2), umeme, kambi (4) za utalii, vituo vitatu (3) vya askari, kituo cha ikolojia (1), hosteli ya wanafunzi (1), malazi ya madereva wa utalii (1), mfumo wa maji safi, na canopy walkway katika hifadhi za Taifa za Nyerere, Ruaha, Udzungwa na Hifadhi ya Mazingira Asilia ya Kilombero. Vilevile, Wizara imenunua matrekta saba (7) pamoja na viambata vyake 23 kwa lengo la kuimarisha miundombinu ya barabara katika maeneo ya hifadhi.

**172. Mheshimiwa Spika,** katika kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu, Wizara kupitia mradi wa REGROW imewezesha vijana 120 kutoka wilaya za Kilolo, Iringa, Mvomero, Chamwino na Rufiji kupata mafunzo ya mbinu za kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu yaliyotolewa na Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii Likuyu Sekamaganga.

**173. Mheshimiwa Spika,** kazi nyingine iliyofanyika ni kuwezesha vikundi 159 vyenye jumla ya wanachama 3,816 kwa kuwapatia fedha mbegu jumla ya Shilingi 1,453,272,934 katika vijiji 15 vya awamu ya kwanza vinavyopakana na hifadhi za Taifa Ruaha, Nyerere, Mikumi na Udzungwa. Sambamba na hilo, katika kuimarisha ushiriki wa jamii kwenye shughuli za uhifadhi na utalii, Wizara imewezesha ufadhili wa masomo ya fani mbalimbali kwa vijana 582 kutoka vijiji 15 katika Wilaya saba (7) za Kilombero, Kilosa, Morogoro, Iringa, Kilolo, Mvomero na Chamwino.

**(ii) Mradi wa Kupambana na Ujangili na Biashara Haramu ya Wanyamapori (Combating Poaching and the Illegal Wildlife Trade in Tanzania)**

**174. Mheshimiwa Spika,** mradi huu unatekelezwa na Wizara kwa ufadhili wa Mfuko wa Mazingira wa Kimataifa (Global Environmental Facility - GEF) na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (United Nations Development Programme - UNDP). Kwa mwaka 2022/2023, Mradi uliidhinishiwa kiasi cha Shilingi 2,916,531,100. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kuandaa Mkakati wa Kitaifa wa Usimamizi wa Maeneo ya Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori 20232033; kuwezesha kufanyika kwa doria za ki-intelijensia na ushirikiano na nchi jirani katika kanda 10; na uratibu wa doria (TCGs) zilizowezesha kukamatwa kwa vipande 52 vya meno ya tembo, nyamapori aina mbalimbali na majangili 70 ambao wamechukuliwa hatua za kisheria.

**175. Mheshimiwa Spika,** Mradi umewezesha watumishi 319 kutoka Kikosi Kazi cha Taifa Dhidi ya Ujangili (NTAP), Kanda za Kiikolojia za Kuratibu Doria za Kupambana na Ujangili (TCGs), Ofisi ya Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Serikali, Jeshi la Uhifadhi na Jeshi la Polisi kupata mafunzo katika masuala ya intelijensia, operesheni na uendeshaji mashtaka; kukamilishwa kwa Mapitio ya Kanuni za Uwindaji wa Wenyeji za mwaka 2021. Aidha, mradi umewezesha kufanya tathmini kwa vikundi 155 vyenye wajumbe 2,726 vilivyopo katika mfumo ikolojia wa Ruaha-Rungwa ili kubaini vikundi vinavyokidhi vigezo vya kuwezeshwa na Mradi. Katika tathmini hiyo, vikundi 45 vilikidhi vigezo na kupewa mafunzo ya ujasiriamali na kuwawezesha kuanzisha umoja wa wafugaji nyuki Manyoni. Vilevile, mradi umewezesha

kuandaliwa kwa Mwongozo wa pamoja wa kubadilishana taarifa za kiintelijensia, uendeshaji wa operesheni za kupambana na ujangili na usimamizi wa wasiri na kuandaa mpango wa kujenga uwezo wa kitaasisi wa kupambana na ujangili na biashara haramu ya nyara.

**(iii) Mradi wa Panda Miti Kibiashara (Private Plantation and Value Chain in Tanzania)**

**176. Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Pandi Miti Kibiashara ni mradi wa ubia wa maendeleo baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Ufini (Finland). Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Mradi uliidhinishiwa kiasi cha Shilingi 3,360,500,000. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kuwezesha kutoa mafunzo kwa viongozi 296 wa Vikundi vya Upandaji miti (Tree Grower Association - TGA) ya namna ya kusimamia na kuendesha TGA; mafunzo kwa wakulima wa miti 5,689; kutoa misumeno 335 ya kupogolea miti kwa TGA 80; utambuzi wa wawekezaji 1,335; na kuwezesha matukio 768 ya huduma za ugani ambapo wakulima 12,354 walishiriki.

**177. Mheshimiwa Spika,** mradi umewezesha kuandaa Mipango ya Usimamizi wa Mashamba ya wakulima 603; kutoa vifaa vya kupambana na majanga ya moto (fire beaters 393 na knapsack fire sprayers 36); kuwezesha kuanzishwa kwa Kamati za usimamizi wa moto za vijiji 80 zenye jumla ya watu 2,612; kuanzisha vikosi vya kupambana na moto vyenye jumla ya watu 1,284; na kutoa pikipiki 14 katika kongani za Njombe (7), Mafinga (4) na Makete (3) kwa ajili ya kuwezesha utoaji wa huduma za ugani kwenye vijiji 80 vilivyopo kwenye mradi. Vilevile, mradi umewezesha vikundi 39 kuandaa maandiko ya biashara kwa ajili ya kuomba mikopo yenye thamani ya Shilingi 726,335,500.

**(iv) Mradi wa Kuwezesha Mnyororo wa Thamani wa Mazao ya Nyuki (Support to Beekeeping Value Chain Programme – BEVAC)**

**178. Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Umoja wa Ulaya. Mradi huu unatekelezwa na pande zote mbili (2) za Muungano ukihusisha mikoa mitano (5) ya Tanzania Bara na mikoa miwili (2) ya

Zanzibar. Kwa mwaka 2022/2023, Shilingi 2,948,860,404 ziliidhinishwa. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na: kukarabati ofisi ya mradi iliyopo Pemba; kununua magari matatu (3) na pikipiki 20 kwa ajili ya maafisa wanaotekeleza mradi. Kwa upande mwingine, mradi umetoa mafunzo ya mbinu za ufugaji bora wa nyuki kwa vyama vya ushirika 19 vyenye jumla ya wafugaji nyuki 1,204; kutoa mafunzo kwa wafanyabiashara wa mazao ya nyuki 102; kutafsiri kwa lugha ya Kiswahili Mwongozo wa Kuandaa Mipango ya Usimamizi wa Hifadhi za Nyuki na Manzuki; na kutoa nakala 24,000 za miongozo mbalimbali ikiwemo Sera, Sheria na Kanuni za ufugaji nyuki.

**179. Mheshimiwa Spika,** Katika hatua nyingine, mradi umekamilisha taratibu za maandalizi ya ujenzi wa bweni la wasichana katika Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki ambapo litakapokamilika litakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi wa kike 350. Kwa lengo la kuhakikisha kuwa Sekta ya Ufugaji Nyuki inasimamiwa ipasavyo kuanzia ngazi ya vijiji, mradi umewajengea uwezo viongozi wa vyama vya ushirika 19 wakiwemo; wajumbe wa Jukwaa la Wafugaji Nyuki Tanzania, Kampuni ya Api-Support, Chama cha Wauzaji Asali nje ya nchi, Ushirika wa wafugaji nyuki Kibondo, Chama cha Wafugaji Nyuki Pemba, na Jumuiya ya Ufugaji Nyuki Zanzibar.

**180. Mheshimiwa Spika,** mradi umeanzisha mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji wa taarifa za wafugaji nyuki ambapo hadi sasa taarifa za wafugaji nyuki 10,085 kutoka katika mikoa ya Tabora, Singida, Katavi, Kigoma, Shinyanga, Pemba Kusini na Pemba Kaskazini zimeingizwa kwenye mfumo. Taarifa hizi zitasaidia maandalizi ya mipango mbalimbali ya kuendeleza ufugaji nyuki katika mikoa hiyo. Aidha, mradi umewezesha kufanya mikutano katika vijiji 297 kwa lengo la kuhamasisha jamii kutenga maeneo kwa ajili ya kufugia nyuki; kuwaunganisha wafanyabiashara sita (6) wanaouza asali nje ya nchi na wafugaji nyuki 296 na vikundi 29; kuwezesha mkutano wa wafugaji nyuki ambapo wafugaji nyuki na wadau wengine takriban 58 walishiriki; kutoa mafunzo kwa makampuni 30 kuhusu utayari wa usafirishaji wa mazao ya nyuki nje ya nchi; kuanza taratibu za kuandaa rajamu (branding) ya asali inayozalishwa nchini kwa kuonesha sifa na tabia zake ili kuweza kuchochea soko la kimataifa; na kuwezesha kampuni 10 za uuzaji na usafirishaji wa asali nje ya nchi

kupata cheti cha ubora kitakachowezesha kampuni hizo kuuza asali katika masoko mbalimbali duniani.

### 5.7 Changamoto na Utatuzi

#### 5.7.1 Changamoto

**181. Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha mwaka 2022/2023, Wizara inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na gharama kubwa za kutangaza utalii; kuongezeka kwa migongano kati ya binadamu na wanyamapori kunakochangiwa na uvamizi wa shoroba, maeneo ya mapito na mtawanyiko wa wanyamapori; uvamizi na uharibifu wa maeneo yaliyohifadhiwa kutokana na shughuli za kibinadamu; na uvamizi wa mifugo kwenye maeneo ya hifadhi. Changamoto nyingine ni ongezeko la matukio ya moto katika maeneo yaliyohifadhiwa; mabadiliko ya tabia nchi yaliyosababisha ukame katika maeneo ya hifadhi na hivyo kuathiri ustawi wa wanyamapori na mazingira ya uhifadhi kwa ujumla; utegemezi mkubwa wa misitu kwa ajili ya nishati na uwepo wa mimea vamizi katika baadhi ya maeneo ya hifadhi hali inayosababisha kuathirika kwa uoto wa asili; kupungua kwa malisho ya wanyamapori; na miundombinu hafifu ya utalii katika maeneo ya hifadhi.

#### 5.7.2 Utatuzi wa Changamoto

**181. Mheshimiwa Spika,** katika kutatua changamoto ya gharama kubwa za kutangaza utalii, Wizara inaendelea na taratibu za namna bora ya kurejesha Tozo ya Maendeleo ya Utalii (Tourism Development Levy - TDL) kwa lengo la kupata fedha za kutosha kutangaza utalii hususan katika masoko ya kimkakati. Aidha, kama ilivyokuwa zamani, taasisi za uhifadhi na utalii zinapaswa kurejeshewa uwezo wa kubaki na sehemu ya fedha zinazokusanya (retention). Vilevile, Wizara inaendelea kutoa elimu na kuhamasisha jamii kuthamini na kuhifadhi rasilimali za maliasili; kuendelea kuhakiki, kupima maeneo ya hifadhi na kuweka alama za mipaka na mabango katika maeneo ya hifadhi; kujenga vituo vya askari na kutoa elimu ya namna ya kujikinga na wanyamapori wakali na waharibifu kwa kutumia mbinu za kitaalamu

na asili; kuimarisha ulinzi wa maeneo yaliyohifadhiwa; kununua vitendea kazi kwa ajili ya kupambana na majanga ya moto katika maeneo ya hifadhi; kuendelea kuhimiza matumizi ya nishati mbadala; kuwezesha jamii inayopakana na maeneo ya hifadhi kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi katika maeneo yao; kuendelea kubuni miradi ya uhifadhi na uendelezaji wa utalii; kuendelea kudhibiti magugu vamizi katika maeneo ya hifadhi; na kuimarisha miundombinu ya utalii na kubuni mbinu za kutangaza utalii.

## 6.0 MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

**183. Mheshimiwa Spika,** Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2023/2024 umezingatia miongozo mbalimbali ikiwemo Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2023/2024 - 2025/2026, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022 - 2025/2026), Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 - 2025, Sera na Sheria mbalimbali, Mpango Mkakati wa Wizara (2021/2022 - 2025/2026), maagizo mbalimbali ya viongozi wakuu wa Serikali na mikataba ya kikanda na kimataifa.

**184. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara itatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia maeneo ya vipaumbele kama ifuatavyo: kuendelea kutangaza utalii ndani na nje ya nchi hususan kwa kutumia Programu maalum ya Tanzania - the Royal Tour na mikakati mingine mikubwa hasa kupitia timu za michezo na matamasha makubwa ya kimataifa; kuibua na kuendeleza mazao ya utalii ya kimkakati ikiwemo utalii wa fukwe, mikutano na matukio, meli, michezo na utamaduni; kuimarisha miundombinu katika maeneo ya hifadhi ili kuwezesha shughuli za utalii kufanyika; kuimarisha uhifadhi na matumizi endelevu ya maliasili, malikale na makumbusho na kuyatangaza kidijitali; na kuendelea na mkakati wa upandaji miti na uzalishaji na uongezaji wa thamani ya mazao ya misitu na nyuki.

### 6.1 Ukusanyaji wa Maduhuli

**185. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2023/2024, makadirio ya maduhuli yatakayokusanywa kutokana na Sekta ya

Maliasili na Utalii ni jumla ya **Shilingi 771,875,687,704.92**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 572,905,619,470.92** zitakusanywa na mifumo ya TEHAMA ya Wizara kwenda Mamlaka ya Mapato Tanzania kutoka vyanzo vya TANAPA, NCAA na TAWA. Aidha, **Shilingi 198,970,068,234** zitakusanywa kupitia mfumo wa MNRT Portal kutoka vyanzo vya Idara na Taasisi nyingine za Wizara.

### 6.2 Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo

**186. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2023/2024, Wizara inakadiria kutumia jumla ya **Shilingi 654,668,208,000.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 486,501,449,000** zitagharamia Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 168,166,759,000** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Fedha za Matumizi ya Kawaida yanajumuisha Mishahara (PE) - **Shilingi 184,288,496,000** na Matumizi Mengineyo (OC) **Shilingi 302,212,953,000**. Fedha za miradi ya maendeleo zinajumuisha **Shilingi 109,879,593,000** fedha za ndani na **Shilingi 58,287,166,000** fedha za nje.

**187. Mheshimiwa Spika**, fedha za Matumizi ya Kawaida **Shilingi 486,501,449,000** zinajumuisha **Shilingi 24,912,433,495** kwa ajili ya Wizara na **Shilingi 461,589,015,505** kwa ajili ya taasisi zilizo chini ya Wizara. Kati ya fedha za Wizara, **Shilingi 8,703,540,445** ni Mishahara na **Shilingi 16,208,893,050** ni Matumizi Mengineyo (OC). Fedha za taasisi zinajumuisha **Shilingi 175,584,955,555** za mishahara na **Shilingi 286,004,059,950** za matumizi mengineyo.

### 6.3 Kazi Zitakazotekelezwa na Wizara na Taasisi zake

#### 6.3.1 Sekta ya Wanyamapori
#### 6.3.1.1 Idara ya Wanyamapori

**188. Mheshimiwa Spika**, Wizara itaendelea kupandisha hadhi Mapori Tengefu na kuanzisha maeneo ya Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori za Chamwino, Ifinga na Ikungi. Kwa upande mwingine, Wizara itaendelea kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Kuzuia ujangili na biashara haramu ya nyara; Mpango kazi wa kuongoa Shoroba za wanyamapori; na kuimarisha usimamizi wa maeneo ya mifumo ikolojia inayovuka mipaka ya nchi. Katika hatua nyingine, Wizara

itaendelea kutoa elimu na kuwajengea uwezo wananchi ili kukabiliana na matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu na kulipa kifuta jasho na kifuta machozi kwa walioathirika.

**189. Mheshimiwa Spika,** Wizara itaandaa Mkakati wa kutekeleza Sera ya Wanyamapori na kufanya Mapitio ya Sheria na Kanuni zinazosimamia sekta ya Wanyamapori. Hii ni pamoja na kuweka utaratibu wa kisheria utakaolazimu mashauri ya uingizaji wa mifugo katika hifadhi kusikilizwa mapema na kwa haraka ili kuepuka gharama za utunzaji na uhifadhi wa mifugo iliyokamatwa. Kwa upande mwingine, Wizara itakamilisha Mtaala wa Mafunzo ya Kijeshi ili uanze kutumika katika vituo vya mafunzo ya Kijeshi vya Mlele na Likuyu Sekamaganga. Sambamba na hilo, Wizara itaendelea kuratibu ujenzi wa maghala nane (8) ya silaha kwenye maeneo ya hifadhi; utatuzi wa migogoro ya ardhi baina ya wananchi na maeneo ya hifadhi; utekelezaji wa mikataba ya ushirikiano wa kikanda na kimataifa na ushiriki wa wake kwenye maonesho mbalimbali ya kitaifa, kikanda na kimataifa yanayohusu wanyamapori.

### 6.3.1.2 Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania – TANAPA

**190. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/2024, Shirika litafanya mapitio ya mipango ya ujumla ya usimamizi na uendelezaji wa hifadhi za Taifa Tarangire, Saadani na Milima ya Udzungwa. Vilevile, Shirika litachimba na kukarabati mabwawa sita (6) kwa ajili ya matumizi ya wanyamapori katika hifadhi za Taifa Mkomazi, Tarangire, Mikumi, Katavi, Ruaha, Saadani na Serengeti. Kwa upande mwingine, Shirika litaboresha maeneo ya malisho ya wanyamapori kwa kudhibiti mimea vamizi katika Hifadhi za Taifa.

**191. Mheshimiwa Spika,** Shirika litaendelea kuboresha miundombinu ya huduma za utalii kwa kujenga barabara mpya zenye urefu wa kilomita 500 na kukarabati kilomita 10,500. Vilevile, Shirika litakarabati kilomita 300 za njia ya miguu za kupanda milimani; kujenga mifumo ya usambazaji wa maji safi na malango 10 ya ukusanyaji mapato katika hifadhi za Taifa Ibanda-Kyerwa (1), Serengeti (2), Kilimanjaro (1), Tarangire (1), Ruaha (1), Katavi (1), Nyerere (1) na Mikumi (2). Katika hatua nyingine, Shirika litajenga studio ya kurusha vivutio vya

utalii mubashara utakaowezesha vivutio kurushwa moja kwa moja kwenye mitandao na chaneli za kimataifa.

**192. Mheshimiwa Spika,** katika kuboresha huduma za utalii, Shirika litajenga vituo vya kutolea taarifa katika hifadhi za Taifa Mikumi na Ruaha na kufanya ukarabati wa kituo cha kutolea taarifa kwa watalii katika Hifadhi ya Taifa Serengeti. Vilevile, Shirika litajenga vituo tisa (9) vya askari katika hifadhi za Taifa Nyerere (2), Mto Ugalla (2), Burigi-Chato (1), Kigosi (1), Ruaha (1), Ibanda-Kyerwa (1) na Rumanyika-Karagwe (1). Sambamba na hilo, Shirika litajenga vituo tisa (9) vya kuthibiti wanyamapori wakali na waharibifu katika maeneo ya wananchi yanayopakana na Hifadhi za Taifa katika wilaya za Korogwe, Namtumbo, Karagwe, Muleba, Morogoro Vijijini, Ulanga, Mbarali, Rufiji na Bariadi.

**193. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/2024, Shirika litajenga Ofisi za Utawala na Usimamizi wa Hifadhi katika Hifadhi za Taifa Kigosi na Rumanyika-Karagwe. Vilevile, Shirika litajenga madaraja matano (5) na vivuko 20 katika hifadhi za Taifa Tarangire, Arusha, Mikumi, Serengeti na Ziwa Manyara. Kwa upande mwingine, Shirika litajenga nyumba 27 za makazi ya watumishi katika hifadhi za Taifa Serengeti, Mahale, Mto Ugalla, Gombe, Rumanyika-Karagwe, Burigi-Chato, Tarangire, Ruaha, Nyerere, Mkomazi na Katavi. Sambamba na hilo, Shirika litajenga viwanja sita (6) vya ndege katika Hifadhi za Taifa Ruaha (3), Mikumi (1) na Nyerere (2) na kukarabati viwanja 24 vya ndege katika Hifadhi za Taifa Nyerere, Serengeti, Katavi, Tarangire, Mto Ugalla na Burigi-Chato. Pia, Shirika litanunua ndege mbili (2) za doria katika hifadhi za Taifa Nyerere na Serengeti kwa ajili ya kudhibiti ujangili na wanyamapori wakali na waharibifu.

**194. Mheshimiwa Spika,** Shirika litaendelea kujenga miundombinu ya huduma za malazi ya kitalii (cottages, rest house, camping sites na hostels) katika hifadhi za Taifa za Kitulo, Nyerere, Burigi-Chato, Ruaha, Tarangire, Mkomazi, Mikumi na Kisiwa cha Rubondo. Aidha, Shirika litakamilisha ujenzi wa uwanja wa mchezo wa gofu katika eneo la Fort Ikoma - Hifadhi ya Taifa Serengeti na kujenga Canopy WalkWays katika Hifadhi ya Taifa Milima Udzungwa kama mazao mapya ya utalii. Katika hatua nyingine, Shirika litatenga maeneo 50 ya uwekezaji

na kutangaza maeneo yenye fursa za uwekezaji katika hifadhi za Taifa na katika maeneo ya malikale kwa ajili ya kuvutia wawekezaji na kuboresha mazingira ya biashara.

**195. Mheshimiwa Spika,** Shirika litanunua vifaa vya kuthibiti majanga ya moto katika Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro na hifadhi nyingine yakiwemo magari maalum, vifaa vya mawasiliano na vifaa vya kudhibiti moto. Vilevile, Shirika litaendelea kuboresha mifumo ya TEHAMA ya ukusanyaji wa mapato na kuimarisha miundombinu ya TEHAMA na kutumia ipasavyo huduma za mawasiliano na kifedha zinazotumika katika kutoa huduma kwa wadau mbalimbali ikiwemo mfumo wa kielektroniki wa Serikali wa kukusanya fedha za umma, Shirika la Simu Tanzania, mabenki na makampuni ya huduma za simu. Aidha, Shirika litaendelea kuimarisha ulinzi na usimamizi wa hifadhi kwa kuboresha matumizi ya sayansi na teknolojia kwa kuweka mfumo wa redio za kidijitali katika vituo vya askari ndani ya hifadhi na kununua vitendea kazi mbalimbali.

**196. Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwingine, Shirika litatekeleza jumla ya miradi 29 ya ujirani mwema. Miongoni mwa miradi hiyo ni miradi ya elimu inayojumuisha ununuzi wa madawati na viti 1,793 katika wilaya za Biharamulo, Chato, Kyerwa, Ushetu, Mbogwe na Ushirombo; ujenzi wa madarasa manne (4) katika wilaya za Kilosa na Kigoma Vijijini; ukarabati wa madarasa manne (4) katika wilaya ya Hai; ujenzi wa bweni moja (1) katika Wilaya ya Makete; na ukamilishaji wa ujenzi wa bwalo moja (1) katika Wilaya ya Mbarali. Aidha, zahanati moja (1) itajengwa katika Wilaya ya Kyerwa; kuchimba visima vitatu (3) vya maji katika wilaya za Bagamoyo, Kondoa na Karatu pamoja na kujenga vituo viwili vya polisi katika wilaya za Tarime na Uvinza.

**197. Mheshimiwa Spika,** Shirika litawezesha ununuzi wa mizinga 200 kwa vikundi viwili (2) katika wilaya za Bagamoyo na Pangani, miradi 10 ya mazingira (kutumia nishati ya gesi mbadala ya kuni kwa ajili ya kupika) katika wilaya za Rombo, Hai, Moshi Vijijini, Siha na Longido na miradi mitatu (3) ya kusaidia vifaa vya ujenzi na usafi katika wilaya za Rombo na Moshi Vijijini. Vilevile, Shirika litawezesha uandaaji wa Mpango wa Matumizi ya Ardhi katika vijiji 75 katika Wilaya za Tarime

(6), Bunda (7), Bariadi (7), Meatu (12) Itilima (9), Busega (4), Morogoro Vijijini (5), Kilombero (5), Ulanga (7), Tunduru (3), Liwale (5) na Kisarawe (5). Aidha, Shirika limeanzisha vikundi 21 vya Benki za Uhifadhi za Kijamii (Community Conservation Banks - COCOBA) katika wilaya za Bunda, Bariadi na Tarime. Elimu ya uhifadhi itaendelea kutolewa katika vijiji 864 vinavyozunguka hifadhi zote za Taifa. Vilevile, Shirika litaendelea kushirikisha jamii zinazoishi jirani na hifadhi katika shughuli za uhifadhi kwa kuimarisha vikundi vya ulinzi shirikishi na vikundi vya klabu za mazingira.

**198. Mheshimiwa Spika,** Shirika litanunua mitambo ya kampuni tanzu ya ujenzi; ujenzi wa ofisi unganishi ya Dodoma na Makao Makuu ya hifadhi za Rumanyika–Karagwe na Kigosi; kujenga malango ya Kidia (Kilimanjaro), Luhanga (Ruaha) na Kanyamkaa (Katavi); ujenzi wa nyumba za watumishi na vituo vya doria katika hifadhi za Taifa Kigosi, Ruaha na Rumanyika-Karagwe; na kutekeleza Mradi wa Faru katika hifadhi za Mikumi na Burigi-Chato.

**6.3.1.3 Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania – TAWA**

**199. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha uhifadhi na ulinzi wa rasilimali za wanyamapori, Mamlaka itaendelea kudhibiti ujangili na biashara haramu ya nyara kwa kuimarisha doria katika mapori ya akiba na tengefu na kutumia intelijensia kubaini makosa ya jinai dhidi ya rasilimali za wanyamapori. Sambamba na hilo, Mamlaka itanunua pikipiki 10 na boti mbili (2) kwa ajili ya kuimarisha shughuli za doria kwa ajili ya mapori ya Akiba Luganzo-Tongwe na Uwanda.

**200. Mheshimiwa Spika,** katika kuboresha miundombinu ya uhifadhi, Mamlaka itanunua mitambo mitatu (3) kwa ajili ya ujenzi wa barabara; kujenga karakana; chumba maalum kwa ajili ya kudhibiti ufuatiliaji wa faru katika Pori la Akiba Maswa; na vituo viwili (2) vya askari kwenye Pori la Akiba Kilombero. Sambamba na hilo, Mamlaka itajenga kilomita 750 za barabara katika mapori ya akiba Rungwa, Kizigo, Muhesi na Lukwati-Piti. Katika hatua nyingine, Mamlaka, itaweka alama za mipaka (Mkuza) na vigingi 2,805 katika mapori ya akiba ya Kilombero, Igombe, Inyonga, Wembere, Ugalla, Luganzo Tongwe na Pori Tengefu la Lunda Nkwambi kwenye mifumo ya

kiikolojia Simanjiro, Mto wa Mbu na Lolkisale ili kuondoa migogoro ya mipaka.

**201. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka itaendelea kukabiliana na matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu kwa kuboresha doria za mwitikio wa haraka; kutumia askari wa wanyamapori wa vijiji; na kutoa elimu kwa jamii ili kuwajengea uwezo wa kukabiliana na wanyama hao. Kwa upande mwingine, jumla ya askari 27 wa vijiji kutoka wilaya tisa (9) watapatiwa mafunzo na kuanza kazi katika vituo 16 vilivyojengwa kwa ajili ya kudhibiti matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu. Vilevile, Mamlaka itaongeza matumizi ya teknolojia ikiwa ni pamoja na kutumia ndege nyuki (drone) na visukuma mawimbi ili kufuatilia mienendo ya wanyamapori.

**202. Mheshimiwa Spika,** katika kuunga mkono mafanikio yaliyoletwa na Programu ya Tanzania - the Royal Tour, Mamlaka itaendelea kuboresha miundombinu ya utalii kwa kujenga kilomita 218 za barabara kwenye mapori ya akiba Kijereshi, Pande, Wamimbiki na Swagaswaga; kukarabati nyumba sita (6) za kulala wageni kwenye Pori la Akiba Wamimbiki; kununua boti moja (1) ya utalii katika Kisiwa cha Lundo; kuchimba visima; na kuweka miundombinu ya maji kwenye mapori ya akiba Msanjesi, Muhesi, na Swagaswaga.

**203. Mheshimiwa Spika,** katika kuboresha ukusanyaji mapato yatokanayo na utalii, Mamlaka itajenga vituo viwili (2) vya kukusanyia mapato katika mapori ya akiba Lundo, Uwanda na vituo viwili (2) vya kuuzia nyara katika majiji ya Mwanza na Arusha. Vilevile, Mamlaka itaboresha miundombinu ya malazi kwenye Shamba la Makuyuni Wildlife Park. Katika hatua nyingine, Mamlaka itaendelea kutangaza vivutio vya utalii na fursa za uwekezaji ndani ya nchi na katika masoko ya kimataifa ya uwindaji wa kitalii na utalii wa picha ikiwemo Marekani, Falme za Kiarabu, Jumuiya ya Ulaya na Asia. Sambamba na hilo, Mamlaka itaendelea kutumia fursa ya biashara ya hewa ya Kaboni kwa kukamilisha makubaliano na wawekezaji.

**204. Mheshimiwa Spika,** katika kuboresha mazingira ya utendaji kazi, Mamlaka itanunua magari 13 kwa ajili ya shughuli za utawala; kujenga ofisi tatu (3) katika mapori ya akiba Muhesi, Wamimbiki na

kwenye mfumo ikolojia wa Simanjiro Lolkisale. Vilevile, Mamlaka itajenga ofisi ya Kanda ya Ziwa; nyumba mbili (2) za watumishi; na kukarabati nyumba 22 kwenye mapori ya akiba Selous, Wamimbiki, Maswa, Kizigo na kwenye mfumo ikolojia wa Simanjiro Lolkisale.

### 6.3.1.4 Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro – NCAA

**205. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/2024, Mamlaka itaendelea kuimarisha ulinzi na uhifadhi wa maliasili na malikale ndani ya Hifadhi na Pori la Akiba Pololeti kwa kufanya siku doria 38,640; kufanya operesheni maalum sita (6) kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama. Vilevile, Mamlaka itahakiki na kuweka vigingi kwenye mipaka ya Pori la Akiba Pololeti. Aidha, Mamlaka itaendelea kufunga mifumo maalumu kwa wanyama walio hatarini kutoweka kwa ajili ya kufuatilia mienendo yao. Katika hatua nyingine, Mamlaka itafanya mikutano 30 na vikao vinane (8) vya kutoa elimu kwa wananchi kuhusu mbinu za kukabiliana na matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu. Sambamba na hilo, Mamlaka itaotesha miche ya miti 460,000 na kuwezesha mafunzo ya ufugaji nyuki kwenye vijiji 20.

**206. Mheshimiwa Spika,** fauka ya hayo, zoezi la wananchi wa Ngorongoro wanaohama kwa hiari litaendelea kuratibiwa vyema kuhakikisha wananchi hao wanapata makazi bora na kuendelea na shughuli zao za kiuchumi kwenye makazi mbadala ya Msomera, Handeni, Tanga.

**207. Mheshimiwa Spika,** katika kukabiliana na changamoto za ongezeko la watu, mifugo na shughuli za kibinadamu ndani ya Hifadhi, Mamlaka itaendelea kuhamasisha wananchi katika vijiji 25 ndani ya hifadhi kuhama kwa hiari kwenda maeneo nje ya Hifadhi. Kwa upande mwingine, Mamlaka itaajiri watumishi 80 kwa ajili ya kuimarisha ulinzi katika Pori la Akiba Pololeti; kununua magari kwa ajili ya utawala; na kumalizia ujenzi wa Makao Makuu katika eneo la Kemyn katika Wilaya ya Karatu.

**208. Mheshimiwa Spika,** katika kuboresha miundombinu ya utalii, Mamlaka itajenga barabara yenye urefu wa kilomita 29.5 kutoka

lango la Lodurae hadi Golini kwa kiwango cha tabaka gumu. Vilevile, Mamlaka itafanya ukarabati wa mara kwa mara kwenye mtandao wa barabara wa kilomita 423 ndani ya hifadhi. Vilevile, Mamlaka itafanya ukarabati wa viwanja vya ndege vya Ndutu na Ngorongoro na kusambaza maji katika maeneo ya Ndutu, Laetoli, Olduvai na kimondo cha Mbozi pamoja na kuboresha miundombinu katika Pori la Akiba Pololeti.

**209. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka itarekebisha njia za watembea kwa miguu katika maeneo ya Empakai, Endoro na Olmot. Vilevile, Mamlaka itaendelea kuanzisha mazao mapya ya utalii katika maeneo ya Lolmalasin, kuanzisha dawati la msaada maalum kwa ajili ya kusikiliza na kutatua kero mbalimbali za wakala wa biashara za utalii. Aidha, Mamlaka kwa kushirikiana na Bodi ya Utalii itaandaa makongamano mawili (2) ya utalii pamoja na kutangaza utalii katika masoko ya ndani na nje.

**210. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka itaendelea kuboresha utalii wa mambo ya kale kwa kuzifukua nyayo na kujenga jengo kwa ajili ya uhifadhi, utalii na utafiti wa nyayo hizo katika eneo la Laetoli. Vilevile, Mamlaka itakarabati miundombinu ya umeme wa jua katika makumbusho ya Olduvai na Zinj monument information na kwenye vituo vitano (5) vya maaskari vya Naiyobi, Kakesio, kilimatembo, Endulen na Kongoni. Sambamba na hilo, Mamlaka itafanya mikutano 14 na wadau wa uhifadhi wa malikale. Aidha, Mamlaka itaendelea kuimarisha nyanda za malisho ya wanyamapori, kwa kung'oa na kufyeka magugu vamizi kwenye eneo la hekta 1,000 la Kreta, Ndutu na Pololeti. Vilevile, Mamlaka itatumia moto mpango katika eneo la ukubwa wa hekta 2,500 kwa lengo la kuboresha nyanda za malisho ya wanyamapori. Sambamba na hilo, Mamlaka itaondoa magugu vamizi na kuotesha uoto wa asili kwenye maeneo ambayo hapo awali yalikuwa makazi ya wananchi waliohama kwa hiari.

### 6.3.1.5 Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania –TAWIRI

**211. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024, Taasisi itaendelea kufanya tafiti za kimkakati za kuimarisha uhifadhi wa wanyamapori na afya ya mifumo ikolojia ya wanyamapori nchini

ikiwemo utafiti zaidi wa namna bora ya kudhibiti migongano kati ya binadamu na wanyamapori, tafiti za magonjwa ya wanyamapori, tafiti za namna bora ya kuongoa shoroba za wanyampori na maeneo ya mtawanyiko, tafiti za mimea vamizi na namna bora ya kunusuru athari zake hasa kwenye maeneo ya hifadhi, tafiti za matumizi ya teknolojia katika uhifadhi, tafiti za nyuki na mazao yake, na kusambaza matokeo ya utafiti. Aidha, Taasisi itaendelea kujenga uwezo wa kutoa huduma, kuidadi wanyamapori, ujenzi wa Jengo la Makao Makuu, ukarabati wa miundombinu chakavu ya Taasisi, kuimarisha miundombinu ya TEHAMA na kuboresha mfumo wa ukusanyaji mapato.

#### 6.3.1.6 Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori Mweka – CAWM

**212. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Chuo kitakamilisha ujenzi wa jengo la kutolea mafunzo la ghorofa mbili (2); kununua magari mawili (2) makubwa kwa ajili ya kuwezesha shughuli za mafunzo; kujenga hanga la wanafunzi na jiko katika eneo la mafunzo Kwakuchinja; kujenga choo na jiko katika eneo la mafunzo lililopo Arashi katika Wilaya ya Ngorongoro; kufanya ukarabati wa nyumba tatu (3) za watumishi, vyumba vinne (4) vya madarasa, hosteli nne (4) za wanafunzi, ofisi moja (1) ya watumishi na miundombinu ya vyoo. Kwa upande mwingine, Chuo kitaandaa Mpango wa matumizi bora ya ardhi katika eneo la mafunzo Kihesa-Kilolo katika Manispaa ya Iringa; kuimarisha miundombinu ya TEHAMA; kufanya maadhimisho ya miaka 60 ya Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori; na kuandaa mitaala nane (8) mipya ya masomo katika nyanja za usimamizi wa wanyamapori na utalii.

#### 6.3.1.7 Kituo cha Mafunzo ya Elimu kwa Jamii Likuyu Sekamaganga - CBCTC

**213. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/2024, Kituo cha mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii – Likuyu Sekamaganga kitatoa mafunzo kwa jumla ya wanafunzi 576 (VGS – 400; utalii na uongozaji watalii – 156; na viongozi na wajumbe wa kamati za maliasili za vijiji – 20). Vilevile, Taasisi itajenga bweni moja (1) na darasa moja (1); mabwawa mawili (2) ya kufugia samaki;

kumalizia ukarabati wa jengo la utawala; bweni la wasichana na nyumba ya watumishi. Sambamba na hilo, Kituo kitawezesha watumishi wawili (2) kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi; kununua samani za mabweni ya wanafunzi; kununua mahema 14; na kutoa ushauri wa kitaalam kwa Jumuiya ya Hifadhi za Wanyamapori (WMA).

**6.3.1.8 Taasisi ya Taaluma ya Wanyamapori Pasiansi – PWTI**

**214. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/2024, Taasisi itadahili wanafunzi 420 katika fani za uhifadhi wa wanyamapori, himasheria na uongozaji wa watalii na usalama. Aidha, taasisi itaendelea kutoa elimu kwa wanafunzi wa kozi ndefu na kozi fupi. Vilevile, Taasisi itaanzisha mtaala katika kiwango cha Stashahada katika masomo ya uaskari wa wanyamapori na utalii. Pia, taasisi itaendelea kuboresha miundombinu ya majengo, vitendea kazi pamoja na kukamilisha uwekaji wa samani na mifumo ya uendeshaji wa maktaba. Sambamba na hilo, Taasisi itaendelea na ujenzi wa uzio wenye urefu wa mita 205; na ujenzi wa bwalo la chakula katika eneo la mafunzo kwa vitendo Fort Ikoma.

**6.3.1.9 Mfuko wa Uhifadhi wa Wanyamapori Tanzania – TWPF**

**215. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Mfuko utaendelea kuwezesha uhakiki wa matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu; kulipa kifuta jasho na machozi kwa wahanga wa matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu; utoaji elimu kwa wananchi kuhusu mbinu za kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu; na kudhibiti ujangili kupitia Kikosi kazi cha Kitaifa cha Kupambana na Ujangili. Sambamba na hilo, Mfuko utawezesha zoezi la kutatua migogoro ya mipaka kati ya jamii na maeneo yaliyohifadhiwa. Aidha, Mfuko utawezesha shughuli za upandishaji hadhi maeneo yaliyohifadhiwa na shughuli za kuidadi wanyamapori; na kufanya mapitio ya sheria na kanuni mbalimbali za Sekta ya Wanyamapori.

### 6.3.2 Sekta ya Misitu na Nyuki

#### 6.3.2.1 Idara ya Misitu na Nyuki

**216. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara itafanya mapitio ya Sheria ya Misitu ya Na. 14 ya mwaka 2002, Sheria ya Ufugaji Nyuki Na. 15 ya mwaka 2002 na Mwongozo wa Uvunaji endelevu na biashara ya mazao ya misitu yanayovunwa katika misitu ya asili. Aidha, Wizara itaandaa Mwongozo wa namna ya kuandaa mipango ya usimamizi wa miti ya asili na mashamba ya miti; Kanuni za bima kwa bidhaa za mazao ya misitu; Mwongozo wa kitaifa wa Uwekezaji kwenye Sekta ya Misitu na Sekta ya Ufugaji Nyuki; Mwongozo wa Usimamizi wa Makundi ya Nyuki wasiouma; Mwongozo wa kufanya utalii wa nyuki katika maeneo ya hifadhi; Kanuni za usimamizi wa matumizi ya nyuki kwenye uchavushaji wa mimea; kufanya mapitio ya kanuni ya tozo ya mazao ya nyuki; na Kanuni za kusimamia shughuli za ufugaji nyuki katika hifadhi za misitu. Kwa upande mwingine, Wizara itafanya uzinduzi wa viwanda vitano (5) vya kuchakata na kufungasha mazao ya nyuki vilivyojengwa katika mikoa ya Tabora, Katavi, Geita na Kigoma. Vilevile, katika kuhakikisha kuwa rasilimali nyuki zinaendelea kutunzwa katika ngazi zote, Wizara itaanzisha hifadhi tano (5) za nyuki na kanda mbili (2) za ufugaji nyuki ndani ya hifadhi za misitu ya vijiji.

**217. Mheshimiwa Spika**, katika kuendeleza dhana ya ushirikishaji jamii kwenye uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu na nyuki, Wizara itaanzisha Baraza la Taifa la wataalam wa masuala ya misitu; itaandaa na kusambaza jarida la Misitu ni Mali pamoja na miongozo mbalimbali inayohusu sekta za Misitu na Ufugaji Nyuki; na kutoa elimu kwa vikundi 15 vya ufugaji nyuki pamoja na wakulima wa miti. Katika hatua nyingine, Wizara itaratibu vikao vinne (4) vya Kamati ya Kitaifa ya Ushauri ya Misitu; vikao vitatu (3) vya Kamati ya Kitaifa ya Ushauri ya Ufugaji Nyuki; na vikao vinne (4) vya Kamati Endeshi ya Mazao ya Misitu Yaliyohandisiwa. Vilevile, Wizara itaratibu Siku ya Ufugaji Nyuki Duniani; Siku ya Upandaji Miti Kitaifa na Siku ya Misitu Duniani. Pia, Wizara itashiriki katika mkutano wa Kongamano ya Wafugaji Nyuki Duniani (APIMONDIA) kwa lengo la kufungua masoko mapya ya

biashara ya mazao ya nyuki nje ya nchi na kuvutia wawekezaji katika sekta ya nyuki.

### 6.3.2.2 Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania – TFS

**218. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2023/2024, Wakala utakamilisha mipango 16 ya usimamizi wa misitu na kuandaa mipango mipya 38 yenye ukubwa wa hekta 581,221. Aidha, Wakala utaimarisha mipaka ya misitu kwa kufanya mapitio ya mipaka yenye urefu wa kilomita 72.3, kufyeka kilomita 4,175, na njia za kuzuia moto zenye urefu wa kilomita 161 pamoja na kuweka vigingi 703 na mabango 499. Wakala utatoa elimu katika vijiji 241 vilivyo jirani na hifadhi za misitu kuhusu upandaji miti, kukabiliana na matukio ya moto na usimamizi wa misitu.

**219. Mheshimiwa Spika,** Wakala utaendesha siku doria 194,700 na operesheni za kimkakati 422 za kuimarisha uhifadhi na kukabiliana na biashara haramu ya mazao ya misitu na nyuki. Aidha, Wakala utawezesha kupandisha hadhi misitu minne (4) yenye ukubwa wa hekta 25,600 kuwa hifadhi za misitu ya Taifa na hifadhi tatu (3) zenye hekta 3,752 kuwa misitu ya hifadhi za mazingira asilia na kuwezesha uandaaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi katika vijiji 10 vinavyopakana na hifadhi za misitu.

**220. Mheshimiwa Spika,** katika jitihada za kuendeleza viwanda vya mazao ya misitu, Wakala utauza jumla ya mita za ujazo 1,133,800 za miti kwa ajili ya magogo, mita za ujazo 7,100 kwa ajili ya kuni na nguzo 12,000 kwa ajili ya matumizi mbalimbali. Vilevile, Wakala utapanda miti katika eneo lenye ukubwa wa hekta 6,806 na kurudishia miti iliyokufa kwenye hekta 1,743. Aidha, Wakala utapalilia eneo lenye hekta 30,256; kupogolea hekta 9,383; na kupunguzia miti kwenye hekta 3,626. Pia, Wakala utakusanya tani 22.3 za mbegu bora za miti na kuotesha miche ya miti 30,995,580 ambayo itapandwa kwenye mashamba ya miti ya Serikali, maeneo ya hifadhi yaliyoharibiwa na kwenye maeneo ya jamii. Vilevile, Wakala utaimarisha mipaka ya mashamba kwa kuweka vigingi 110 na mabango 131, kufungua barabara mpya zenye urefu wa kilomita 75, kukarabati madaraja 25 na kalavati 34 katika mashamba ya miti 20. Katika kupambana na matukio ya moto kwenye mashamba ya miti,

Wakala utasafisha njia za moto zipatazo kilomita 5,870; mipaka yenye kilomita 92; kujenga minara mipya mitatu (3) ya kuangalizia moto na kukarabati mingine 15; pamoja na kutoa elimu kwa vikundi vya kuzima moto vyenye jumla ya watu 300.

**221. Mheshimiwa Spika,** kufuatia jitihada za kuendeleza ufugaji nyuki nchini, Wakala utapanda miti 150,000 ya chakula cha nyuki, kuzalisha makundi 250 ya nyuki na kuvuna tani 41.2 za asali na tani 1.7 za nta kutoka mizinga 16,400 ya nyuki. Vilevile, Wakala utatoa elimu kwa wafugaji nyuki 1,228 kuhusu mbinu bora za ufugaji nyuki na kutengeneza mizinga 1,000 kwa ajili ya kuigawa kwa wananchi wanaopakana na maeneo ya hifadhi. Pamoja na masuala mengine, Wakala utaendelea kuhakikisha kuwa asali inayouzwa Tanzania ina ubora wa kiwango cha juu kwa kukusanya sampuli 70 kutoka katika wilaya 30 na kuzipeleka maabara ya kimataifa kwa ajili ya kupimwa ubora.

**222. Mheshimiwa Spika,** katika jitihada za kuendeleza utalii ikolojia, Wakala utaimarisha miundombinu ya utalii katika vivutio vyake kwa kujenga kilomita 16 za njia za kutembea watalii na kambi tatu (3) za watalii katika hifadhi ya mazingira asilia Itulu Hill na Shamba la Miti West Kilimanjaro. Vilevile, Wakala utakarabati kilomita 295 za njia za kutembea watalii, kilomita 149 za barabara za msituni, na kilomita 54 za kuendeshea magari (drive routes). Wakala utaendelea kutangaza utalii ikolojia na utamaduni kwa kuandaa vipeperushi 13,416, programu saba (7) za redio na kushiriki katika matamasha mbalimbali ya ndani na nje ya nchi.

**223. Mheshimiwa Spika,** Wakala utaendelea kuimarisha mazingira ya kazi kwa kuwezesha watumishi 91 kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu na watumishi 618 kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi. Aidha, Wakala utajenga ofisi 11, vituo vya ulinzi hifadhini 19, nyumba za watumishi tisa (9) na kukarabati ofisi tatu (3), nyumba za watumishi 32, vizuia 17 vya kukagulia mazao ya misitu na nyuki. Vilevile, Wakala utanunua magari 32, pikipiki 37, trekta moja (1), boti moja (1) na mtambo mmoja (1). Vilevile, Wakala utafanya mikutano 36 ya wadau kuhusu masuala ya uhifadhi wa misitu, ufugaji nyuki na utalii; na

mikutano nane (8) kwa ajili ya kuandaa mikataba ya makubaliano kuhusu biashara ya mazao ya misitu na nyuki.

### 6.3.2.3 Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania – TAFORI

**224. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Taasisi itaendelea kufanya utafiti kwenye eneo la uboreshaji wa mfumo wa taarifa za usimamizi wa misitu na nyuki; kufanya tathmini ya rasilimali za misitu kwa ajili ya kuongeza tija katika viwanda vya mazao ya misitu katika mikoa ya Kanda ya Ziwa, Mashariki na Kusini; na kufanya tathmini ya mchango wa sekta ya misitu na nyuki kwenye Pato la Taifa kwa kutumia Green Accounting. Vilevile, Taasisi itafanya utafiti ili kubaini sifa na tabia za kipekee kwenye asali inayozalishwa nchini ili kuwa na rajamu (brand) kwenye masoko ya ndani na kimataifa. Katika hatua nyingine, Taasisi itaendelea na tafiti za kudhibiti mimea vamizi katika wilaya za Longido, Ngorogoro, Siha na Monduli; kufanya tafiti ya teknolojia sahihi ya kuzalisha nishati mbadala pamoja na kufanya tathmini ya ukuaji wa miti aina ya mianzi kwenye mikoa ya Kanda ya Mashariki, Kusini-Mashariki na Nyanda za Juu Kusini.

### 6.3.2.4 Vyuo vya Taaluma ya Misitu na Nyuki

**225. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki kitadahili wanafunzi 450 wa mafunzo ya muda mrefu kwa ngazi ya Astashahada na Stashahada pamoja na kununua vifaa na mashine za karakana kwa ajili ya mafunzo. Kwa upande mwingine, Chuo cha Viwanda vya Misitu kitadahili wanafunzi 400; kujenga bweni la wasichana lenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 350; kununua mtambo wa kukausha mbao; kununua vifaa vya TEHAMA; na kuendelea kutoa huduma za ugani na kuotesha miti katika shule za sekondari zilizopo katika Manispaa ya Moshi. Katika hatua nyingine Chuo cha Misitu Olmotonyi kitadahili wanafunzi 1,000 wa mafunzo ya muda mrefu katika ngazi ya Astashahada na Stashahada; kufanya mapitio na kuandaa mitaala ili iweze kuendana na matakwa ya NACTVET; na kununua vifaa vya kufundishia.

### 6.3.2.5 Mfuko wa Misitu Tanzania – TaFF

**226. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Mfuko utaendelea kuwezesha na kugharamia miradi 167 inayoendelea na miradi mipya 114 ya uanzishwaji wa vitalu vya miti; upandaji miti; na ufugaji nyuki. Aidha, Mfuko utatoa ruzuku kwa ajili ya miradi sita (6) ya utafiti wa kimkakati wa misitu na ufugaji nyuki; na miradi ya kujenga uwezo kwa Vyuo vya Mafunzo ya Misitu, Viwanda vya Misitu na Ufugaji Nyuki vilivyo chini ya Wizara. Vilevile, Mfuko utawezesha miradi 20 ya kuendeleza na kutengeneza nishati mbadala ya kupikia kwa lengo la kupunguza kasi kubwa ya ukataji miti. Aidha, Mfuko utawezesha miradi 20 ya uanzishaji wa mashamba ya miti. Kwa upande mwingine, Mfuko utaimarisha mazingira ya utendaji kazi kwa kuanza ujenzi wa ofisi katika Jiji la Dodoma. Vilevile, kwa lengo la kuendelea kutangaza nchi yetu kimataifa, Mfuko utakuwa mwenyeji wa mkutano wa 13 wa Shirikisho la Mifuko ya Uhifadhi wa Mazingira Barani Afrika lijulikanalo kama CAFÉ.

### 6.3.3 Sekta ya Utalii
### 6.3.3.1 Idara ya Utalii

**227. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara itakamilisha mapitio ya Sheria ya Utalii Na. 29 ya mwaka 2008 kwa lengo la kuboresha mazingira ya biashara za utalii; kufanya kaguzi na uhakiki wa wakala wa biashara za utalii katika kanda nne (4); pamoja na kujenga uelewa kuhusu sheria, kanuni na miongozo ya uendeshaji wa biashara za utalii nchini. Katika hatua za kuendeleza mazao ya utalii ya kimkakati, Wizara itaendelea na jitihada mbalimbali za kukuza utalii wa fukwe, ikolojia, historia, meli, mikutano na matukio. Sambamba na hilo, Wizara itabainisha vivutio vya utalii na maeneo ya fukwe katika Mikoa ya Mara, Morogoro, Katavi, Tanga na Rukwa kwa ajili ya fursa za uwekezaji na uendelezaji wa shughuli za utalii na kufungua maeneo ya Kusini mwa nchi ambako kuna vivutio vingi vya utalii. Vilevile, Wizara itaendelea kuratibu mchakato wa kuitangaza Tanzania katika ligi kubwa duniani ikiwemo soka na kikapu katika nchi za Uingereza, Hispania na Marekani, matamasha makubwa na tuzo za utalii za kitaifa.

**228. Mheshimiwa Spika**, katika hatua nyingine, Wizara itaendelea kupanga huduma za malazi nchini katika daraja za ubora wa nyota katika mikoa ya Mbeya, Kilimanjaro na Mwanza na kufanya tathmini ya ubora wa huduma katika mikoa ya Dar es Salaam na Arusha. Aidha, Wizara itafanya mikutano minne (4) ya Kamati ya Kitaalam ya Ushauri katika masuala ya utalii na mikutano mitano (5) ya wadau wa utalii yenye lengo la kuhamasisha uwekezaji na uendelezaji wa mazao ya utalii. Vilevile, Wizara itaandaa Programu ya Kitaifa ya Uendelezaji Utalii (NTDP) pamoja na kuratibu Maadhimisho ya Siku ya Utalii Duniani na kushiriki katika mikutano na matukio ya utangazaji na uendelezaji utalii ndani na nje ya nchi.

#### 6.3.3.2 Bodi ya Utalii Tanzania – TTB

**229. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara kupitia Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) kwa kushirikiana na Kamati ya Kitaifa ya Kuitangaza Tanzania kupitia Filamu ya Tanzania The Royal Tour itaendelea kusambaza filamu hiyo kwenye mashirika mbalimbali ya ndege, mitandao mikubwa ya utalii duniani na kuendelea kuwasisitiza wadau kuendelea kuionesha katika mikutano na matukio mbalimbali. Aidha, Wizara itaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kutangaza na kuhamasisha utalii ndani na nje ya nchi kupitia Kituo cha Kutangaza Utalii Kidigitali (Digital Marketing Command Centre - DMCC); mitandao ya kijamii ikiwemo YouTube, Amazon, Google, Facebook, IMDb na WeChat ambayo inafikiwa na watu wengi zaidi. Aidha, itatangaza kimkakati zaidi vivutio vya utalii kupitia mashirika makubwa ya utalii Duniani ikiwemo TripAdvisor (wanaohudumia watalii takriban milioni 400 duniani kwa mwezi) na Expedia (wanaohudumia watalii zaidi ya milioni 350 duniani kwa mwezi) na Safari Club International (yenye wanachama zaidi ya 50,000 wa makampuni na wakala wa uwindaji wa kitalii). Vilevile, Bodi itaandaa Onesho la saba (7) la Swahili International Tourism Expo (S!TE) pamoja na ziara za mafunzo (FAM Trips) kwa makundi mbalimbali ikiwemo wakala wa biashara za utalii, waandishi wa habari, mabalozi wa hiari, watu mashuhuri na wawekezaji katika masoko ya utalii. Katika hatua nyingine, Bodi itaendelea kushirikiana na wadau kuratibu matamasha, matukio, maonesho pamoja na ziara za utangazaji utalii (Roadshows) ndani na nje ya nchi. Juhudi hizo zinalenga kuitangaza Tanzania katika

masoko ya utalii ya msingi kimkakati na yale yanayoibukia kwenye mabara ya Amerika, Ulaya, Afrika, Mashariki ya Kati, Asia na Pasifiki.

**230. Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwingine, Bodi itaendelea kutangaza utalii kupitia makala na filamu za Tanzania katika mashirika ya ndege pamoja na kushirikiana na Ofisi za Balozi za Tanzania zilizopo nje ya nchi. Sambamba na hilo, Wizara itawekeza kwenye uzalishaji wa makala zaidi za video na picha za kimataifa (photos, films and documentaries) hasa kwa kushirikiana na wazalishaji wa kimataifa hususan kutoka Hollywood kwa lengo la kuendelea kuitangaza Tanzania. Aidha, Bodi itatumia vituo mbalimbali vya habari vya kitaifa na kimataifa kuandaa na kurusha vipindi maalumu na makala za utangazaji utalii. Vilevile, Bodi itaandaa Mkakati wa Uendelezaji wa Utalii wa Mikutano na Matukio wenye lengo la kuongeza idadi ya watalii. Aidha, Bodi itaendelea kutangaza utalii kupitia michezo ndani na nje ya nchi pamoja na kuandaa makala moja (1) ya kutangaza utalii.

**6.3.3.3 Wakala wa Chuo cha Taifa cha Utalii – NCT**

**231. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Chuo kitadahili wanafunzi 1,500 katika ngazi ya Astashahada na Stashahada pamoja na kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa wadau 500 katika mnyororo wa utalii. Aidha, Chuo kitaendelea na ujenzi wa Jengo la Mafunzo kwa Kampasi ya Arusha na kuanza hatua za awali za ujenzi wa Kampasi ya Mwanza. Katika hatua nyingine, Chuo kitaanzisha programu ya mafunzo ya uratibu wa shughuli za utalii na usafirishaji (Travel and Tourism) katika Kampasi ya Arusha. Vilevile, Chuo kitaanzisha kituo cha mafunzo ya muda mfupi na biashara katika Jiji la Dodoma pamoja na kitengo cha ujasiriamali kupitia programu ya Incubation. Lengo la kuanzisha kitengo hicho ni kuandaa wanafunzi na wahitimu ili kukuza uwezo wa kujitegemea, kufanya shughuli za ujasiriamali na kuwezeshwa kufanya uchanganuzi wa biashara.

### 6.3.4 Sekta ya Mambo ya Kale
### 6.3.4.1 Idara ya Mambo ya Kale

**232. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara itaandaa kanuni za utekelezaji wa Sheria ya Mambo ya Kale Sura 333; Sheria ya Makumbusho ya Taifa Sura 281; na Mpango Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Malikale ya mwaka 2008. Aidha, Wizara itatangaza maeneo 20 ya malikale katika Gazeti la Serikali kuwa Urithi wa Taifa; kutatua migogoro ya mipaka katika maeneo matano (5) ya malikale yaliyopo Kunduchi-Dar es Salaam, EngarukaArusha, Amboni-Tanga, Chole-Mafia na MumbaArusha; kukamilisha mwongozo wa kutambua maeneo ya malikale yenye sifa za kuwa Urithi wa Taifa; kuandaa andiko la Mpango wa miaka 10 wa maeneo ya kipaumbele ya utafiti wa malikale nchini; na kukusanya taarifa za maeneo ya Urithi wa Taifa yaliyopo katika mikoa ya Katavi, Mara, Shinyanga, Songwe na Manyara kwa ajili ya kuhuisha orodha ya maeneo ya Urithi wa Taifa.

**233. Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwingine, Wizara itaunda Kamati ya Kitaifa ya Ushauri ya Uhifadhi wa Malikale nchini; kuendelea kufanya tathmini ya maeneo ya malikale; kufanya vikao sita (6) vya wadau kujadili masuala yanayohusu uimarishaji wa sekta ya malikale; kuwezesha huduma na vitendea kazi; kushiriki katika maonesho ya kitaifa na kimataifa; na kuendelea na maandalizi ya mfumo wa kidijitali ili kurahisisha mchakato wa utoaji wa leseni za tafiti za kisayansi, utafutaji tunu na filamu katika maeneo ya malikale.

### 6.3.4.2 Shirika la Makumbusho ya Taifa Tanzania – NMT

**234. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Shirika litajenga miundombinu ya maonesho kwenye vituo vipya vitatu (3) vya malikale vilivyopo Kigamboni-Dar es Salaam, MkwajuniTendaguru na Mikumbi mkoani Lindi ili kukuza utalii wa malikale katika ukanda wa kusini. Aidha, Shirika litaongeza wigo wa uhifadhi kwenye mikusanyo ya akiolojia na paleontolojia kwa kuboresha bohari mbili (2) za mikusanyo hiyo. Sambamba na hilo, Shirika litaendelea kufanya tathmini ya uhifadhi na ukarabati wa majenzi ya kale katika maeneo ya Lindi, Kigamboni-Dar es Salaam, Pangani-Tanga, Kua-Mafia na

Mikindani-Mtwara. Hali kadhalika, Shirika litafanya tafiti tano (5) katika masuala ya urithi wa utamaduni na kuendelea kuhamasisha jamii kuanzisha makumbusho mpya na binafsi. Vilevile, Shirika litaendelea kutangaza vivutio vya urithi wa kiutamaduni kidijitali na kuhamasisha utalii wa ndani kwa kutumia maonesho, matamasha, warsha, matukio na programu za elimu zenye kujenga uelewa kwa vizazi vya sasa kuhusiana na maadili, desturi za kitanzania, uzalendo na uhifadhi. Katika hatua nyingine, Shirika litaendelea na taratibu za uanzishwaji wa Makumbusho ya Marais, Dodoma; na kituo cha utafiti na maabara ya uhifadhi, Arusha. Vilevile, Shirika litaendelea kutekeleza Mpango wa Miaka 10 wa Kuenzi, Kutangaza na Kuhifadhi Urithi wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

### 6.3.4.3 Mfuko wa Mambo ya Kale – NAF

**235. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Mfuko utawezesha uhakiki na upimaji wa maeneo matatu (3) ya malikale ili kupunguza migogoro; kuwezesha utoaji elimu kwa wadau juu ya uhifadhi na uendelezaji wa malikale; kufanya tathmini ya hali ya uhifadhi katika maeneo ya malikale yaliyotangazwa katika Gazeti la Serikali yaliyopo katika mikoa ya Tanga, Pwani na Dar es Salaam; kuwezesha uandaaji wa mpango wa uhifadhi wa mji wa kihistoria Bagamoyo-Pwani na Pangani-Tanga. Kazi nyingine ni kugharamia wataalam 10 wa malikale kupata mafunzo ya ukarabati wa majenzi na magofu ya kale; kuwezesha vikao vitatu (3) vya wadau kujadili masuala yanayohusu uhifadhi na uendelezaji wa sekta ya malikale; kuwezesha ukamilishaji wa andiko la eneo la njia ya kati ya biashara ya utumwa na vipusa ili kuorodheshwa kwenye maeneo ya Urithi wa Dunia; kuwezesha uratibu wa urejeshwaji wa malikale zilizo nje ya nchi; na kuwezesha utekelezaji wa Mpango wa Miaka 10 wa Kuenzi, Kutangaza na Kuhifadhi Urithi wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

### 6.4 Miradi ya Maendeleo

**236. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara inakadiria kutumia **Shilingi 168,166,759,000** kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 109,879,593,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 58,287,166,000** ni fedha za nje. Fedha za maendeleo

**Shilingi 168,166,759,000** zinajumuisha **Shilingi 59,415,166,000** kwa ajili ya kutekeleza miradi tisa (9) ya Idara na Vitengo vilivyo chini ya Wizara; na **Shilingi 108,751,593,000** za miradi itakayotekelezwa na Taasisi (TANAPA, NCAA, TAWA na NCT).

**237. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara itatekeleza miradi ya maendeleo ifuatayo:

i. Mradi wa Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma (Public Finance Management and Reform Programm VI);

ii. Mradi wa Usimamizi wa Maliasili na Kuendeleza Utalii Kanda ya Kusini (Resilient Natural Resources Management for Tourism and Growth Project - REGROW);

iii. Mradi wa Kukabiliana na Ujangili na Biashara Haramu ya Wanyamapori (Support to Combat Poaching and Illegal Wildlife Trade in Tanzania);

iv. Mradi wa Kujenga Uwezo wa Maeneo ya Hifadhi, Mapori ya Akiba na Kikosi Dhidi Ujangili;

v. Mradi wa Panda Miti Kibiashara (Private Plantation and Value Chain in Tanzania); Mradi wa Kujenga Uwezo wa Taasisi na Mafunzo ya Misitu na Ufugaji Nyuki (Capacity Building in Forestry and Beekeeping);

vi. Mradi wa Kuwezesha Mnyororo wa Thamani wa Mazao ya Nyuki (Support to Beekeeping Value Chain Programme – BEVAC); vii. Mradi wa Uendelezaji wa Utalii wa Mikutano na Matukio (MICE Tourism Development Project); na viii. Mradi wa Usimamizi wa Mifumo ya Chakula, Matumizi Bora ya Ardhi na Urejeshaji wa Uoto wa Asili Tanzania (Food Systems, Land Use and Restoration in Tanzania's Landscapes – FOLUR).

## 7.0 SHUKRANI

**238. Mheshimiwa Spika,** ninapenda kutumia nafasi hii tena kukushukuru wewe binafsi, Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa ushirikiano mnaotoa katika kuliongoza Bunge letu Tukufu. Pia, ninawashukuru wadau wote kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Kipekee, nizishukuru nchi marafiki, washirika wa maendeleo, Jumuiya za Kikanda, mashirika ya kimataifa, taasisi za kiserikali pamoja na wadau wengine wakiwemo sekta binafsi kwa ushirikiano wao katika kuendeleza Sekta ya Maliasili, Malikale na Utalii na uchumi wa nchi kwa ujumla. Nachukua fursa hii kutaja baadhi yao kama ifuatavyo: Serikali za Canada, China, Falme za Kiarabu, Korea Kusini, Marekani, Morocco, Namibia, Norway, Ubelgiji, Ufaransa, Ufini, Ujerumani, Uswisi na Jumuiya ya Umoja wa Nchi za Ulaya. Mashirika na taasisi za Kimataifa ni pamoja na: AfDB, AWF, AWHF, ENABEL, FAO, FZS, GEF, GIZ, ICCROM, ICOM, ICOMOS, ILO, IMF, ITC, IUCN, KfW, NORAD, PAMS Foundation, Trade Aid, UNDP, UNESCO, UNWTO, USAID, WCS, WHC, WTTC, World Bank, Wild Aid, WMF na WWF.

Wadau wa sekta ya utalii nchini: TCT, TATO, TAHOA, TAOA, TAHA, HAT, TAWTO, TWEA na wadau wote wanaoshiriki kikamilifu katika shughuli za uhifadhi wa maliasili, malikale na uendelezaji utalii. Aidha, ninapenda kuwashukuru wananchi wote walioshiriki kikamilifu katika shughuli za uhifadhi wa maliasili, malikale na uendelezaji utalii. Nitumie fursa hii kuwaomba wadau wote kuendelea kutoa ushirikiano kwa Wizara ili iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

## 8.0 MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2023/2024

**239. Mheshimiwa Spika,** ninaomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 654,668,208,000** kwa matumizi ya Fungu 69 - Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 486,501,449,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 168,166,759,000** ni za miradi ya maendeleo.

**240. Mheshimiwa Spika,** fedha za matumizi ya kawaida zinajumuisha **Shilingi 184,288,496,000** za mishahara na **Shilingi 302,212,953,000** za

matumizi mengineyo. Fedha za miradi ya maendeleo zinajumuisha **Shilingi 109,879,593,000** fedha za ndani na **Shilingi 58,287,166,000** fedha za nje.

**9.0 HITIMISHO**

**241. Mheshimiwa Spika,** napenda kuhitimisha kwa kuendelea kuwaomba Watanzania wote kushiriki katika uhifadhi na uendelezaji wa utalii na ninatoa shukrani zangu za dhati kwako wewe na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara ya Maliasili na Utalii: https://www.maliasili.go.tz

**242. Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana. Sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii aje awasilishe maoni ya Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge. Namuaona Makamu Mwenyekiti akija kuwasilisha kwa niaba ya Mwenyekiti, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga. *(Makofi)*

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika natanguliza kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye anatujalia mambo yote katika dunia hii, lakini pia nakushukuru nawe kwa kunipa fursa hii. Na kabla sijaanza kusoma taarifa hii naomba taarifa yetu yote ya Kamati iingizwe kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge kama ilivyowasilishwa.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati na kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 naomba nitumie fursa hii adhimu kukushukuru kwa kunipatia fursa ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya bajeti ya Wizara ya Maliasili

na Utalii (Fungu 69), kwa mwaka wa fedha 2022/2023 pamoja na maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Aidha, majukumu ya Kamati kuhusiana na uchambuzi wa bajeti ya wizara au taasisi inazozisimamia ikiwemo bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii, yameelezwa kwa kina katika kifungu cha 7 (i) (a) na Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari 2023.

Mheshimiwa Spika, utayarishaji wa taarifa hii umezingatia masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023 kama ifuatavyo: -

(a) Sehehumu ya kwanza inatoa utangulizi wa jumla.

(b) Sehemu ya pili inaeleza kuhusu uchambuzi wa Bajeti Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na namna Wizara ilivyotekeleza ushauri na mapendekezo ya Kamati.

(c) Sehemu ya tatu inachambua Makadirio na Mapato ya Matumizi ya Wizara ya Malisili na Utalii kwa mwaka fedha 2023/2024.

(d) Sehemu ya nne inafafanua kuhusua mambo ambayo Kamati iliyabaini, ushauri na mapendekezo yake kwa Wizara na Serikali kwa ujumla; na

(e) Sehemu ya tano ambayo ni ya mwisho inahusu hitimisho ikijumlisha shukurani na kutoa hoja kwa Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, namna Kamati ilivyotekeleza majukumu yake. Ili kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii ilikutana kuanzia tarehe 21 – 23 Machi, 2023 na kufanya uchambuzi wa kina wa Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kutathimini utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/2023, pamoja na makadirio na mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/2023 pamoja na uzingatiaji wa ushauri na mapendekezo ya Kamati. Katika uchambuzi wake kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii (Fungu 69) kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Kamati ilijielekeza katika maeneo yafuatayo: -

(a) Ukaguzi wa miradi iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2022/2023.

(b) Utekelezaji wa vipaumbele vya Wizara kwa mwaka fedha 2022/2023.

(c) Hali ya ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2023.

(d) Hali ya upatikanaji wa fedha kutoka Hazina kufikia Februari, 2023.

(e) Utekelezaji wa maoni na ushauri wa mapendekezo yaliyotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi wa miradi iliyotengewa fedha. Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara ya Maliasili na Utalii (Fungu 69) ilipanga utekelezaji jumla ya miradi nane ya Wizara na Miradi ya Taasisi za *TANAPA, NCAA, TAWA* na *NCT* ambayo iliidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya shilingi bilioni 180.4, zikijumuishwa fedha za ndani shilingi bilioni 109.88 na fedha za nje shilingi bilioni 70.56. Aidha, kabla ya kuanza uchambuzi wa bajeti Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa baadhi ya miradi iliyotengewa fedha na kutekelezwa na Wizara ya Maliasili na Utalii na Taasisi zake katika Mikoa Manyara, Arusha na Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya ukaguzi ya miradi iliyotengewa fedha. Mradi wa Ujenzi wa Barabara kushuka ndani ya kreta (*Seneto Descend Road)* katika eneo la Ngorongoro. Mradi huu unaotekelezwa na Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro *(NCCA)* kwa utaratibu wa *force account* kwa kutumia mafundi maalum wa ujenzi wa kutumia mawe kutoka Jiji la Mwanza ulitengewa shilingi bilioni 1.9 na mradi ulikuwa umekamilika kwa 100%

na kugharimu shilingi bilioni 1.7 sawa na 93.33% ya ya fedha iliyoidhinishwa. Barabara ya *senator* hadi uwanda wa kreta ina urefu wa kilomita 4.2 na inaanzia njia panda ya barabara kuu itokayo Karatu Mkoani Arusha kwenda Serengeti Mkoa wa Mara.

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya mradi huu ni pamoja na kupunguza gharama za mradi kwani kilomita moja imegharimu shilingi 423,000,000 kiasi ambacho ni nusu ya gharama za ujenzi wa kilomita moja ya barabara ya lami. Aidha, teknolojia ya matumizi ya mawe ni rafiki katika uhifadhi wa mazingira kwani haikinzani na kanuni jumla ya uhifadhi.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Kiwanja cha Ndege na Jengo la Kupokelea Wageni katika Hifadhi ya Taifa ya Tarangire. Utekelezaji wa mradi huu unalenga kuboresha miundombinu ya uwanja ili uweze kukidhi matakwa ya ubora wa viwango vya kimataifa. Kiasi cha shilingi 211.58 kilitengwa kwa ajili ya sehemu ya kwanza ya utekelezaji wa Mradi huu wenye vipengele sita vya utekelezaji. Wakati Kamati inatembelea mradi huu, utekelezaji wake ulikuwa umekamilika na tayari umeanza kutumika.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhishwa na matengenezo ya uwanja huu kwani yamesaidia kuboresha mazingira ya kuruka na kutua kwa ndege zinazoleta watalii katika Hifadhi ya Taifa ya Tarangire, jambo lililochangia kuongeza idadi ya watalii na mapato ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili ya mradi ni ujenzi wa jengo kwa ajili ya wageni wanaoingia na kutoka hifadhini kupitia Kiwanja Kidogo cha Ndege cha Kuro ambapo mradi huu wenye awamu ya pili ulitengewa shilingi milioni 700.9. Awamu ya kwanza ya mradi ilianza kutekelezwa Mei, 2021 na kukamilika Disemba, 2022 kwa gharama ya shilingi milioni 374.19 sawa na 53% ya fedha yote iliyotengwa kwa ajili ya mradi huu. Wakati Kamati inatembelea na kukagua mradi huu, utekelezaji ulikuwa umefikia 60% na Kamati imeridhishwa na utekelezaji uliofanyika.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Ukarabati wa Maonesho na Maktaba katika eneo la Azimio la Arusha na Elimu Viumbe. Mradi huu unahusu ukarabati na maboresho ya kituo cha makumbusho cha Azimio la Arusha, ambapo shilingi milioni 112.7 zilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wake na hadi Kamati inatembelea na kukagua 94% ya fedha hiyo ilikuwa imetumika. Sehemu ya pili ni mradi wa maboresho ya kituo cha makumbusho ya Elimu Viumbe ambao ulitengewa shilingi milioni 272.2 kwa ajili ya kujenga onesho la Tembo, sanamu tatu za tembo, sanamu moja ya Twiga, sanamu moja ya Faru na sanamu moja ya Kiboko.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Shughuli za Chuo cha Viwanda vya Misitu *(FITI)* Moshi. Katika mwaka wa fedha 2022/2023 chuo kilipanga kukusanya maduhuli ya shilingi 670,000,000 kutokana na ada na mauzo ya mbao na samani. Hadi Februari, 2023 chuo kilikuwa kimekusanya shilingi 375.9 sawa na 56.11% ya lengo. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba, chuo kinakabiliwa na uchakavu wa mashine na teknolojia iliyopitwa na wakati, jambo linaloathiri uzalishaji wa samani zitakazomudu kushindana kwenye soko. Kamati inashauri Serikali kukipatia chuo hiki mashine za kisasa na wataalamu zaidi.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya Utekelezaji wa Miradi. Tathmini ya Kamati kuhusiana na utekelezaji wa miradi inaonesha kwamba kuna mafanikio ya kuridhisha hasa katika miradi ya kwenye maeneo ya hifadhi za Taifa. Mfano ni ujenzi wa barabara ya seneto kwenye Hifadhi ya Ngorongoro kwa kutumia mawe, mradi ambao umeboresha mazingira na barabara ya kuingilia kreta, kutoa ujuzi wa kujenga kwa mawe kwa wananchi wa maeneo jirani na hifadhi hiyo na kupunguza gharama za ujenzi wa barabara. Pia, maboresho ya kiwanja kidogo cha ndege cha Kuro yamechangia kuboresha mazingira ya wageni kuingia na kutoka katika hifadhi ya Taifa ya Tarangire, na hivyo kuongeza idadi ya watalii na mapato ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, maoni, Ushauri na Mapendekezo kuhusu miradi. Fedha za maendeleo zisipotolewa kwa wakati zinaathiri utekelezaji wa miradi, hivyo Serikali itoe kikamilifu fedha za miradi, lakini pili ujenzi wa barabara za maeneo ya hifadhi kwa kutumia

teknolojia ya mawe ni wa gharama nafuu na barabara zitadumu kwa muda mrefu, na tatu Serikali ione uwezekano wa kutumia teknolojia ya ujenzi wa barabara kwa njia ya mawe katika maeneo mengine ya hifadhi kwani mawe ni rafiki wa mazingira ya hifadhi.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina kuhusiana na utekelezaji wa miradi ni kama inavyoonekana kwenye ukurasa wa tatu hadi kumi na tatu wa taarifa ya kamati.

Mheshimiwa Spika, hali ya ukusanyaji wa maduhuli hadi Februari, 2023. Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara ya Maliasili na Utalii (Fungu 69) ilikadiria kukusanya shilingi 670,000,000,000 kati ya fedha hizo shilingi bilioni 469.3 zinakusanywa kupitia mfumo wa Mamlaka ya Mapato *(TRA)* kutoka vyanzo vya mapato vya *TANAPA, NCAA* na *TAWA* na shilingi bilioni 201.49 zinakusanywa kutokana na vyanzo vya mapato vya idara, mifuko na taasisi kupitia mfumo wa *MNRT - Portal.*

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Februari, 2023 Wizara ilikuwa imekusanya shilingi bilioni 548.66 sawa na 82% ya lengo la makusanyo. Aidha, kati ya fedha hizo shilingi 445.3 zimekusanywa kutokana na vyanzo vya *TANAPA, NCAA* na *TAWA* na shilingi 103.34 zimekusanywa kutoka kwenye idara, mifuko na taasisi zilizo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba wastani wa makusanyo ya maduhuli kwa Fungu 69 ni 82%. Kiwango hicho ni kikubwa ikilinganishwa na matarajio ya makusanyo katika kipindi hicho. Kamati inashauri wizara kuboresha/kuimarisha mfumo wa ukusanyaji mapato wa wizara *(MNRT Portal)* ili kuongeza makusanyo kwa taasisi zake. Aidha, watendaji wa taasisi ambazo makusanyo yake ni hafifu wasimamiwe kikamilifu na kuhimizwa kuongeza juhudi katika ukusanyaji wa mapato. Kielelezo Na. 01 kinaonesha makusanyo ya maduhuli kwa fungu hili.

Mheshimiwa Spika, hali ya upatikanaji wa fedha hadi Februari, 2023. Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara ya Maliasili na Utalii (Fungu 69) iliidhinishiwa shilingi bilioni 624.1, kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 443.7 sawa na 71.09% ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na na shilingi bilioni 180.4 sawa na

28.91% ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Aidha, katika fedha za matumizi ya kawaida, shilingi bilioni 267.9 sawa na 60.38% ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 175.9 sawa na 39.64% ni kwa ajili ya mishahara.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Spika, hadi Februari, 2023 Wizara ilikuwa imepokea shilingi bilioni 420.3 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kiasi hicho ni sawa na 67.29% ya fedha yote iliyoidhinishwa kwa Wizara. Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, kati ya fedha zilizopokelewa shilingi bilioni 265.4 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na 59.81% ya fedha iliyoidhinishwa kwenye eneo hilo, na shilingi bilioni 154 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo, sawa na 85.71% ya fedha iliyotengwa kwa ajili ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika fedha za matumizi ya kawaida zilizopokelewa shilingi bilioni 98.47 kwa ajili ya mishahara sawa na 55.98% ya fedha iliyotengwa kwa ajili lengo hilo, na shilingi bilioni 166.9 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo sawa na 62.32% ya fedha iliyoidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi zaidi wa Kamati umebaini kwamba, katika fedha za maendeleo zilizopokelewa, shilingi 119.46 zilikuwa fedha za ndani sawa na 109% ya fedha za ndani zilizotengwa na shilingi bilioni 35.18 ni fedha za nje sawa na 49.86% ya fedha za nje zilizotengwa. Kamati imebaini kwamba, fedha za miradi kutoka nje zilipatikana kwa kiwango cha chini (49.86%) ikilinganishwa na fedha za maendeleo kutoka ndani ambacho kielelzo cha pili kinafafanua zaidi.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, mwenendo wa upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida ni 59.81% wastani huu ni chini ya lengo ikilinganishwa na matarajio katika kipindi hicho cha bajeti ambayo ni 66.6% ya bajeti iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo Kamati. Taarifa ya Kamati kuhusu uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2022/2023 pamoja na mambo mengine, ilitoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo tisa (9) ili yaweze kuzingatiwa na kutekelezwa na Wizara kwa lengo la

kuboresha na kuongeza tija katika uendeshaji wa sekta ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa vipaumbele vya Wizara. Hali ya makusanyo ya maduhuli, hali ya upatikanaji wa fedha na utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo ya kamati, ufafanuzi wake ni kama inavyoonekana kwenye ukurasa wa kumi na tatu hadi kumi na nane wa taarifa ya kamati.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa mpango na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Ili kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 kanun (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, Kamati ilichambua na kujadili Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na uchambuzi wa kamati ulijielekeza katika maeneo yafuatayo: -

(i) Makadirio ya Mapato kwa mwaka wa fedha 2023/2024;
(ii) Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024;
(iii) Ulinganisho wa Bajeti ya Wizara dhidi ya Bajeti ya Taifa;
(iv) Mambo muhimu yanayogusa sekta ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Mapato kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ya Maliasili na Utalii (Fungu 69) imekadaria kukusanya maduhuli ya shilingi bilioni 771.87. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, makadirio haya yameongezeka kwa shilingi bilioni 108.27 sawa na 16.32% ikilinganishwa na makadirio ya mwaka wa fedha 2022/2023 ambayo yalikuwa shilingi bilioni 663.59.

Mheshimiwa Spika, kati ya makadirio hayo yatakayokusanywa na Wizara shilingi bilioni 572.9 sawa na 74.22% ya lengo, zitakusanywa kupitia mfumo wa *TRA* kutoka vyanzo vya *TANAPA*, *NCAA* na *TAWA*. Aidha, shilingi bilioni 198.97 sawa na 25.78% zitakusanywa kupitia mfumo wa *MNRT - Portal* kutoka vyanzo vya idara, mifuko, taasisi za Wizara ambapo Kielelezo cha tatu kinafafanua zaidi.

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka 2023/2024. Katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ya Maliasili na Utalii (Fungu 69) inakadiria kutumia shilingi bilioni 642.67 ambazo zinajumuisha fedha za matumizi ya kawaida shilingi bilioni 474.5 sawa na 73.83% ya bajeti yote, na shilingi bilioni 168.2 sawa na 26.17% ya bajeti yote kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Katika fedha za matumizi ya kawaida shilingi bilioni 184.2 sawa na 38.84% ni kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 290.2 sawa na 61.16% ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, Aidha, katika fedha za maendeleo shilingi 109.88 sawa na 65.34% ni fedha za ndani na shilingi bilioni 58.28 ambapo ni sawa na 34.66% ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya uchambuzi kwa kulinganisha bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii (Fungu 69) kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na 2023/2024 na kubaini kwamba, bajeti ya wizara imeongezeka kwa 2.97% kutoka shilingi bilioni 624.14 mwaka 2022/2023 hadi kufikia shilingi 642.67 kwa mwaka 2023/2024. Kamati inapongeza hatua hiyo ya Serikali kwa kuona umuhimu wa kuongeza bajeti ya Wizara hii muhimu katika maendeleo ya wananchi na uhifadhi endelevu wa raslimali zetu za asili.

Mheshimiwa Spika, Ulinganisho wa Bajeti ya Wizara dhidi ya Bajeti ya Taifa. Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii dhidi ya bajeti ya Taifa, imepungua kutoka 1.52% hadi 1.45%. Bajeti ya Matumizi Mengineyo imeshuka kutoka 5.96% hadi 5.20% Bajeti ya mishahara imepungua kutoka 1.81% hadi kufikia 1.69% Bajeti ya Maendeleo kutokana na fedha za ndani imeongezeka kidogo kutoka 0.91% hadi 093% Bajeti ya maendeleo kutokana na fedha za nje imepungua kutoka 2.08% hadi 1.78%.

Mheshimiwa Spika, mambo muhimu yanayogusa sekta ya Maliasili na Utalii. Hatua ya Serikali kuinusuru Hifadhi ya Ngorongoro. Kamati inaipongeza hatua ya Serikali yenye lengo la kuinusuru hifadhi ya Ngorongoro kwa kuwahamisha kwa hiari wakazi wanaoishi ndani ya hifadhi hiyo. Uamuzi huo wa Serikali unalenga kupunguza ongezeko la watu na mifugo, makazi ya kudumu na holela, shughuli za

binadamu zinazotishia kupoteza hadhi ya hifadhi hiyo kama eneo la urithi wa dunia.

Mheshimiwa Spika, kamati inatambua Wizara imebainisha maeneo mbadala ya Handeni - Tanga na Kitwai - Manyara kwa ajili ya makazi ya wananchi wanaohama kutoka hifadhini. Hadi Novemba, 2022 jumla ya kaya 489 zenye watu 2,629 na mifugo 14,094 zilikuwa zimehama. Aidha, kaya 1,524 zenye watu 8,715 na mifugo 32,842 zimejiandikisha kuhama kwa hiari katika awamu zinazofuata. Kwa kuwa wananchi wamehamasika na wameridhia na wako tayari kuhama kutoka hifadhini, Kamati inaishauri Serikali kutoa fedha za kutosha kwa wakati na kukamilisha zoezi hili na wananchi hao wanaosubiri kuhamishwa wasiendelee kusubiri kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, Changamoto ya Wanyama Wakali na Waharibifu. Migongano baina ya binadamu na wanyamapori ni moja ya changamoto zinazokabili uhifadhi wa wanyamapori nchini na imekuwa ukisababisha madhara kwa pande zote, kwa wanyama na binadamu kuuawa au kujeruhiwa pamoja na uharibifu wa mazao na mali. Migongano hii inatokana na wananchi kufanya shughuli za kilimo kwenye maeneo ya mapito ya wanyama pori au wanyama kutafuta malisho na maji nje ya hifadhi hasa wakati wa kiangazi.

Mheshimiwa Spika, kamati inathamini hatua za Wizara katika kukabiliana na hali hii ambazo ni pamoja na kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa kusimamia utatuzi wa migogoro baina ya binadamu na wanyamapori ya 2024, kwa kuendesha doria na kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu, kuelimisha wananchi mbinu za kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu, kufuatilia mwenendo wa migongano na ujenzi wa vituo 16 vya kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu katika maeneo ya kipaumbele hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo Wizara inakabiliwa na changamoto ya upungufu wa Askari wa Uhifadhi, upungufu wa magari, helikopta na pikipiki zitakazotumiwa na Askari Wahifadhi na mgambo katika doria za kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu. Aidha, ukosefu wa maji na chakula ndani ya maeneo

yaliyohifadhiwa kulingana na mahitaji unasababisha wanyamapori watoke nje ya maeneo yao ili kutafuta maji na chakula, na hivyo kukabiliana na binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali kuchukua hatua stahiki za muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu ili kutafuta ufumbuzi wa changamoto zinazosababishwa na muingiliano baina ya wanyama wakali na waharibifu, na hivyo kuepusha madhara yanayosababishwa na muingiliano huu. Aidha, Wizara ishirikiane na Wizara za kisekta kuondoa ushoroba za wanyamapori kupitia zoezi la kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi. Vilevile, Serikali iboreshe viwango vya fidia kwa wananchi kutokana na madhara yanayosababishwa na wanyama ili vizingatie hali halisi ya maisha na thamani ya uharibifu au madhara yaliyotokea.

Mheshimiwa Spika, Hali ya Sekta ya Utalii Nchini. nchi yetu imejaliwa vivutio vingi vya utalii vinavyohusisha maliasili kama vile wanyamapori, misitu, bahari, maziwa, fukwe nzuri na utamaduni. Vivutio hivi vimeifanya sekta ya utalii kuendelea kutoa mchango mkubwa katika uchumi wa Taifa kwa kuchangia 17% ya pato ghafi la Taifa, 25% ya mauzo yote ya nje na kutoa ajira 1,600,000 kabla ya UVIKO - 19.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua na kupongeza jitihada za Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali katika kukuza, kuendeleza na kutangaza vivutio vya utalii hususani, kwa kutumia programu maalumu ya Tanzania - *The Royal Tour*. Jitihada hizo zimeongeza idadi ya watalii wa nje kwa 57.7% kutoka 922,692 mwaka 2021 hadi kufikia watalii 1,454,920 kwa mwaka 2022, na watalii wa ndani kutoka 788,933 mwaka 2021 hadi 2,363,260 kwa mwaka 2022 sawa na ongezeko la 199.5%.

Mheshimiwa Spika, aidha, idadi ya wakala wa biashara za utalii waliosajiliwa na kupatiwa leseni imeongezeka kutoka wakala 1,869 mwaka 2018/2019 hadi kufikia wakala 5128 mwaka 2021/2022 sawa na174.4%. Katika kipindi hicho, mapato yaliongezeka kutoka shilingi bilioni 5.5 kwa mwaka 2018/2019 hadi shilingi bilioni 7.1 mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua juhudi za Serikali kupitia Mipango Kabambe ya Kuimarisha Utangazaji wa Utalii kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo 2023/2024 – 2025/2026 ambao utagharimu shilingi bilioni 565. Kamati inapongeza juhudi hizo, hata hivyo ina mashaka iwapo utekelezaji wake utafanikiwa kwani chanzo cha fedha hicho hakijulikani na fedha hiyo haionekani kwenye bajeti ya mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Spika, ni ushauri wa Kamati kwamba, Serikali ishirikishe wadau wa utalii na sekta binafsi katika maamuzi mbalimbali ya kisera ikiwa ni pamoja kugharamia mpango huo ili lengo liweze kufikiwa. Aidha, mpango huo uende sambamba na kuhakikisha kazi nzuri ya kuendeleza na kutangaza utalii nchini iliyofanywa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan – Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Programu ya Tanzania-*The Royal Tour* inakuwa endelevu, kwa kuweka mazingira mazuri yatakayoendelea kuvutia watalii nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Utendaji wa Taasisi za Uhifadhi Wizara ya Maliasili na Utalii inasimamia taasisi nne za uhifadhi ambazo ni Mamlaka ya Hifadhi za Taifa Tanzania *(TANAPA),* Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro *(NCAA)* na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania *(TFS)* na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania *(TAWA)*.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua kazi nzuri ambayo imekuwa ikitekelezwa na taasisi hizi Mfano, kutokana na utendaji wa *TANAPA* iliweza kupata tuzo mbalimbali ikiwemo Tuzo ya Hifadhi Bora Barani Afrika ambapo Serengeti ilishinda kwa miaka minne mfululizo (2019, 2020, 2021 na 2022) inayotolewa na *World Travel Awards,* aidha *TAWA* imekuwa ikifanya kazi nzuri katika usimamizi na uendeshaji wanyamapori akiba na mapori tengefu.

Mheshimiwa Spika, vilevile ukiondoa *TFS,* taasisi zilizobaki zimekuwa zikifanya kazi nzuri katika ukusanyaji wa mapato. Taasisi hizo ambazo ukusanyaji wa mapato umekuwa ukitekelezwa kupitia mfumo wa *TRA,* zimekuwa zikifanya vizuri ikilinganishwa na taasisi ambazo ukusanyaji wa mapato unafanyika kupitia mfumo wa *MNRT - Portal.*

Kwa mfano katika mwaka huu wa fedha hadi Februari, 2023 taasisi hizo zilikusanya mapato kwa wastani wa 87.67% *(TAWA 69%, NCAA* 90% na *TANAPA* 104%).

Mheshimiwa Spika, pamoja na kufanya kazi nzuri, taasisi hizi zinakabiliwa na changamoto kadhaa, ikiwa ni pamoja na ufinyu wa bajeti ikilinganishwa na majukumu ya *TAWA* inayosimamia mapori 32 na *TANAPA* inayosimamia Hifadhi za Taifa 22. Katika mwaka wa fedha 2022/2023, *TANAPA* iliidhinishiwa Shilingi bilioni 105 kwa ajili matumizi mengineyo, wakati mahitaji halisi yalikuwa Shilingi bilioni 222.

Pili, upungufu wa watumishi. Mfano, taasisi za uhifadhi wanyamapori zina upungufu wa jumla ya Askari wa Hifadhi 1,687 *(TANAPA 466, NCAA 290* na *TAWA 931);*

Tatu, upungufu wa magari, helikopta na pikipiki zinazotumika na Askari wa Hifadhi na Mgambo katika doria ya kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu; na

Nne, ni ukosefu wa maji na chakula ndani ya maeneo yanayohifadhiwa kulingana na mahitaji na kusababisha mtawanyiko wa wanyamapori kutoka nje ya maeneo.

Mheshimiwa Spika, maelezo zaidi kuhusiana na Uchambuzi wa Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2023/2024 na mambo muhimu yanayogusa sekta ya maliasili na utalii, yanapatikana kuanzia ukurasa wa 19 hadi 34 wa Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nne ni Maoni na Ushauri wa Kamati. Baada ya ukaguzi wa miradi iliyotengewa fedha katika mwaka huu wa fedha 2023/2024, uchambuzi wa kina kuhusu Taarifa na Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2022/2023 na Taarifa ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kwa Wizara ya Maliasili na Utalii (Fungu 69), naomba kuwasilisha maoni hayo na ushauri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ushauri wa kwanza ni kuhusu migogoro katika maeneo ya hifadhi. Kumekuwa na migogoro baina ya wananchi na

maeneo ya hifadhi, ambayo inachangiwa na kukosekana kwa uelewa wa kutosha kwa wahifadhi na wananchi kuhusiana na mipaka sahihi ya hifadhi. Hali hiyo, inasababisha uhasama kati ya wananchi na mamlaka kwenye maeneo ya hifadhi, pale Serikali inapotaka kuwandoa wananchi waliovamia maeneo ya hifadhi, kuanzisha hifadhi au kurekebisha mipaka ya hifadhi. Ili kurekebisha hali hiyo Kamati inashauri mambo yafuatayo:-

(a) Wananchi waelimishwe vya kutosha kuhusiana na mipaka ya hifadhi ili watambue wako kwenye maeneo ambayo hawapaswi kuwepo;

(b) Serikali itumie taratibu stahiki zenye staha wakati wa kuwaondoa wananchi ambao wamevamia maeneo ya hifadhi ili kuondoa uwezekano wa kuleta uhasama baina ya wananchi hao na mamlaka ya uhifadhi;

(c) Serikali ihakikishe wananchi na wawakilishi wao wanashikirikishwa kikamilifu katika kila hatua;

(d) Serikali iweke mpango mkakati wa kujenga barabara kuzunguka Hifadhi za Taifa hasa zenye migogoro ili zitumike kama mipaka; na

(e) Kuwe na ushirikishwaji wa Wizara za kisekta na taasisi nyingine za Serikali zinazohusika na masuala ya hifadhi na ardhi, wakati wa uwekaji wa alama za mipaka, uanzishwaji wa hifadhi au uanzishwaji wa vijiji.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa pili ni Kuhusu Utambuzi na Utangazaji wa Vivutio Vingine vya Utalii. Nchi yetu imebarikiwa kuwa na vivutio vingi vya utalii ambavyo bado havijatambulika. Kwa hivyo, Kamati inashauri yafuatayo:-

(a) Serikali iandae na kutekeleza kikamilifu mikakati madhubuti ya kutambua na kutangaza vivutio vingine vya utalii kama ilivyo kwenye utalii wa wanyama na kuongeza wigo mpana wa mambo yatokanayo na utalii.

(b) Serikali izitumie Mamlaka za Serikali za Mitaa kuibua na kutangaza vivutio vya utalii ambavyo viko katika maeneo hayo; na

(c) Serikali ishirikishe sekta binafsi na wadau wengine wa sekta za utalii katika kuibua na kutangaza vivutio vipya vya utalii nchini jambo ambalo litakawezesha kuvifanya vifahamike na kuvutia watalii.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa tatu ni upatikanaji hafifu wa fedha za maendeleo. Upatikanaji hafifu wa fedha za maendeleo unaathiri utekelezaji wa miradi na maendeleo na kusababisha ikwame au kuchelewa kukamilika. Hivyo, Kamati inashauri yafuatayo:-

(a) Serikali itenge na kutoa fedha za maendeleo za kutosha na kwa wakati ili kuwezesha utekelezaji wa miradi hiyo;

(b) Serikali iendelee kupunguza utegemezi wa fedha za nje kwenye utekelezaji wa miradi kwani upatikanaji wake siyo wa uhakika; na

(c) Serikali iongeze fedha za ndani kwenye utekelezaji wa miradi, kwani zimekuwa na uhakika katika upatikanaji wake.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa nne ni Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania *(TAWA)*. Taasisi hii ilianzishwa kwa amri ya kisheria *(establishment order)* na chini ya kifungu cha 8 cha Sheria ya Kuhifadhi Wanyamapori Na. 5 ya mwaka 2009 ili kuweza kusimamia wanyamapori wa akiba, mapori tengefu, jumuiya ya hifadhi za wanyamapori na maeneo ya ardhi oevu.

Mheshimiwa Spika, Kamati imekuwa ikiishauri Serikali kukamilisha mchakato na kuwasilisha Bungeni Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya Wanyamapori itakayobainisha majukumu ya chombo hiki na kuanzishwa kwa bodi ya utendaji yenye nguvu ya kisheria katika kutekeleza majukumu ya kukisimamia chombo hiki.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa tano ni kasi ya ukusanyaji wa maduhuli kwa Mfumo wa *MNRT – Portal*. Kasi ya ukusanyaji wa maduhuli kwenye Wizara na Taasisi zake ambazo zinakusanya kupitia mfumo huu ikilinganishwa na taasisi ambazo zinakusanya kupitia mfumo wa *TRA* (asilimia 87) hadi kufikia robo ya tatu ya mwaka wa bajeti. Sasa Kamati inashauri yafuatayo:-

(a) Serikali iwasimamie kikamilifu Watendaji wa Taasisi ambazo zinakusanya maduhuli kwa mfumo huo wa *MNRT;*

(b) Wizara iweke viashiria muhimu vya kiutendaji kwa watendaji wa taasisi na idara zake na kuwawekea malengo ambayo wanapaswa kuyafikia; na

(c) Aidha, Serikali iendelee kuongeza ubunifu katika kutangaza na kuvitambulisha vivutio vya utalii nchini.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa sita ni mradi wa usimamizi wa maliasili na kuendeleza utalii Kanda ya Kusini. Utekelezaji wa mradi huu umesaidia kuboresha miundombinu katika hifadhi, utatuzi wa migogoro baina ya wanyama na binadamu, pamoja na uwezeshaji wa shughuli za kiuchumi ambazo zimesaidia kuimarisha uhifadhi na kuongeza kipato kwa wananchi na maeneo yanayozunguka hifadhi.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa saba ni Sera, Sheria na Kanuni Zilizopitwa na Wakati. Changamoto zinazoshuhudiwa katika sekta ya utalii, maliasili, malikale na kumbukumbu za Taifa kwa sehemu kubwa zinachangiwa na sera, sheria na kanuni zilizopitwa na wakati. Mfano, ni Sera ya Taifa ya Misitu ya mwaka 1998, Sera ya Taifa ya Utalii ya 1999, Sera ya Taifa ya Ufugaji Nyuki ya 1998 na Sheria ya Mambo ya kale Na. 2 ya Mwaka 1964 na marekebisho yake ya mwaka 1979.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali ikamilishe mchakato wa kuzipitia sera na sheria hizo na nyingine ambazo zimepitwa na wakati ili kuwezesha utendaji wa sekta hizi ambao utaendana na mabadiliko na maendeleo yaliyopo katika sekta hizi.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya mwisho ni hitimisho. Napenda kutumia fursa hii kwa niaba ya Kamati kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge, kwa namna ambavyo mmekuwa mkitimiza majukumu yenu kwa weledi na umakini mkubwa na hivyo kuliwezesha Bunge letu Tukufu kutimiza wajibu wake kwa ufanisi. Aidha, nawashukuru kwa moyo wa dhati Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, kwa ushirikiano na jinsi wanavyojitoa kikamilifu katika kipindi chote cha ziara za ukaguzi wa miradi iliyotengewa fedha na uchambuzi wa bajeti ya Wizara hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kuwashukuru Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa na Naibu Waziri, Mheshimiwa Mary Masanja kwa ushirikiano wao mkubwa kwa Kamati ambao umechangia kuiwezesha Kamati kutekeleza shughuli zake kwa ufanisi hasa katika sekta hii. Nawashukuru pia watendaji wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii chini ya uongozi wa Katibu Mkuu, Dkt. Hassan Abbasi, akisaidiwa na Naibu Katibu Mkuu, Ndg. Ludovick Nduhiya, kwa ushirikiano na mchango wao kwa Kamati katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya kikanuni ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, kwa namna ya pekee namshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Nenelwa Mwihambi kwa kuongoza vyema uratibu wa shughuli za Kamati na Bunge kwa ujumla. Aidha, namshukuru Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndugu Michael Chikokoto, Makatibu wa Kamati hii Ndugu Haika Mtui na Ndugu Chacha Nyakega, wakisaidiwa na Ndugu Pauline Mavunde, kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kuhakikisha maandalizi ya taarifa hii yanakamilika kwa wakati. Aidha, nawashukuru Watumishi wote wa Bunge kwa mchango wao kwa Kamati inapotekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu lipokee na kuijadili taarifa hii na kukubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii (Fungu 69), kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja hapo awali.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*[Imetolewa chini ya Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu Bunge Toleo la Februari, 2023]*

## SEHEMU YA KWANZA

### 1.0 MAELEZO YA JUMLA

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023[1], naomba nitumie fursa hii adhimu kukushukuru kwa kunipatia fursa ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, kuhusu utekelezaji wa majukumu na bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii (Fungu 69), kwa mwaka wa fedha 2022/2023 pamoja na maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Aidha, majukumu ya Kamati kuhusiana na uchambuzi wa bajeti ya Wizara au taasisi inazozisimamia ikiwemo bajeti ya Wizara hii ya Maliasili na Utalii, yameelezwa kwa kina katika kifungu cha 7(1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023[2].

---

[1] 118 (9) Baada ya Waziri kuwasilisha Hotuba ya Bajeti kwa mujibu wa fasili (1), Mwenyekiti wa Kamati iliyopitia Makadirio husika na Msemaji wa Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni watatoa maoni yao kwa muda usiozidi dakika thelathini kila mmoja.

[2] 7.-(1) Majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge za kisekta yatakuwa yafuatayo:- (a) kushughulikia bajeti ya Wizara au Taasisi inazozisimamia;

**Mheshimiwa Spika**, utayarishaji wa taarifa hii umezingatia masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 kama ifuatavyo:-

a) Sehemu ya Kwanza inatoa utangulizi wa jumla na maelezo kuhusu msingi na muundo wa taarifa;

b) Sehemu ya Pili inaeleza kuhusu uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na namna Wizara ilivyotekeleza ushauri na mapendekezo ya Kamati;

c) Sehemu ya Tatu inachambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

d) Sehemu ya Nne inafafanua kuhusu mambo ambayo Kamati iliyabaini, ushauri na mapendekezo yake kwa Wizara na Serikali kwa ujumla; na

e) Sehemu ya Tano ambayo ni ya mwisho inahusu hitimisho la taarifa, ikijumuisha shukrani na kutoa hoja kwa Bunge lako Tukufu.

**1.1 Namna Kamati ilivyotekeleza Majukumu yake**

**Mheshimiwa Spika**, masharti ya Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 yanazitaka Kamati zote za kisekta ikiwemo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuchambua taarifa za utekelezaji wa bajeti za Wizara inazozisimamia na kufanya ulinganisho wa makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha unaofuata[3].

Kwa kuzingatia masharti hayo ya kikanuni, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, ilitekeleza wajibu huo tarehe 21 – 23 Machi, 2023 kwa kufanya uchambuzi wa kina wa Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Uchambuzi huo ulihusu kutathmini utekelezaji wa

[3] Baada ya kutembelea miradi, Kamati za Bunge za Kisekta, kwa kipindi kisichozidi siku tisa, zitafanya vikao vya kuchambua taarifa za utekelezaji wa Bajeti za Wizara inazozisimamia kwa mwaka wa fedha unaoisha na kufanya ulinganisho kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaofuata

bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2022/2023, pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 PAMOJA NA UZINGATIAJI WA USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wake kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii (**Fungu 69)** kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Kamati ilijielekeza katika maeneo yafuatayo:-

a) Ukaguzi wa miradi iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2022/2023;

b) Utekelezaji wa vipaumbele vya Wizara kwa mwaka wa fedha fedha 2022/2023;

c) Hali ya ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2022/2023;

d) Hali ya upatikanaji wa fedha kutoka Hazina kufikia Februari, 2023; na

e) Utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati;

### 2.1 Ukaguzi wa Miradi iliyotengewa fedha

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara ya Maliasili na Utalii (Fungu 69) ilipanga kutekeleza jumla ya miradi nane (8) na miradi ya taasisi (TANAPA, NCAA TAWA na NCT) ambayo iiidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya **shilingi 180,436,165,000/=** zikijumuisha fedha za ndani **shilingi 109,879,593,000/=** na fedha za nje **shilingi 70,556,572,000/=**.

Aidha, ili kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023[4], kabla ya kuanza uchambuzi wa bajeti, Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa baadhi ya miradi iliyotengewa fedha na kutekelezwa na Wizara ya Maliasili na Utalii na taasisi zake. Ziara ya Kamati ilihusisha mikoa mitatu (3) ambayo ni Manyara, Arusha na Kilimanjaro ili kubaini hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi hiyo, mafanikio na changamoto ili hatimaye Kamati iweze kulishauri kikamilifu Bunge lako Tukufu juu ya hatua stahiki za kuchukuliwa.

### 2.1.1 Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi iliyotengewa fedha

(a) **Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Kushuka Ndani ya Kreta (Seneto Descend Road) katika eneo la Ngorongoro.**

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu unaotekelezwa na Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCCA) kwa utaratibu wa *force account* kwa kutumia mafundi maalum wa ujenzi wa kutumia mawe kutoka Jiji la Mwanza ulitengewa **shilingi 1,901,510,000/=**. Hadi wakati Kamati inatembelea na kukagua utekelezaji wake, mradi ulikuwa umekamilika kwa asilimia mia moja na kugharimu **shilingi 1,774,760,000/=** sawa na **asilimia 93.33** ya fedha iliyoidhinishwa. Sehemu kubwa ya fedha ilitumika kwenye ununuzi wa vifaa vya ujenzi na malipo ya mafundi.

Barabara ya seneto hadi uwanda wa kreta ina urefu wa kilomita 4.2 na inaanzia njia panda ya barabara kuu itokayo Karatu mkoani Arusha kwenda Serengeti mkoani Mara.

Kabla ya kuanza kujengwa barabara hii ilikuwa ni mchanganyiko wa udongo na changarawe. Ujenzi wake umefanyika katika sehemu nne ambazo ni ukaguzi na upimaji wa barabara, usanifu, uchongaji wa mawe ya kujengea barabara na ujenzi wa barabara.

Utekelezaji wa mradi huu umekuwa na mafanikio makubwa ikiwa ni pamoja na kupunguza gharama za mradi kwani kilomita moja

[4] 117(1) Baada ya kuwasilishwa kwa mapendekezo ya mpango na kiwango cha ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaofuata kwa Wabunge, Kamati za Bunge za kisekta zitatembelea na kukagua utekelezaji wa miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha unaoisha, kwa siku zisizozidi saba.

imegharimu **shilingi 423,000,000/=** kiasi ambacho ni nusu ya gharama za ujenzi wa kilomita moja ya barabara ya lami.

Aidha, teknolojia ya matumizi ya mawe ni rafiki katika uhifadhi wa mazingira kwani haikinzani na kanuni ya jumla ya uhifadhi. Vilevile, ujenzi wa barabara hii kwa mawe utawezesha vivutio vya utalii kufikika katika kipindi chote cha mwaka, na hivyo kuchangia ongezeko la watalii na mapato yatokanayo na utalii.

(b) **Mradi wa Kiwanja cha Ndege na Jengo la Kupokelea Wageni katika Hifadhi ya Taifa ya Tarangire**

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 2022 ya Chama Cha Mapinduzi na Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP III 2021/2022 – 2025/2026) ili kuongeza idadi ya watalii kufikia milioni tano (5) na kukusanya mapato yanayofikia Dola za Marekani bilioni sita (US$ 6,000,000,000/=) ifikapo mwaka 2025/2026. Aidha, utekelezaji wa mradi huu unalenga kuboresha miundombinu ya uwanja ili uweze kukidhi matakwa ya ubora wa viwango vya kimataifa (ISO 9001:2015)

**Mheshimiwa Spika,** sehemu ya kwanza ya mradi huu ni matengenezo makubwa ya Uwanja Mdogo wa Ndege wa Kuro, ambayo yanatekelezwa na TANAPA katika Hifadhi ya Taifa ya Tarangire kwa kutumia fedha za Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO – 19. Kiasi cha **shilingi 211,583,375/=** kilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu chini ya Mkandarasi M/S Fraju Group Ltd.

Mradi huu una vipengele sita (6) ambavyo vinahusu matengenezo ya eneo la kutua na kupaa ndege; ujenzi wa sehemu ya kuruhusu ndege kukata kona, ujenzi wa njia za kutembea ndege, ujenzi wa eneo la maegesho ya ndege na ujenzi wa alama za mipaka ya uwanja. Wakati Kamati inatembelea na kukagua mradi huu, utekelezaji wake ulikuwa umekamilika kwa asilimia mia moja na tayari umeanza kutumika.

Kamati imeridhishwa na matengenezo ya uwanja huu kwani yamesaidia kuboresha mazingira ya kuruka na kutua kwa ndege zinazoleta watalii katika hifadhi ya taifa ya Tarangire, na hivyo kuchangia kuongeza idadi ya watalii na mapato kwa taifa.

**Mheshimiwa Spika,** sehemu ya pili ya mradi ni ujenzi wa jengo kwa ajili ya wageni wanaoingia na kutoka hifadhini kupitia Kiwanja Kidogo cha Ndege cha Kuro. Mradi huu wenye awamu mbili ulitengewa **shilingi 700,964,309/=** na unatekelezwa na Mkandarasi M/S Laki Construction Co. Ltd kutoka Arusha.

Awamu ya kwanza ya mradi ilianza kutekelezwa Mei, 2021 na kukamilika Disemba, 2022 kwa gharama ya **shilingi 374,187,211/**= sawa na **asilimia 53** ya fedha yote iliyotengwa kwa ajili ya mradi huu. Awamu hiyo inahusisha vipengele sita (6) ambavyo ni usafishaji wa eneo, ujenzi wa msingi, ujenzi wa nguzo pamoja na kuta, upauaji kwa kutumia paa la zege, umaliziaji na uwekaji wa madirisha ya chuma

Wakati Kamati inatembelea na kukagua mradi huu, utekelezaji ulikuwa umefikia **asilimia 60.** Awamu ya pili utekelezaji wake unaendelea kwa kutumia sehemu ya fedha iliyobaki na inatarajiwa kwamba, iwapo fedha itatolewa kwa wakati na kiwango cha kutosha, utekelezaji wake utakamilika mapema katika mwaka ujao wa fedha.

Kamati imeridhishwa na utekelezaji uliofanyika katika awamu ya kwanza ya mradi huu. Hata hivyo, inasisitiza kwamba, Serikali ihakikishe utekelezaji wa awamu ya pili unafanyika haraka iwezekanavyo ili jengo hilo likamilike na kuanza kutumika na hivyo kuboresha mazingira ya kupumzika wageni wanaoingia na kutoka hifadhini kupitia Kiwanja Kidogo cha Ndege cha Kuro sambamba na kupunguza muda wa kuhudumiwa wawapo uwanjani hapo.

Hata hivyo, Kamati iliarifiwa kwamba, kumekuwa na ucheleweshaji wa malipo ya Wakandarasi jambo lililosababisha utekelezaji wa mradi huo kusimama. Kamati inashauri Serikali kuchukua hatua stahiki ili kuhakikisha kwamba, wakandarasi wanalipwa kwa wakati mara wanapowasilisha hati za madai Hazina kwa kazi ambazo zimekamilika.

(c) **Mradi wa Ukarabati wa Maonesho na Maktaba katika eneo la Azimio la Arusha na Elimu Viumbe**

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa mradi huu ni sehemu ya matumizi ya fedha ambazo Makumbusho ya Taifa ilipata kutokana na mgao wa fedha (**shilingi bilioni 90.2**) za Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO – 19 zilizoelekezwa Wizara ya Maliasili na Utalii.

Makumbusho ya Taifa iliidhinishiwa **shilingi 2,450,000,000/=** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali katika vituo sita (6) vya makumbusho na miongoni mwa vituo hivyo ni makumbusho ya Azimio la Arusha na makumbusho ya Elimu Viumbe, mkoani Arusha.

**Mheshimiwa Spika,** sehemu ya kwanza ya mradi huu inahusu ukarabati na maboresho ya kituo cha makumbusho cha Azimio la Arusha, ambapo **shilingi 112,708,709/=** zilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wake na hadi wakati Kamati inatembelea na kukagua utekelezaji wa mradi huu **asilimia 94** ya fedha hizo ilikuwa imetumika.

Kazi ambazo zimefanyika katika maboresho hayo ni pamoja na ukarabati wa jengo zima la kituo ambao umehusisha pia kufumua na kusuka upya mfumo wa umeme, kuongeza ukubwa wa ukumbi wa maonesho kwa kujenga chumba kipya, ukarabati wa vyoo na miundombinu ya maji, ukarabati wa maktaba, kufunga taa za kisasa kwenye ukumbi wa maonesho, pamoja na kuunganisha mkongo wa taifa na kufunga vifaa vya TEHAMA kwenye ukumbi wa maonesho na maktaba.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imeridhishwa na kazi ambayo imefanyika kwani inaendana na thamani ya fedha iliyotengwa. Hata hivyo, ni ushauri wa Kamati kwamba kutokana na maboresho makubwa yaliyofanyika katika kituo hicho, Serikali inahitaji kukitangaza zaidi ili kiweze kuvutia watalii zaidi na hivyo kuongeza pato la taifa.

**Mheshimiwa Spika**, makumbusho ya Arusha yamebeba historia ya nchi yetu baada na kabla ya uhuru. Makumbusho haya yalifunguliwa na Baba wa Taifa, Mwl. J.K Nyerere, tarehe 05 Februari, 1977 wakati wa kuadhimisha miaka 10 ya kutangaza Sera ya Ujamaa na

Kujitegemea. Kutokana na uchakavu wa jengo la makumbusho hayo, idadi ya wageni ilipungua sana na hivyo kuathiri mapato ya Serikali yaliyotokana na viingilio.

**Mheshimiwa Spika,** sehemu ya pili ni mradi wa maboresho ya kituo cha makumbusho ya Elimu Viumbe ambao ulitengewa **shilingi 272,235,790/=** kwa ajili ya kujenga onesho la Tembo (sanamu tatu za tembo), sanamu moja ya Twiga, sanamu moja ya Faru na sanamu moja ya Kiboko.

Aidha, shughuli nyingine ni pamoja ukarabati wa stoo ya uhifadhi, maboresho ya maabara ya biolojia na ununuzi wa vifaa vya maabara, kujenga vizimba vya onesho jipya la reptilia na kufunga vifaa vya TEHAMA.

Hadi wakati Kamati inatembelea na kukagua utekelezaji wa mradi huu, asilimia 93 ya fedha ilikuwa imetumika na bado kulikuwa na uhitaji zaidi wa fedha ili kukamilisha kazi zaidi, ambazo hazijaguswa. Kazi hizo ni pamoja na ukosefu wa kangavuke (*generator*) ili kukidhi dharura ya umeme inapotokea, ukosefu wa fedha za kujenga tanki la kuhifadhia maji ili kukidhi dharura ya maji yanapokatika, na ununuzi wa gari kwa ajili ya shughuli za vituo vya makumbusho vya Arusha.

Kamati inaipongeza Wizara kwa hatua hii ya ukarabati wa kituo cha makumbusho cha elimu viumbe, kwani yatachangia kuongeza idadi ya wageni wanaotembelea vituo vya makumbusho ya taifa na kufikia lengo la watalii milioni 2 katika eneo hilo.

(d) **Utekelezaji wa Shughuli za Chuo cha Viwanda vya Misitu (FITI) Moshi**

**Mheshimiwa Spika,** Chuo cha Viwanda vya Misitu kilianzishwa mwaka 1976 kwa msaada wa Serikali ya Sweden kwa madhumuni ya kutoa mafunzo ya viwanda vya misitu kwa waliokuwa wafanyakazi wa Shirika la Viwanda vya Mbao Tanzania (TWICO). Chuo kilisajiliwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi tangu mwaka 2005 na tangu wakati huo kimetoa wahitimu zaidi ya 1600 wa astashahada na stashahada.

Katika mwaka wa fedha 2022/2023 chuo kilipanga kukusanya maduhuli ya **shilingi 670,000,000/=** kutokana na ada na mauzo ya mbao na samani. Hadi Februari, 2023 chuo kilikuwa kimekusanya **shilingi 375,900,000/=** sawa na **asilimia 56.11** ya lengo. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba, chuo kinakabiliwa na uchakavu wa mashine na teknolojia iliyopitwa na wakati, jambo linaloathiri uzalishaji wa samani zitakazomudu kushindana kwenye soko. Kamati inashauri Serikali kukipatia chuo hiki mashine za kisasa na wataalamu zaidi ili kiweze kuzalisha samani za kisasa na hivyo kuweza kushindana katika soko la samani za ndani na nje.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, katika kipindi hicho chuo kilikadiria kupokea ruzuku ya **shilingi 255,425,000/=** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi 50,000,000/=** kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Hadi kufikia Februari, 2023 chuo kilikuwa kimepokea **shilingi 104,000,000/=,** sawa na **asilimia 41** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi 50,000,000/=,** sawa na asilimia 100 kwa ajili ya shughuli za maendeleo.

Uchambuzi wa Kamati ulibaini changamoto kadhaa kwa chuo hiki ikiwa ni pamoja na kukosa muundo wa utumishi kulingana na sheria ya NACTVET tangu mwaka 2008 kilipotambuliwa na NACTVET baada ya kupata ithibati kamili. Jambo hili limekwamisha chuo kuzingatia matakwa ya baraza la ithibati, na kusababisha baadhi ya watumishi kuacha kazi.

Kamati inashauri Wizara kulitafutia ufumbuzi suala la muundo wa chuo hiki ili kukiwezesha kutekeleza majukumu yake kikamilifu kwa mujibu wa sheria ya NACTVET na pia kuwafanya watumishi wajiamini na kuwa na utulivu katika utekelezaji wa majukumu yao.

### 2.1.2 Tathmini ya Utekelezaji wa Miradi

**Mheshimiwa Spika,** tathmini ya Kamati kuhusiana na utekelezaji wa miradi inaonesha kwamba kuna mafanikio ya kuridhisha hasa katika miradi ya kwenye maeneo ya hifadhi za Taifa. Mfano ni ujenzi wa barabara ya seneto kwenye Hifadhi ya Ngorongoro kwa kutumia mawe, mradi ambao umeboresha mazingira na barabara ya kuingilia kreta, kutoa ujuzi wa kujenga kwa mawe kwa wananchi wa maeneo jirani na hifadhi hiyo na kupunguza gharama za ujenzi wa barabara.

Pia, maboresho ya kiwanja kidogo cha ndege cha Kuro yamechangia kuboresha mazingira ya wageni kuingia na kutoka katika hifadhi ya taifa ya Tarangire, na hivyo kuongeza idadi ya watalii na mapato kwa taifa

Hata hivyo, utekelezaji wa miradi mingine unakumbwa na ucheleweshaji wa fedha za wakandarasi na hivyo kuchelewesha kukamilika kwa miradi hiyo. Aidha, bado ufinyu wa bajeti inayotengwa kwa ajili ya miradi unaathiri utekelezaji wa miradi ya Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na taasisi zilizo chini yake.

**Mheshimiwa Spika,** ukosefu wa muundo wa utumishi kulingana na sheria ya NACTVET kwa chuo cha viwanda vya misitu (FIT) kunaathiri utendaji wa chuo hicho na kusababisha watumishi kuondoka.

Aidha, uchakavu wa mashine na kukosa teknolojia ya kisasa kunakikwamisha chuo kujiendesha kwa ushindani na kuendana na kasi ya mabadiliko ya teknolojia katika tasnia ya mbao nchini.

**2.1.3 Maoni, Ushauri na Mapendekezo kuhusu miradi**

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia ziara ya ukaguzi wa miradi na yote yaliyobainika, Kamati inatoa maoni na mapendekezo yafuatayo:-

i. Fedha za maendeleo zisipotolewa kwa wakati zinaathiri utekelezaji wa miradi, hivyo Serikali itoe kikamilifu fedha za miradi;

ii. Ujenzi wa barabara za maeneo ya hifadhi kwa kutumia teknolojia ya mawe ni wa gharama nafuu na barabara zitadumu kwa muda mrefu; na

iii. Serikali ione uwezekano wa kutumia teknolojia ya ujenzi wa barabara kwa njia yam awe katika maeneo mengine ya hifadhi kwani mawe ni rafiki wa mazingira ya hifadhi.

## 2.2 Utekelezaji wa vipaumbele vya Wizara kwa mwaka wa Fedha 2022/2023

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa Vipaumbele vya Serikali kwa ujumla unazingatia maeneo kadhaa ikiwa ni pamoja na Dira ya Maendeleo ya Taifa, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 – 2025, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (FYDP III) mwaka 2021/22 – 2025/26 na maelekezo mengine.

Wizara ya Maliasili na Utalii ina dhamana kwenye sekta ya utalii, maliasili, malikale na kumbukumbu za Taifa kwa kuhakikisha inaimarisha usimamizi, ulinzi na uhifadhi endelevu kwa faida ya kizazi cha sasa na kizazi kijacho na kuhakikisha taifa linanufaika na sekta hizo. Kwa mantiki hiyo, usimamizi sahihi wa sekta hii utawezesha kuzingatiwa kwa malengo yaliyowekwa na Katiba yetu Ibara ya 8 (1) (b) ya kuhakikisha ustawi wa wananchi[5].

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati unaonesha kwamba, bado sekta ya utalii, maliasili, malikale na kumbukumbu za taifa zinakabiliwa na changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja ufinyu wa bajeti, mwamko hafifu wa wananchi na ushirikishwaji mdogo wa sekta binafsi katika sekta hizi, migogoro baina ya wananchi na maeneo yaliyohifadhiwa, wananchi kuvamiwa na wanyamapori wakali na waharibifu, na kasi ndogo ya ongezeko la watalii wa ndani na nje.

Changamoto hizo zinakwamisha kufikiwa kwa malengo ya ilani ya uchaguzi ya CCM inayoitaka Serikali kukuza utalii na kuongeza idadi ya watalii kufikia milioni tano ( 5) ifikapo mwaka 2025 na kuongeza mapato hadi kufikia Dola za Kimarekani bilioni 6.0 mwaka 2025.

## 2.3 Hali ya ukusanyaji wa maduhuli hadi Februari, 2023

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara ya Maliasili na Utalii **(Fungu 69)** ilikadiria kukusanya **shilingi 670,000,000,000/=** Kati ya fedha hizo **shilingi 469,364,418,596/=** zinakusanywa kupitia mfumo wa Mamlaka ya Mapato (TRA) kutoka vyanzo vya mapato vya TANAPA, NCAA na TAWA; na **shilingi**

---

[5] 8 (1) Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Nchi inayofuata misingi ya demokrasia na haki ya kijamii, na kwa hiyo ((b) lengo kuu la Serikali litakuwa ni ustawi wa wananchi;

**201,492,165,325/=** zinakusanywa kutokana na vyanzo vya mapato vya idara, mifuko na taasisi kupitia mfumo wa MNRT - Portal.

Hadi kufikia Februari, 2023 Wizara ilikuwa imekusanya **shilingi 548,664,273,286**/= sawa na **asilimia 82** ya lengo la makusanyo. Aidha, kati ya fedha hizo **shilingi 445,323,592,303**/= zimekusanywa kutokana na vyanzo vya TANAPA, NCAA na TAWA na **shilingi 103,340,680,982/=** zimekusanywa kutoka kwenye idara, mifuko na taasisi zilizo chini ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba wastani wa makusanyo ya maduhuli kwa **Fungu 69** ni asilimia 82. Kiwango hicho ni kikubwa ikilinganishwa na matarajio ya makusanyo katika kipindi hicho. Kamati imeridhishwa na mwenendo huo wa makusanyo, na inaipongeza Wizara kwa hatua iliyofikiwa.

Uchambuzi zaidi umebaini kuwa taasisi ambazo maduhuli yanakusanywa kupitia mfumo wa TRA zilifanya vizuri zaidi ikilinganishwa na zile ambazo maduhuli yanakusanywa kwa kutumia mfumo wa Wizara (MNRT – Portal). Taasisi hizo (TANAPA, NCAA na TAWA) zilikusanya kwa wastani wa **asilimia 87**, wakati zile zinazokusanya kupitia mfumo wa Wizara zilikusanya kwa wastani wa **asilimia 51**. Aidha, mfuko wa misitu ulikusanya kwa kiwango cha chini sana, asilimia 24 kati ya taasisi zote zilizo chini ya Wizara.

**Kamati inashauri Wizara kuboresha/kuimarisha mfumo wa ukusanyaji mapato wa Wizara (MNRT Portal) ili kuongeza makusanyo kwa taasisi zake. Aidha, watendaji wa taasisi ambazo makusanyo yake ni hafifu wasimamiwe kikamilifu na kuhimizwa kuongeza juhudi katika ukusanyaji wa mapato. Kielelezo Na.01** kinaonesha makusanyo ya maduhuli kwa fungu hili.

**Kielelezo Na. 1: Ukusanyaji wa Maduhuli hadi Februari, 2023**

| Fungu 69 | Makadirio | Makusanyo | Asilimia |
|---|---|---|---|
| Wizara | **9,507,352,003** | **7,250,184,740** | **76.26** |
| Taasisi | **184,397,895,325** | **96,149,869,024** | **52.14** |
| Mifuko (TaFF) | **7,586,918,000** | **1,805,405,938** | **23.79** |
| Taasisi zinazotumia TRA (TANAPA, NCAA, TAWA) | **469,364,418,596** | **445,323,592,303** | **94.88** |

*Chanzo: Randama ya Wizara ya mwaka 2023 na Usanifu wa Kamati*

### 2.4 Hali ya upatikanaji wa fedha hadi Februari, 2023

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara ya Maliasili na Utalii (**Fungu 69)** iliidhinishiwa **shilingi 624,142,732,000/=** kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake. Kati ya fedha hizo **shilingi 443,706,567,000/=, sawa** na **asilimia 71.09** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na na **shilingi 180,436,165,000/=** sawa na **asilimia 28.91**ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Aidha, katika fedha za matumizi ya kawaida, **shilingi 267,921,860,000**/= sawa na **asilimia 60.38** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **shilingi 175,884,707,000**/= sawa na **asilimia 39.64** ni kwa ajili ya mishahara.

**Mheshimiwa Spika,** hadi Februari, 2023 Wizara ilikuwa imepokea **shilingi 420, 028,514,979/=** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kiasi hicho ni sawa na **asilimia 67.29** ya fedha yote iliyoidhinishwa kwa Wizara.

Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, kati ya fedha zilizopokelewa **shilingi 265,384,198,126/=** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na **asilimia 59.81** ya fedha iliyoidhinishwa kwenye eneo hilo, na **shilingi 154,644,316,852/-** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo, sawa na **asilimia 85.71** ya fedha iliyotengwa kwa ajili ya maendeleo.

Aidha, katika fedha za matumizi ya kawaida zilizopokelewa **shilingi 98,467,935,833/=** ni kwa ajili ya mishahara (PE) sawa na **asilimia 55.98** ya fedha iliyotengwa kwa ajili lengo hilo, na **shilingi 166,916,262,293/=** ni kwa ajili ya matumizi menginiyo (OC) sawa na **asilimia 62.32** ya fedha iliyoidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi zaidi wa Kamati umebaini kwamba, katika fedha za maendeleo zilizopokelewa, **shilingi 119,461,591,501/=** zilikuwa fedha za ndani sawa na **asilimia 109** ya fedha za ndani zilizotengwa na **shilingi 35,182,725,351**/= zilikuwa fedha za nje ambazo ni sawa na **asilimia 49.86** ya fedha za nje zilizotengwa.

Kamati imebaini kwamba, fedha za miradi kutoka nje zilipatikana kwa kiwango cha chini (49.86%) ikilinganishwa na fedha za maendeleo kutoka ndani (109%). Kamati inasikitishwa na mwenendo huo kwani ni changamoto ambayo imekuwa ikijirudia katika utekelezaji wa bajeti ya Serikali. **Kielelezo Na. 02** kinafafanua zaidi kuhusu upatikanaji wa fedha.

**Kielelezo Na. 2 Upatikanaji wa fedha hadi Februari, 2023**

| Matumizi | | Kilichoidhinishwa | Kilichopokelewa | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| **OC** | | 267,821,860,000 | 166,916,262,293 | 62.32 |
| **Mishahara** | | 175,884,707,000 | 98,467,935,833 | 55.98 |
| **Maendeleo** | **Ndani** | 109,879,593,000 | 119,461,591,501 | 108.72.0 |
| | **Nje** | 70,556,572,000 | 35,182,725,351 | 49.86.0 |
| | **Jumla** | 180,436,165,000 | 154,644,316,852 | 85.71 |
| **Jumla Kuu** | | 624,142,732,000 | 420,028,514,979 | 67.29 |

***Chanzo**: Randama ya Wizara mwaka 2023 na Usanifu wa Kamati.*

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, mwenendo wa upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida ni **asilimia 59.81**. Wastani huu ni chini ya lengo ikilinganishwa na matarajio katika kipindi hicho cha bajeti ambayo ni **asilimia 66.6** ya bajeti iliyoidhinishwa.

### 2.5 Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo Kamati

**Mheshimiwa Spika**, taarifa ya Kamati kuhusu uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2022/2023 pamoja na mambo mengine, ilitoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo tisa **(9)** ili yaweze kuzingatiwa na kutekelezwa na Wizara kwa lengo la kuboresha na kuongeza tija katika utendaji wa sekta ya Maliasili na Utalii.

Katika kikao cha Kamati na Wizara kilichofanyika tarehe 21 Machi, 2023 Kamati ilibaini kwamba, kwa sehemu kubwa Wizara inaendelea na utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilihitaji ufafanuzi wa kina na majibu ya Wizara yalionesha nia njema ya Serikali kuendelea kutekeleza maoni ya Kamati. Kamati inaendelea kusisitiza kwamba, **utekelezaji wa Ushauri, maoni na mapendekezo hayo ufanyike kikamilifu ili kuboresha utendaji wa sekta ya maliasili, utalii, malikale na kumbukumbu za taifa ambazo ni miongoni mwa sekta zinazoliingizia taifa fedha za kigeni ili ziendelee kuchangia zaidi katika pato la taifa, na hivyo kukidhi matakwa ya Ilani ya CCM ya mwaka 2020 (Ibara 67 – 70).**

## SEHEMU YA TATU

### 3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

**Mheshimiwa Spika**, ili kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, Kamati ilichambua na kujadili Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Uchambuzi wa Kamati ulijielekeza katika maeneo yafuatayo:-

a) Makadirio ya Mapato kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

b) Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

c) Ulinganisho wa Bajeti ya Wizara dhidi ya Bajeti ya Taifa;

d) Mambo muhimu yanayogusa sekta ya Maliasili na Utalii

### 3.1 Makadirio ya Mapato kwa mwaka wa fedha 2023/2024

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ya Maliasili na Utalii **(Fungu 69)** imekadaria kukusanya maduhuli ya **shilingi 771,875,687,705/=**. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, makadirio haya yameongezeka kwa **shilingi 108,286,520,984**/= sawa na **asilimia 16.32** ikilinganishwa na makadirio ya mwaka wa fedha 2022/2023 ambayo yalikuwa **shilingi 663,589,166,721**/=

Kati ya makadirio hayo yatakayokusanywa na Wizara **shilingi 572,905,619,470/=** sawa na **asilimia 74.22** ya lengo zitakusanywa kupitia mfumo wa TRA kutoka vyanzo vya TANAPA, NCAA na TAWA. Aidha, **shilingi 198,970,068,234**/= sawa na **asilimia 25.78** ya makadirio zitakusanywa kupitia mfumo wa MNRT - Portal kutoka vyanzo vya idara, mifuko na taasisi za Wizara. . < **Kielelezo Na. 03** kinafafanua zaidi.

Kamati inaipongeza Wizara kwa hatua ya kuongeza makadirio ya mapato katika mwaka ujao wa fedha, kwani inaona uwezekano wa kufikia lengo kutokana na mwenendo wa makusanyo katika mwaka huu wa fedha ambapo Wizara ilikusanya kwa asilimia **asilimia 82**. Aidha, Kamati inashauri Wizara iendelee kuzisimamia kikamilifu, taasisi ambazo zimeonekana kuwa dhaifu katika ukusanyaji wa mapato katika mwaka huu wa fedha ili ziweze kuimarisha mifumo ya ukusanyaji na hivyo kuongeza mapato.

**Kielelezo Na. 3: Ulinganisho wa Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli 2022/2023 na 2023/2024**

| Fungu 69 | 2022/2023 | 2023/2024 | Ongezeko/ Punguzo | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| **Wizara** | 9,507,352,003 | 9,607,000,000 | 99,647,997 | 1.05 |
| **Taasisi** | 184,717,396,125 | 189,363,068,234 | 4,645,672,109 | 2.52 |
| **Kupitia TRA (TANAPA, NCAA, TAWA)** | 469,364,418,596 | 572,905,619,470 | 103,541,200,874 | 22.06 |

*Chanzo: Randama ya Wizara ya mwaka 2023 na Usanifu wa Kamati*

**3.2 Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka 2023/2024**

**Mheshimiwa Spika,** ili iweze kutekeleza malengo na vipaumbele vilivyowekwa katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ya Maliasili na Utalii (**Fungu 69**) inakadiria kutumia **shilingi 642,668,208,000/=** ambazo zinajumuisha fedha za matumizi ya kawaida **shilingi 474,501,449,000/=** sawa na **asilimia 73.83** ya bajeti yote, na **shilingi 168,166,759,000/=** sawa na **asilimia 26.17** ya bajeti yote kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Katika fedha za matumizi ya kawaida **shilingi 184,288,496,000/**= sawa na **asilimia 38.84** ni kwa ajili ya mishahara (PE) na **shilingi 290,212,953,000/=** sawa na **asilimia 61.16** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC).

Aidha, katika fedha za maendeleo **shilingi 109, 879,593, 000/=** sawa na **asilimia 65.34** ni fedha za ndani na **shilingi 58,287,166,000/=** sawa na **asilimia 34.66** ni fedha za nje.

***Mheshimiwa Spika,*** *Kamati ilifanya uchambuzi kwa kulinganisha bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii* ***( Fungu 69)*** *kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na 2023/2024 na kubaini kwamba, Bajeti ya Wizara imeongezeka kwa* **asilimia 2.97** *kutoka* ***shilingi 624,142,732,000/=*** *mwaka 2022/2023 hadi kufikia* ***shilingi 642,668,208,000/=*** *mwaka 2023/2024. Kamati inapongeza hatua hiyo ya Serikali kuona umuhimu wa kuongeza bajeti ya Wizara hii muhimu katika maendeleo ya wananchi na uhifadhi endelevu wa raslimali zetu za asili.*

*Uchambuzi zaidi wa Kamati umebaini kuwa katika maeneo yote kuna ongezeko, isipokuwa kwenye fedha za maendeleo kutoka nje ambazo zimepungua kwa* ***asilimia 17.34*** *ikilinganishwa na fedha zilizotengwa kwenye eneo hilo katika mwaka huu wa fedha.*

*Maeneo mengine ambayo bajeti imeongezeka ni kwenye matumizi mengineyo (OC) kwa* **asilimia 8.36**. na *mishahara (PE) kwa* **asilimia 4.78** *ikilinganishwa na kiasi kilichotengwa mwaka 2022/2023 kama inavyoonekana kwenye* **Kielelezo Na.04.**

**Kielelezo Na. 4 : Ulinganisho wa Bajeti 2022/2023 na 2023/2024**

| Mwaka | Matumizi ya Kawaida | | Maendeleo | |
|---|---|---|---|---|
| | PE | OC | Ndani | Nje |
| 2022/23 | 175,884,707,000 | 267,821,860,000 | 109,879,593,000 | 70,556,572,000 |
| 2023/24 | 184,288,496,000 | 290,212,953,000 | 109,879,593,000 | 58,287,166,000 |
| Ongezeko/ Punguzo | 8,403,789,000 | 22,391,093,000 | 0 | 12,296,406,000 |
| Asilimia -% | 4.78 | 8.36 | 0 | -17.43 |

*Chanzo: Taarifa za Wizara na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza hatua ya kupungua kwa fedha za maendeleo kutoka nje kwani inaonesha dhamira ya Serikali kupunguza utegemezi wa fedha za nje katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwani zimekuwa ama zinatolewa kwa ufinyu au kutototolewa kabisa na hivyo kuathiri utekelezaji wa miradi. Hata hivyo, Kamati ilitarajia kuona ongezeko la fedha za maendeleo ya ndani ili kutoathiri utekelezaji wa miradi iliyopangwa katika mwaka ujao wa fedha, jambo ambalo halijafanyika.

**Ni maoni ya Kamati kwamba, Serikali iendelee kupunguza utegemezi wa fedha za maendeleo kutoka nje, huku ikiongeza fedha za ndani kwenye eneo hilo na hivyo kuwezesha utekelezaji wa miradi iliyopangwa.**

**3.3 Ulinganisho wa Bajeti ya Wizara dhidi ya Bajeti ya Taifa**

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati ulijielekeza pia kwenye ulinganisho wa bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii dhidi ya bajeti ya Taifa. Ulinganisho huo uliangalia bajeti ya Wizara kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 na mwaka wa fedha 2023/2024 dhidi ya bajeti ya Taifa katika kipindi hicho. Matokeo ya uchambuzi wa Kamati ni kwamba:-

a) Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii dhidi ya Bajeti ya Taifa imepungua kutoka **asilimia 1.52** hadi **asilimia 1.45**

b) Bajeti ya Matumizi Mengineyo imeshuka kutoka **asilimia 5.96** hadi **asilimia 5.20.**

c) Bajeti ya mishahara ilipungua kutoka **asilimia 1.81** hadi kufikia **asilimia 1.69**

d) Bajeti ya Maendeleo kutokana na fedha za ndani imeongezeka kidogo kutoka **asilimia 0.91 hadi asilimia 093**

e) Bajeti ya maendeleo kutokana na fedha za nje imepungua kutoka **asilimia 2.08** hadi **asilimia 1.78**

**Kielelezo Na. 5: Bajeti ya Wizara (Fungu 69) dhidi ya Bajeti ya Taifa**

| BAJETI YA WIZARA DHIDI YA BAJETI YA TAIFA 2022/2023 | | | |
|---|---|---|---|
| **AINA** | **BAJETI TAIFA** | **BAJETI YA ARDHI** | **ASILIMIA** |
| **OC** | 4,493,500,000,000.00 | 267,821,860,000.00 | 5.96 |
| **MISHAHARA** | 9,740,800,000,000.00 | 175,884,707,000.00 | 1.81 |
| **MAENDELEO NDANI** | 12,122,100,000,000.00 | 109,879,593,000.00 | 0.91 |
| **MAENDELEO NJE** | 3,399,200,000,000.00 | 70,556,572,000.00 | 2.08 |
| **DENI LA SERIKALI** | 11,308,400,000,000.00 | - | - |
| **JUMLA** | **41,064,000,000,000.00** | **624,142,732,000.00** | **1.52** |
| **BAJETI YA WIZARA DHIDI YA BAJETI YA TAIFA 2023/2024** | | | |
| **AINA** | **BAJETI TAIFA** | **BAJETI YA ARDHI** | **ASILIMIA** |
| **OC** | 5,578,433,000,000 | 290,212,953,000 | 5.20 |
| **MISHAHARA** | 10,882,126,000,000 | 184,288,496,000 | 1.69 |
| **MAENDELEO NDANI** | 11,873,900,000,000 | 109,879,593,000 | 0.93 |
| **MAENDELEO NJE** | 3,282,100,000,000 | 58,287,166,000 | 1.78 |
| **DENI LA SERIKALI** | 12,771,500,000,000 | 0 | |
| **JUMLA** | **44,388,059,000,000.00** | **642,668,208,000.00** | **1.45** |

*Chanzo: Taarifa ya Mapendekezo ya Mfumo na Ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2022/2023 na 2023/2024, Randama ya Wizara ya Maliasili na Utalii 2022/2023 na 2023/2024*

## 3.4 Mambo muhimu yanayogusa sekta ya Maliasili na Utalii.

### 3.4.1 Hatua ya Serikali kuinusuru Hifadhi ya Ngorongoro.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua na kupongeza hatua ya Serikali yenye lengo la kuinusuru hifadhi ya Ngorongoro kwa kuwahamisha kwa hiari wakazi wanaoishi ndani ya hifadhi hiyo. Uamuzi huo wa Serikali unalenga kupunguza ongezeko la watu na mifugo, makazi ya kudumu na holela, shughuli za binadamu zinazotishia kupoteza hadhi ya Hifadhi hiyo kama eneo la urithi wa dunia.

Ingawa Sheria ya Hifadhi ya Ngorongoro (1959) iliweka msingi wa kuendesha hifadhi hii kama eneo la matumizi mseto, (multiple land use), ni ukweli usiopingika kwamba, ongezeko la watu, mifugo na shughuli za kilimo katika eneo hilo vinatishia ustawi wa hifadhi hiyo. Hivyo uamuzi wa Serikali kuhamisha watu kwa hiari kutoka hifadhini ni wa kupongezwa kwani unalenga kuhakikisha uhifadhi endelevu wa eneo la hifadhi ya ngorongoro kwa kizazi cha sasa na vijavyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua na kuipongeza Wizara kwa kubainisha maeneo mbadala ya Handeni - Tanga na Kitwai - Manyara kwa ajili ya makazi ya wananchi wanaohama kutoka hifadhini. Hadi Novemba, 2022 jumla ya kaya 489 zenye watu 2,629 na mifugo 14,094 zilikuwa zimehama. Aidha, kaya 1,524 zenye watu 8,715 na mifugo 32,842 zimejiandikisha kuhama kwa hiari katika awamu zinazofuata.

Tangu kukamilika kwa awamu ya kwanza, muda mrefu (miezi sita) umepita na Serikali haijaanza utekelezaji wa awamu ya pili licha ya kaya nyingi kuonesha utayari wa kuhama. Wizara ilisema iko katika mchakato wa kutafuta fedha kwa ajili ya zoezi hili. Hata hivyo, muda mrefu umepita na Kamati haifahamu kinachoendelea kuhusiana na utekelezaji wa mpango huu. Ni mtazamo wa Kamati kwamba, Serikali isiache zoezi hili likapoa kwani litatoa fursa kwa wapotoshaji na watu wasioitakia mema hifadhi ya ngorongoro kwa kuendelea kueneza propaganda na uzushi kwa lengo la kukwamisha zoezi hili.

Kwa kuwa Wanachi wamehamasika, wameridhia na wako tayari kuhama kutoka hifadhini, Kamati inaishauri Serikali kutoa fedha za

kutosha kwa haraka na kwa wakati ili kukamilisha zoezi hili na wananchi hao wanaosubiri kuhamishwa wasiendelee kusubiri kwa muda mrefu. Kukamilika kwa zoezi hili kutasaidia kuinusuru hifadhi ya ngorongoro dhidi ya uharibifu unaotishia kutoweka kwake kutokana na shughuli za binadamu. Aidha, Serikali iharakishe mchakato wa kufanya marekebisho ya sheria iliyoanzisha Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ili iweze kwenda sambamba na mabadiliko ambayo yematokea.

### 3.4.2 Changamoto ya Wanyama Wakali na Waharibifu

**Mheshimiwa Spika,** Migongano baina ya binadamu na wanyamapori ni moja ya changamoto zinazokabili uhifadhi wa wanyamapori nchini na imekuwa ukisababisha madhara kwa pande zote, kwa wanyama na binadamu kuuawa au kujeruhiwa pamoja na uharibifu wa mazao na mali. Migongano hii inatokana na wananchi kufanya shughuli za kilimo kwenye maeneo ya mapito ya wanyama pori au wanyama kutafuta malisho na maji nje ya hifadhi hasa wakati wa kiangazi.

Kamati inathamini hatua za Wizara katika kukabiliana na hali hii ambazo ni pamoja na kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa kusimamia utatuzi wa migongano baina ya binadamu na wanyamapori (2020-2024) kwa kuendesha doria za kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu, kuelimisha wananchi mbinu za kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu, kufuatilia mwenendo wa migongano na ujenzi wa vituo 16 vya kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu katika maeneo ya kipaumbele hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio hayo Wizara inakabiliwa na changamoto ya upungufu wa Askari wa Uhifadhi, upungufu wa magari, helkopta na pikipiki zitakazotumiwa na Askari Wahifadhi na VGS/mgambo katika doria za kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu. Aidha, ukosefu wa maji na chakula ndani ya maeneo yaliyohifadhiwa kulingana na mahitaji unasababisha wanyamapori watoke nje ya maeneo yao ili kutafuta maji na chakula, na hivyo kukabiliana na binadamu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri Serikali kuchukua hatua stahiki za muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu ili kutafuta ufumbuzi wa changamoto zinazosababishwa na muingiliano baina ya wanyama wakali na waharibifu, na hivyo kuepusha madhara yanayosababishwa na muingiliano huu. Aidha, Wizara ishirikiane na Wizara za kisekta kuongoa shoroba za wanyamapori kupitia zoezi la kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi. Vilevile, Serikali iboreshe viwango vya fidia kwa wananchi kutokana na madhara yanayosababishwa na wanyama ili vizingatie hali halisi ya maisha na thamani ya uharibifu au madhara yaliyotokea.

### 3.4.3 Hali ya Sekta ya Utalii Nchini

**Mheshimiwa Spika,** nchi yetu imejaliwa vivutio vingi vya utalii vinavyohusisha maliasili kama vile wanyamapori, misitu, bahari, maziwa, fukwe nzuri na utamaduni. Vivutio hivi vimeifanya sekta ya utalii kuendelea kutoa mchango mkubwa katika uchumi wa Taifa kwa kuchangia **asilimia 17** ya pato ghafi la taifa, **asilimia 25** ya mauzo yote ya nje na kutoa ajira **1,600,000** kabla ya UVIKO 19.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua na kupongeza jitihada za Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali katika kukuza, kuendeleza na kutangaza vivutio vya utalii hususani, kwa kutumia program maalumu ya *Tanzania - The Royal Tour.* Jitihada hizo zimeongeza idadi ya watalii wa nje kwa asilimia 57.7 kutoka **922,692** mwaka 2021 hadi kufikia watalii **1,454,920** mwaka 2022, na watalii wa ndani kutoka **788,933** mwaka 2021 hadi **2,363,260** mwaka 2022 sawa na ongezeko la **asilimia 199.5.**

Aidha**,** idadi ya wakala wa biashara za utalii waliosajiliwa na kupatiwa leseni imeongezeka kutoka wakala 1,869 mwaka 2018/2019 hadi kufikia wakala 5128 mwaka 2021/2022 sawa na **asilimia 174.4**. Katika kipindi hicho, mapato yaliongezeka kutoka **shilingi bilioni 5.5** kwa mwaka **2018/2019** hadi **shilingi bilioni 7.1** mwaka 2021/2022

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua juhudi za Serikali kupitia Mipango Kabambe ya Kuimarisha Utangazaji wa Utalii kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo 2023/2024 – 2025/2026 ambao utagharimu

**shilingi bilioni 565**. Kamati inapongeza juhudi hizo, hata hivyo ina mashaka iwapo utekelezaji wake utafanikiwa kwani chanzo cha fedha hicho hakijulikani na fedha hiyo haionekani kwenye bajeti ya mwaka ujao wa fedha.

Ni ushauri wa Kamati kwamba, Serikali ishirikishe wadau wa utalii na sekta binafsi katika maamuzi mbalimbali ya kisera ikiwa ni pamoja kugharamia mpango huo ili lengo liweze kufikiwa. Aidha, mpango huo uende sambamba na kuhakikisha kazi nzuri ya kuendeleza na kutangaza utalii nchini iliyofanywa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassani – Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Programu ya ***Tanzania-The Royal Tour*** inakuwa endelevu kwa kuweka mazingira mazuri yatakayoendelea kuvutia watalii kuja nchini.

**Mheshimiwa Spika,** nihitimishe eneo hili kwa kukumbusha kwamba, sekta ya utalii inahitaji uwekezaji mkubwa ili kuleta matokeo yenye tija na mchango stahiki katika pato la taifa. Ni ukweli usiopingika kwamba, licha ya nchi yetu kuwa na vivutio vingi vya utalii, bado vivutio hivyo havijatambuliwa, kuendelezwa na kutangazwa kikamilifu kutokana na changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na ufinyu wa bajeti. Nchi yetu inatenga bajeti ndogo sana ya kutangaza utalii ikilinganishwa na washindani wetu. Kwa mfano katika kipindi cha miaka mitano (2014/2015 - 2018/2019) Tanzania ilitumia Dola za Marekani milioni 8.4 **(shilingi bilioni 19.56)** kuitangaza sekta ya utalii, wakati nchi tatu za Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara, ambazo ni washindani wakubwa wa Tanzania, zilitumia kati ya Dola za Marekani milioni 49.4(**shilingi bilioni 114.40)**; Dola milioni 116.7 (**shilingi bilioni 271.9)** na Dola milioni 330.5 (**shilingi bilioni 770.07)** mtawalia. **Kielelezo Na.06** kinafafanua zaidi.

**Kielelezo Na. 6 Bajeti ya kutangaza Utalii ya Tanzania dhidi ya Washindani wakubwa Kusini mwa Jangwa la Sahara**

| Mwaka | Tanzania | Nchi "M" | Nchi "K" | Nchi "S" |
|---|---|---|---|---|
| 2014/15 | 1,700,000 | - | 7,900,000 | 56,100,000 |
| 2015/16 | 900,000 | 9,800,000 | 10,600,000 | 62,200,000 |
| 2016/17 | 2,600,000 | 14,000,000 | 42,300,000 | 65,300,000 |
| 2017/18 | 1,700,000 | 11,900,000 | 25,400,000 | 71,300,000 |
| 2018/19 | 1,500,000 | 13,400,000 | 30,500,000 | 75,600,000 |
| JUMLA | 8,400,000 | 47,000,000 | 116,400,000 | 330,500,000 |

*Chanzo: Bodi ya Utalii Tanzania na usanifu wa Kamati*

### 3.4.4 Utendaji wa Taasisi za Uhifadhi

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maliasili na Utalii inasimamia taasisi nne za uhifadhi nchini ambazo ni Mamlaka ya Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA) na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA).

Kamati inatambua kazi nzuri ambayo imekuwa ikitekelezwa na taasisi hizi ambazo zimechangia kuboresha uhifadhi nchini na hivyo kukuza sekta ya utalii inayotokana na wanyamapori, utalii wa misitu, picha na uwindaji. Mfano, kutokana na utendaji wake TANAPA iliweza kupata tuzo mbalimbali ikiwemo Tuzo ya Hifadhi Bora Barani Afrika ambapo Serengeti ilishinda kwa miaka minne mfululizo (2019, 2020, 2021 na 2022) inayotolewa na "World Travel Awards na Hifadhi ya Taifa Serengeti ilitangazwa na gazeti maarufu duniani la "Forbes" kuwa moja ya vivutio bora duniani vya utalii kutembelea kwa mwaka 2021.

Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyapoti Tanzania (TAWA) tangu ilipoanzishwa ili kuchukua majukumu ya kiutendaji ya Idara ya Wanyamapori kuhusu usimamizi wa rasilimali ya wanyamapori nje ya Hifadhi za Taifa na Hifadhi ya Ngorongoro, imekuwa ikifanya kazi nzuri sana katika uendeshaji wa Mapori ya Akiba na Mapori Tengefu.

**Mheshimiwa Spika**, taasisi hizi zimekuwa zikifanya vizuri sana katika ukusanyaji wa mapato. Taasisi hizo ambazo ukusanyaji wa mapato

umekuwa ukitekelezwa kupitia mfumo wa TRA, zimekuwa zikifanya vizuri ikilinganishwa na taasisi ambazo ukusanyaji wa mapato unafanyika kupitia mfumo wa MNRT Portal. Kwa mfano katika mwaka huu wa fedha hadi Februari, 2023 taasisi hizo zilifanikiwa kukusanya mapato kwa wastani wa asilimia 87.67 (TAWA 69%, NCAA 90% na TANAPA 104%)

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kufanya vizuri taasisi hizi zimekuwa zikikabiliwa na changamoto kadhaa. Changamoto hizo ni pamoja:-

i. Ufinyu wa bajeti. Bajeti inayotengwa kwa ajili ya taasisi hizi ni ndogo sana ikilinganishwa na majukumu ambayo zinatekeleza, hasa kwa kuzingatia kwamba, TAWA na TANAPA zina mtawanyiko mkubwa wa hifadhi za taifa (remoteness and distribution of national parks), mapori ya akiba na mapori tengefu. TANAPA inasimamia hifadhi za taifa 22 na TAWA inasimamia mapori 32. Hata hivyo bajeti inayotengwa kwa taasisi hizi bado imekuwa chini ya uhitaji halisi.

Mfano katika mwaka wa fedha 2022/2023, TANAPA iliidhinishiwa shilingi **bilioni 105** kwa ajili matumizi mengineyo (OC) wakati mahitaji halisi yalikuwa shiling**i bilioni 222**. Hadi mwaka wa fedha 2019/2020 wakati TANAPA ikihudumia hifadhi 16 zenye ukubwa wa kilomita za mraba 57,000 bajeti ya OC ilikuwa shilingi **bilioni 104**. Mwaka wa fedha 2019/2020 TANAPA iliongezewa hifadhi sita (6) zenye eneo la ukubwa wa mita za mraba 47,471 na kufanya eneo lote ambalo TANAPA inalisimamia kuwa na ukubwa wa kilomita za mraba 104,578 (sawa na asilimia 11.6 ya eneo lote la nchi) na ndipo OC ikaongezeka hadi **shilingi bilioni 105.**

ii. Upungufu wa watumishi. Mfano taasisi za uhifadhi wa wanyamapori zina upungufu wa jumla ya askari wahifadhi 1,687 (TANAPA 466, NCAA 290 na TAWA 931);

iii. Upungufu wa magari, helikopta na pikipiki zitakazotumika na askari wahifadhi na VGS/mgambo katika doria za kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu; na

iv. Ukosefu wa maji na chakula ndani ya maeneo yaliyohifadhiwa kulingana na mahitaji na kusababisha mtawanyiko wa wanyamapori kutoka nje ya maeneo yaliyohifadhiwa kwa ajili ya kutafuta maji na chakula.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, baada ya ukaguzi wa miradi iliyotengewa fedha katika mwaka huu wa fedha, uchambuzi wa kina kuhusu taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023 na taarifa ya makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kwa Wizara ya Maliasili na Utalii (Fungu 69), ninaomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kama ifuatavyo:-

### i. Migogoro katika maeneo ya hifadhi

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwa na migogoro baina ya wananchi na maeneo ya hifadhi, ambayo inachangiwa na kukosekana kwa uelewa wa kutosha kwa wahifadhi na wananchi kuhusiana na mipaka sahihi ya hifadhi. Hali hiyo, inasababisha uhasama kati ya wananchi na mamlaka kwenye maeneo ya hifadhi, pale Serikali inataka kuwandoa wananchi waliovamia maeneo ya hifadhi, kuanzisha hifadhi au kurekebisha mipaka ya hifadhi. Ili kurekebisha hali hiyo Kamati inashauri mambo yafuatayo:-

(a) Wananchi waelimishwe vya kutosha kuhusiana na mipaka ya hifadhi ili watambue kwamba wako kwenye maeneo ambayo hawapaswi kuwepo kwa mujibu wa sheria;

(b) Serikali itumie taratibu stahiki zenye staha wakati wa kuwaondoa wananchi ambao wamevamia maeneo ya hifadhi ili kuondoa uwezekano wa kuleta uhasama baina ya wananchi hao na mamlaka za uhifadhi;

(c) Serikali ihakikishe wananchi na wawakilishi wao wanashikirikishwa kikamilifu katika kila hatua inayochukuliwa kutatua migogoro

ambayo imebainishwa kati ya hifadhi na wananchi ikiwa ni pamoja na kuweka mipaka;

(d) Serikali iweke mpango mkakati wa kujenga barabara kuzunguka Hifadhi za Taifa hasa zenye migogoro ili zitumike kama mipaka; na

(e) Kuwe na ushirikishwaji wa Wizara za kisekta na taasisi nyingine za Serikali zinazohusika na masuala ya hifadhi na ardhi, wakati wa uwekaji wa alama za mipaka, uanzishwaji wa hifadhi au uanzishwaji wa vijiji.

**ii. Utambuzi na utangazaji wa vivutio vingine vya utalii**

**Mheshimiwa Spika**, nchi yetu imebarikiwa kuwa na vivutio vingi vya utalii ambavyo bado havijatambuliwa na kutangazwa kikamlifu ili viweze kuchangia katika mapato ya nchi. Vivutio hivyo ni pamoja na utalii wa fukwe, utalii wa malikale, utalii wa mikutano na utalii wa misitu. Kamati inashauri yafuatayo:-

(a) Serikali iandae na kutekeleza kikamilifu mikakati madhubuti ya kutambua na kutangaza vivutio vingine vya utalii kama ilivyo kwenye utalii wa wanyama ili kuongeza wigo wa mapato yatokanayo na utalii;

(b) Serikali izitumie Mamlaka za Serikali za Mitaa kuibua na kutangaza vivutio vya utalii ambavyo viko katika maeneo hayo ili kuviwezesha kuchangia katika uchumi wa maeneo husika, pamoja na pato la taifa kwa ujumla;

(c) Serikali ishirikishe sekta binafsi na wadau wengine wa sekta ya utalii katika kuibua na kutangaza vivutio vipya vya utalii nchini jambo litakalowezesha kuvifanya vifahamike na kuvutia watalii;

**iii. Upatikanaji hafifu wa fedha za maendeleo**

**Mheshimiwa Spika,** upatikanaji hafifu wa fedha za maendeleo unaathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kusababisha ikwame au kuchelewa kukamilika na hivyo kuathiri mazingira ya hifadhi zetu. Kamati inashauri yafuatayo:-

(a) Serikali itenge na kutoa fedha za maendeleo za kutosha na kwa wakati ili kuwezesha utekelezaji wa miradi kwa wakati na hivyo kufikia malengo yaliyokusudiwa;

(b) Serikali iendelee kupunguza utegemezi wa fedha za nje kwenye utekelezaji wa miradi kwani upatikanaji wake siyo wa uhakika, jambo linaloathiri utekelezaji wa miradi; na

(c) Serikali iongeze fedha za ndani kwenye utekelezaji wa miradi kwani zimekuwa na uhakika katika upatikanaji wake.

**iv. Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania (TAWA)**

**Mheshimiwa Spika**, taasisi hii ilianzishwa kwa amri ya kisheria *(establishment order)* na chini ya kifungu cha 8 cha Sheria ya Kuhifadhi Wanyamapori Na. 5 ya mwaka 2009 ili kiweze kusimamia mapori ya akiba, mapori tengefu, jumuiya za hifadhi ya wanyamapori na maeneo ya ardhi oevu. Aidha, kazi za chombo hiki zinasimamiwa na Bodi ya Ushauri badala ya Bodi ya Utendaji, jambo linaloathiri utendaji wake kwani bodi hiyo haina nguvu ya kisheria katika kutekeleza majukumu yake.

Kamati imekuwa ikiishauri Serikali kukamilisha mchakato wa kuwasilisha Bungeni Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya Wanyamapori itakayobainisha majukumu ya chombo hiki na kuanzisha bodi ya utendaji yenye nguvu ya kisheria katika kutekeleza majukumu ya kukisimamia chombo hiki. Hata hivyo, ushauri wa Kamati umekuwa hauzingatiwi jambo ambalo linaisikitisha. Kamati inaendelea kusisitiza Wizara izingatie na kutekeleza ushauri wake, kwani unalenga kuwezesha uwepo wa Bodi ya utendaji yenye nguvu ya kisheria, itakayosimamia kikamilifu utendaji wa TAWA.

**v. Kasi ya Ukusanyaji wa Maduhuli kwa mfumo wa MNRT - Portal**

**Mheshimiwa Spika**, kasi ya ukusanyaji wa maduhuli kwenye Wizara na Taasisi zake ambazo zinakusanya kupitia mfumo wa MNRT Portal iko chini (asilimia 52) ikilinganishwa na taasisi ambazo zinakusanya kupitia mfumo wa TRA (asilimia 87) hadi kufikia robo ya tatu ya mwaka wa bajeti. Kamati inashauri yafuatayo:-

(a) Serikali iwasimamie kikamilifu Watendaji wa taasisi ambazo zinakusanya maduhuli kwa mfumo wa MNRT - Portal ili kuhakikisha wanaongeza kasi ya ukusanyaji;

(b) Wizara iweke viashiria muhimu vya kiutendaji (KPI) kwa watendaji wa taasisi na idara zake na kuwawekea malengo ambayo wanapaswa kuyafikia katika utendaji ikiwa ni pamoja na ukusanyaji wa mapato;

(c) Aidha, Serikali iendelee kuongeza ubunifu katika kutangaza na kuvitambulisha vivutio vya utalii nchini ili kuwavutia watalii wa nje na ndani kwa lengo la kuongeza mapato na kuboresha maisha na ustawi wa jamii;

**vi. Mradi wa Usimamizi wa Maliasili na Kuendeleza Utalii Kanda ya Kusini (REGROW)**

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa mradi huu umesaidia kuboresha miundombinu katika hifadhi, utatuzi wa migogoro baina ya wanyama na binadamu, pamoja na uwezeshaji wa shughuli za kiuchumi ambazo zimesaidia kuimarisha uhifadhi na kuongeza kipato kwa wananchi wa maeneo yanayozunguka hifadhi. Kamati inashauri yafuatayo:-

(a) Serikali iharakishe utekelezaji wa awamu ya kwanza ili kuwezesha kuanza kwa utekelezaji wa awamu zinazofuata;

(b) Serikali ifanye tathmini ya kutosha kuhusu utekelezaji wa mradi huu ili hifadhi nyingine ziweze kunufaika na mradi huu katika awamu ya pili ya mradi; na

(c) Serikali iharakishe mkakati wa kujenga viwanja vya ndege sita katika hifadhi za Ruaha, Mikumi na Nyerere ili kurahisisha usafiri kwa watalii wa ukanda wa kusini.

**vii. Sera, sheria na kanuni zilizopitwa na wakati**

**Mheshimiwa Spika**, changamoto zinazoshuhudiwa katika sekta ya utalii, maliasili, malikale na kumbukumbu za taifa kwa sehemu kubwa

zinachangiwa na sera, sheria na kanuni zilizopitwa na wakati. Mfano ni Sera ya Taifa ya Misitu (1998); Sera ya Taifa ya Utalii (1999); Sera ya Taifa ya Ufugaji Nyuki (1998) na Sheria ya Mambo ya kale Na. 2 ya mwaka 1964 na marekebisho yake ya mwaka 1979.

Kamati inaishauri Serikali ikamilishe mchakato wa kuzipitia sera na sheria hizo na nyingine ambazo zimepitwa na wakati ili kuwezesha utendaji wa sekta hizi ambao utaendana na mabadiliko na maendeleo yaliyopo katika sekta hizi ulimwenguni na hivyo kuwezesha kupatikana kwa tija stahiki.

**SEHEMU YA TANO**

**5.0 HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, napenda kutumia fursa hii kwa niaba ya Kamati kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge, kwa namna ambavyo mmekuwa mkitimiza majukumu yenu kwa weledi na umakini mkubwa na hivyo kuliwezesha Bunge letu Tukufu kutimiza wajibu wake kwa ufanisi.

Aidha, nawashukuru kwa moyo wa dhati Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, kwa ushirikiano na jinsi walivyojitoa kikamilifu katika kipindi chote cha ziara za ukaguzi wa miradi iliyotengewa fedha na uchambuzi wa bajeti ya wizara hii hadi kukamilika kwa taarifa hii. Kwa umuhimu wake, natamani kuwatambua Wajumbe wa Kamati kwa kutaja majina yao. Hata hivyo, kwa kuzingatia ufinyu wa muda tulionao naomba majina yao kama yalivyoorodheshwa katika taarifa hii yaingie kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard). Majina ya Wajumbe hao ni haya yafuatayo:-

1. Mhe. Timotheo Paul Mnzava, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Najma Muntazar Giga, Mb – Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Shaabani Omar Shekilindi, Mb
4. Mhe. Cecilia Daniel Paresso, Mb
5. Mhe. Innocent Seba Bilakwate, Mb
6. Mhe. Ester Lukago Midimu, Mb
7. Mhe. Khalifa Salum Suleiman, Mb

8. Mhe. Maida Hamadi Abdallah, Mb
9. Mhe. Josephine Thabita Chagula, Mb
10. Mhe. Neema William Mgaya, Mb
11. Mhe. Alaudin Hasham Salim, Mb
12. Mhe.Nancy Hassan Nyarusi, Mb
13. Mhe. Festo Richard Sanga , Mb
14. Mhe. Asia Abdulkarimu Halamga, Mb
15. Mhe. Taska Restituta Mbogo, Mb
16. Mhe. Suleiman Haroub Suleiman, Mb
17. Mhe. Oliver Daniel Semuguruka, Mb
18. Mhe. Lucy Thomas Mayenga, Mb
19. Mhe. Agnes Mathew Marwa, Mb
20. Mhe. Munira Mustafa Khatib, Mb
21. Mhe. Dkt. Florence G. Samizi,Mb

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kuwashukuru Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa (Mb) na Naibu Waziri, Mhe. Mary Masanja (Mb) kwa ushirikiano wao mkubwa kwa Kamati ambao umechangia kuiwezesha Kamati kutekeleza shughuli zake kwa ufanisi hasa katika sekta hii.

Nawashukuru pia watendaji wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii chini ya uongozi wa Katibu Mkuu, Dkt. Hassan Abbasi, akisaidiwa na Naibu Katibu Mkuu, Ndg Ludovick Nduhiya, kwa ushirikiano na mchango wao kwa Kamati katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya kikanuni ya Kamati.

Mwisho lakini si kwa umuhimu, kwa namna ya pekee namshukuru Katibu wa Bunge, Ndg. Nenelwa Mwihambi (*ndc*), kwa kuongoza vyema uratibu wa shughuli za Kamati na Bunge kwa ujumla. Aidha, namshukuru Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndg. Michael Chikokoto (*ndc*), Makatibu wa Kamati hii Ndg. Haika Mtui na Ndg. Chacha Nyakega, wakisaidiwa na Ndg. Pauline Mavunde, kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kuhakikisha maandalizi ya taarifa hii yanakamilika kwa wakati. Aidha, nawashukuru Watumishi wote wa Bunge kwa mchango wao kwa Kamati inapotekeleza majukumu yake.

Baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu lipokee na kuijadili taarifa hii na likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii (**Fungu 69**), kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja hapo awali.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja na ninaomba kuwasilisha.

Timotheo Paul Mnzava, Mb
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII**
02 Juni, 2023

**SPIKA:** Ahsante sana Makamu Mwenyekiti kwa wasilisho hilo kwa niaba ya Kamati.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea na ratiba yetu, wapo wageni ambao hawakupata nafasi humu ndani wakati tukitangaza. Sasa niwatangaze. Wapo wageni 18 wa Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa ambaye ni Waziri wa Maliasili na Utalii na hawa ni viongozi wa Chama cha Mapinduzi kutoka Wilaya ya Rufiji, wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Rufiji, Ndugu Rajabu Omary Mbonde. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni 90 wa Mheshimiwa Zaytun Swai ambao ni wanafunzi wa *Nalopa School* kutoka Jijini Arusha. Tunao pia wageni 11 wa Mheshimiwa Riziki Lulida ambao ni viongozi na wanachama wa *Habari Conservation Organisation* kutoka Jijini Dodoma. Tunao wageni 31 wa Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma kutoka Manyoni, Mkoa wa Singida. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo pia wanafunzi 100 na walimu 15 kutoka Shule ya Msingi Barbra ya Jijini Arusha, hawa wamekuja kwa ajili ya mafunzo. Karibuni sana wageni wetu Bungeni. *(Makofi)*

Baada ya kusoma tangazo hilo la wageni, tunaanza uchangiaji. Wapo Wabunge ambao wameleta majina yao hapa wakiwa na jambo la kusema katika Wizara hii kwa maana ya ushauri. Tutaanza na Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, atafuatiwa na Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, ajiandae.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nitoe mchango wangu kwenye Wizara hii ya Maliasili na Utalii. Awali ya yote nianze kwa kumpongeza sana kwa dhati kabisa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna alivyoamua kutoa mwelekeo wa jinsi anavyotaka sekta hii ifanye kazi, lakini namna anavyotaka Watanzania wanufaike na sekta hii ya uhifadhi, lakini pamoja na utalii kwenye nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda nitakwenda haraka kwenye maeneo matatu. Eneo la kwanza, nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu yote ya Wizara na taasisi zao zote kwa kupata imani ya Mheshimiwa Rais kuendelea kuongoza Wizara hii. Mheshimiwa Waziri nimesema nimpongeze kwa sababu, yako mambo mawili nataka kumshauri yeye na wenzake kwenye Wizara.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza Mheshimiwa Waziri, nimekupongeza ili nikushauri. Pamoja na kuwa Waziri wa Wizara hii, Wizara hii ni muhimu, taasisi za uhifadhi zinafanya kazi kubwa na kazi nzuri. Nakuomba usiwe Waziri tu, ukawe baba na ukawe mlezi wa Wizara hii. Ukawe baba na ukawe mlezi wa watumishi wa sekta na taasisi zote zinazosimamiwa na Wizara yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ninalotaka kumshauri Mheshimiwa Waziri, kwa miaka kadhaa tumekuwa na changamoto kidogo kwenye Wizara hii. Kila ukija uongozi yanakuja mambo mapya, zinakuja kauli mpya, inakuja mikakati mipya; nakuomba kwenye awamu yako uache alama. Katengeneze mifumo ya uhakika itakayoweza kufanya kazi kwenye Wizara hii, hasa kwenye eneo la sekta ya utalii ili utalii uweze kufanya vizuri ulete matokeo kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ninalotaka kulizungumza ni kuhusu wanyama wakali na waharibifu. Changamoto hii ni kubwa sana na iko kwenye maeneo mengi. Ni changamoto ambayo inawatesa na kuwaumiza sana wananchi wetu, malalamiko na manung'uniko ya wananchi yamekuwa makubwa. Ukienda Korogwe, zaidi ya kata nane tembo wanaharibu mazao ya wananchi, tembo wanaua na wanaharibu mali za wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natambua, nathamini na kupongeza juhudi kubwa inayofanywa na Serikali. Imefanyika kazi kubwa sana kuanzisha vituo vya Askari, kuongeza Askari wa Doria, kununua magari, kununua pikipiki, lakini kubwa sana ni utayari wa Serikali kuendelea kulipa kifuta machozi kwa wananchi wetu. Mambo haya ni makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo haya ambayo Serikali imefanya, bado tatizo hili ni kubwa, lazima kama nchi na Serikali mjue yako mambo lazima tuendelee kuyafanya. Jambo la kwanza nishauri, Wizara hii iwe *serious* kwenye shughuli ya kuongoa shoroba zetu. Pili, mapitio ya Wanyama, mapito ya wanyama yaweze kutambulika vizuri na yasilete madhara kwa watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili. Tujifunze kwenye nchi nyingine teknolojia mbalimbali za namna ya kukabiliana na hali hii ili tuwasaidie wananchi wafanye kazi zao kwa amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, Mheshimiwa Waziri amesema, moja ya changamoto na sababu kubwa ya changamoto hii ni ongezeko kubwa la watu na ongezeko kubwa la shughuli za kibinadamu. Kwa mujibu wa Taarifa za Sensa, mwaka 2022 tulikuwa na watu milioni 44 na ukiangalia idadi ya watu mwaka 2022 ukilinganisha na sensa ya mwisho 2002 nyuma yake, ongezeko lilikuwa ni la asilimia 2.7. Sensa ya mwaka 2022 tumefika Watanzania milioni 61,741,000 na wastani wa ongezeko la watu kwa mwaka kwa mujibu wa Taarifa za Sensa ni asilimia 3.2. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ongezeko hili siyo dogo. Unaweza kutumia ongezeko hili kuvuta picha ya miaka 10 inayokuja hali itakuwaje?

Miaka 20 inayokuja hali itakuwaje? Tukiendelea kupiga kelele hapa bila kuweka mikakati madhubuti hatuwezi kumaliza jambo hili.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali; Wizara ya Ardhi, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Wizara ya Mifugo, Wizara ya Kilimo tukae pamoja tuweke mpango wa kupanga nchi hii. Haiwezekani tukalima kila mahali, haiwezekani tukachunga kila mahali, haiwezekani tukajenga kila mahali, lazima tuje na mkakati wa Kitaifa wa kupanga nchi yetu ili mambo haya yaweze kwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la mwisho ninalotaka kuchangia siku ya leo ni zoezi la kuhamisha watu kwa hiyari kutoka kwenye Hifadhi, Eneo la Ngorongoro. Nakushukuru Mheshimiwa Waziri amelisema vizuri kwenye hotuba yake na ametoa tamko kwamba halijasitishwa na hakuna mabadiliko yoyote. Ninamshukuru sana na ninampongeza kwa jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mpaka mwezi Novemba mwaka 2022 na kwenye Taarifa ya Kamati tumesema, kaya ambazo zilikuwa zimeshahama ni 489, watu 2,629 na mifugo 14,000, lakini tunapozungumza tangu wakati huo wa Novemba, tayari kuna kaya 1,524 zimejiandikisha na ziko tayari kuhama ambazo hizi kaya zina watu 8,715. Hizi kaya zina mifugo 32,842 pamoja na tamko ambalo amelitoa Mheshimiwa Waziri. Nafurahi kwamba nachangia wakati Waziri Mkuu, ambaye ndio Mtendaji Mkuu wa shughuli za Serikali akiwa ndani ya ukumbi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri anasema jambo hili halijasimama na hakuna mabadiliko, lakini tangu tumemaliza awamu ya kwanza ya kuhamisha watu kutoka Ngorongoro ni miezi sita. Mlikuja kwenye Kamati mwezi wa Pili na mwezi wa Tatu mkasema mna mipango ya kutafuta fedha. Tumekaa miezi sita, fedha hazijapatikana? Kwa nini zoezi hilo haliendelei? Sawa ametuambia kwamba jambo hili lipo na halijabadilika, lakini haiwezekani kwa zoezi kubwa, kwa zoezi muhimu kama hili ambalo Bunge hili tulilibariki, nchi hii imelikubali, inakwenda kuiokoa na kulinusuru eneo la Hifadhi ya Ngorongoro tukakaa miezi sita tunasubiri. Tunasubiri nini miezi sita? Hizi

kaya zaidi ya 1,000 zipo tayari zinasubiri. Zinasubiri kwa muda gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inawezekana jambo hili likawa siyo la maliasili peke yake. Nimesema nimefurahi kwa sababu Waziri Mkuu yupo. Tunapokwenda kuhitimisha bajeti hii ya maliasili Serikali ituambie. Pamoja na kauli kwamba kazi hii inaendelea na jambo hili halijabadilika, mtuambie tumekwama wapi? Ni kwa nini jambo hili haliendi mbele? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, athari ya jambo hili ni kwamba likipoa, yanaanza mambo mengine ya ajabu ajabu. Mmeona watu wamekwenda mpaka Ulaya kuanza kushitaki, wameanza kulalamika, tumerudishwa nyuma. Inawezekana labda kuna mtu anataka kuhujumu hili zoezi. Kama hakuna mtu anataka kuhujumu suala la kuhamisha watu Ngorongoro tukiwa tunahitimisha bajeti hii, Wizara, Serikali kwa ujumla mtuambie. Msituambie tu maneno kama zoezi linaendelea, mtuambie mmefika wapi? Kama kuna changamoto, ni nini? Tunataka kuona zoezi hili likikamilika ili tuendelee na hatua nyingine za mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma na Mheshimiwa Festo Richard Sanga, ajiandae.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii nami niweze kuchangia hotuba hii kwenye siku Tukufu, leo siku yetu ya Ijumaa. Namshukuru sana Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Spika, nianze kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa aliyoifanya kwenye utalii na nikubaliane kabisa na Mheshimiwa Waziri alivyosema kwamba, Mheshimiwa Rais anastahili kuwa mhifadhi namba moja. Amefanya juhudi kubwa tumeziona katika kuhakikisha kwamba, nchi yetu inafunguka katika suala zima la utalii, pamoja na juhudi nyingine zote alizofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya kwenye nchi yetu, Mheshimiwa Waziri wa Maliasili pamoja na timu yake nzima kwa kazi kubwa wanayoifanya. Tumeona Mheshimiwa Rais amepambana sana kuifungua nchi yetu, kuhakikisha watalii wanaongezeka kwa kiasi kikubwa sana. Hiyo ndiyo imesababisha kuongeza mapato yetu ya Serikali kwa sababu ya kuona kwamba watalii wetu wanaongezeka kwa kiasi kikubwa sana. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa maana ya Waziri pamoja na msaidizi wake, pamoja na Katibu Mkuu na Menejimenti yao nzima kwa sababu, inaonekana kabisa upele umepata mkunaji. Kwa kweli, wanafanya kazi kubwa sana kwenye suala zima la maliasili, mimi nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watalii tulionao sasa haijawahi kutokea toka tupate uhuru. Ni watalii wengi sana wameingia. Ndivyo hivyo tunavyoenda kupata mapato mengi sana ya Serikali. Mapato yameongezeka kwa kiwango kikubwa, tumemsikia Waziri na Mwenyekiti wa Kamati ameongea hapa, nawapongeza sana. Narudi kumpongeza Rais kwa kufungua nchi yetu kidemokrasia, kiuchumi, na sasa nchi yetu inaaminika kwa kiasi kikubwa. Hii ni kazi nzuri iliyofanywa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nimefurahi sana na kaulimbiu ya watu wa Maliasili inayosema Wakati ni Sasa. Nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeona wakati anaongea watalii ni wengi, lakini tunajua kabisa vyumba vya hoteli ni vichache. Nawaomba, tumeambiwa Wakati ni Sasa, hii ni fursa, Waheshimiwa Wabunge twendeni tukakope tukajenge hoteli. Huu ni muda sasa wa kuwatangazia Watanzania, wananchi wetu, hizi ni fursa ambazo tunazitaka. Tukajenge hoteli, hoteli ya kitalii unaweza ukaweka tu chumba cha matofali ya kuchoma, ukaezeka manyasi na ukapata Dola 100, Dola 200 kwa siku. Kwa hiyo, hii ni fursa, tunakupongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kuendelea kufanya kazi ya kuweka vivutio

vikubwa na hatimaye kupata fursa ya Watanzania. Wakati ndiyo huu, nami nakubali Wakati ni Sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika na ndugu zangu Watanzania, wakati huu ndiyo wakati na sisi kufanya biashara zetu. Mama amefungua nchi. Kwenye nchi yenyewe ameleta maendeleo, lakini anataka na sisi Watanzania tupate maendeleo kupitia sekta hii ya utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi inasema kufikia 2025 tunatakiwa tuwe na watalii 5,000. Naamini sana Wizara hii chini ya Mheshimiwa Mchengerwa, kwa kazi kubwa anayoifanya, tunaamini 2025 tutakuwa na watalii zaidi ya 10,000, na hii itabaki kuwa ni sifa yetu Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende moja kwa kwenye suala la changamoto ya vijiji na hifadhi. Tumeona changamoto ni kubwa, wananchi wanalalamika sana kutokana na Sheria ya Ardhi na hifadhi kuingiliana. Niwaombe wataalamu wetu, kama alivyosema Mbunge aliyepita, mdogo wangu, Mheshimiwa Mnzava, mkae hizi taasisi zote kwa pamoja mziangalie sheria zenu upya mziweke vizuri ili kwenda kutoa malalamiko kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, tunamwona Mheshimiwa Waziri Mchengerwa amekwenda Mbeya, lakini amekwenda Tarime kulikuwa na shida kubwa, amekaa tena na wale watu vizuri. Kuna watu walikuwa wamesusa wamerudi; Mheshimiwa Mchengerwa tunakupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeangalia mimi mwenyewe kwenye *YouTube* ukiongea pale Tarime, Mbunge umeongea naye vizuri, Mwenyekiti wa Chama na wale watu waliorudi. Kwa kweli wewe uko kwenye Serikali kama Waziri lakini wewe kweli ni Mjumbe wa *NEC,* unaangalia Chama chako cha Mapinduzi; nakupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye mikakati yenu umetutajia mikakati 10, nakupongeza sana kwa mikakati yote hiyo 10 uliyoitaja, pamoja na ununuzi wa helikopta, kuongeza askari, lakini mmesema kuweka

mazungumzo na wale watu waliopo kwenye changamoto, lakini kuwapa elimu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri asichoke, yeye hii ni Serikali yake, ni chama chake, asichoke na wataalamu wake kuwapa watu elimu kwa utaratibu, kuongea nao kwa heshima na unyenyekevu, wale ndio wapigakura wetu, lazima tuongee nao vizuri. Hatukatai kwamba wanafanya makosa, lakini waelimishwe kwa utaratibu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Esther Matiko.

Umeshazima kisemeo? Kuna mtu kisemeo chake kimewaka humu ndani ndiyo maana cha kwake hakiwaki. Nani amewasha kisemeo? Unaonesha kwa mkono sasa sijui unaonsha wapi. Tayari? Nani mwingine amewasha kisemeo ambaye hajaruhusiwa kusema?

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, tayari imekubali.

**SPIKA:** Haya.

**TAARIFA**

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Ninataka nimpe taarifa mchangiaji, ali-*quote* Ilani ya Chama Cha Mapinduzi akaonesha kwamba imeonesha kwamba kufikia 2025 watalii wawe 5,000. Ninataka tu niwambie asiache hiyo *figure* ikaenda hivyo, maana kasema 10,000; *target* ni milioni tano, kwa sababu sasa hivi tuko kwenye *million plus,* sasa akisema 5,000 inamaana unafupisha zaidi, unaturudisha nyuma zaidi. Kwa hiyo naomba tu arekebishe vizuri kwamba ni milioni tano na kuelekea kwenye milioni kumi, siyo watalii 5,000.

Mheshimiwa Spika, ni hiyo tu taarifa ndogo sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, kwa sababu Mheshimiwa Esther ni mdogo wangu nimeipokea, kuwa anataka kuonekana tu. Naomba niendelee.

Mheshimiwa Spika, tunajua wazi kazi kubwa inayofanywa na Wizara na tunaendelea kuwapongeza sana. Lakini Mheshimiwa Mchengerwa umekuwa Waziri wa mfano, wewe ni mnyenyekevu na mchapakazi, wala huinui mabega yako juu, ukikuta *missed call* ya mtu hata uko *busy* jioni utampigia; tunakupongeza sana.

Mheshimiwa Spika, niongee kuhusu Tabora. Mheshimiwa Waziri naomba uandike na kalamu yako, Katibu Mkuu wewe umeoa Tabora, tena umeoa Ukoo wa Fundikira, tunaomba uandike haya ninayoyaongea. Tabora hakuna watalii hata kidogo ingawa tuna vivutio vingi. Cha kwanza, tuna Mbuga ya Ugalla lakini hakuna hoteli nzuri na wala hakuna barabara ya kutupeleka huko Ugalla, pia hakuna mawasiliano kwa maana ya simu. Tunaomba sana Mheshimiwa Waziri uliangalie hilo, lakini mtu-*link* na ofisi za *tours* za Arusha na wapi, watu watakapokuja waelekezwe maana ta Tabora, Ugalla n.k.

Mheshimiwa Spika, Tabora tuna Ngome ya Jeshi ya Mjerumani ambayo sasa hivi ni Ngome ya Jeshi. Kuna handaki inatoka chini kwenye ngome mpaka *railway station,* walikuwa wanakamwatwa watumwa wanapelekwa kupandishwa treni chini ya ardhi. Tunaamini huo utakuwa utalii mkubwa kama mkiamua kuutangaza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna Waarabu walikuja pale kwa ajili ya kukamata watumwa wakajenga jengo kubwa ambalo alikuja kukaa David Livingstone, na walikuwa watumiwa kutoka Congo, Rwanda, Burundi na Kigoma, wanafikia pale Tabora ndipo wanasafirishwa kupelekwa Bagamoyo, Zanzibar na hatimaye Uarabuni; vyote hivyo ni vivvutio vikubwa sana ambavyo vipo katika Mkoa wetu wa Tabora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, 1958 ulifanyika Mkutano Mkuu wa *TANU* pale Tabora na kujenga Mnara ulioandikwa Uamuzi wa Busara, ndipo palipotokea vuguvugu la kupata Uhuru mwaka 1961. Vuguvugu lile

lilitokea Mkoa wa Tabora, tulipiga kura tatu, ya Muasia, ya Mzungu na Mwafrika, Mwafrika alishinda na Baba wa Taifa alihutubia mkutano ule kwa mara ya kwanza, alitoa machozi. Huo ni utalii mkubwa sana Mheshimiwa Mchengerwa.

Mheshimiwa Spika, tunaomba muendelee kutangaza watu waje waone chimbuko lao la Uhuru wa Tanzania lilitokea wapi. Kuna mnara mkubwa ambao hautengenezwi sasa umebakia. Kuna jengo ulipofanyika Mkutano Mkuu wa *TANU* 1958 wa kuhakikisha msingi wetu wa kupata uhuru ulitokea pale; vyote hivyo ni vivutio.

Mheshimiwa Spika, tuna mtani wetu anaitwa Fundikira ambako Katibu Mkuu, Dkt. Abbasi ameoa. Pale *opposite* na nyumba yake kuna mlima, ule mlima kuna siku aliuziwa yule mzee. Sasa anakwenda kwenye ule mlima kwenye matambiko. Kila alipokuwa akikanyaga ardhi alama za nyayo za miguu yake zinabaki. Ni jambo kubwa sana la kufikirisha, unaweza ukafikiri alikuwa binadamu wa namna gani, lakini alikaa chini akapiga ngoma zake za matambiko, makalio yako pale na ile ngoma na fimbo vilitokea pale, havifutiki viko pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo yote hayo ni utalii mkubwa sana. Mimi namshangaa Dkt. Abbasi, tutakunyang'anya mke kwa sababu haututekelezei mambo yetu ya Tabora. Na hapa ni kwao kabisa na mke wake, kwa hiyo tunaomba sana hili ni jambo kubwa la utalii na litekelezwe.

Mheshimiwa Spika, nimesema kuhusu David Livingstone. Hilo jengo walilokuwa wanahifadhia watumwa lipo, wanapelekwa kwenye ngome ya Jeshi la Mjerumani ambayo sasa hivi ni ngome ya Jeshi, kuna njia ya chini kwa chini inakwenda inatokezea *railway station,* ndiko walikokuwa wanabebwa watumwa na kupelekwa humo. Hiyo njia kwa sasa naambiwa imeharibika; lakini mkiifuatilia ile njia ni kivutio kikubwa sana, Wajerumani wengi watakuja kuona jengo lao la utawala, ngome yao ya Jeshi na njia iliyokuwa ikibeba watumwa kupeleka huko.

Mheshimiwa Spika, kuna njia kuu ya watumwa waliokuwa wanapokelewa kutokea Burundi, Congo, wanapitishwa sehemu

inaitwa Utusini. Ilikuwa wakipita wanapanda miembe, ndiyo maana mnaona Tabora kuna miembe mikubwa. Kuna *Tabora Boys,* alisoma Baba yetu wa Taifa, Mwalimu Nyerere, mpaka leo bweni lake lipo ukienda utaliona, na kitanda alichokuwa analala Mwalimu Nyerere kipo mpaka leo; ni utali mkubwa sana kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kuna Shule ya *St. Mary's,* leo inaitwa Mihayo Sekondari, ndiyo alifanya kazi ya kufundisha akiwa mwalimu kwa mara ya kwanza pale. Wote huu ni utalii mkubwa ndani ya Mkoa wetu wa Tabora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya yetu ya Kaliua kuna tatizo kubwa la Vijiji vya Usinge na Kakoko. Hivi vijiji vilipitiwa na mawaziri nane, wale mawaziri walisema wananchi wale waongezewe eneo kwa sababu kuna kaya 1,300; lakini kinachotokea sasa wanaambiwa wahame pale. Na nimesikia Mheshimiwa Waziri anasema yale yote yaliyosemwa na Kamati ya Mawaziri Nane yaendelee kuwa vilevile…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana, muda umekwisha, malizia sentensi.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, atafuatiwa na Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Mheshimiwa Francis Mtega ajiandae.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Samia kwa ubunifuu alioufanya kwenye Filamu yake ya *Royal Tour.* Na huo ni mfano mzuri, kwamba unapoandaa kitu kizuri lazima usemwe, lakini ukisemwa usikate tamaa ili mafanikio yaje yatokee badaye.

Mheshimiwa Spika, la pili, nikushukuru sana Mchengerwa, na ninakupongeza sana. Nimpongeze pia Rais kuwahamisha kama *pair* wewe pamoja na Dkt. Abbasi…

**SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma, huyu anaitwa Mheshimiwa Mchengerwa.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nisamehe. Ninakupongeza sana Mheshimiwa Mchengerwa kwa kuchaguliwa kwako kuiongoza Wizara hii, pamoja na Dkt. Abbas. Mimi kama mdau wa michezo nakumbuka kazi kubwa nzuri mliyoifanya kwenye Wizara ya Michezo. Mpaka leo tunaona Yanga inacheza fainali; hiyo ni kazi yako nzuri sana. naamini *system* uliyoondoka nayo kule tunakukumbuka mpaka leo. Sasa tunaomba na huku kwenye utalii uache alama ileile, na ninakuamini utafanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, nitazungumza mambo machache. Mheshimiwa Waziri, kwanza katika kipindi ambacho Watanzania tunaoishi pembeni mwa hifadhi tulikuwa na bahati na raha ilikuwa ni kipindi cha mama huyu mwenye huruma, mama Samia. Alipounda timu ya Mawaziri Nane hakuwawekea mipaka, aliwaambia nendeni mkalete changamoto halafu mnishauri.

Mheshimiwa Spika, lakini mlichokwenda kukifanya kule kiukweli si sahihi. Na mimi nataka kujiuliza, hivi kweli ninyi mnaamini kwamba mtu mpaka anakwenda kukaa yale mazingira, ujue kumemshinda huku, hakununuliki. amekwenda kukaa pale kwa sababu ya shida zake. Mtu anayevumilia kukaa jirani na simba na tembo maana yake hana namna nyingine ya kufanya, na mwingine amekaa zaidi ya miaka 30. Ukienda leo na *plan* ya kumwondoa hii ni kutengeneza migogoro isiyoisha na Serikali. Na wewe Mheshimiwa Mchengerwa umekuta sisi Tanzania tuna timu za mwendawazimu lakini umetutengeneza mpaka tumekwenda fainali, achana na hayo mambo ya ku-*create* migogoro ya ujirani mwema.

Mheshimiwa Spika, siku moja nilimwona Mheshimiwa Waitara analia hapa na nikaona watu wanasema Mkurya ametudhalilisha; na mimi nina asili hiyo. Kwanza, ni kwa sababu humu labda viti

vimefungwa na hizi *mic,* hasira ikikupanda Kikurya unachukua kitu chochote unasukuma mbele ili hasira yako ipumue. Kwa hiyo alipolia alilia kabisa akiwa anapumua ili hasira zake ziishe.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Mheshimiwa Waziri, hebu utafute namna. Labda tulikosea, unajua tukikosea si vibaya kujikosoa. Hili Jeshi la Wanyamapori tangu tumelitengeneza hebu jaribu kuangalia kabla ya Jeshi Usu na sasa, migogoro iko wapi? Kwa sababu siamini huo utaalamu mnaoutumia kutengeneza hilo jeshi kweli mnawatuma kwenda kupiga watu? Mimi sielewi; mbona majeshi mengine hayako hivyo, yana taratibu zake? Yaani hawa imekuwa ni tatizo. Mnatengeneza Jeshi la kwenda kuwabaka dada zetu, kweli? Hii haiwezekani. Nikuombe Mheshimiwa Waziri utakapokuja hapa usiponiambia mpango mkakati kama hili jeshi lilitengenezwa kimakosa utakuwa Waziri mzuri sana ukilifumua na kutengeneza jeshi jipya na la kisasa. Haiwezekani tukawa na watu wanapiga watu tu, kila siku kupiga watu; haiwezekani.

Mheshimiwa Spika, mimi nakaa kwenye maeneo hayo yanayopakana na mapori ya hifadhi; ni tatizo. Ukitaka kujua njoo ukae, usije na magari, ukae siku moja tukuweke kwenye familia kama wiki halafu ufanye kosa kidogo uone utakavyopata mpite mpite. Kwa hiyo tukilalamika humu mtusikilize; nadhnai kuna makosa tumefanya kwenye uundaji wa Jeshi Usu. Lazima uje na mpango wa kulirekebisha, wale wabovu ondoa, baki na watu walio na nia ya kulinda maliasili, siyo kutengeneza migogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka kujiuliza; Maliasili mnatukamatia ng'ombe, sawa, tuna makosa, mnawapiga mnada, rundo la ng'ombe mnauza kwa bei mnazotaka wenyewe. Na nimejifunza, kwa sababu niliwahi kuongea – kuna Mawaziri sijui kama wako humu au wametoka – kwamba minada inakuwa kama dili, lakini mkifukuzwa tunaanza kusikia mnafuga ng'ombe. Kwa hiyo mnawafuata kiujanja ujanja, mnanunua ndani kwa ndani mnawafuga. Hizo ni laana! Na mtakufa vibaya, lazima niwaambie.

Mheshimiwa Spika, hebu jifikirie umenikamatia ng'ombe wangu 100, yaani naona wanakwenda sina uwezo wa kwenda polisi kwa

sababu kuna bunduki. Haya, nina kosa, unawachukua ng'ombe wangu unawauza, mimi narudi maskini. Halafu baada ya miezi sita unaanza kunihudumia na hela ya *TASAF*. Hiyo ni akili ya *design* gani jamani? Kwani ni chanzo cha mapato?

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, na makosa mengine tengenezeni utaratibu wa kutuonya. Unamkuta mtu ameingia mita 100, mita 200 ng'ombe wanachungwa au wanakunywa maji, unazoa ng'ombe wangu wote nirudi tu nyumbani nainze kusema maliasili; mtakufa vibaya. Lazima niwaloge; hiyo lazima tuambizane ukweli.

Mheshimiwa Spika, maana nikienda polisi utanishinda, mahakamani sina hela ya kwenda, mtalogwa mtakufa vibaya, lazima Mheshimiwa Waziri. Hebu rudisha moyo, tengeneza ujirani mwema ule wa maana. Kama huna maafisa mahusiano kwenye Jeshi Usu lako tafuta maafisa mahusiano watengeneze mahusiano. Mtatuchonganisha bure na Mawaziri, mara mkienda kule mnashika hasira mnasema na matusi, lazima. Kwa sababu sisi tunalia.

Mheshimiwa Spika, mimi ukinichukulia ng'ombe wangu ambao nategemea mtoto wangu wangu yuko chuo kikuu, mwingine anasoma sekondari. Haya, wamekwenda, ukienda kule kuna bunduki; nakaa tu kimya kweli? Na hii Serikali kweli tumekosa chanzo cha mapato mpaka chanzo cha mapato kiwe kuuza ng'ombe?

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mchengerwa, hiki kitu jamani kwa kweli hakiwezekani. Fikirieni namna, makosa mengine muonye, mbona ninyi mnakosea na tembo akija huku hatuwashitaki, tunawaambia tu mambo yanaisha? Ninyi kosa lenu ni kuchukua tu na kupiga faini. Mheshimiwa Mchengerwa, mimi sitaki kuamini kama na wewe utaendelea kuwa Waziri wa mafaini; haiwezekani. Nikuombe uwe Waziri utakayetengeneza hifadhi tuzione kama mali zetu, siyo za Wizara.

Mheshimiwa Spika, sisi wote ni Watanzania, na mimi nilipongeze sana aliposimama ndugu yetu hapa wa Kiteto, tulimwambia, na ndugu yangu wa Monduli. Tulikuwa tunamshauri mpaka *canteen,* huyu hapa, kwamba kwa staili Serikali ilivyoamua kuwahamisha, yaani

kutoa mpaka na gari ng'ombe wa Kimasai mara ya ya kwanza amepanda fuso, halafu unapiga kelele, nyumba, maji, shule. Tumemshauri sana Mheshimiwa humu, na akina Mheshimiwa Ole-Sendeka mpaka yakaisha.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nataka kuuliza; kule Nyatwali ni Tanzania, wale ni wananchi. Halafu mimi nataka kujiuliza Mheshimiwa Waziri ukipanda hapo uniambie ni hifadhi gani ambayo labda umekwenda kuangalia huko duniani, maana sisi tunatembea, nikishindwa kutembea na-*google;* kwamba unatoka mbugani unakatiza lami unakwenda moja kwa moja ziwani, pembeni kuna kijiji kinaitwa Lamadi, huku kuna Bunda. Kule ziwani sisi tunatega samaki, kule ziwani tunanywesha ng'ombe wetu, halafu na simba tukutane nao kulekule. Mna mpango gani ndugu zangu? Yaani mmefikiria kitu gani, au mtaweka fensi kuzia sasa simba wasiende?

Mheshimiwa Spika, mimi najuiliza mara mbilimbili, hizi ni *research* za *design* gani? Ndiyo maana wakati mwingine mimi najiuliza, siyo kwamba napingana sana na *degrees* za darasani, yaani matendo yenu huwa yananichanganya mpaka nafika mahli najiuliza mara mbili.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana jana nilikuwa nasikiliza kwenye nishati, watu wanasema tumnyang'anye *TBS* turudishe tena aliyekuwepo, wakati Bunge hilihili tulijadili, na ninyi ni wasomi, tukapitisha, *TBS* hatujampa uwezo, anategemea kukopakopa kama Musukuma hapa.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi najiuliza hiyo *research* kweli mnadhani itatufikisha? Kwani kimepungua nini; mmeambiwa kwamba wanyama wamebanana Serengeti mpaka mfukuze kile kijiji wale wanyama wawe wanakwenda? Je, kule kwenye ziwa ukikutana na wavuvi nani anawalinda? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kule kwenye ziwa tukikutana sisi tunaonywesha ng'ombe wetu maji nani anawalinda? Wale wanyama miaka yote toka mbuga imeanza wanajua huku wanaishi binadamu, sasa mkiwaambia wapite mpaka kule huku pembeni Lamadi na huku

Bunda, nani anaweka ulinzi? Mnataka kutuletea matatizo, na ninajua hamtafaulu.

Mheshimiwa Spika, hivi kweli mnataka ku-*achieve* kitu gani kufukuza wale wananchi halafu unamlipa mtu milioni mbili? Halafu walewale wanawaangalia Wamasai wamebebewa ng'ombe kwenye fuso; hapana bwana, hii keki ni yetu sote Mheshimiwa Mchengerwa. Maeneo mnayo mengi, kama mmepungukiwa, kama wanyama wamejaa beba leta hata Geita kule tuna mbuga haina wanyama. Haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho; mimi nina Hifadhi inaitwa Rubondo, ni kisiwa. Ile kata inahesabika kata ya Musukuma, kata ya Geita Vijijini, lakini langu kuu limewekwa Chato, sina tatizo. Sasa, historia ya ile hifadhi ni kwamba ina matambiko yetu ya Kizinza, mlango mkuu ulikuwa Nkome, na upo, na ofisi zipo, lakini yaliyopita si ndwele, turudishe lile geti la Nkome. Kama kule meli sisi bado tunahitaji tu kuwa na boti kwa sababu hata ukiingilia kule Mganza inabidi uje mpaka hifadhi, halafu halafu vile vivutio vyote viko karibu kabisa na jimbo langu. Kwa hiyo nikuombe, ile ni kata yangu. Mimi sitaki kufunga geti la Chato, lakini ninachotaka tuwe na geti la pili, ule utalii wa magari uanzie kwenye jimbo langu ili na sisi tuone Wazungu, siyo tuwe tuna-*google* tu ndiyo tunaona Wazungu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nina imani kwamba Mheshimiwa Mchengerwa utakapokuja hapa kikubwa kwangu, Nyatwali iwe sawa na…

**SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa, Ahsante sana.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: …** Loliondo; pili, utaratibu wa kulitengeneza Jeshi Usu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu michango ikishatolewa humu ndani watu wanaichukulia kwa uzito sana, sasa Mheshimiwa Musukuma hapa amezungumza kuhusu utafiti;

utafiti ni wa muhimu, na wasomi pia ni wa muhimu. Kwa sababu kama nchi hatuwezi tu kuwa tunaamka na mawazo haya leo, kesho tunaamka na mengine, na kesho kutwa na mengine; hapana, kwa sababu ya yale mapungufu tuliyonayo binadamu na yale mabadiliko ambayo tunayo, utafiti ni wa muhimu. Kwa hivyo wasomi tunawahitaji kwa ajili ya utafiti huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Festo Richard Sanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Francis Mtega.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia kwenye bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nianze kumpongeza Mheshimiwa Rais Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa sababu yeye ndio ameitengenezea njia Wizara ya Maliasili na Utalii ikafanya vizuri sana kwenye suala la ukuaji wa utalii nchini kupitia *the royal tour.* Kwa maana ya filamu yetu ambayo imetangaza vyanzo vingi ambavyo tunavyo nchini na hifadhi zetu na baadaye tukafanya vizuri na kwa *East Africa* na ikiwezekana kwa Afrika nzima tukawa tunaongoza kwa idadi kubwa ya watalii ambao wamekuja kutokana na hii filamu ambayo Mheshimiwa Rais ameitengeneza. Kwa hiyo nipongeze sana hilo ambalo Mheshimiwa Rais amelifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, cha pili niweze kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kaka yangu Mchengerwa ulikotoka umeacha miguu yako salama sana kwa sababu unafahamu na Wabunge wanafahamu na Watanzania wanafahamu kwamba kati ya Wizara ambazo zilikuwa kidogo tuseme ziko kwenye utulivu ilikuwa ni Wizara ya Michezo lakini ulivyopita wewe umeonesha kwamba Wizara ya michezo inaweza kuwa ni Wizara ambayo Watanzania wote wakajivunia lakini kelele zote zikawa zimeisha lakini pia *business as usual* ikawa imeondoka kwenye Wizara ya Michezo na hatimaye kila mmoja anakumbuka miguu uliyoikanyaga kwa Wizara ya Michezo. Wewe pamoja na Katibu Mkuu Dkt. Abbas ambaye mnashirikiana kwa ukaribu sana. Hongera sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya kwetu ni matarajio kwamba hata kwenye Wizara hii, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ambayo kwa kweli kwa historia Mawaziri wengi sana hawajadumu kwa muda mrefu kutokana na changamoto ambazo zipo kwenye Wizara hii lakini tunaamini wewe utakwenda kuwa mwarobaini kwa ajili ya kutusaidia kutatua changamoto hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, la kwanza nitazungumzia ongezeko la wageni. Ongezeko la wageni, tunaona kabisa takwimu zinaonesha kwamba tumetoka kwenye 1,700,000 na baadaye tumefika 3,800,000 kwa maana wageni wameongezeka kwa wingi sana. Mheshimiwa Waziri sasa ninaushauri kwenye jambo hili. Ushauri wangu wa kwanza tengeneza *chain*, mnyororo wa jinsi gani mgeni ameingia, amehudumiwa, amefika hifadhini, amelala, ametoka kwenye nchi yetu na *in your record* ujue mtalii huyu je, alirudi au hakurudi? Kwa sababu takwimu zinaonesha pia tuna changamoto ya watalii kutokurudi, sasa je, sababu ni nini? Mheshimiwa Waziri kwa hiyo, ninakuomba kwa sababu unataka kuifanya hii wizara iwe ni ya kiutofauti na watalii waongezeke zaidi naomba usaidie kujua *chain*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimejifunza watu wanaokaa muda mrefu na watalii ni pamoja na madereva kwa maana kwenye *tour guides* wanajua mambo mengi sana ambayo watalii wanayazungumza. Usi-*base* sana kuzungumza na hawa ambao ni *stakeholders* wa sekta ya utalii kwa maana ya hawa wakubwa lakini nenda kwa hawa wa chini ambao ni madereva na hata *tour guides* wale wadogo, wapagazi pia. Jifunze watalii wanazungumnza nini kuhusu utalii wetu ndani ya nchi. Mheshimiwa Waziri kwa hiyo unaweza ukajifunza mambo mengi sana ambayo yanaweza kusaidia sekta yetu ya utalii kukua.

Mheshimiwa Spika, pia hifadhi za utalii zimekuwa ni zile zile kwa muda mrefu ambazo zinatamkwa. Mheshimiwa Rais kwa sasa amekuwa na mpango wa *the hidden* Tanzania, ni muda mwafaka sasa na nyie kwenda kuionesha dunia kwamba Tanzania kuna vivutio tofauti na hivi vya Serengeti na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, mojawapo ikiwa ni hifadhini kwetu Kitulo ambapo ni Jimbo la Wilaya ya Makete. Pale Kitulo ni moja kati ya hifadhi ya tofauti kabisa barani Afrika. Utofauti wake ni kwamba ni hifadhi ya maua ni bustani ya Mungu, ambayo Mheshimiwa Waziri nadhani mnaweza mkatumia pia hifadhi hii ikaweza kutusaidia na Mheshimiwa Rais ametupatia barabara ya lami ya kutoka Mbeya kwenda Makete, sasa hivi tunapita katikati ya hifadhi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni muda mwafaka mradi wa *re-grow* unaweza ukaenda kuisaidia hifadhi ile ikakua na ikawa na manufaa kwa ajili ya wananchi wetu wa Jimbo la Makete lakini na Watanzania wenzetu wote. Mheshimiwa Waziri pia nikuombe kuongeza idadi ya wanayama, mlitupatia pundamilia, mmetupatia wanyama wengine swala. Tunaomba muongeze idadi ya wanyama kwenye hifadhi hii kwa ajili ya kuendelea kukuza hifadhi zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na kwenye hili jambo pia la kukua kwa maana ya ongezeko la wageni. Nikuombe sana *flow* imekuwa ni kubwa sana ya wageni kwenye Taifa letu. Jambo ambalo tumepata changamoto ni malazi. Tulienda Karatu na unakumbuka tulivyokuwa kule, tumeona *flow* ya watalii ni kubwa na vyumba vya malazi vimeisha kabisa. Sasa sekta za kibenki zimelekea sana kwenye sekta ya kilimo na sekta nyingine. Ni muda mwafaka sasa wa kukaka katikati na benki ukazungumza nazo ikiwemo benki ambayo Serikali ina hisa nyingi Azania Benki ikaweza kusaidia na ikaweza kutangaza fursa za watanzania kukopa na kujenga na kuwekeza kwenye sekta ya utalii ili utalii wetu uweze kuongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kulizungumzia ni jambo la *reforms*. Mheshimiwa Waziri lazima ufanye *reforms.* Hili niseme kwa sekta yako ya utalii hatuwezi kuendelea na *business as usual* kwenye suala la uendeshaji wa Wizara ya Maliasili na Utalii. Watakukasirikia, watakuchukia, watafanya kila kitu lakini ni lazima ufanye *reforms. Reforms* ya kwanza ni namna jinsi gani tunaweza kuutangaza utalii wetu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri ukumbuke kwamba sisi tuko kwenye namba moja Barani Afrika kati ya Taifa lenye vivutio vya

asili. Tanzania tunaongoza Barani Afrika, sasa haiwezekani kwenye mataifa madogo kuliko Tanzania yanafanya vizuri kwenye sekta ya utalii tena wana kivutio kimoja tu yawezekana ni Nyani lakini sisi tuna vivutio vingi tumeshindwa kufanya vizuri kwenye utangazaji wa utalii wetu.

Mheshimiwa Spika, sasa niombe kupitia bodi ya utalii Tanzania nina Imani kubwa sana Mkurugenzi wa Bodi ukimsikiliza mawazo yake ni makubwa sana muweze kwenda kutangaza utalii zaidi kuliko hapa ambapo Mheshimiwa Rais ametangaza.

Mheshimiwa Spika, nimeona una mpango wa kutangaza kupitia kwenye timu za mipira kwa maana kwenye michezo mbalimbali. Sasa Mheshimiwa Waziri tusirudi kwenye mkenge ule ule. Wakati ule tulitangaza utalii wetu kupitia *Sunderland* ikaenda ikazama, ikazama na utalii wetu. Ni muda mwafaka sasa kwenda kutafuta timu ambayo ina *consistency* nzuri kwenye *performance* ambazo zitaenda kutufanya tusikike na tufanye vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri kwa sababu nina *records* nimekuwa ni mdau wa michezo na wewe umekuwa mwanasheria kwenye mpira wetu Tanzania. Unajua kabisa timu inayofanya vizuri na watu wanaongezeka kwenye kui-*support* na inapofanya vibaya watu wanatoweka. Mnavyoenda kutafuta hizi timu kama mnatafuta ni *Manchester*, kama ni *Real Madrid* kama ni *PSG* ni nini, ninaomba Mheshimiwa Waziri usiingie mkenge wa kutafuta timu ndogo ndogo zikazama na utalii wetu. kwa sababu gani? Mheshimiwa Waziri nimejifunza hilo sana kupitia *Sunderland* ambavyo jinsi iliweza kutoweka.

Mheshimiwa Spika, pili Mheshimiwa Waziri lazima kwenye kuongeza Watalii tuwe na neno moja la kuitangaza Taifa letu. Tutambulike kwa neno moja leo hii ukienda huyu anasema *visit* Tanzania, ukitoka hivi anasema Tanzania ni *forgettable* sijui mwingine anaenda hivi. Lazima tuwe na slogan moja ya kufanya utalii wetu utambulike kwa namna moja kwenye Taifa letu. Kwa hiyo, *reforms* zingine utaendelea kuzifanya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni suala la Ngorongoro. Tumehamisha watanzania wenzetu pale wameelekea kule Handeni kwa maana ya kupisha uotoasili wa Ngorongoro. Mheshimiwa Waziri lile jambo lazima mchakato uende haraka sana. Kumbuka kwamba maadui zetu na marafiki zetu wa karibu hawatutakii mema kuona sisi tunafanya hili jambo. Tulijitanabaisha, tulijionesha kwamba tuna uwezo wa kufanya hilo jambo na tumeweza kwa kiwango kikubwa na nipongeze Mheshimiwa Rais lakini kuendelea ku-*delay* wale watu unaweza kuona wanaanza kurudi sasa. Wanarudi kwa njia tofauti, tofauti kupitia makongamano kuhamasisha vitu kama hivi. Acha huu mchakato tuumalize kwa haraka andika historia Mheshimiwa Waziri kwamba uikamilishe hii safari kwa haraka ili wananchi wetu wa Ngorongoro wapate eneo salama na mchakato wa Ngorongoro uishe. Majirani wanatumia hawa watu kutugombanisha, majirani wanatumia hawa watu kuhakikisha kwamba utalii haukui, majirani wanatumia hawa watu kuhakikisha kwamba tunakwama. Kwa hiyo, mchakato wa Ngorongoro uweze kukamilika vizuri.

Mheshimiwa Spika, jambo langu lingine ni kwenye suala la migogoro. Kwanza nikupongeze umeshaanza ziara ya kuzunguka kwenye Mikoa tofauti tofauti. Mheshimiwa Waziri tunaomba sana changamoto ya Mawaziri nane ambao walikuwa wanazunguka, lazima tukubali changamoto ilikuwepo. Mara nyingi walikuwa wanafika muda mwingine Mkoani hawafiki kwenye kiini kabisa cha migogoro kule chini.

Mheshimiwa Waziri sasa tumia fursa hiyo, nikuombe sana nenda kwenye maeneo yale kwa sababu migogoro yetu mingi Tanzania ni kwa sababu ya kukosa ushirikishwaji. Ukiwasikiliza wale wananchi ambao walikuwa wanakupongeza juzi kwamba toka waisikie Serikali wewe ndio Waziri wa kwanza umegusa kufika kule Serengeti na ukawasikiliza. Lile jambo sisi kama Wabunge tunajifunza kumbe wananchi wako tayari kupokea maelekezo ya Serikali lakini changamoto ni kwamba Serikali haiwafikii wanafika pale wanawamrisha wananchi, hawawashirikishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokuwashirikisha wananchi ndio kunasababisha migogoro mikubwa zaidi. Ni vema mkafika pale

mkakutana na wazee wa eneo lile, mkakutana na wenyeviti wa vijiji wa eneo lile kwenye maeneo tofauti. Mheshimiwa Waziri na utakapokuja hapa nikuombe utupe umeainisha migogoro mingapi mikubwa nchini ambayo unampango mkakati nayo ya kwenda kuitatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kukuteua kitendo cha kufika kule Serengeti kimetupa majibu ya kwamba sehemu kubwa ya viongozi hawafiki chini kwenye migogoro. Wananchi hawana changamoto kabisa, kwa mfano kule Makete sasa hivi tumeanza tena migogoro na hifadhi ya *TANAPA* kwa sababu wananchi hawakushirikishwa. Mheshimiwa Waziri kwa hiyo, nikuombe sana, nakupongeza kwa sababu umenisaidia kumaliza migogoro kwenye Mpanga, Kipengele na wananchi wa Makete nawashukuru sana watu wa Maliasili na Utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mgogoro kati ya *TANAPA*-Kituro na wananchi wangu wa vijiji vya Makwaranga, Isapurano na maeneo ya Igenge maeneo mengine kama Makwaranga, maeneo kama Kigara yanatokana kwa sababu *TANAPA* wakifika wanachomeka bikoni wanaondoka. Huu sio utaratibu mzuri. Taifa letu halina shida sana, migogoro inatengenezwa na sisi viongozi. Kwa hiyo, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, lakini baada ya kusema hayo niseme jambo moja tu kwamba ninamtakia kila lakheri Mheshimiwa Waziri ulifanya vizuri kwenye Wizara uliyopita ya Michezo…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa kengele ya pili imegonga.

**MHE.FESTO R. SANGA:** Naam.

**SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga.

**MHE.FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana, nimtakie kila lakheri Mheshimiwa Waziri. Wewe ndio Ronaldo wetu,

Messi wetu tumekuachia mchezo huu cheza sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Mtega.

**MHE. FRANCIS L. MTEGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii niweze kutoa mchango wangu katika Wizara hii ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kutoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri anayofanya kwa watanzania wote hasa hasa ile ziara ya *Royal Tour* kwa kweli imeleta watalii wengi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakumbuka tulifika Arusha, Mkuu wa Mkoa alikiri kwamba changamoto kubwa sasa ni namna ya ku-*manage* magari yanavyomiminika kule Ngorongoro. Ukizingatia kwamba tulitoka kwenye *Covid-19* basi hayo yalikuwa mafanikio ya hali ya juu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kutoa shukrani za dhati kwa viongozi wakuu, Makamu wa Rais Mheshimiwa Dkt. Phillip Mpango, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri wanazofanya lakini nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, Nimpongeze Naibu wake Mheshimiwa Mary Masanja. Niwapongeze watendaji wakuu wa Wizara Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, watendaji wote na wafanyakazi wote kwa ujumla kwa kazi nzuri wanazoendelea kufanya kuhifadhi, kulinda uhifadhi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utajikita zaidi kutatua migogoro baina ya *TANAPA* na wakulima, *TANAPA* na wafugaji lakini wanyama dhidi ya wananchi. Kabla sijaanza mchango wangu nina salamu za pekee kutoka kwa wana Mbarali kwa Mheshimiwa Rais. Wanamshukuru sana kwa uamuzi wake thabiti wa kumaliza mgogoro wa *DN* Na. 28. Ni mgogoro uliodumu kwa miaka mingi sana,

umesumbua sana wananchi wa Mbarali wamesita kuendeleza kuwekeza kwenye maeno yenye mgogoro hivyo kurudisha nyuma maendeleo yao, lakini Serikali ya Awamu ya Sita wanakwenda kuumaliza kabisa wanasema ahsante sana mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jumla ya vijiji 29 vinaenda kurudishwa kwa wananchi ambalo ni eneo lenye ukubwa wa hekta 74,000 kwa hiyo wananchi wa Mbarali kwa kweli wanashukuru sana kupewa eneo hili. Pia wanashukuru kwa uthamini unaoenda kufanywa kwa vijiji vitano tuna baadhi ya vitongoji ambavyo vitabakia kwenye hifadhi na *process* nzima inavyoendelea na wanafurahi kwamba watalipwa fidia na kuoneshwa maeneo mengine ambayo watayatumia kwa kilimo na ufugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani hizo sasa nianze mchango wangu kwa kumsihi Mheshimiwa Waziri kwamba namwamini sana. Kama walivyosema wenzangu ameonesha maajabu makubwa kwenye Wizara ya Michezo tuko juu sana. Pia ameenda Serengeti kule ametatua vizuri mgogoro na mimi namwomba tuongozane Mbarali ili akajionee mwenyewe vizuri tushirikiane kutatua migogoro ya Mbarali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mgogoro wa kwanza unasababishwa na vijana wale walioaminiwa kwenda kufanya doria kwenye mipaka na uhifadhi. Badala ya kufanya kazi waliyotumwa wanaenda kuingia kwenye maeneo ya wananchi na kufanya vitendo visivyokubalika. Wengi wao wanaswaga mifugo na kuiingiza hifadhini, sasa hii inachochewa na taratibu au Sheria iliyowekwa ya kutaifisha mifugo ya wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu Mheshimiwa Waziri hebu angalia utaratibu huu vizuri kama unatija kweli kwa sababu inawezekana wale ambao sio waadilifu wanatumia mwanya huu kupora mifugo makusudi pengine wajinufaishe wao wenyewe badala ya kuingiza fedha Serikalini. Hivyo nakuomba sana tuongozane ukachunguze mwenyewe nikuoneshe wahusika walifanyiwa vitendo vile. Muda ule ambao ulivyokuwa mfupi ikauzwa haraka haraka

wanunuzi wenyewe kwa kweli inatia shaka nakuomba tuongozane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mgogoro wa pili, vijana wale huwa wanakuja mitaani na kufanya vitu ambavyo havistahili, kupiga watu kwa tuhuma ndogo ndogo ambazo hazina uhakika. Wakiona mtu amebeba kuni barabarani wanamkamata wanampiga eti umetoa hifadhini kitu ambacho sio kweli lakini pia huwa wanaweza wakafika wakaizuia mifugo sehemu na kuiingiza mashambani wanasimamia ili ile mpunga wa watu kitu ambacho kwa kweli kinatia huzuni sana.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri kwa hiyo, nakuamini sana, ni mchapakazi, ni hodari, ni mbunifu twende Mbarali ukatatue hii migogoro naamini itaisha kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimefurahi sana kuona kwamba kuna azimio linaletwa Bungeni la kuridhia mipaka mipya baina ya Hifadhi ya Ruaha na wananchi wa Mbarali kwa kweli ni jambo la kheri. Tunaamini ikifikia hatua hii migogoro yote itakua imeisha Mbarali sasa tutalala na usingizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuhitimisha niombe kwamba baada ya kufika Mbarali baada ya kujiridhisha mwenyewe, niko tayari kutoa ushirikiano wa hali ya juu kwako na kwa Serikali yangu yote. Nipo tayari kujitolea kutetea, kulinda maslahi ya Serikali lakini pia maslahi ya wananchi wa Mbarali kama walivyonituma mwakilishi wao. Nikizingatia kiapo cha uaminifu na kiapo cha kulinda na kutetea Katiba ya Jamhuri yetu ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nikushukuru Mheshimiwa Waziri na timu yako yote nina Imani kubwa sasa na wewe kwamba tutaenda Mbarali. Tutaenda kumaliza migogoro yote ya wana Mbarali.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa sehemu ya kwanza ya hiki kikao chetu cha leo. Niwasome baadhi ya Wabunge

ambao tutaanza nao wakati wa mchango tutakaporejea. Yupo Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, Antipas Zeno Mgungusi, Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, Mheshimiwa Riziki Said Lulida, Mheshimiwa Tecla Mohamedi Ungele na wengine wataendelea kutajwa kadri michango itakavyokua inakwenda.

Waheshimiwa Wabunge wapo wageni wengine ambao wameingia Bungeni. Wageni 14 wa Mheshimiwa Daniel Sillo ambao ni walimu kutoka Babati Mkoa wa Manyara, karibuni sana. (Makofi)

Wapo wageni wa tatu wa Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula kutoka Chuo cha Mipango Dodoma, Wapo wageni 29 wa Mheshimiwa Nikodemas Maganga ambao ni watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe Mkoa wa Geita, karibuni sana. Wapo wageni wengine 10 wa Mheshimiwa Vedastus Manyinyi ambao ni wanafunzi wa Chuo cha Mipango kutoka Musoma Mkoa wa Mara, Wapo wageni 37 wa Mheshimiwa Deo Sanga ambao ni wenyeviti, makatibu, wenezi ngazi ya kata za CCM na Katibu wa Mbunge kutoka Makambako Mkoa wa Njombe na hawa wameongozana na mtoto wa Mheshimiwa Deo Sanga, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge wapo pia wageni wawili wa Mheshimiwa Deus Sangu kutoka Mkoa wa Rukwa, karibuni sana. Wapo pia wageni 18 wa Mheshimiwa Abdul-Aziz Mohamed Abood kutoka jimboni kwake, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia wapo wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo na hawa ni wanafunzi 151 na walimu kutoka Shule ya Msingi Feza ya Jijini Arusha, karibuni sana bungeni. *(Makofi)*

Sasa sijaelewa ni vile hawaelewi Kiswahili ama haiitwi Feza Shule ya Msingi inaitwa Feza *Primary* kwa hiyo, wamezoea Kingereza ama ni Feza *Secondary* sijajua lakini Tangazo linasema. Ni Dar es Salaam sio Arusha? Aaa! Sawa, nadhani mleta tangazo. *(Makofi)*

Haya sasa ngoja basi niwasome upya kwa sababu hapa wamesoma Arusha. Wanafunzi ambao wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ni wanafunzi 151 na walimu kutoka Shule ya Msingi

Feza ya Jijini Dar es Salaam. Katika hao wanafunzi nimeletewa ujumbe hapa kwamba yupo mtoto wa Mheshimiwa Masauni Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge hao ndio wageni tulioko nao leo na wengine wataendelea kuingia mchana na wataendelea kutangazwa kadri muda unavyokwenda. Yupo na wa Mheshimiwa Mchengerwa? Yule si alitajwa asubuhi nilifikiri yeye ameshatoka. Haya Wabunge wenye watoto wao mnaweza kusimama. Watoto wa Wabunge huko juu na watoto wa Mawaziri mnaweza kusimama wote kwa pamoja, haya karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge ahsanteni sana, baada ya kusema hayo nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni hii leo.

*(Saa 7.02 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirejea)*

*Mwenyekiti (Mhe. David M. Kihenzile) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa Fedha 2023/2024

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na uchangiaji. Namwita Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, wakati huo Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi, pamoja na Mheshimiwa Mwita Marwa Waitara, wanajiandaa.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi ya kuchangia bajeti hii ya Maliasili na Utalii. Nianze kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote wa Wizara. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais, Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kuitangaza nchi yetu katika eneo hili la utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri alifanya vizuri sana kwenye michezo, lakini kwa historia ya zile Wizara tano ngumu (mifupa migumu) ni pamoja na Maliasili na Utalii. Sisi tunakutakia kila la heri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu nianze na janga la moto kwenye Mlima Kilimanjaro ambalo linatokea mara kwa mara. Kwanza, sasa niwape Wizara habari njema kwamba Mheshimiwa Rais ameleta fedha za kukarabati Uwanja wa Ndege wa Moshi, kazi inaendelea, utakuwa ni uwanja wa Kisasa. Sasa ni jukumu lenu kuona ni namna gani mnaweza kuweka huduma za zimamoto kwa kutumia ndege mkishirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani ili kupambana na janga lile la moto linapotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri pia mfanye juhudi ya kujua ni nini huwa kinasababisha na ni namna gani mnaweza kuwa mnazuia moto huo kutokea mara kwa mara? Ni muhimu sana mfanye hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utalii unahitaji *investment* na ukiangalia nchi kumi bora ambazo zinafanya vizuri sana kwenye utalii, sisi tuko hapo katikati. Ukiangalia *gap* kati ya nchi ya kwanza inayoongoza kwa watalii wengi ambayo ni Egypt, ukija ya pili ni Morocco ,halafu *South Africa* na Tunisia ambazo mapato yake yanaanzia dola milioni 13 mpaka Nane hapo kwa Tunisia. Uwekezaji wao kwenye *tourism* ni mkubwa sana. Tunahitaji katika miaka hii ya Bunge hili Mheshimiwa Waziri uje na mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona kuna mchangiaji asubuhi alisema kuweka matangazo kwenye timu za mpira. Mimi nadhani wakati mwingine siyo lazima tu-*copy* kila kitu. Kwa mfano, hapa nchini nafikiri kuna tangazo ukiliweka kwenye jezi ya Yanga unapoteza hata

baadhi ya washabiki wa Simba. Tutafute njia ambayo ni *inclusive* itakayoleta watu wengi kwenye matangazo yetu ambayo tutafanya. Siyo lazima kwenye timu za mpira kwa maana ya jezi lakini angalau uwanjani ili tuvute watu wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji hauishii kwenye kutangaza. Hapo kwenye kutangaza nitakuja na mawazo mbadala hapo baadaye. Kuna suala la miundombinu, hili sisi tunafeli sana. Barabara ya kutoka Ngorongoro kwenda Serengeti kupitia geti la Nabi, barabara ile hata kama mzungu amekuja hapa kwa ajili ya *adventure,* pale utakwenda kumvunjavunja, magari yanaumia na fedha hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *project* ya kuweka lami kwenye ile barabara ilisimamishwa kipindi cha nyuma, siamini Wazungu wanakuja ili waishi kwenye maisha ya barabara ngumu ya kutingishika na kuumiza magari kama ile ya kutoka Ngorongoro kwenda Serengeti. Hebu liangalieni upya kwa sasa. Wakati mwingine siyo lazima msikilize watu. Hata watu waliosema tusijenge bwawa letu hili walisema ni kwa sababu za kimazingira, lakini hatuwezi kufa kwa njaa kwa sababu eti tunasubiri mbunga ambayo ni *world heritage*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ile barabara tuangalie, tunaweza kuitengeneza vizuri hata kama siyo kwa lami, bali kwa teknolojia nyingine ambayo haitaleta shida na usumbufu mkubwa. Kwa barabara ilivyo ni hasara kwa magari na kwa wageni wale wanaokwenda pale. Kwa hiyo, kwenye miundombinu ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kwenye Mlima Kilimanjaro miundombinu ni pamoja na zile *camp*. *Camp* zile ziboreshwe bila kuharibu mazingira, ziwe na mazingira mazuri. Siyo lazima mtu akipanda mlima basi vyoo anavyotumia vionekane ni vyoo vya hali hafifu, hapana. Tuboreshe mazingira ya Mlima Kilimanjaro kwenye zile *camp* na tuhakikishe kwamba tunapata wateja wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye miundombinu mliongelea suala la vitanda kwenye *presentation* yenu kwenye semina. Mheshimiwa

Waziri, mimi nina ushahidi. Kuna baadhi ya watu wanataka kuwekeza kule kwenye mbuga, kuweka hivyo vitanda tena vya gharama kubwa, lakini kuna baadhi ya makampuni yameshika maeneo miaka mitatu, minne kwa ajili ya kuwekeza na hawajawekeza na hayo maeneo ni *potential.* Kwa nini msiwafutie hao walioshikilia hata kama ni matajiri ili tuwape hao wawekezaji ambao wapo tayari kuwekeza hata sasa hivi? Hata ukinifuata, nitakuonesha baadhi ya maeneo na hao watu ambao wako tayari. Wenzetu wanakuja mpaka na *coordinates.* Ukiuliza unaambiwa hili ni la mwekezaji fulani, miaka mitano hajawekeza. Basi tuangalie namna ya kuwekeza hivyo vitanda ili tuwe na vitanda vya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kwenye hoteli, ni moja ya kitu kinachosababisha tuwe hatuna wageni wengi. Ninatoa tu mfano wa jumla, ule mkutano wa wanashheria ule wa *(TLS)* unafanyika kwenye miji michache sana Tanzania kwa sababu gani? Haufanyiki Dar es Salaam kwa sababu wengi wanaishi pale, unafanyioka Arusha kwa sababu kuna vitanda vingi na *accommodation* ya kutosha. Wakija hapa Dodoma, tayari tuna ukumbi mzuri wa ku-*accommodate* watu 2000, 3000 lakini watalala wapi kwa hapa Dodoma? Kwa hiyo, suala la hoteli ni muhimu sana katika uwekezaji au ukuzaji wa utalii kama sehemu ya miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine, nafikiri Serikali yetu inatakiwa iwe na macho na maamuzi ambayo yamekwenda mbele zaidi. Kwa mfano, kuna hoteli ile ya Ngurdoto *Mountain Lodge* ambao ni uwekezaji mkubwa wa mzawa, bahati mbaya ameondoka, biashara imekwenda vibaya, Serikali imeacha pale, ajira za watu zimekufa, eneo lile limekufa. Kwa nini Serikali isi-*intervene* kwa kununua *share* au kuingia makubaliano na wawekezaji ili tuwekeze eneo kama lile na tuwe na maeneo haya ya utalii ambayo tunayahitaji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri kwenye miundombinu kuna kazi kubwa sana ya kufanya na siyo lazima wafanye Serikali. Wanaweza kuweka mpango mzuri na wa kuwavutia wawekezaji wakawekeza kwa wingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la gharama. Moja ya matatizo ambayo yanaukumba utalii wa Tanzania ni kwamba watalii wanasema *destination* yetu imekuwa ni ghali sana. Mimi najua moja ya maeneo yenye gharama kubwa ni pamoja na *landing fees* za viwanja vyetu vya ndege. Hebu tuangalie namna ya ku-*harmonize*. Tunaweza tukatoa hata *holiday* ya miaka kadhaa, tukaangalia namna ya kupata hayo mapato kupitia sehemu nyingine ili utalii uweze kukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye gharama hizi ni pamoja na mikopo. Wakati ule tumepayta janga la UVIKO niliwahi kutoa wazo, nikasema ni vizuri Serikali iongee na mabenki kwa watu wa utalii iwe kama wakulima, wanakopeshwa lakini wanalipa kwa wakati, kwenye kipindi cha *high season.* Kipindi cha *low season,* zile *interest* na *principle* zisimamishwe ili waweze kujiweka sawa na *season* inapoanza waende. Kama wakulima wanavyokopeshwa kwamba kipindi cha mavuno kinajulikana ndipo wanaanza kulipa mikopo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiweza kuwapunguzia gharama wawekezaji, maana yake tutaweza kuwasaidia sasa nao wawaajiri wale wafanyakazi wadogo kwa muda mrefu na tukakuza ajira kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nilishaliongelea mara mbili tatu ni suala la *park fees.* Haiwezekani tukawa na *park fees* ambazo ni *uniform* tu. Mbunga ambazo zinafanya vizuri, hazina tofauti kubwa na mbuga ambzo hazina watu kabisa. Sasa ni nini tutatoa *incentives* kwa watu kupeleka watalii kwenye mbunga hizi ambazo hazifanyi vizuri? Tuangalie, kuwe na tofauti kubwa kiasi kwamba mtu ataona nita-*save* ili aende kwenye mbuga hizi ambazo hazifanyi vizuri. Kwa hiyo, nafikiri hayo ni maeneo ambayo tunaweza tukawekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *manpower* ni tatizo kubwa kwa nchi yetu ya Tanzania. Mtu yeyote anaweza akaenda kwenye hoteli zilizopo Zanzibar; asilimia kubwa ya wale wafanyakazi *active* Zanzibar na porini, ni wale wanaotoka nje kwa nchi jirani. Waswahili unakuja

kuwakuta huku chini kwenye kazi ambazo hawa-*interact* na wageni. Kwa nini tusiwekeze? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *VETA,* kwa kweli kwenye kuwaandaa wafanyakazi wa utalii hawafanyi vizuri. Tena kuna mtu aliniambia, Tanzania ndiyo nchi pekee unakuta mpaka mfanyakazi wa ndege ana-*attitude,* yaani hawezi kukuchekea hata kama ana *stress* zake. Sasa *industry* hii inahitaji watu kwanza *manpower* iende kwenye lugha, wapishi wazuri na hata *supporting staff*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *Airport* zetu na *entry point,* kwa mfano mtu wa *immigration* ni vizuri achaguliwe yule mtu ambaye anaweza kuongea lugha vizuri, anawasiliana kwa ukarimu na yuko *sharp*. Hivyo hivyo, ukienda *TRA* kwenye *entry points* kwa maana ya *Airport* na baadhi ya zile *border* ambazo zinapitisha watalii. Sasa ukifika kwenye hizi *border* zetu, watu wenyewe waliopo wana *attitude* tayari hata kabla hujaingia, hawakaribishi watu vizuri, hawaongei vizuri, lugha inawagonga. Hapo hatujaenda kwa ma-*guide,* wapishi na hata wahudumu wa hoteli. Kwa hiyo, kwenye *manpower* ni lazima tuwe na mpango wa muda mrefu wa kuhakikisha tunakuwa na *manpower* ambayo inaweza ika-*support* ukuaji wa utalii. Baadhi ya maeneo watu wanakwenda kwa sababu ya *manpower* tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nigusie kidogo mambo ambayo nafikiri yanaweza kusaidia kukuza utalii. Kwenye *presentation* ya Wizara walisema tuna-*deal* tu na maliasili, tumeacha uwekezaji. Ni kweli, kwa sababu baadhi ya uwekezaji unahitaji hela, na kama siyo nguvu ya wwekezaji wenyewe, basi Serikali i-*intervene*. Kuna vitu havihitaji nguvu, vinahitaji *advocacy*. Kwa mfano, nikimwuliza mtu yeyote hapa ni kwa nini ile *cable car* ilisimamishwa na nini *implication* za kusimamishwa na ni namna gani tunaweza kuwa na kitu mbadala pale kwenye Mlima Kilimanjaro ambacho haki-*intervene* lakini kinaongeza mapato? Hakuna. Hata hivyo, watu wamezuia *cable car* na wanaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maeneo tunaweza kuewekeza. Michezo ya *golf*, kuna *game* ilikuwa ifanyike kule *Kili Golf,* uendeshaji

wa baiskeli kama *Toure Kilimanjaro* tuka-*boost* kama ilivyo *Kilimanjaro Marathon…*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Priscus Tarimo, ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi, aweze kuchangia.

**MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi hii ya kuwa mchangiaji wa pili jioni ya leo katika Wizara hii ambayo nina maslahi nayo moja kwa moja. Kwanza, na-*declare interest,* hii ni Wizara yangu kwa maana nimefanya kazi kwa zaidi ya miaka 11. Nimefundishwa kazi na kulelewa na Wizara hii ambayo ninaipenda sana. Sasa nina machache ya kumshauri Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ni mgeni, sasa nichukue fursa hii kumshauri. Sina mengi ya kusema, labda mengine tutazungumza wakati mwingine, lakini leo nimshauri tu. Aidha, Bunge la Septemba, Novemba na yanayofuata kama tutaona tunayoshauri hayajafanyiwa kazi, basi tutaona namna ya kuzungumza, lakini kwa sasa nimshauri, sina cha kumlaumu na nimhakikishie leo sitashika Shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpitishe kwa mambo machache ambayo yako *pending* kwenye Wizara yake ambayo yanahusiana na maeneo yetu ya kijimbo na wananchi wetu. Kwanza, kwangu Malinyi na Bonde la Kilombero wanafahamu kuhusu Kijiji chetu cha Ngombo, ilizungungumzwa na Tume ya Mawaziri wanane kwamba Kijiji kile kifutwe kwa sababu ya *sensitivity* ya uhifadhi na kadhalika, jambo ambalo tulimalizana nao kwenye mkutano wa wananchi, lakini kilichofuata ni kwamba wananchi wanatakiwa wapewe fidia ili waweze kuhama pale Ngombo na kutafuta maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa jambo hili ni la muda mrefu tangu mwaka 2022, lakini hadi sasa hakuna kinachoendelea au hakuna ambacho Mbunge ana taarifa nacho. Sasa hofu ni kwamba mwezi wa Kumi na Kumi na Moja watu wanaandaa mashamba kulima, watu wa Ngomnbo sijui watalima wapi? Nasema hivi kwa sababu wanapaswa walime wapate chakula, ila wakilima watagombana na watu wa maliasili kwamba wamelima hifadhini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa nini wasitoke mapema wapewe hela yao kama ambavyo tumekubaliana? Sasa muda ukifika tutaanza tena kugombana. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri alichukue hili alifanyie kazi haraka. Ilikuwa ni jambo gumu kufikia hatua hii, lakini muda umefika, naomba liishe mapema ili watu wasije wakaonekana ni wakorofi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kulikuwa na biashara ya viumbe pori hai, wale wanyama na wadudu wadogo wanaosafirishwa kwenda nje ya nchi wanafanya watu wa *TWEA,* ilisimamishwa karibia mwaka 2016 leo miaka mitano au sita. Nilizungumza hapa Bungeni kipindi fulani, Serikali waliahidi watafanyia kazi, lakini juzi nimesikia hapa Mheshimiwa Waziri anatoa maelekezo kwamba huenda jambo hili likaruhusiwa na biashara ika-*resume*. Ni jambo la heri kabisa na ninawatakia heri na ninatamani kuona hilo linafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna suala la upandishaji hadhi pori la akiba la Kilombero *(Kilombero Game Controlled Area)* kuwa *game reserve*. Nimeona imefanyika na *GN* inatembea mitandaoni kwenye ma-*group* ya *WhatsApp* kwamba eneo hili limeshapandishwa hadhi sasa linakuwa ni *game reserve* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina tatizo kidogo na hilo kwa maana sina shida na upandishaji hadhi wa maeneo, ndiyo umuhimu wa uhifadhi kulingana na *sensitivity* yake, lakini *procedure* yake sina amani nayo sana. Sasa nimesema nisizungumze sana ili tusigombane, Mheshimiwa Waziri ni mgeni. Nadhani wanafahamu kuna utaratibu wanapaswa kushirikisha wananchi tuweze kujadili mambo haya yaweze kwenda vizuri na mwisho wa siku tujue tunafanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya maeneo ya Kijiji yanaingia kwenye eneo hilo amablo linatajwa, kuna baadhi ya maeneo ya wananchi wa kawaida yanaingia mle. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri hili alifanyie kazi au tutazungumza na nitapata mrejesho kutoka ofisini kwenu. Tusijadili sana hapa kwa sababu nina vitu vingine vya kuvisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kuna suala la wanyama vamizi, (wanyamapori wasumbufu). Kule kwangu Malinyi tuna *National Park* ya Nyerere, bado kuna *Selous* na kadhalika. Tembo wamekuwa wakisumbua sana kama ambavyo wanafanya sehemu kubwa ya nchi, lakini bado usaidizi haupo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nimetoa hizi *highlights* uzichukue. Hata hivyo, bajeti ya mwaka 2022 niliahidiwa hapa kwamba Malinyi itakuwa moja kati ya wilaya kadhaa ambazo zitapata vituo vya kudumu vya Askari wa Wanayamapori. Nadhani *TANAPA* na *TAWA* wali-*share,* sasa natarajia kuona pengine wakati wa kuhitimisha utasema hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba nianze kuchangia. Nilikuwa nampitisha tu Waziri nina mambo makubwa mawili ya wizara hii. Kwanza, napenda nimshauri Waziri, natamani abadilishe *thinking* au *approach* ya *conservation* ya nchi hii. Pili, kwenye Jeshi letu la uhifadhi kwa maana ya *Conservation Paramilitary,* namna muundo wake ulivyokaa kidogo haujashiba na kidogo haujatosheleza. Kwa hiyo, haya ndiyo mambo makubwa mawili ambayo nilisema nataka nianze kuchangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *approach* ya uhifadhi ninaozungumzia, mara zote nimekuwa nawaambia wenzangu jambo la ushirikishwaji ndiyo kila kitu kwenye uhifadhi, na ninadhani dunia nzima ndivyo inavyotakiwa kuwa. Wizara yangu ambayo ninaipenda, *we have been too militarily,* kila jambo ni vurugu, kugombana, hata migogoro mingi ambayo inaendelea kila Mbunge akisimama hapa anazungumzia migogoro ni kwa sababu ya kutoshirikisha wananchi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kushirikisha kwa namna gani? Wananchi, wenzao ni wawakilishi watu wa kuchaguliwa kwa maana

ya Mbunge na Waheshimiwa Madiwani kwenye maeneo yetu. Watu wa Serikali na hata ile Tume ya Mawaziri wanane, ukiwauliza wanasema, tumefanya ushirikishaji nchi nzima. Ushirikishaji wenyewe, wanaenda mikoani kuzungumza na Mkuu wa Mkoa, wanaenda Wilayani kuzungumza na *DC,* Wakurugenzi na vyombo vya ulinzi na usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sisi kiutaratibu unajua jeshini kiongozi huwezi ukawa unashauriana na watu wa ulinzi, kwa maana ya Polisi, wanajeshi wa kawaida hawa, watu wa uhifadhi ni maelekezo, "ndiyo Afande, jambo limekwisha." Sasa unakuta Serikali inajadiliana yenyewe. Kwa hiyo, Serikali inatoka Wizarani wanakwenda kujadiliana mkoani ambayo ni Serikali tena. Wanashuka chini wanakwenda wilayani, wanazungumza na *DC* ambayo Serikali tena na watu wa kuchaguliwa kwa maana ya Wabunge na Madiwani ushirishwaji siyo mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nawashauri wenzangu, ili isionekane sisi ni wakorofi, hakuna mtu ambaye anataka mambo yaharibike au uhifadhi uharibike. Sisi Malinyi na Bonde la Kilombero Samaki ilikuwa unaokota bure kama takataka, tunakula hivyo, lakini leo samaki ni gharama kubwa Malinyi, Ulanga na Kilombero kuliko hata Dar es Salaam. Maeneo ni kweli yameharibika na kadhalika ni changamoto kubwa. Hakuna anayependa kuona uhifadhi unakufa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara kadhaa nimesimama hapa kueleza, mimi ni mhifadhi na nilishaapa na ni msimamo wangu, siko radhi kushiriki kuharibu uhifadhi kwa sababu ya umashuhuri wa kisiasa, lakini wenzangu hatuelewani kwa sababu hatusikilizani, *approach* yao siyo sahihi na mimi siwezi kunyamaza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninawauliza mara kadhaa, miaka ya nyuma Jeshi la Uhifadhi au niseme zamani maliasili nzima hatukuwa na silaha za kutosha, hatukuwa na magari ya doria ya kutosha, hatukuwa na Askari wa kutosha, lakini sasa hivi kila kitu kimeongezeka. Tuna Askari wengi, silaha za kutosha, tuna magari ya kutosha, lakini je, uhifadhi uko salama? Uhifadhi hauko salama. Sasa

jambo hili linapaswa liwafikirishe kwamba *they have to change approach* ya *conservation.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tushirikishe sisi tutazungumza vizuri na watu tuwaelekeze na tutakubaliana, mambo yatakwenda, lakini muda mwingi hawashirikishi Madiwani wala Wabunge. Wanasema hawa wanasiasa wakorofi. Wanafanya vikao kama siri. Jambo jema la *conservation* ni la wote, lakini linafanywa siri kama la magendo, Wabunge na Madiwani wanatengwa hawawashirikishi. Unaona mtandaoni vitu fulani vimeshafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ni mgeni kwenye Wizara hii, ni kijana lakini sina mashaka na uzalendo wako, nakupa nafasi, fanyia kazi. Naomba kwa sababu bahati nzuri wewe sio mhifadhi, nadhani ni mwanasheria, hebu tusaidie kubadilisha *thinking approach towards conservation*. Hatupingi, lakini wenzangu hawaelewi hawashirikishi wanataka waseme bwana hawa wenzetu wanasiasa wakorofi; sisi ni wanasiasa lakini pia wataalamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ni mhifadhi, lakini humu kuna wanasheria na pia kuna Ma-*engineer*. Kila taaluma iliyoko Serikalini iko Bungeni. Tushirikisheni tutafanya mambo yaende kuwa marahisi, hakuna kiasi chochote cha silaha au Jeshi, uhifadhi na kadhalika ambao kinaweza kusaidia uhifadhi upone bila ushirikishaji. Tusikilizeni, hata nikisema Waheshimiwa Wabunge tufanye vikao tutumie mafuta yetu tutafanya. Lakini wanakuwepo wanaangalia sijui *DC,* kule kwa Mkurugenzi wanaongea vikao vya ndani, mimi nakaa nawaaangalia, lakini mwisho wa siku utaonekana. Kwa hiyo mimi sisemi kwa sababu Waziri ni mgeni, tutaongea wakati mwingine *in case* nikiona mambo hayaendi kama ambavyo inapaswa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kuhusu muundo wa Jeshi la Uhifadhi ambao upo sasa hivi. Kuna changamoto kadhaa, Mheshimiwa Waziri naomba uzisikilize. Ya kwanza Jeshi la Uhifadhi halina Mkuu wa Jeshi la Uhifadhi, kwa maana Kamishna Jenerali, kama Jeshi hili ni moja. Lakini ya pili kuna changamoto ya majina kijeshi kwenye vyeo ambavyo maafisa wadogo na wapiganaji

wanavyo. Lakini la mwisho ni kuhusu mrundikano wa Makamishna wa Kanda wa Jeshi moja la Uhifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi hili nadhani mnafahamu, kama Jeshi lingine ambalo tunayo hususani Polisi, Magereza na kadhalika wana Makamishna Jenerali. Kwa hiyo nilitaka nijue kama Jeshi la Uhifadhi tumekubaliana ni moja basi lazima liwe na Kiongozi Mkuu pale juu lakini leo hakuna. Kamishna wa *TFS* anafanya mwenyewe, wa *TAWA the same* Kamishna wa Ngorongoro, Kamishna wa *TANAPA* kila mtu anafanya mwenyewe ndiyo *final.* Lakini nikawa nimeuliza hata swali siku moja hapa Bungeni, kwamba *in case* Rais anataka kuongea na Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama, Wakuu Jeshi la Uhifadhi mnampeleka nani? Hapa Wizara ikanijibu ikasema Katibu Mkuu ndiye anakaimu. Katibu Mkuu ni mtu mkubwa sana kukaa na hawa Makamishna Jenerali kwenye *level.* Hata hawa Wizara ya Mambo ya Ndani kuna Wakuu wale Makamishna Jenerali lakini pia kuna Katibu Mkuu wao, hata Jeshi la Wananchi kule kuna *CDF* Mkuu wa Chombo lakini kuna Katibu Mkuu, Maliasili kuna shida gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Mheshimiwa Waziri alifanyie kazi jambo hili na pia nishauri, washauriane jambo hili na ndugu zangu, pengine Makamishna wa Jeshi la Uhifadhi pengine najua wazee wangu labda wana hofa na wanasema mimi nitakuwa nani kukiwa na Bosi juu. Niwatoe hofu tunatengeneza mfumo wa kudumu kwa ajili ya nchi siyo kwa ajili ya kwao. Kesho wao hawatakuwa pale walipo kama ni Makamishna, kesho mimi sitakuwa hapa kama Mbunge. Kwa hiyo tutengeneze kitu ambacho kimekamilika. Mpaka leo hakielezeki kwa nini hakuna, haielezeki. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri naomba nikupe kama changamoto ili ulifanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kuhusu suala la vyeo vile vya kijeshi kwa maafisa wadogo pamoja wale wapiganaji. Mtu mwenye nyota mbili, wanafahamu majeshi yote hususani Magereza, Polisi, anaitwa inspekta, huku Jeshi la Uhifadhi hawatumii majina hayo wanasema huyu ni *Conservation Officer One* au *Two* na kadhalika. Yule Koplo au *Sargent* anaitwa Conservation *ranger two and whatever,* vitu vya namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikasema hayo ni majina mazuri lakini majina ya kiutumishi ya kiraia, kwa sababu hata Polisi mwenyewe anaitwa *Police Officer,* Magereza anaitwa *Prison Officer,* lakini *military naming* anaitwa *Inspector au Assistant Inspector* au Mratibu, *wherever wherever.* Kwa nini Jeshi la Uhifadhi hakuna? Haielezeki. Sasa shida naona ilianzia muda mrefu iliyoundwa kikosi cha raia huko katika Jeshi la Uhifadhi kutengeneza mfumo wa Jeshi labda ni shida ndio ilianzia hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba Mheshimiwa Waziri ulichukue hili ulifanyie kazi, ni vitu ambavyo havieleweki. Hawa maafisa wanapokutana na wenzao wa Jeshi la Polisi, Jeshi la Wananchi, wamevaa kiraia anataja cheo gani? Anasema mimi ni *Conservation Officer* Nyota mbili hizi sawasawa na Luteni unaanza kujieleza kwa nini. Jeshi halina maelezo ukishakiona kimesomeka *straight forward;* na kwa majeshi hili si jambo jipya. Sasa hawa *TANAPA, TAWA, TFS* Ngorongoro wanaonekana kama umekuja na kitu cha peke yako kutoka peponi ni suala la kukopi vyeo vya polisi ku-*paste* huku biashara imeisha, wakijichekecha nani anatosha wapi, lakini hawafanyi. Kwa hiyo nikushauri Mheshimiwa Waziri lifanyie kazi hili kwa sababu ni kituko. Jeshi jipya bado halija-*commend…*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa kutoka wapi? Mheshimiwa Shabiby.

**TAARIFA**

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni kweli nataka kumsaidia mchangiaji, kama ni kweli hawa hawaeleweki, wana vyeo lakini havieleweki vyeo vyao ni vipi basi tuseme tu hawa ni Mgambo. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Antipas, unapokea taarifa?

**MHE. ANTIPAS. Z. MGUNGUSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napata ukakasi kwa jina alilolitumia lakini kimsingi ni kweli, ni Jeshi ambalo halijanyooka, sasa jina zuri sijalifahamu ni lipi. Kwa hiyo Mheshimiwa

Waziri Mgeni nikushauri kwa nia njema kabisa hata mimi nilikuwa *Officer* nilikuwa *Assistant Inspector* nimestaafu nikiwa na nyota yangu pale nikikutana na wenzangu nimevaa kiraia nashindwa kujieleza, *story* ni nyingi. kwamba unajua hii iko vile, *why?* Nyota moja ni *Assistant Inspector*, inyooke hivyo. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri naomba hili ushauriane na makamishna usishauriane na watumishi wenzangu wa Jeshi hili, tafuta vyomba, kaa navyo, wapeni mfumo maelekezo watekeleze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kwenye *angle* hii, nilizungumza, hata kitabu changu niliandika kuhusu maisha yangu ya jeshi, na nimeshauri vitu vingi sana. Tungekuwa Jeshi linalofanya kazi kwa umoja hizi *division, TAWA na TANAPA*, wangekuwa pamoja kusingekuwa na utitiri wa hivi vyeo na kadhalika. Leo hii kuna Kamishna wa *TANAPA* wa Kanda ya, lakini wakati huo *TAWA* nao wana Kamishna wa Kanda ya Kusini, *TFS* wanafanya vivyohivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huku Iringa, Mbeya kuna Kimondo sijui kuna vitu kama viwili vya Ngorongoro. Kwa hiyo Ngorongoro nao waweke Kamishna wao kwa ajili ya vitu, havieleweki. Alipaswa awepo mtu mmoja ndiye awe Kamishna wa Jeshi la Uhifadhi wa Kanda fulani, wengine wote wadogo wenye *station* watalipoti kwake na yeye atapeleka juu. Lakini kinachofanyika sasa hivi kwa kweli sina imani nacho. Naamini wenzangu Wizarani mnakiona, naongea kwa nia njema kabisa. Tunatengeneza mfumo wa jeshi ambao umenyooka na si kwa ajili ya mtu mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi. Mheshimiwa Waziri natamani Bunge la mwezi wa tisa tusiongee mambo haya na wala tusigombane. Nashukuru sana ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi, nilimwita Mheshimiwa Mwita Marwa Waitara, wakati huo Mheshimiwa Riziki Said Lulida pamoja na Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, anajiandaa.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Tangu asubuhi jina langu linakosewa. Ninaitwa Mwita Mwikwabe Waitara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru kwa nafasi ya kuchangia Wizara ya Maliasili na Utalii, na nataka nitumie nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Tarime Vijijini, kumshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia kwa sababu ya maelekezo yake mazuri ambayo angalau hali ya utulivu imerejea kule jimboni kwangu. Nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kauli yake ambayo aliitoa hapa Bungeni amabyo pia iliendelea kupooza watu wa Tarime. Nimshukuru pia Mheshimiwa Spika, alitoa mwongozo mzuri mara kadhaa. Lakini pia nimshukuru sana Mheshimiwa *Comrade* Mohamed Mchengerwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huyu Waheshimiwa Wabunge ndiye Waziri wa Maliasili wa kwanza kufanya mkutano Tarime na ukaisha kwa amani watu wakacheka wakaondoka. Na Mheshimiwa Mchengerwa Wazee wa Tarime wamekuandalia zawadi, siku ukirudi Mheshimiwa Waziri wa Kilimo kama ulivyoahidi kabla ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenda pale utapata kitu kinaitwa kichuli ya kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru pia Mheshimiwa Mchengerwa, anajua kutibu makovu. Mheshimiwa Mchengerwa namna ambavyo uliingia Tarime uliacha hawa wanaitwa Majeshi ya Uhifadhi pembeni ukaenda kiraia ukaingia moja kwa moja kwenye mkutano, walijenga imani kuanzia muda ule mpaka unaondoka Tarime, nakushukuru sana. Na ile, walisema tu kuwa Mheshimiwa Mbunge tukipata watu kama akina Mheshimiwa Mchengerwa kwenye migogoro, hata kama mgogoro hauishi watu wanapona bila kupata matibabu, hongera sana Mheshimiwa Mchengerwa. Ndiyo maana unasifiwa namna ambavyo uli-*handle* mambo ya Michezo. Hii ni Wizara ambayo ilikuwa haina jina kubwa lakini ameipa heshima kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaturajia sisi ambao tunakaa karibu na Hifadhi ya Serengeti Mheshimiwa Mchengerwa ufanye mambo makubwa zaidi yale ya Wizara ya Michezo, na usuluhishe migogoro

kwa sababu asilimia 50 ya nchi hii ni hifadhi za Taifa. Kwa hiyo ukiweza kuleta amani na mahusiano mazuri kati ya wananchi na hifadhi zetu maana yake kura za Mama Samia, kura za Wabunge, kura za Madiwani na kura za Chama cha Mapinduzi ziko kwenye mikono salama. Tunakutakia kila la kheri katika jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Mhcengerwa alipokuja kule alipewa ujumbe, kwamba pamoja na kwamba yamefanyika mambo mazuri sana lakini kauli ya Mheshimiwa Naibu Waziri watu wa Tarime wanahitaji waombe radhi kwa kauli ile. Kwamba yeye ametumwa na Serikali ni kauli ya Mama na kwa hiyo kule si chooni. Watu tisa walikufa wakapotea mpaka leo; aliulizwa na akina mama wenzake. Mheshimiwa Rais ndiye mfariji namba moja wa Taifa kwa mujibu wa Katiba. Viongozi lazima mkinge kumuongelesha Mheshimiwa Rais mambo maovu ambayo hayana maana sana, lakini pia kutoa matumaini pasipokuwa na matumaini, kupeleka amani mahali ambapo hakuna amani. Kauli ile tu Mheshimiwa Waziri ndiyo imebaki kwenye Wizara yako; mengine yote Mungu akubariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa humu Bungeni ilisheheni vitu vingi sana, alizungumza namna ambavyo ng'ombe wa watu wanataifishwa, alionyesha mahusiano mabovu yaliyopo, aliangalia shida ya malisho, akaangalia shida za kilimo, akaangalia kila kitu. Mimi ningekushauri, pamoja na Waziri wa Ardhi, ile hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ya hali ya migogoro nchini ichukuliwe, kila Waziri achukue kipande chake atengeneze mpango kazi wa utekelezaji, mtakuwa mmetibu sehemu kubwa sana ya migogoro ya ardhi na mahusiano katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, amesema jambo zuri na wenzangu wamezungumza. Kwamba, migogoro hii huwezi kufanya peke yako, kuna viongozi kule. Kuwa kiongozi, kwamba umekuwa Waziri au umekuwa si kwamba umekuwa na akili nyingi kuliko wote, shirikisha. Kuna watu wana utashi pale na kuna watu wana uelewa. Timu uliyosema utaunda tushirikishe tukushauri ni jambo jema, utapata mambo mengi sana na utamsaidia Mheshimiwa Rais na migogoro; tunaamini kwamba bajeti ijayo

malalamiko ya Mbuga kuwalipa wananchi itapaungua humu Bungeni. Kwa hiyo tunakushukuru kwa hatua hiyo ambayo umeona. Mimi namfuatilia; hata kama amekaa Wizara tatu kwa miaka mitatu, ni kwamba Mheshimiwa Rais anamtumia vizuri, kuna vitu vya msingi sana kwake na ndiyo maana watu wote wanamuunga mkono katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo migogoro kule Mkoa wa Mara. Hifadhi ya Serengeti asilimia 75 iko katika Mkoa wa Mara. Lakini mgogoro huu utaukuta Bunda, Tarime, Serengeti, na unakwenda mpaka kule Arusha, mgogoro unaenda mpaka Simiyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni kwamba, ni vizuri ukae vizuri na watu hawa ili uweze kutatua. Mnapokwenda kujadili migogoro ya hifadhi msione kuwa wanyama ni bora kuliko watu. Kuona kwamba wanyama ni bora lakini pia na watu ni bora pia tuna wahitaji. Kama tunafanya uhifadhi tunufaike ni kwa ajili ya watu wetu. Ni vizuri watu wasilie wanyama wanacheka, watoto wafurahie matunda ya nchi hii. Kazi hiyo umepewa Mheshimiwa Mchengerwa, na tunaamini kwamba unaweza ukaifanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano tunayo barabara ya kutoka Serengeti kule inaenda mpaka Ngorongoro, imeahidiwa ijengwe kwa kiwango cha lami lakini hijajengwa. Pale Serengeti hakuna hata uwanja wa ndege. Ukiuliza inakotoka bidhaa inayotumika pale hifadhini inatoka nje ya Mkoa wa Mara. Hakuna ajira, hakuna kazi kwa akina mama, vijana wetu wanazurura pale mtaani wanakutana hawapati ajira, mahusiano mema hayapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hata mazungumzo yanakuwa ya uadui mkubwa kwa sababu wanaona kwamba wanufaika ni watu wengine ilhali Hifadhi ipo kwetu. Kwa mfano Tarime, mimi nalalamika hapa kila siku lakini hakuna hata senti moja kama *service levy* kutoka Hifadhi ya Serengeti kuja Tarime pale. Sisi tunaambulia tembo kuua watu, tembo kula mazao, ng'ombe kupotea, watu kupotea, watu kufirisika na uhasama. Pia hata hiyo *CSR* hakuna mpango mkakati, ukiuliza hawezi kukuambia ni kitu gani hasa wanataka kufanya. Wanaweza wakachimba kisima leo kesho wakakuambia kisima kipo

hifadhini. Tunaomba hii mipango pia iwekwe sawasawa ili watu waweze kunufaika vizuri, tunahitaji pale uwanja wa ndege ili tuweze kufanya kazi ya kitalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mheshimiwa Mchengerwa amekuja kule Kuhancha Golong'a na Nyanungu, yote tutazungumza lakini watu wangu pale ambao ninawawakilisha hapa Bungeni wanahitaji sehemu ya kuchungia mifugo yao, wanahitaji sehemu ya kulima, wanahitaji sehemu ya kuishi. Wale ni wakulima na wafugaji wala si wafanyabiashara. hata ukiwapelekea fedha wakila ikiisha watarudi palepale, na ndiyo maana walikwa na hasira kubwa. Lakini maneno yako yana matumaini, kwamba tulieni Mama anawasikiliza na utarudi mgogoro utaisha, na kwamba waendelee kulima. Kauli hiyo imeponya makovu yote ambayo ambayo yalikuwa yanakwamisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimuombe Mheshimiwa Waziri. Tulimpa risala Kalikatonga, alipata risala Nyanungu na Gorong'a, yale ndiyo maombi ya watu wa Tarime na mimi ndiye Mbunge wao; naomba ayafanyie kazi tutampa heko sana kwa kufanya kazi hiyo. Wale watu wana makovu tangu wakati wa uhuru. Ni wakati huu wa Mama Samia, kama Mama, mzazi, mlezi na mwenye huruma wapete unafuu wa maisha yao. Wao wana matumaini, wajenge nyumba za kudumu, mifugo yao iishi wasomeshe watoto ili wapate maisha bora sawa na Watanzania wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile hakuna namna ya kupata maji kule tofauti na kuchota maji ya Mto Mara. Kama mtaweka miundombinu pale kwa teknolojia ya kupata maji wakati wote tutawashukuru sana. Maji ya chumvi hata mimi nimekulia pale wote wamepeleka katika Hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikuambie Mheshimiwa Mchengerwa jambo ambalo linajadiliwa sana kule Bunda. Habari ya Nyatwali imeleta taharuki kubwa na kwa kweli wanaona kama watu hawa wanabaguliwa. Tusifanye *double standard*, watu wale wa Ngorongoro wamepelekwa kule Kilindi wale wamepewa usafiri watu wa Tarime na Bunda waliona. Wamewezeshwa kwa miundombinu,

kuna huduma za kijamii, kuna maji, kuna shule, kuna huduma za afya zinapatikana, wakapata pia na fedha ya kuanzia maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watu wa Nyatwali wakipewa milioni mbili hauwapi eneo la kwenda kuishi, wana makaburi yao, wana familia kubwa, wana watoto, wanasomesha, wakaanze maisha lakini mambo haya Mheshimiwa Waziri hebu jiweke ungekuwa ni wewe ungefanyaje? Ni *very unfair*. Hapa mimi naona ni kama kuna watu wengine wanapendwa zaidi wengine hawapendwi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mngetaka kutatua migogoro hii ni vizuri mkaangalia *as whole,* kwa ujumla wake. Wote ni Watanzania tunapenda hifadhi ziwepo, nchi ni ya kwetu lakini watu wasiishe kulalamika na kulialia kama wanabaguliwa. Kazi hiyo Mheshimiwa Waziri umepewa, mimi naamini unaweza kuifanya kazi hiyo, na nitakupa ushirikiano na Mheshimiwa Rais amekuamini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi hapa nilipo leo naweza nikaenda Nyanungu nikatembea mtaani kwa sababu Mheshimiwa Waziri ametoa kauli nzuri sana. Naweza nikaenda Kuyanja nikapokelewa nikapewa uji na Kichuli kwa sababu umetoa kauli nzuri. Nikienda Nyakatonga nitalala, nilikuwa siwezi kwenda kulala. Na kwa taarifa yako Mheshimiwa Waziri nilikuwa nimeamua nisiende maeneo yale mpaka mtakapo toa kauli. Kwa hiyo sasa Bunge likiisha nimeshapanga ratiba ya kwenda kuongea na watu wangu kwa kuwa Mama amesema mgogoro utaisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wote hawa wanampongeza sana Mheshimiwa Mchengerwa, wanampa ushirikiano na wanamuunga mkono Mheshimiwa Rais. Tunachotaka ni kutatua migogoro hii ya hifadhi na wananchi. Hifadhi iwepo, watu wawepo, maendeleo yawepo, watu wasome, watu wajenge na siasa iendelee, na 2025 tunataka Chama cha Mapinduzi kishinde kila kona kupitia kwako kwa kuondoa migogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo sishiki shilingi ninafuraha kubwa kwa kweli kwa Mheshimiwa Waziri nakuunga mkono kwa asilimia 100. Ahsante sana kwa nafasi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara. Nilimwita Mheshimiwa Riziki Said Lulida wakati huo Mheshimiwa Tecla Mohamedi Ungele na Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan, wanajiandaa.

**MHE. RIZIKI S. LULINDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru nami kwa kunipatia hii nafasi ya kuchangia hoja ya Wizara ya Maliasili. Mimi naitwa Mama mjusi, Mama *Selous*, Mama Mazingira lakini vilke vile ni Balozi wa Utalii; nilipewa tuzo hii na Mheshimiwa Rais. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa tuzo aliyonipa, kwa hiyo nitasema nitaongea ukweli na sitamwangusha. Kwa vile mimi ni mwanahifadhi lazima kwanza nitasimama na hifadhi na haki za binadamu ndani ya maliasili zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri, nilikuwa naye katika michezo, kazi aliyoifanya katika michezo mpaka timu ya watu wenye ulemavu tuliweza kufikia katika mpira wa *World Cup*. Na imani yangu wale waliokwenda kurithi kule watafanya kazi kama aliyofanya Mheshimiwa Waziri na Katibu Mkuu tufike tena, maana mwaka huu tena kuna mpira wa Afrika utafanyika Misri. Matumaini yangu ni kwamba timu yangu imejiandaa, na wale tuliokuwa naowalioingia sasa hivi tuwe nao vizuri ili hawa vijana ambao wamecheza katika mpira wa watu wenye ulemavu; sasa hivi tunazungumzia vijana kumi wako Ulaya huko wanalipwa katika *professional soccer;* Mheshimiwa Waziri na Katibu Mkuu hongereni sana. Vilevile nimpongeze Naibu Waziri kwa kazi kubwa anayoifanya ya kupambana na hali ngumu sana. Hii ni Wizara moja wpo katika Wizara ambazo ni ngumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi katika uhifadhi nitazungumzia kwanza Mbuga kubwa, ikiwemo Ruaha, Serengeti lakini pia tuna Mbuga ya Selous nayo ni mbuga kubwa ya kwanza Afrika lakini ya pili duniani. Lakini niizungumzie ya tatu, tuna *corrido* za wanyama ambazo ni ambazo wanapita. Asilimia 20 ya ardhi ya Tanzania ilitengwa kwa ajili ya uhifdhi, faida yake ya Uhifadhi tumetegemea kupata mvua, tunategemea mito itatiririka ili maji yasaidie katika kilimo, hivyo kuondoa uhifadhi ndio maana unaona sasa hivi ni ukame

unakuwa mwingi kutokana na maeneo mengi yameharibiwa. Mimi nalizungumza hili kwa ninayoyajua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbuga ya kwanza ambayo ninataka niizungumzie ni Mbuga ya Ruaha *(Ruaha National Park)*. *Ruaha National Park* inategemea maporomoko ya *Congo Basin* ambayo yanateremsha Usangu, Usangu inaingia Ruaha, Ruaha maji yake yanakwenda Kihansi, kilombero yanaingia Rufiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya maji yanasaidia Wizara ya Nishati na Madini, tukiyaharibu maeneo haya nchi itaingia gizani na matokeo yake itakuwa ni malalamiko makubwa zaidi. Na gizani hapa siyo Tanzania Bara tu, umeme unatoka katika maeneo ya Kilombero mpaka Rufiji unakwenda mpaka Zanzibar. Ina maana nchi itakuwa gizani, na itakapokuwa nchi gizani uchumi wa nchi utaporomoka, hivyo tuwe waangalifu sana. Na ukiangalia *Ruaha National Park* ukubwa wake si mkubwa hivyo kama watu wanavyofikiria. Niliangalia katika *google* wameniambia *Ruaha National Park* ina ukubwa wa *square* mita za mraba 13,800, nimeangalia Selous 44 niliangalia Serengeti 12,500. Niwapongeze ma-*DG,* Wakurugenzi Wakuu wa *TANAPA*, Mkurugenzi Mkuu wa Ngorongoro, *TAWA* na washikadau wote wa maliasili kwa kweli wanafanya kazi kubwa sana ya kupambana na watu ambao si waaminifu. Kuna watu waaminifu na watu wengine wanaingia ndani siyo watu waaminifu. Mimi nuilikuwa na mojawapo mdau ambaye nimezunguka Tanzania nzima na Wabunge baada ya kupata kelele kelele hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge tukaenda kujionea uhalisia, wafugaji wanaingia ndani ya mbuga na ng'ombe wakiwa na bunduki za kihalifu *machine gun.* Hivi kweli wewe katika mbuga kuna simba kuna tembo, kuna nyati makundi kwa makundi, wewe unaingiaje pale, ina maana wewe ni muhalifu na wafugaji wengi wanatumika. Tukubaliane Waheshimiwa Wabunge wafugaji wengi wanatumika na una muona mfugaji ana mifugo 4,000, ukiwa na ng'ombe 4,000 zungumza kuwa wewe ni bilionea una bilioni 1.2. Kitu ambacho hata Mbunge sitegemei kuwa na hela kama hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni yangu tufanye *database* ya kuwajua wafugaji wote wenye ng'ombe wengi halafu tuwatengenezee mifumo utajiri wao ule uweze kuwasaidia na tutajua kama wafugaji hawa ng'ombe wale ni wao au wanatumika na watu wengine kama mlivyoona Ngorongoro. Katika kuhamisha Ngorongoro tulitegemea watu watakuja Handeni na ng'ombe wengi sana. Waliambiwa kuna ng'ombe 5,000, 4,000, 3,000 siku wanakuja kuhama mtu anakuja na ng'ombe watano, ng'ombe 10 kitu ambacho mengi yalioletwa katika taarifa unaweza ukapata katika mitandao ni vitu vya kuzusha na kuwafanya watu na nchi iingie katika taharuki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninazungumza hiyo ukiichukulia Mbuga ya Serengeti kwa ukubwa wa *square* mita za mraba 12,500, kwa kweli unategemea Mto Mara upate maji na kama utakuwa unategemea Mto Mara kupata maji watavua, watapata samaki na vitu vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo unamuona mfugaji anaingia mule ndani kila siku tumege tumege tukapomaliza kumega mtasema bado Mto Mara umeshakauka. Je, mimi nayaona mapori makubwa makubwa yameachwa Tanzania hayajatumika, naomba Wizara ya Ardhi isimame na Wizara ya Maliasili watengeneze mfumo na mpango mkakati wa kuhakikisha baadhi ya wafugaji wanakaa katika mazingira mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano hai, wafugaji walipelekwa Mkoa wa Lindi, Mtwara walikataa leo Lindi maeneo yote waliyopewa wamehama, wamekimbilia Selous, unaona neno hilo. Wamehakikisha kuwa misitu yote kuanzia Rufiji wamekata na sasa hivi Lindi ni jangwa. Wamekimbia maeneo walipewa kila mfugaji *square* mita za mraba 5,000 mtu wa kawaida ambaye huwezi kupata lakini wameshakata misitu, wamekata kila kitu wamechoma mkaa, sasa hivi tunazungumzia Selous wanakwenda Selous. Sasa tunajiuliza kweli huu ni ufugaji au ni uharibu, tujiulize na tujipe tathmini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbuga ya Tendaguru; Tendaguru ni eneo ambalo tuna misitu ya na miti aina ya mipingo hapa ndipo alipotoka yule mjusi mpaka mimi napata jina la Mama mjusi. Tumekwenda na Naibu Waziri, wafugaji wote wamehamia pale

waliokatiwa maeneo yao maeneo chungu nzima walipewa wamekwenda kukaa Tendaguru. Matokeo yake Tendaguru tembo hawakanyagi anamuogopa mfugaji, Tendaguru simba hakanyagi anamuogopa mfugaji, Tendaguru unaiona imekaa pale wamejaa wafugaji na mifugo yao wanaharibu mazingira wanamaliza miti ya mipingo kauli za viongozi nazo zinarudi kwenda kuangali nilitoa amri hawa wafugaji waende katika maeneo yao lakini bado wamebakia maeneo hayo kwa nini hawajaondoka lakini akiongea mtu akiondoka wafugaji hawagusi tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi leo tunaizungumzia Milola, tembo wanakimbilia Milola tembo wanakimbilia maeneo ya pembeni kwa vile nini, maeneo yao yamezingirwa. Tunaanzia Nyasa anavukwa *corridor* kuingia Namtumbo, *corridor* limevamiwa na hizo ziko ndani ya *GN*. Tunatoka Namtumbo tunaingia ndani ya Selous wafugaji wako ndani ya Selous hivyo wakikaa ndani ya Selous na wanaingia na magobore tembo wanakimbia katika maeneo ya wakulima.

Mheshimiwa Spika, sasa hii kitu tukubaliane ninaomba tukitoka hapa tutaandaa timu ya kuhakikisha timu hii itakwenda kujua wafugaji hawa ni wapi? Na ni wachache kweli, wafugaji wako Kilimanjaro, wanafuga hakuna migogoro, wafugaji wako Arusha, wanafuga hakuna migogro wafugaji wako Shinyanga Mwanza lakini hawa wanayehamahama si wafugaji ni wafanyabiashara na wanatumika na hii kutumika tunaifanya nchi ina - *paralyze*. *(Makofi)*

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**TAARIFA**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lulida pokea taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa Mama yangu pale Mheshimiwa Lulida, kwa kweli kule kusini hakuna wafugaji kule kuna wachungaji. Wafugaji wapo hapo Ruvu kama ulivyosema wako Ruvu wako huko Kigoma wapo hapo

Kongwa wale ndio wafugaji, kule kuna wachungaji na ndio maana wanasumbua.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Riziki Said Lulida, unapokea taarifa?

**MHE. RIZIKI SAID LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapokea taarifa mimi natoka Selous, nimezaliwa Selous, ninaijua Selous tumekaa na tembo tukiwa marafiki lakini baada ya …

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, … wafugaji kwenda kuhama hama Tanzania nzima leo nasikia Mbeya…

**MWENYEKITI:** Ahsante sana na muda wako umekwisha.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haijafika dakika kumi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Nilimwita Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso wakati huo Mheshimiwa Tecla Mohamedi anajiandaa.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika Hoja ya Wizara ya Maliasili. Kwanza nianze kwa kumpongeza Waziri kwa kuteuliwa kuongoza wizara hiyo ni miongoni mwa Wizara ambazo tuseme ni ngumu au zina changamoto nyingi. Historia inaonesha Wizara hii haijawahi kuwaacha Mawaziri salama huwa hawamalizi muda wao, huo ndio ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sisi tunakutakia kheri na tumeona jinsi ambavyyo umefanya kwenye Wizara ya Utamaduni, sasa uko Wizara ya Maliasili, jitahidi tu utulie, uielewe vizuri wizara na

sekta zake zote, upate ufahamu ufanye *engagement* na wadau mbalimbali, usikilize maoni ya wananchi, usikilize maoni ya Wabunge, utatue changamoto za muda mrefu na utafanikiwa na unaweza ukadumu hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo nianze pia kwa kutoa pole kwa familia ya baba mmoja wa familia ambaye ameuwawa leo asubuhi na tembo akiwa shambani kwake katika Kata ya Oldeani, Wilaya ya Karatu, Mungu amlaze mahali pema peponi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme pia hoja yangu ya kwanza migogoro mingi ambayo tunaiona kati ya hifadhi na wananchi na yote ambayo yanaendelea kwa namna moja ama nyingine, migogoro hii ni ya siku nyingi baadhi ya maeneo ni migogoro ambayo imechukua muda mrefu. Ni migogoro ambayo ukimuuliza leo mwananchi wa kawaida ambaye yupo kwenye haya maeneo ambayo yanazunguka hifadhi, kwanza mwananchi huyo haioni umuhimu wa hifadhi wala haitamani kwa sababu anapambana na hiyo changamoto ya muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukimwambia mwananchi kwamba sekta hii ni sekta muhimu kwa uchumi wa nchi, ni sekta muhimu kwa kuliingizia nchi fedha za kigeni hawezi kukuelewa. Kwa sababu wameshakumbana na changamoto ya muda mrefu ambayo haitatuliki. Kwa hiyo, tunahitaji Mheshimiwa Waziri, unahitajika kwanza kurudisha imani kwa wananchi wote ambao wamekumbwa na hizi changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kujenga mahusiano mazuri, kumfanya mwananchi aone umuhimu wa hifadhi katika eneo lake yaani aone umuhimu na kutambua. Sasa wataweza kuona na kutambua kama atasikilizwa na baadhi ya changamoto ambazo amekumbana nazo za muda mrefu ziweze kuondoka na hatimaye kwisha kabisa. Naamini inawezekana, hasa migogoro hii ukisikiliza wataalamu wanasema kabisa migogoro hii ni kwa sababu kuna wananchi wamevamia shoroba, kuna wananchi wameingia kwenye maeneo ya hifadhi, kuna mifugo inaingizwa hifadhini na mambo wakadha wa kadha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najiuliza mfano swali moja ni kwa namna gani kwanza tumetambua shoroba zote? Hivi kuna takwimu sahihi ya kutambua shoroba zote ndani ya nchi hii? Halafu kuziainisha kwa kuweka labda *category A, B, C* zipi ambazo zimevamiwa kabisa kiasi kwamba hakuna namna inabidi tuziachie au zipi ambazo sasa zimevamiwa kwa kiasi kidogo zinaweza zikanusurika kwa kufanya maamuzi magumu ku-*compensate* na kuondoa wale wananchi na kuwapelekea maeneo mengine ili kuhakikisha shoroba zinaweza kendelea kuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni mambo ambayo yanatakiwa yafanyike kwa utulivu kwa usahihi na kufanya maamuzi magumu kwa kuwekeza fedha kama kweli tunataka kuona migogoro hii ina pungua lakini kuimarisha hizo shoroba. Ni kwa sababu tunahitaji hifadhi, tunahitaji wananchi wetu tunawahitaji, tunahitaji mambo yote. Tunahitaji hifadhi na sekta kwa ujumla isaidie katika uchumi wa nchi lakini haya yote tutakapoyahitaji maana yake lazima tufanye *balancing* ya mambo yote haya kwa pamoja lakini kingine kinachokosekana, unakuta kwenye eneo la shoroba kumejengwa mpaka ofisi hata za Serikali. Tunaambiwa hapo Mvomero, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya imejengwa kwenye shoroba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unajiuliza hivi mpaka inajengwa inatengenezwa *plan* mpaka inajengwa kumbe imejengwa kwenye shoroba. Tafsiri yake ni kwamba ama hakuna *proper coordination* sahihi ama utaratibu wa kupanga ardhi yetu haukamiliki au haufanyiki kwa wakati ama kuna uzembe na vinginevyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naamini kati ya kazi kubwa ambayo itakiwa kufanywa sasa ushirikiane na sekta zingine zinazohusika kwa maana ya Wizara zingine. Mfanye matumizi bora na kuzitambua haya yanayoenekana leo yasijirudie. Yaani tujue na kuzitambue kwamba hapa ni shoroba, hapa panatakiwa kujengwa hapa hapatakiwi hapa ni hifadhi hapa ni mpaka na kila kitu ndipo ambavyo tutaweza kwenda kupunguza na kuondoa migogoro hii ambayo inatukabili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine kubwa ambayo wananchi wengi wanajiuliza na mimi nikiwepo najiuliza. Hivi ni kwa nini inapotokea mwananchi kwa namna moja ama nyingine ama amekutwa kwenye shoroba au ameingia hifadhini au wanyama wamekufa, kwa nini inatumika nguvu kubwa na askari wa Jeshi la Uhifadhi, hivi ni kwa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameongea vizuri sana Mheshimiwa Musukuma asubuhi hapa ni kwa nini ni mafunzo yao ndio yanawafanya kwamba ukimuona mtu ni sawa sawa umemuona jangili unamfyatua tu risasi au ni nini yaani kwanini nguvu kubwa sana inatumika? Haya mambo yanasikitisha sana, yaani iko namna ya kuangalia ama kulifumua jeshi hili kwa ujumla na kuangalia namna iliyobora ama sijui wapewe maelekezo ama wapewe mafunzo kwa upya ama kuangalia mafunzo yao. Nadhani hatua ya kwanza sio kutumia nguvu kubwa, tuone namna ambayo inaweza kama kweli mwananchi ana makosa kuna namna, ndipo ambavyo hata askari akimkuta mwizi hawezi kumpiga risasi hivi hivi si atamkamata atampeleka kituoni na hatua zingine zitaweza kuendelea. Kwa hiyo, nadhani hata jeshi hili liwe na namna bora ya kuhakikisha inakabiliana na migogoro hii kwa namna iliyo sahihi bila kumuumiza mwananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo langu la Karatu tunapakana na Hifadhi ya Ngorongoro, tuna changamoto kubwa sana ya wanyama kuingia kwenye vijiji vya wananchi. Tuna kata karibia sita ambazo tumekuwa na changamoto ya muda mrefu ya wanyama kutoka hifadhini na kuingia kwenye maeneo ya wananchi. Kama ambavyo nimeeleza kuna mtu mmoja leo amefariki na wengine kadhaa huko nyuma wamejeruhiwa na mazao kuweza kuharibiwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nafahamu kuna mpango kupitia bajeti ya mwaka huu ambayo inafanywa na Hifadhi ya Ngorongoro kujenga fensi ya umeme ya kilometa 30 ili wanyama wasianze kutoka kwenda kwenye maeneo ya hifadhi. Hili ni jambo jema sana tunawapongeza kwa hilo lakini kama haitoshi pia kuna vituo vya polisi vitajengwa takribani 15 kupitia fedha za mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba kama ambavyo mmeweka kwenye bajeti yenu hiyo *electrical fence* ambayo mnataka kuweka tunaomba muweke kwenye vipaumbele yale maeneo ambayo ni korofi zaidi. Muyatangulize haya na maeneo mengine yaweze kufuata lakini pia Mheshimiwa Waziri unaweza kuchukua *sample* hii ya Ngorongoro kupeleka kwenye maeneo mengine Nchi nzima ambapo kwa kiwango kikubwa wanakabiliana na changamoto hii ya wanyama kutoka kwenye maeneo ya hifadhi kwenda kwenye maeneo yao kwa kuweka hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, najua ni gharama kidogo lakini ifike mahali hichi tunachokipata kutokana na Sekta hii ya Utalii irudi kwa wananchi kwa kuwapa unafuu, kwa kuweka hizo fensi ili wananchi waendelee kuishi kwa amani katika maeneo yao. Mifano mizuri mnaweza kwenda kujifunza hata *South Africa* wanatumia sana hii ili kuhakikisha wanyama wanabaki salama kwenye eneo la hifadhi lakini mwananchi kwenye eneo lake nalo anabaki salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwapongeze sana Ngorongoro kwa hatua hii tunamba basi mtekeleze ili Wananchi wa Karatu kwenye haya maeneo waweze kuishi salama katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala liliotokea juzi Mto wa Mbu, eneo la Jangwani. Mheshimiwa Waziri nimekusikiliza pia kwenye hotuba yako, nimesikitika kidogo. Kwanza mpaka leo vijana wawili ambao walikutwa kwenye ziwa na askari wa uhifadhi ambao walifungwa pingu walipigwa, mpaka leo hawajulikani walipo. Tunaomba mtuambie hawa vijana wako wapi familia zao zinalia, zinawatafuta kijana mmoja ni wa Karatu na kijana mwingine ni wa Mto wa Mbu. Vijana hawa mpaka leo hawajulikani, tunatamani kujua na wanatamani kujua na Mheshimiwa Waziri ikikupendeza uende ukae na hawa wananchi wa maeneo haya uwaambie na uwasikilize, kwa sababu kwenye hotuba yako umesema hawa wananchi walikuwa wanavamia walikuwa wanavamia boti ya askari wa uhifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sikiliza, askari wa uhifadhi wana boti za umeme, wananchi wa kawaida wanabodi za kawaida. Hivi inakuaje yaani mwenye boti ya kawaida ambaye haina nguvu na huyu mwenye boti ya umeme eti huyu wa umeme anatishiwa na mwingine, *how come*? Yaani haingii akilini. Mkatuambia hapa juzi kuna wananchi wameondoka na pingu, hivi askari wale wa Jeshi la Uhifadhi wana bunduki na mitutu, kuna mwananchi atathubutu kwenda kumchukulia hiyo pingu wakati amebeba hizo silaha, haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba haki za wananchi hawa familia hizi zinalia halafu msiseme uongo pale ambapo pana ukweli mseme muombe radhi kwa sababu makosa yanatokea hakuna aliyemkamilifu, muombe radhi mseme ukweli, mzifikie familia hizi, msikie kilio hichi kilichofanyika ni unyama wa kupitiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na hawa vijana wawili waliopotea, wawili wamefariki wengine bado majeruhi, kwa nini haya? Ndio haya nasema kwa nini inafikia askari hawa wa Jeshi la Uhifadhi wanatumia nguvu kubwa kukabiliana na wananchi pale ambapo inatokea hii changamoto? Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri ikikupendeza na kama utaona inafaa basi watembelee wananchi hao ukutane nao, usikie kutoka kwenye midomo yao itakuwa vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala mengine mawili kwa haraka haraka nimesikia kengele imegongwa. Suala moja ni mamlaka ya usimamizi ya wanyamapori *TAWA*. Hii *TAWA* imeanzishwa kwa amri ya kisheria chini ya kifungu cha nane cha Sheria ya Uhifadhi ya Wanyamapori na ina bodi ya ushauri haina bodi ya kiutendaji. Huko nyuma Kamati imeshauri mara nyingi sana iletwe sheria hapa Bungeni ya kuhakikisha *TAWA* inaundwa *properly* kwa mujibu wa sheria. Tuonaomba Mheshimiwa Waziri utapitia ripoti za Kamati utaziona, tunaomba *TAWA* ipewe mamlaka yenye nguvu kwa sababu ina kazi kubwa ya kusimamia mapori mengi ndani ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine Ziwa Manyara, Ziwa Manyara linaendakwisha na linaenda kupotea kabisa kwa sababu

ziwa lile limejaa tope, maji hata yakiingia pale yakae muda mrefu. Mwisho wa siku tutaipoteza Hifadhi ya Manyara, tunaomba sana zifanyike jitihada za kuhakikisha Ziwa Manyara linakombelewa na linarudi kwenye hali yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho…

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, …tunaomba ujenzi wa barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ujenzi wa Barabara ya Serengeti, barabara ile haipendezi kwa wageni wanaofika kwenye eneo hili. Tunaomba mlifikirie mjenge kwa namna iliyobora bila kuharibu mazingira bila kuleta athari yeyote kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana nilimwita Mheshimiwa Tecla Mohamedi Ungele.

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kunipa nafasi hii nami nichangie kwenye Wizara ya Maliasili na Utalii. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uzima. Napongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa na juhudi aliyoifanya kwenye ile shughuli ya *Royal Tour* ambayo ameendelea kuitangaza Tanzania katika uso wa dunia, lakini pia kuongeza mapato ya Taifa, kuongeza idadi ya utalii wa ndani na nje ya nchi, tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napongeza juhudi za Mheshimiwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa Majaliwa kwa kazi kubwa anayoifanya ya kutatua migogoro na kushirikiana na wizara hii kwa ajili ya kuweka hali iwe ya usalama katika Nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona amepambana na amejitahidi sana kwa shughuli ile kwa kazi ile na kadhia ile iliyokuwa ya

Ngorongoro lakini pia na nchi nzima kona zote wanashuhudia utendaji wake wa kazi wa uweledi na ufanisi mkubwa, tunamshukuru sana. Alikuja hata maeneo ya huko Lindi, maeneo ya Nachingwea akaenda kuona na kuwapa pole wananchi waliotajwa na kadhia ya Tembo mwaka jana lakini pia akawapatia chakula na kuwapa pole wale walioathirika kwa kuuliwa na ndugu zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza pia kwa kazi ya Wizara hii, Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii ya Maliasili na utalii hata kwenye ngazi ya mikoa kule na wilaya mbalimbali kwa kweli tunashukuru utendaji wao wa kazi tunauona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wizara hii ndio inatunza ule uhalisia wa siri ambao Mwenyezi Mungu alitupatia. Tuendelee kuitunza ardhi na miti na kila kitu ili itupatie usalama na afya kwa ujumla kwa kweli tunawapongeza sana. Sisi Wanalindi tunaahidi kabisa kutunza vyanzo vile vya maji na misitu na tuona kwa kiasi kikubwa Mkoa wa Lindi unachangia maji na uhalisia na uasili wa Bwawa la Mwalimu Nyerere ili kuhakikisha kabisa *sustainability* ya ile bwawa na tumeona matokeo yake na mafanikio yake tutayaona kama waziri wa jana aliyekuwa amemalizia ku-*present* jana katika ile Wizara ya Nishati. Tunaona kazi ni kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza pia kwa kazi ya Wizara hii ambayo inaendelea kutunza Utalii. Hata sisi Lindi pia tuna vivutio vingi vya utalii. Tunaona kule Kilwa Kisiwani, Tendaguru, tunaona kule pia kwenye Bwawa ambalo lina viboko ambao wana rangi ya *pink* ambao ni nadra sana katika dunia hii kuwaona. Kuna vivutio vingi, karibuni sana Lindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Lindi ni mojawapo ya mikoa iliyoathirika sana katika kadhia ya tembo. Hali kule siyo shwari, ni tete. Tumeona mwaka 2022 Wizara hii ilijitahidi, katika mikakati yake mojawapo ni kupeleka ndege kule. Walipeleka ndege ya kuswaga wale tembo kuwapeleka kwenye hifadhi na jambo lile lilifanikiwa na wananchi walifurahia sana wakaendelea na kilimo na maendeleo kwa ujumla. Tuliwashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanyama wale wamerudi tena. Wamerudi tena kwa kasi kubwa, wako makundi kwa makundi, wameendelea kuharibu mazao, wameua watu na wanaendelea kuua kila kuchapo. Wilaya zile za Nachingwea, Liwale, Milola, Kilwa na maeneo yote yale kule yameathirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali siyo shwari. Hivi sasa ninapozungumza, maeneo yale kuna njaa kali. Wananchi wale hawana chakula, watoto hawaendi shuleni kwa sababu ya tembo. Tembo wanazagaa kama vile unavyoona ng'ombe walivyozagaa. Kwa kweli hali siyo shwari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua pia mchango mkubwa…

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**TAARIFA**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa taarifa.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Tecla Ungele kwamba hali kweli siyo shwari, kuna tembo wengi ambao wanazagaa katika maeneo ambayo ameyataja, lakini kwa nyongeza sasa kuna fisi ambao wanasumbua wananchi nawanakula wananchi. Wananchi wameathirika sana na wanyama hawa, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ungele, unapokea taarifa?

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua pia mchango mkubwa anaofanya Mkuu wa Mkoa wetu wa Lindi Mama Zainab Telack na Wakuu wa Wilaya zote za Mkoa wa Lindi na viongozi wengine, na pia hata Jeshi la Uhifadhi Kanda ya Kusini wanafanya kazi kubwa kweli. Wakiitwa mahali wanakwenda. Ninachosema ni kwamba, wahifadhi wale wamezidiwa na idadi ya tembo. Nakumbuka Mheshimiwa Mama Salma Kikwete, Mbunge wa Mchinga alishukuru kwa

kujengewa kituo pale Milola na kupatiwa Askari na gari jipya, tukafurahi sana, lakini bado Askari wale wamezidiwa. Namomba wapewe chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Lindi tumezawadiwa na Mwenyezi Mungu kuwa na eneo kubwa lakini lenye rutuba na wananchi wa Mkoa wa Lindi ni wakulima wanaopenda kulima chakula, wakala chakula chao na mazao ya kilimo na mazao ya biashara. Sisi kwa desturi yetu tusingependa kupewa chakula. Mtu mwenye uwezo wa kufanya kazi, anafanya kazi akapata chakula, kwa sababu tunaamini chakula cha kuletewa hakiwezi kukidhi mahitaji ya familia, lakini pia kwetu sisi ni fedheha kuletewa chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi hali ilivyo, kuna ulazima kabisa Serikali ipeleke chakula. Wananchi hawana chakula, watoto wa shule hawana chakula, na pia hii kadhia ya tembo hii inaathiri hata utendaji wa Wizara nyingine, Wizara ya Kilimo watu hawalimi vizuri; Wizara ya Elimu, watoto hawasomi. Kwa hiyo, naona miaka ijayo 10, 20 au 50 kule tutaendelea kuwa masikini kwa sababu mojawapo ya kumkomboa mwananchi ni elimu. Sasa kama leo mtoto haendi shuleni kwa sababu ya kadhia ya tembo, unategemea tutaendelea kuwa na maisha gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini kifanyike? Nasema hili kwa maumivu na uchungu na unyenyekevu mkubwa. Tunaomba huo mkakati wa kurekebisha sheria na sera za uhifadhi ufanyike haraka iwezekanavyo. Tumesikia Kamati wame-*suggest* hicho kitu, lakini pia tunaomba fidia. Kuna watu walioathirika wale, tunaona kimya tu, hakuna kinachoendelea. Kuna watu wamekufa pale Nungunichile, Namikango, Iyonja, kule Barikiwa na maeneo mengi tu kule Liwale vifo vinaendelea siku kwa siku. Tunaomba fidia zao zifanyike angalau ndugu zao wafute machozi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kufanyike utafiti wa kina kwenye Wizara hii, kwa nini bado kunaendelea?

Tulisema kwamba shoroba unapita mahali fulani lakini mbona sasa hivi ng'ombe ndiyo wamehamia kwenye vijiji vyetu kabisa na vijiji vile vilikuwepo miaka yote? Kwa nini sasa hivi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaomba ufanyike mkakati mkubwa wa kuondoa wale wanyama.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umekwisha.

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri afike kule Nachingwea, Liwale, Kilwa na Milola aje aone hali halisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Tecla Mohamedi Ungele. Nilimwita Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan, lakini nafasi yake itachukuliwa na Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, wakati huo Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo pamoja na Mheshimiwa Ally Juma Makoa wanajiandaa.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi, Mwenyezi Mungu akubariki. Kwanza kabisa nianze kuipongeza Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi ambayo inaongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuweka jitihada kubwa katika Wizara hii ili iendelee kutuongezea mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa mambo yote ambayo ameyafanya kwenye Wizara alikotoka huko, kuhakikisha mpaka Yanga wamefikia hiyo hatua ambayo wameifikia, tunaamini pia ni jitihada zako zimeonekana huko. Yupo msanii mmoja alishawahi kuimba huko nyuma kwamba, "Hiki ni kisiki cha mpingo, wenye shoka wameshindwa, unakuja na panga unajisumbua."

Sasa tunaamini kwamba Mheshimiwa Waziri, wewe umekuja kwenye hii Wizara yenye kisiki cha mpingo, uje na msumeno ili uweze kutoa hicho kisiki cha migogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba tu kuchangia katika maeneo mawili. Moja ni ushauri. Ushauri wangu kwanza niombe Wizara hii kwa kushirikiana na Wizara nyingine zile ambazo zinaunda ile Kamati ya Mawaziri Nane kwamba tuangalie hata nchi nyingine ambazo zimeendelea, mfano, *South Africa* wame-*specialize* kwenye mambo kadhaa. Kwa mfano ukienda Durban ni sehemu inayohusika na viwanda tu. Ukienda Johannesburg ni sehemu ambayo inahusika na biashara na sisi tuangalie kwamba yako baadhi ya maeneo ambapo tutenge maeneo iwe ni *special* kwa ajili ya wafugaji wetu ili pia mifugo isiingie hifadhini na pia isiwaingilie wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, iko mikoa hapa inajulikana kabisa kwamba ni mikoa ambayo inategemewa na nchi hii kwa ajili ya kuzalisha chakula. Mfano Songea, Iringa, Njombe, Songwe, Mbeya, Katavi na Rukwa, lakini hata Mkoa wa Morogoro. Sasa pia mikoa hii ambapo inaendelea kugubikwa na wafugaji pia tunashindwa hata kuitambua mifugo yetu tuwaweke sehemu moja ili ile azma ya Mheshimiwa Ulega ya kutaka kuwapandia majani sehemu moja, itakuwa ni rahisi kuitambua mifugo hii na tuweze kuwahudumia vizuri lakini itawasaidia sana watu wa maliasili mifugo hii isiendelee kuingia hifadhini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, mimi nina maombi hapa kutoka kwa wananchi wa Jimbo la Momba. Kwa ridhaa yako naomba mhudumu apite aweze kumpelekea Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Waziri sisi watu wa Jimbo la Momba miaka ya 1974 kipindi kile cha Sogea cha Mwalimu Nyerere, wazazi wetu kutoka huko vijijini nikimaanisha babu zetu, waliambiwa watoke kwenye vijiji vya mbali wakae sehemu za karibu ili huduma za kijamii ziweze kuwapata kwa pamoja, kukiwa kuna lengo zuri na wakaachia mapori yao ya kutosha ili wakae kwenye vijiji kwa pamoja waweze kupata huduma za kijamii kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wazazi hawa, babu zetu hawa, waliamua kuachia hayo maeneo kwa nia njema kwa Serikali na maeneo hayo yakawa ni maeneo ya hifadhi. Sasa kipindi hicho cha mwaka 1974, watu hawa walikuwa wanakadiriwa kuwa chini ya watu 20,000. Sasa hivi tunavyoongea kwenye sensa ambayo imefanyika mwaka jana 2022, wananchi wa Jimbo la Momba tuko zaidi ya 270,000. Sasa tumeongezeka, katika vijiji hivyo 72 kuna maeneo machache tu wanaomba wapate kipande kidogo cha ardhi Mheshimiwa Waziri ili waendelee kuendesha shughuli zao za kilimo kwa sababu sisi shughuli yetu kubwa ni kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba kwa moyo wa unyenyekevu na uadilifu mkubwa, kwenye Kitongoji cha Kanyara ambacho kijiji chake ni Tontera kwenye Kata ya Chilulumo kwenye Kitongoji cha Mbaro kwenye Kijiji cha Mlomba Kata ya Chitete, kwenye Kitongoji cha Moravian Kijiji cha Itumbula Kata ya Ivuna, kwenye Kitongoji cha Mbao na Chiula kwenye Kijiji cha Ntungwa na Mkomba ambapo Kata yake ni Mkomba. Wananchi hawa wote wamezungukwa na hifadhi. Wananchi hawa wote wamezaliana hawana mahali pa kwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tunatambua kwamba nia ya Serikali ni njema, nia ya Serikali ni nzuri kwamba ni lazima tutunze maeneo yetu ili vizazi na vizazi vije kurithi. Sasa kama msipotaka kutupa hata kipande kidogo cha ardhi, hawa babu zetu ambao waliamua kuyaachia maeneo haya wakaamua ku-*sacrifice* kwa ajili ya sisi kizazi chetu, tusipopewa sisi tutaenda wapi? Wananchi hawa wasipokumbukwa ili wapate kipande kidogo; na hawaombi ekari 1,000, hawaombi ekari 500, wanaomba ekari chache tu ili waweze kuendelea kuendesha shughuli zao. Mtakapoendelea kutuacha hatuna mahali pa kwenda, sisi tutageuka kuwa watumwa ndani ya ardhi yetu wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunavyoongea miaka 30 iliyopita Bunge lilikuwa kule Msekwa ndiko Wabunge walikuwa wanakaa, lakini baada ya mahitaji kuongezeka sasa hivi tuko mahali hapa. Maana yake kulionekana kuna uhitaji wa kuongezewa Bunge ili kuwe na uwakilishi. Kwa hiyo, sisi mkituweka kwenye kundi la

kutufunga kwamba tunatunza kwa ajili ya vizazi vijavyo, maana yake mnakihukumu kizazi cha sasa kwa ajili ya kizazi kinachokuja. Sasa hawa wananchi ambao babu zao waliamua kutunza kwa ajili ya wajukuu zao, baba zetu wamevumilia sasa tumezaliwa kizazi kama hiki cha kwangu. Vijana hawana mahali pa kulima, vijana hawana mahali wanaweza wakajenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa dhati ya moyo wangu nikuombe sana sana Mheshimiwa Waziri na ikikupendeza nikuombe sana tunaomba uje ufanye ziara kwenye Jimbo la Momba kwa masikio yako ili angalau uweze kusikia namna ambavyo wananchi hawa wanaendelea kuomba. Tunakuomba sana, tunakuomba mno na kwa unyenyekevu mkubwa, kama ambavyo wananchi wa maeneo mengine wamefurahishwa. Wananchi wa Mara ambavyo Mheshimiwa Rais aliwaona akawakumbuka akaona iko haja ya kurekebisha tena mipaka ya uhifadhi. Hata sisi tunaomba mipaka ya uhifadhi ije irekebishwe ili wananchi hawa kwa moyo wa unyenyekevu waweze kupata sehemu ya kuendesha shughuli zao. Mimi nakuomba sana na ninarudia tena kuomba sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama bajeti hii itapita sisi hatukupata tena eneo la kulima, hata yale ambayo tulikuwa tumeendelea kuwaahidi wananchi kwamba watapata afadhali, tutaonekana ni waongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Naomba niwaletee tangazo kutoka Mezani, ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge waliopo Bungeni jioni hii.

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, Mbunge, ambaye ni Waziri wa Maliasili na Utalii, Ndugu Exper Pius kutoka *USAID,* Tuhifadhi Maliasili, karibu sana. *(Makofi)*

Pia tunao wageni wawili wa Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, Mbunge ambao ni binti zake kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Tunao wageni tisa wa Mheshimiwa Aloyce Kwezi, Mbunge ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma kutoka Kaliua Mkoa wa Tabora, karibuni sana na ahsanteni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na uchangiaji, nilimwita Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, wakati huo Mheshimiwa Ally Juma Makoa na Jacqueline Msongozi wanajiandaa.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuchangia hoja ya Hotuba ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Kwanza kabisa, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, Muumba Mbingu na Dunia kwa kutujalia uhai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwa kiongozi namba moja kuitangaza nchi yetu ya Tanzania kwenye Filamu ya *Royal Tour* ambayo imeiweka Tanzania katika ramani ya dunia. Napenda pia nimpongeze Waziri, Mheshimiwa Mchengerwa pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Mary Masanja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda nichukue nafasi hii kuwapongeza Wakurugenzi wote; Mkurugenzi wa Misitu, Profesa Silayo; Mkurugenzi wa *TANAPA,* Mheshimiwa Mwakilema, na Katibu Mkuu Mheshimiwa Dkt. Abbasi, lakini nawapongeza pia watendaji wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kazi nzuri ambayo wanaendelea kuifanya bila kumsahau Mkurugenzi wa *TAWA* na watendaji wengine wa Ngorongoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu utajikita sana kwenye migogoro ya wananchi na wafugaji lakini kwenye mambo ya malikale pia kwenye sheria ambazo zimepitwa na wakati ambazo bado zinatumika. Kwa nianze na migogoro ya wananchi kati ya wananchi na wahifadhi. Migogoro hii ukiiangalia kwa undani imesababishwa na

sababu ya Wizara yenyewe kutokuweka mipaka yake. Hivi karibuni ndiyo kumekuwa na uwekaji wa mipaka hiyo. Hifadhi nyingi mipaka yake haijulikani na hili lilisababisha wananchi wengi kwenda kujenga kwenye maeneo ya hifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, ushauri wangu kwa Wizara hii ya Maliasili na Utalii ishirikiane na Wizara ya Ardhi iweze kutambua maeneo yake kwa sababu kinachojitokea sasa hivi ambacho Wizara inakuja inasema hapa ni ushoroba wa wanyama, hapa hawa wananchi wamevamia, na vijiji vingine, kwa mfano, tulikwenda kule Kilosa, tulikuta vijiji vya Ng'ombo viko katikati ya hifadhi, lakini kuna zahanati na shule, vitu ambavyo vimewekwa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa basi, unakuta kwamba hakuna ule uelewano kati ya TAMISEMI na Wizara ya Ardhi pamoja na Wizara ya Maliasili. Kwa sababu kijiji kinapoanzishwa kinasajiliwa na Serikali inakitambua kama ni Kijiji, inakiwekea shule, lakini kinakuwa ndani ya hifadhi. Hivyo basi, ili twende pamoja na tuache kulaumu kwamba wananchi wanavamia maeneo ya hifadhi, ni bora Wizara ya Maliasili na Utalii ikatambua hifadhi zake iweke mipaka yake kwa kujenga barabara kuzungushia hifadhi hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye ushoroba. Utasema kwamba wananchi wamejenga kwenye ushoroba, wananchi hawaanzishi kijiji kwa siku moja. Kijiji hakioti kama uyoga, au mji hauanzi kwa siku moja ukasema kwamba hawa wananchi wamejenga kwenye ushoroba. Kijiji huwa kinaanza kidogo kidogo na miji pia inaanza kidogo kidogo kwa nyumba moja na ya pili: Ni kwa nini wahifadhi au Idara ya Maliasili unapoona kwamba kuna kijiji kinaanzishwa kwenye eneo la maliasili wasiwakataze wale wananchi, waambiwe kwamba hapa ni shoroba? Unangoja mwananchi amejenga nyumba yake ya thamani unakuja kubomoa kwamba hapa ni Shoroba na malipo yake yanakuwa ni kidogo? Kwa hili naomba nisiwaunge mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningependa kulizungumzia hapa, pia ni ile Kamati ya Mawaziri Nane. Kamati ya Mawaziri Nane ilipita, ikaainisha kwamba yale mamlaka ya kuendelea

na ile kazi ibaki kwa Wakuu wa Mikoa. Niwaombe Kamati ya Mawaziri Nane mweze kurudi kwenye mikoa mliyopita mkatatue matatizo ya ardhi yaliyoko. Kuna wengine wanaambiwa mmejenga maeneo yasiyostahili, mmejenga kwenye hifadhi, au mmejenga kwenye vyanzo vya maji. Kwa hiyo, nawaomba, mlipita mkiwa mnaenda maeneo ya mjini, nawaomba mtakaporudi sasa muende *site*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikupongeze tu Waziri, Mheshimiwa Mchengerwa kwa kwenda Tarime na kwenda Mbarali na nikuombe usiache kufanya hivyo. Usifanye kazi ya kukaka kwenye kompyuta ofisini, fanya kazi ya kwenda *site* ili uone maeneo yako yakoje? Ukikaa kuangalia kwenye kompyuta pori hili lina ukubwa gani, hii kazi itakuwa ngumu kwako mwanangu. Ni ushauri wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia hapa ni kuhusu kutangaza utalii mwingine. Tunaona *TV* kila siku zikimtangaza tembo, zinatangaza sijui nini, tunaomba pia mtangaze utalii mwingine kama wa fukwe, utalii wa malikale na pia mweze kuangalia vivutio vingine viko wapi? Hasa hapa sasa naomba nizungumzie watu wa malikale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa malikale ni wazembe, hawafatilii malikale zilizopo kwenye mikoa. Katika yetu kuna sehemu nyingi sana ambazo ni vivutio kwa wananchi na ambavyo ambavyo pia vinaweza vikaleta pesa kwa Serikali yetu ya Tanzania, lakini wao malikale wamejikita sehemu moja. Kila mkoa una historia yake, kuna mambo ya machifu na mengine mengi. Unakuta kuna mikoa ambayo ina historia ya biashara ya utumwa, kuna maeneo ambayo wakoloni (labda niseme wageni walivyokuja kwa mara ya kwanza waliingilia pale), kuna wavumbuzi wa kwanza ambao walikwenda maeneo yale. Sehemu kama hizo, hawa watu wa malikale wanatakiwa waifatilie. Tulikwenda pale Arusha…

**MBUNGE FULANI:** Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mchangiaji, endelea kuchangia.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, amenikoroga kidogo huyu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee. Nilikuwa nazungumzia malikale, kwamba malikale wafanye utaratibu wa kuainisha maeneo yao, washilikiane na watu wa TAMISEMI waainishe maeneo yao. Maeneo yao mengi hawana *happy*, maeneo yao mengi yamevamiwa kwa sababu wameyaacha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la malikale limeanza tangu tulivyopata Uhuru wa nchi hii. Lakini malikale wamekuwa mambo yao hayaendi, huoni kwamba kuna msukumo hapa wa malikale lakini nafikiri sijui ni bajeti ndogo au ni kitu. Tungeomba hawa malikale waweze kuongezewa. Kuna vitu vingi kama kule Mkwawa kuna Kinjekitile, kuna mambo ya Machifu wa zamani wanatakiwa kuwa kwenye historia ya nchi hii ili sisi tutakapokwenda watoto wetu wawezi kusoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba sana…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Taska Mbogo, ahsante sana kwa mchango wako. *(Makofi)*

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nusu dakika, robo dakika. Ninaomba *TANAPA* iongezewe bajeti, tulikuwa na hifadhi 16 zikaongezwa hifadhi sasa hivi ziko hifadhi 22, fedha ni kidogo. *TAWA* pia waongezewe, kwa sababu mapoli yaliongezwa lakini pesa hazikuongezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Namwita Mheshimiwa Ally Juma Makoa aweze kuchangia.

**MHE. ALLY J. MAKOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Na mimi nimpongeze Mheshimiwa Rais wa

Jamuhuri ya Muungano wa Tanzani Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa anavyoendelea kuilea hii Wizara akiwa na matumaini makubwa kwamba ni Wizara ambayo kiukweli ikitendewa haki yake kutokana na wingi wa vivutio tulivyonavyo itaweka mchango mkubwa sana kwenye Pato la Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuona hayo ameendelea kufanya mabadiliko. Utaona amembadilisha Mheshimiwa Mchengerwa na Katibu Mkuu wake wote wameletwa kwenye Wizara hii. Lengo ni kuchochea ufanisi katika Wizara ili Taifa liweze kupata mapato kutokana na hifadhi zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Waziri Mchengerwa kwa namna alivyoanza kuyatekeleza majukumu yake kwenye Wizara hii, na ninaamini ataiweza. Ni Wizara ngumu lakini ninamfahamu kidogo, nimeweza kukaa nae nikiwa bosi wake kule Pwani, nilikuwa nikimfutilia, naamini ataiweza kazi hii. Kama alivyoweza Wizara ya Michezo sina mashaka naye. Lakini pia ana Naibu Waziri mzuri. Akiweza kumtumia vizuri Naibu Waziri wake ni mwanamke jasiri pia, ni jasiri na utaona hata kwenye matamko yake na yuko *serious* na kazi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yake ina changamoto kubwa mbili. Changamoto ya kwanza ni migogoro baini ya hifadhi zake pamoja na vijiji, na changamoto ya pili ni mwingiliano wa wanyama na binadamu. Hizi ni changamoto kubwa ambazo atategemea *either* zitamsumbua ama Mungu akimjalia akizipatia basi atakuwa ameweza kuitendea haki Wizara hii. Ataweka historia kubwa katika nchi hii, na unaona hata mwelekeo wa bajeti tunavyochangia hakuna ukali sana, kwa sababu tuna matumaini makubwa kwamba amekuja hapo pamoja na Katibu Mkuu wakishirikiana vizuri na Makamishna wale, ni watu wazuri. Wana Bodi nzuri, na kwa kweli wakishirikiana wataitendea haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mifumo ya makusanyo tunaona wanaenda vizuri na tunaona ongezeko la watalii pamoja na fedha katika Taifa letu. Sasa waendelee kuimarisha hivyo ili wampe moyo Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la migogoro ya mipaka mimi nishauri jambo moja. Mheshimiwa Waziri hebu usirithi hii migogoro kwa maana ya historia yake, hebu jaribu *make* sasa vizuri wewe na *cabinet* yako yote muanze kuiangalia hii migogoro. Kuna migogoro mingine inaweza ikatatuliwa kwenye ngazi ya mapori yenyewe. Kuna baadhi ya maeneo, mimi nilipata bahati mmeniletea pale swagaswaga kijana Reuben ni kijana mzuri sana kwenye pori la swagaswaga, ni mkuu wa pori lile. Yeye ametumia mfumo wa kushirikisha wananchi katika ku-*solve* migogoro iliyopo katika eneo lake, na amefanikiwa sana. Ni kwa mara ya kwanza Reuben amekuwa akisifiwa na wananchi wa Kondoa wanaozunguka lile pori kwa sababu kwanza anafikika na anawafikia watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi wameweza kutatua mgogoro wa mpaka ambao ulikuwa unataka uzuke kwenye maeneo ya Iyoli, Kingale na Tampori. Wamekuja maafisa ardhi walikotoka hatujajua wametoka wapi? wakaweka mipaka mipya iliyoanza kusababisha taharuki kwa wananchi. Wananchi waliponipigia nikampigia mkuu wa pori Bwana Reuben, amekwenda kwa wananchi wakashirikiana kwenda kuitambua mipaka ya asili na wakaiyona. Jana walikuwa wanashirikiana kuhamisha vile vigingi ambavyo viliwekwa kimakosa kuvirudishia pale, na hivyo mgogoro ule *automatically* unaondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo nikushauri kwamba hata ile taarifa ya Mawaziri nane usiitegemee sana, sehemu kubwa itakupotosha tu, kwa sababu kiukweli haijafanya kazi kama alivyokusudia Mheshimiwa Rais. Tumia sasa nafasi uliyonayo na nafasi yako wewe kwenda kuijua hii migogoro, utaimaliza kiuraisi kama ulivyoweza kwenda Mara kule kwa watani wetu hawa wakakuelewa, ukija pale Kondoa kwa Warangi watakuelewa tu. Kwa sababu ni watu waele sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mgogoro ambao uko pale Mongoroma ambao unasababisha wananchi wanashindwa kufanya kazi zao. Tunauita mgogoro ni kwa sababu tu tunaendelea kukubali kurithi maneno ya migogoro. Lakini hata ukimwagiza Reuben akaenda akaonyeshwa mipaka ambayo wananchi walishirikiana na wale waliyotangulia ataiona na atatoa hivyo vigingi vipya

vilivyowekwa atavihamisha wananchi wataendelea na maisha yao. Kuna maeneo kama hilo nalozungumzia kuna wakazi zaidi ya 4,000 wakazi zaidi ya 2,000 wamekaa muda wote wanawajukuu na vitukuu leo kuu-*solve* mgogoro ule huwezi ukasema uwaondoe wale watu ilhali huna pakuwapeleka. Lakini kama tutafuata maelekezo ya Mheshimiwa Rais ambayo alielekeza ile kamati kwamba kama maeneo yenyewe si mazalia ya wanyama na kama maeneo yenyewe si chanzo cha maji na wananchi wameisha kaa muda mrefu kuna haja gani ya kusema kwenda kuwatoa na hauna pakuwapeleka pale? nikuwaacha waendelee kukaa, kateni lile eneo waonyesheni wananchi mipaka yao ili waendelee kuishi na kujenga nyumba nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo wanashindwa hata kujenga nyumba kwa sababu ya hizo taharuki ambazo zisizo na msingi. Kwa hiyo ninakushauri Mheshimiwa Waziri, ni vema sasa wewe mwenyewe ukimtumia Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Watalamu ulionao kwakweli mnaweza mkafanya mambo makubwa na mkaacha hizi hifadhi zikabaki kuwa salama. Hakuna namna leo mtawaweka salama hata askari wetu, kwa sababu leo kama kutakuwa na migogoro kati ya askari wetu wanaolinda kule na wananchi hatutafanikiwa kutunza hifadhi zetu vizuri. Lakini kama wananchi hawa watakuwa sehemu kama wale niliokwambia, wananchi wa Iyoli na Tampori ambao baada ya kuu-*solve* huo mgogoro sasa wenyewe wamekuwa ni walinzi. Ibaki sasa wananchi wawaombe tu kwamba tunaombeni mtuongezee maeneo halafu iwe ni hiari kwenu kuwapa au kutowapa lakini wawe wanajua haya maeneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo naweza nikakushauri sasa, ameongea vizuri Mheshimiwa Mbunge wa Malinyi, aliongea vizuri kuhusiana na mfumo za ajira za askari wetu hawa. Pamoja na ule mchango wake mzuri aliyoutoa nikuombe Mheshimiwa Waziri uangalie askari wetu hawa wote, wote askari hawa ni askari wa hifadhi wanasoma chuo kimoja, wanalinda wote tembo, wanalinda simba na mahifadhi yote wanalinda wao. Isije ikatokea sasa kuna taasisi nyingine wanapewa mishahara mikubwa na taasisi nyingine wanapewa mishahara midogo matokeo yake ufanisi unakuwa hakuna. Ndiyo maana unapata vijana ambao wanakwenda swaga

ng'ombe za wananchi kwenye hifadhi halafu wanazichukua wanakwenda kuwapiga faini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu wanakuwa hawana, kipato chao kinakuwa kidogo; na kama ilivyo kawaida, kwamba wanadamu huwa tuna wivu. Kwamba kwanini wenzetu walipwe kikubwa sisi tulipwe kidogo. hebu fanyeni ku-*harmonize* watu wote/askari wetu wote walipwe sawa. Makamishna wote wawe sawa katika *level* hiyo hiyo wote wafanane ili kuwe na ufanisi mzuri na isipatikane askari anaetamani kwenda kwenye taasisi nyinge kutokana na malipo madogo yanayopatikana kwenye taasisi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** ahsante sana kwa mchango wako Mheshimiwa Ally Juma Makoa. Nilimwita Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi wakati huo wafuatao wanajiandaa. Wa kwanza ni Mheshimiwa Deus Clement Sangu, Mheshimiwa Jeremiah Mrimi Amsabi pamoja na Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ili namimi niweze kuchangia kwenye hii Bajeti ya Wizara ya Maliasili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kwanza kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wangu kipenzi Dtk. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi nzuri sana aliyoifanya kupitia suala la *Royal Tour,* kiasi ambacho sasa imetoa taswira nyingine kabisa katika nchi yetu ya Tanzania kwenye masuala ya utalii. Nampongeza sana mama yetu huyu kwa sababu amekuwa akijitoa, ni mzalendo wa nchi yetu hii ya Tanzania. Hata nyinyi wenyewe pia Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi nchi imetulia kila kitu kinaenda sawa, uchumi unaendelea kukua, miradi yote inaendelea kutekelezwa, mikubwa na midogo yote inakwenda barabara, heko nyingi sana kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nichukue nafasi hii pia kumpongeza sana Waziri mwenye dhamana ya utalii ambaye ni kaka yangu Mohamed Mchengerwa lakini pia na *delegation* yake yote kwa namna ambavyo wanachapa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niende kwenye matukio ya tembo kuuwa na kujeruhi katika Wilaya ya Tunduru kwa kipindi cha mwaka 2020 mpaka kufikia sasa 2023. Kwa masikitiko makubwa sana naomba niseme kwamba tembo tunawapenda sana, ni rasilimali ya Taifa na wamezaana sana na ni kivutio kikubwa sana kwa watalii. Lakini mimi najiuliza tu, hivi ili mtalii aje amtambue tembo inabidi tembo hao wawe wanasindikizwa na sifa ya maelfu ya tembo wangapi? Kwa sababu tembo hawa wamekithiri wanafika mpaka kwenye makazi ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwetu kama ni shambani ukiweka viazi kwenye nyumba wanapenda ile harufu ya viazi wanakuja wanabomoa mpaka nyumba wanachukua viazi wanaenda kuvitumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nataka niseme hivi, natoa wazo sasa kwamba ni kwanini Mheshimiwa Waziri hawa tembo tusifikirie kuwavuna baadhi? tunawavuna wapungue kidogo kwa sababu bado wana kizazi waendelee kuzaa. Wale wanaopungua sasa maana yake ni nini, tutaenda kutoa yale meno tutayaweka kwenye Benki yetu ya Taifa ya Rasilimali za Taifa lakini pia nyama zile tutaweza kuuza kwenye mabucha yetu kwa sababu wako watu ambao wanakula. Kwa hiyo hii ni mali kwa mali. Tukiwavuna hadha pia itapungua. Wakati wanaendelea kuzaa basi wanachi wapate hafuweni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema kwamba mwaka 2020 katika Wilaya ya Tunduru pamoja na Namtumbo pia watu tisa walikufa na watatu kujeruhiwa; 2021 kufa watu wawili na saba kujeruhiwa, 2022 kufa watu nane na sita kujeruhiwa, 2023 kufa watu sita na sita kujeruhiwa katika Wilaya ya Tunduru tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya watu ambao wamekufa katika Wilaya ya Tunduru tangu mwaka 2020 mpaka 2023 walikuwa ni watu 25 na waliyojeruhiwa ni watu kumi saba, ni watu wengi sana, rasilimali ya nchi hii inapotea. Hata hivyo endapo kama wanapata majeraha na kufa bado inaonekana kwamba mnyama anathamani zaidi kuliko binadamu. Sasa hebu tuondoke kwenye hiyo adha. Kama kuna kanuni au sheria inatakiwa irekebishwe kwa mustakabali huo kwa maana yaku-*balance* binadamu na wanyama basi mimi nataka niseme hivi sheria hiyo iletwe hapa Bungeni ili tuirekebishe. Na kimsingi hauwezi kulinganisha mnyama na binadamu hasilani abadani haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nataka niseme kwamba fidia inayotolewa kwa mwananchi akiuwa ni shilingi laki moja tofauti na thamani ya binadamu lakini pia mwananchi aendapo kama ataliwa mazao yake fidia anayopewa ni shilingi laki mbili, laki moja mpaka laki tano. Mwisho huyo anakuwa amefilisika kabisa na wameona kwamba hili shamba ni kubwa wanaona aibu hata kumwambia kwamba haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niende kwenye migogoro ya vijiji ambavyo vinazungukwa na wanyamapori. Nimpongeze Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuona umuhimu wa kushughulikia migogoro hii. Kwamba sasa hivi punde nimesikia kuna taasisi au nchi imetoa fedha takriban bilioni 149 hivi kwa jili ya kusaidia mikoa ambayo inakutana na changamoto hiyo ya kuvamiwa na kushughulikiwa na wanyamapori. Kwa hiyo changamoto za wakulima na hifadhi za wanyamapori imekuwa ni kubwa kiasi ambacho sasa ameona kwamba atafute fedha kwa ajili ya kwenda kushughulikia changamoto hizo. Pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Rais, na niombe Wizara ifanye vizuri sana kwa ajili ya kumpa sapoti Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niende kwenye suala ambalo kimsingi nataka niliseme, linahusiana na suala la kauli, lugha mbaya kwa wananchi. Kabla sijalisema hilo naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Mchengerwa, Mheshimiwa Mchengerwa anafanya kazi nzuri sana. Tunamsemea hapa vizuri kwa sababu *you deserve the*

*best,* unafanya vizuri kabisa si, kwamba unapendelewa, sifa hiyo unastahili. Kwakweli unafanyakazi nzuri; na wengine wamesema ulitoka kwenye michezo, ulitoka kwenye utumishi kote huko umefanya vizuri umeacha alama. Sasa hivi uko maliasili na utalii tunategemea kwamba Wizara hii sasa inakwenda kuchanja mbuga na kuleta matokeo chanya katika nchi yetu hii ya Tanzania. Hongera sana nikutie moyo, endelea kufanya kazi na sisi kama kuna jambo lolote la kukusaidia ndani ya Bunge hili lilete tukusaidie, tuchakate ili kazi iweze kwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza pia kwa namna ambavyo amekuwa akitatua migogoro anatatua migogoro kidiplomasia, anakwenda *site* anazungumza na wananchi. Mwananchi hata kama alikuwa ana-*burden* gani anajikuta kabisa anacheka, anafurahi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikia Mheshimiwa Mchengerwa akiwa Wilaya ya Mbarali ambako kulitokea changamoto, ameondoka kule wananchi wanafuraha sana; endelea kufanya hivyo Mheshimiwa Mchengerwa. Lakini pia nimesikia amekwenda kule Tarime Vijijini, nako amefanya vizuri, tumeoa *clip* zake na ambavyo anaongea na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu Mchengerwa anafahamu kwamba ili sisi tukae humu ndani ya jumba hili ni lazima wananchi wapige kura kumchagua Mheshimiwa Rais, kuwachagua Wabunge, kuwachagua Madiwani na hata Wenyeviti wa Vitongoji anafanyakazi nzuri. Lakini wako wengine wanasahau kwamba ili kukaa humu ndani basi hakuna haja ya kutambua hivyo vitu. Ni muda mfupi sana jamani, tusisahau, na ni muda mfupi sana wa kukaa humu baadaye tunatoka kwenda kuomba kura kule. Sasa kama hatutambui umuhimu wa wale wananchi maana yake mwisho wa siku tutakwenda kule na tutarushiwa mawe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme jambo moja kwa masikitiko makubwa sana. Leo hii niseme kwamba nilikuwa nategemea Wizara hii inapokuja na bajeti yake basi Naibu Waziri wa

Maliasili awe alishakwenda kule Tarime Vijijini ameomba msamaha kwa wale wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, imetembea *clip* yake nchi nzima ambayo ilikuwa na maneno, ambayo siyo mazuri, siyo maneno ya kiungwana, maneno ambayo kiukweli hayana mahusiano mazuri na wananchi yanachonganisha baina ya Serikali na wananchi, ni maneno ya udhalilishaji kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nataka niseme ni maneno ya udhalilishaji kwa wananchi. Huwezi kwenda kuwaambia wananchi eti kwamba mnageuza huko porini ni sehemu ya kwenda kujisaidia, hapana siyo sawa. Kwa sababu hawa wananchi maana yake ni nini? Hawajui suala la usafi, hawana vyoo, hawajawahi kujenga vyoo. Naomba kupitia Bunge lako Tukufu huyu Mheshimiwa Naibu Waziri aende kuomba msamaha, sisi kama wananwake wenzake tunaksikia aibu kuongea maneno ya udhalilishaji kama yale kwa wananchi wale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana aende akaombe msamaha kwa wananchi wale ambao alitumia kauli mbaya kuwajibu, wale ni wananchi wa Tanzania. Tunawategemea kwa kazi alizofanya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, anastahili apewe kura zote 100% badala…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msongozi muda wako umekwisha.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, umesahau, kwa hiyo naomba sekunde moja tu. Kwa hiyo sasa nataka mimi nitashika shilingi kwenye eneo hili endapo kama Naibu Waziri hataomba msamaha hapa wakati tuna - *wind up*, aombe msamaha kwa wananchi wale kwa kile ambacho aliwatendea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno haya nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, sasa namwita Mheshimiwa Deus Clement Sangu, aweze kuchangia.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii niwe mchangiaji jioni ya leo, kwenye hotuba muhimu sana ya bajeti hii ya maliasili na utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna ambavyo amekuwa akiijali sana Wizara hii na namna ambavyo anapambana kukuza utalii, lakini upambanaji wake umejidhihirisha wazi kupambana na migogoro na sisi ni mashahidi anaendelea na ndio maana amemuweka waziri makini ambaye kila mtu aliyesimama hapa anaamini matumaini makubwa tunyao juu yako, juu ya utatuzi wa migogoro inayoendelea sehemu mbalimbali hapa nchini. Nikupongeze pia msaidizi wako Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa wizara kwa namna ambavyo mnafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nina mambo mawili; la kwanza, nitaelezea jambo la muhimu sana la kiuchumi linaloendelea ndani ya bonde la Ziwa Rukwa. Mnamo mwaka 2019 Serikali kupitia Wizara ya Madini ilitoa kibali cha Kampuni ya *Noble Helium* kuja kufanya utafiti ndani ya bonde la Ziwa Rukwa. Bonde la Ziwa Rukwa linahusisha Mkoa wa Rukwa wenyewe, sehemu Katavi na Songwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wamekuja na wameanza kazi yao tangia 2019, 2020, 2021 na 2022 na utafiti wanaoendelea nao umekuja na matumaini makubwa na sasa kwa utafiti tu wa awali inaonekana kwamba, Tanzania sasa ni nchi ya tatu duniani kwa *deposit* ya *helium* ambayo ni gesi adimu, ni *critical material* ambayo inatumika sehemu nyingi kama mnavyojua siwezi kutaja, kuna sehemu nyingi ambayo gesi ya *helium* ni muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni moja kati ya gesi ghali ambayo inauhitaji mkubwa duniani kwa hiyo sisi kama Tanzania kupitia bonde la Ziwa Rukwa, tumepata bahati kubwa ya kuwa na *deposit* kubwa na wanasema kwamba *helium* iliyo ndani ya bonde la Ziwa Rukwa ni *green helium*, ni *pure* kuliko yoyote ile inayopatikana duniani sehemu yoyote. Ukienda Marekani amabo wanaongoza na ukienda Qatar ambayo ni wa pili na sasa Tanzania tutakuwa wa tatu. *Best helium* inapatikana ndani ya bonde la Ziwa Rukwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika eneo walilopewa kufanya utafiti takribani kilomita za mraba 1467. Kilomita za mraba 167 ziko kwenye hifadhi na hifadhi hiyo ni ndani ya Ziwa Rukwa ambalo Ziwa Rukwa kwa ukubwa wake 80% inamilikiwa na Rukwa - Likwati na Uwanda *Game Reserve*, zote hizo zinamiliki maeneo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa walianza *initiative* ya kuomba kibali ili waruhusiwe Kwenda kufanya utafiti maeneo hayo, lakini mzunguko waliopewa zaidi ya miaka miwili, kunaenda nenda rudi. Waliambiwa mara ya kwanza wafanye *environmental impact assessment,* waka-*engage* hiyo *process,* wakatoa taarifa yao, wakapeleka taarifa *NEMC*. *NEMC* inka–*certify* kwamba hamna madhara yoyote na shughuli yenyewe inafanyika ndani ya mwezi mmoja. Baadaye walivyorudisha kwako huko *TAWA* wakasema hapana, nendeni tena Wizara ya Madini ndio watuandikie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wameenda Wizara ya Madini basi kumekuwa na kurushiana mipira mingi. Sisi pale tunaenda kupata faida kubwa, tunaenda kuongeza pato la Taifa, tunaenda kupata kipato ambacho *installation* ikishakamlika tunaenda kuingiza dola milioni 100 kila mwaka, tunaenda kuongeza ajira na mambo mengi yanaambatana na uvumbuzi wa gesi hii ya *helium.* Sasa huyu mtu ame-*invest* zaidi ya dola za kimarekani milioni 30. Anapewa mizunguko hiyo na sasa hivi amekodi vifaa vikubwa ambavyo vinagharimu kila mwezi wanalipa zaidi ya dola za kimarekani milioni 100.5. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vifaa vya *airborne survey* anavyo pale *site* kule Rukwa, lakini sababu tu ya kufanya maamuzi. Nakuamini ndugu yangu Mheshimiwa Mchengerwa kamalize jambo hilo wamalize utafiti suala la *drilling* litakuja baadaye. Tuta–*discuss* tuone je, kuendelea kuwa na *reserve* hizi au tuamue ku-*drill* tuingize mabilioni ya fedha, utakuwa uwamuzi wa Serikali hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliongea na waziri wa madini Mheshimiwa Doto Biteko na wewe sasa nakuletea rasmi katika mchango wangu, angalieni mkae pamoja hawa watu wanaingia hasara kila mwezi kupoteza dola za kimarekani zaidi ya milioni moja kusubiria maamuzi ya Serikali ni kuwapa *frustration* wawekezaji

wataona kwamba hatuko *serious* watanzania kwa jambo nyeti kama hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba niliseme kwa namna hiyo, naamini huyu ni msikivu ndani ya muda mfupi tutamaliza, hawa watu tutawa-*sort* waendelee na kazi yao ya utafiti na baadaye ripoti watatupa kama Serikali tufanye maamuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hilo nije na jambo la pili la muhimu ni migogoro inayoendelea na imesemwa na Waheshimiwa Wabunge wengi. Hapa nianze kwanza tena kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa namna alivyoridhia maeneo mengi ya hifadhi na kwangu mimi nilikuwa na mgogoro mkubwa sana pale Uwanda *Game Reserve* kwenye kata ya Kilangarani, Kata ya Kitete pale Kata ya Kapenta na Nankanga tayari maeneo yale yalirudishwa kwa wananchi. Kumebakia Kijiji kimoja ambacho tuna mgogoro Kijiji cha Nsanga ambapo mipaka haikueleweka kulikuwa na mvutano kati ya wanakijiji wa Nsanga na wale wataalamu mliotuma kwenda kuweka *demarcation* ya mipaka, hawajaelewana.

Mheshimiwa Mwenyekiti naomba hili ni jambo dogo tukali-*sort* hili suala la mipaka na migogoro ya mipaka tuimalize kwa *style* hii kwenye hifadhi ya Uwanda *Game Reserve*. Lakini baada ya pale sasa vioja ndio vilianza na hapa naamini kwamba askari wetu wa hifadhi wengi, wale wasiokuwa waadilifu walitamani migogoro ile iendelee kwa sababu wanaonekana ni *beneficiary* wa migogoro ile. Nasema hivyo kwa sababu nitaanza mwezi wa pili, jambo hili tumelimaliza Desemba Mwaka jana, mwezi wa pili tu fujo zikaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mweneo yale ambayo Mawaziri walipita wakawapa wananchi, askari tabia zao wanaenda wanamvamia mwananchi wanaswaga ng'ombe wanaingiza kwenye hifadhi. Sasa mwananchi mmoja pale Nankanga anaitwa Nasuminzi ali-*resist*, alivyo–*resist,* askari wakaamua watumie nguvu kubwa wakamtandika risasi mguuni na baadaye nilitaarifiwa mwezi ule wa pili, nikawaambia nendeni polisi mkaripoti na ng'ombe wakawa wamenyang'anya. Baadaye iulivyofika ile *issue* kule polisi, tukaendelea na mazungumzo, baadaye busara ikatumika ikabidi

wakae waelewane, yakaisha yule mwananchi akapewa ng'ombe, wakasema tutamsaidia matibabu, mpaka leo waliahidi watamtibu hawajafanya hivyo kwa masikitiko makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamempiga risasi kwa kuswaga ng'ombe wenyewe mle ndani na mimi nililetewa na tumeshirikishana na vyombo vyote vya usalama kuona namna ya ku–*handle* hii *situation* na sisi tumegeuka kuwa Wizara kwa namna fulani ku–*suppress* baadhi ya mambo ambayo tunaweza tukamaliza katika *level* zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haijaishia hapo kuna mzee mmoja alikuwa na baiskeli anatembea tu, wakamkuta wakasema bwana wewe unasenya kuni humu ndani wakamtandika viboko, wakamchana chana mgongoni nalo hilo tukataka tena kuli-*solve* wakampa tu shilingi 200,000 za kwenda kufanya matibabu. Nikadhani labda kwa mambo haya kwa sababu tuna-*resolve* haya mambo katika *level* ya chini tutayamaliza, naona wenzangu hawaelewi sisi ni wawakilishi wa wananchi na siwezi kukubali kuona mwananchi anaumia nikaka kimya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 26 Mei, kuna mambo mengine ya hovyo yametokea kule. Wameenda pale tena wanavizia hawa watoto wadogo wadogo, askari wanaenda na gari tena kutumia magari yetu ya Serikali, mafuta yetu, silaha zetu, wakaswaga ng'ombe kule ndani ya hifadhi. Walivyoswaga ng'ombe wakakamata wale ng'ombe wakasema sasa mtalipa. Wale wananchi nina orodha hapa na namba zao za simu nitakukabidhi Mheshimiwa Waziri ili tuanze na mambo haya yanayotuchafua na yanamchafua Mheshimiwa Rais. Wamelipa pale 26,920,000 na hizi hazina *control number,* wala hazina risiti. Watu wamechukua wameweka mfukoni na ndio maana nimesema kuna watu wanafurahia hii migogoro kwa sababu inawanufaisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe ndani ya tukio la doria moja tu mnaingiza 26,920,000 kuna utajiri wa namna hiyo? Doria moja ya usiku mmoja. Hawajaishia hapo! Risiti hawajatoa, wameenda wananchi

sasa hivi wanavuna, wiki iliyopita nilitengeneza timu yangu kama Mbunge ofisi yangu, nikajihakikishia haya mambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wameenda kule *site* wamekuta wananchi wameanzisha *task force* nyingine ya kuwanyang'anya mipunga, meeneo yale yale tuliyokubaliana walime. Walilima mwezi wa kumi na mbili na mimi ndiyo nilienda kuwatuliza wananchi kwamba limeni tu tayari na Mheshimiwa Rais kaweka sawa. Wamelima wanawaona, wamepalilia wamewaona, wameanza kuvuna wiki iliyopita wanataka mpunga tena wanachukua wanamnyang'anya mwananchi hapa mpunga, wanauza hapa anaona na hela wanatia mfukoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnadhani kutakuwa na amani Mheshimiwa Mchengerwa? naomba pale utume timu maana yake na sisi tunajipanga kama hamtachukua hatua tutajua namna yaku-*deal* na wale watu. Hatuwezi kukubali dhuluma, Serikali yetu hii haipendi dhuluma, wala hamkumtuma mtu akafanye dhuluma na nimekuwa nikiwa-*engage* mimi ni mtu mvumilivu sana na mstaarabu sana. Nimewa-*engage* taratibu twende tuelewane lakini naona hawa wenzangu hawanielewi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba tuma timu na uzuri watu wako menejimenti yako yote iko hapa. Ndani ya siku chache wawarudishie watu mpunga wao wote, nina majina hapa na wanajua na hizi hela hizi ambazo hazikukatiwa risiti 26,920,000 tujue zimeenda wapi? Nani amechukua? Na amechukua kwa sababu gani? La sivyo mzee! Nakuamini kabisa lakini nataka nisite baadaye jumatatu kushika shilingi, lakini naamini jambo hili *weekend* hii tutalimaliza likae salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ninakushuluru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, nilimwita Mheshimiwa Jeremiah Mrimi Amsabi ili aweze kuchangia.

**MHE. JEREMIAH M. AMSABI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsnate sana. Awali ya yote nimpongeze sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia kwa uongozi wake madhubuti katika nchi yetu ambao umeendelea ku-*push* maendeleo makubwa katika Taifa letu. Jambo ambalo kila mmoja wetu anashuhudia kila sehemu ya nchi yetu maendeleo yapo na ikijumuisha Jimbo letu la Serengeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri ndugu yetu Mchengerwa, nimesikia habari zako nimeona wakati ukiwa Wizara ile ya Utamaduni na kwa kipekee kabisa nimewahi kuleta kwako habari za kujenga kwa haraka barabara ile ya lami ya kutoka Tarime mpaka Mugumu, kutoka kule makutano mpaka Mugumu kwa ajili ya kuboresha utalii kufikika kwa Serengeti na nimeona jinsi ambavyo umepambana kusaidia na ku–*push* barabara ile. Kwa hiyo, nakupongeza nimeona kazi yako ni kubwa ni nzuri na nikueleze watanzania tunayo matarajio makaubwa sana juu ya mabadiliko katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wizara hii ni ya kibiashara, Watanzania tunahitaji fedha nyingi ili tuboreshe nchi yetu kwa hiyo utaenda kutusaidia kuhakikisha nchi sasa inapata fedha nyingikupitia Wizara hii. Tunampongeza pia Naibu wako Mheshimiwa Mary Masanja toka ameingia tumeshirikiana naye sana kila wakati kutatua changamoto mbalimbali kule na amekuwa mstari wa mbele sana katika ku–*push* ujenzi wa uwanja wa ndege katika Mji wa Mugumu kule Serengeti. Kwa hiyo tunakupongeza sana Naibu Waziri endelea kuchapa kazi pamoja na Waziri wako tuko pamoja na ninyi. Nampongeza pia Dkt. Abas, Katibu Mkuu kwa utendaji mzuri, Naibu Katibu Mkuu Bwana Anderson, Kamishna wa *TANAPA* ndugu yetu William Mwakilema, Mkuu wa hifadhi ya Serengeti ndugu Msindai wanafanya kazi kubwa nzuri kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ilani yetu ya Uchaguzi 2025, tulibainisha kuwa tunahitaji kukuza kiwango cha watalii wanaokuja nchini waongezeke mpaka kufikia milioni tano. Ndipo sasa kwa muktadha huu ninayo mambo machache ya kuchangia kwa ajili ya kuona namna gani tunaweza tukafikia hili pamoja na kuboresha uhifadhi. Moja, niombe sana Serikali iende kuhakikisha inaongeza

fedha katika utangazaji wa vivutio vyetu na hapa nishauri kabisa ni vyema tuone kuweka mfuko maalum kwa ajili ya *promotion* ya *tourism sites* au *tourism attractions* katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona Mheshimiwa Rais alikuja na ubunifu mzuri kabisa wa ile filamu ya *Royal Tour* baada ya pale hatujaona ubunifu mwingine ukiendelea, hatujaona kazi nyingine kubwa endelevu katika kuitangaza Tanzania kimataifa, lakini tukianglia sana wataalamu wapo na watu wapo weneye uwezo, nia wanayo. Tunadhani tu sasa Serikali iende kuongeza pesa ya kutosha kwa ajili ya kuona kwamba tunaitangaza nchi yetu kwa kiwango kiubwa, ili tupate fedha nyingi. Nimeona azma hii Mheshimiwa Mchengerwa unayo umeisema leo sasa basi tuiombe Serikali ikuongezee fedha za kutosha ili kazi hii ifanyike kwa ubora mkubwa kabisa, tuweze kujipata kipato kikubwa na nchi yetu ipate maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine tuhakikishge vivutio vyetu vinafikika vizuri kwa haraka na kwa gharama nafuu na katika hili nishauri kivutio kikubwa katika nchi yetu ninachokifahamu mimi. Vipo vingine lakini kivutio hiki katika hifadhi ya Serengeti cha *crossing* ya wale *wild beast* katika Mara *River* ni moja na vivutio bora kabisa duniani. Kiko katika vivutio 15 bora, lakini kwa nini hatupati watalii wengi katika eneo hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya sababu ni kwa sababu ni mbali sana, hapafikiki inachukua muda mrefu sana watalii kufika kule, magari yanaharibika sana njiani, watalii huchoka sana, wanatumia masaa mengi barabarani, wanakosa *comfortability,* gharama kubwa ya kufika huko, barabara zinakuwa mbovu muda mwingi, umbali mrefu siyo mzuri kwa usalama wa watalii na hivyo basi wamewahi kufanya tafiti na tumesoma ripoti nyingi za wale mawakala wakubwa wa utalii duniani, wakiwemo *Hot Wire,* wakimwemo *Agoda* na wakiwemo *Expedia* wamesema ili watalii waende katika sehemu fulani kwa ajili ya kutalii, yako mambo yanayo-*lead* ile *decision* yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, 42% ni ubora wa kivutio, 20% ni ubora wa huduma za malazi, chakula na usalama, 20% ni kufikika kwa

kivutio, ubora wa miundombinu ya barabara na usafirishaji, 18% ni unafuu wa gharama. Sasa basi ukiangalia pamoja na kivutio kizuri, pamoja na uwepo wa vivutio vingi sio sababu ya kutosha watalii kuendela kuja kwa wingi katika nchi yetu. Mfano mzuri tunaona Serengeti na hata nikienda kwa mfano mmoja rahisi tu, ukiangalia kutoka katika viwanja yetu vya ndege mpaka kufika sehemu hii ya kwa Kogatende ambako wanyama wale wanakatiza ule Mto Mara kuingia upande ule wa Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoka *KIA* mpaka Kogatende ni kilomita 610, kutoka uwanja wa ndege wa Arusha mpaka kwa Kogatende ni kilomita 557. Kutoka Mwanza *Airport* mpaka Kogatende pale Mara *River* ni kilomita 340. Kutoka Seronera kutoka Musoma, uwanja wa Musoma mpaka pale kwa Kogatende ni kilomita 187, kutoka Seronera *central* Serengeti mpaka kwa Kogatende ni kilomita 183, lakini kutoka Mji wa Mugumu mpka kwa Kogatende ni kilomita 56 peke yake na hili ndilo eneo ambalo limependekezwa kujenga uwanja wa ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri nikuombe sana andika historia, jenga uwanja ule 147,000,000 wataalam wameshauri, tafiti zimefanyika, nikuombe Mheshimiwa Mchengerwa chukua hatua, hii itasaidia watalii kuongezeka, itasaidia kukua kwa uchumi kwa watu wa Mkoa wa Mara hususani Wilaya ya Serengeti ambao sisi tunapakana na hifadhi hii, tunahitaji kuona pia na sisi tunanufaiuka na utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutawasaidia watalii wengi kupunguza gharama za kuja kwetu, kupunguza umbali huu maana ya ke ni kupunguza gharama. Ni kupunguza kulala vituo vingi na hii itafanya watalii kwa *comfortability* kubwa tukijenga uwanja ule. Pia tunaenda kuongeza ajira nyingi kwa watu wa Mugumu na Serengeti kwa ujumla, tunaenda kusababisha kuongeza au kuboresha utalii na ule uhifadhi kwa sababu sasa ule utitiri wa vile viwanja vya ndege ndani ya Serengeti vinaenda kupungua. Pia tunaenda kuongeza maeneo ambayo watu wengi wanaweza wakajenga mahoteli ya kitalii katika Mji wa Mugumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kuomba sasa wizara hii iende kuangalia namna bora ya kuongeza na kuboresha

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. JEREMIAH M. AMSABI:** …uhifadhi katika hifadhi ya Serengeti kwa kushirikisha sana wananchi ili kupunguza migogoro ya wanayama wanaingia na kuvamia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja nakuomba dakika moja tu nimalizie. Sasa wananchi wengi sana wa Serengeti wamepata shida, wanyama wanaingia kila wakati, Mheshimiwa Mchengerwa nikuombe sana tusaidie kuona kwamba tunawashirikisha wananchi. Kama hatuweki tutumie teknolojia ya fensi, basi twende kuchukua wananchi wengi waweze kuelimishwa, waweze kuelekezwa, mambo ya kukamata wanayama wale ng'ombe na nini na wananchi wanaoingia waelimishwe sana.

**MWENYEKITI:** Haya ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako.

**MHE. JEREMIAH M. AMSABI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa kuchangia kuanzia sasa utakuwa ni dakika nane na hatutaongeza. Kuna ambao watabaki pia ambao hawatapata fursa ya kuchangia leo, tutawapeleka Jumatatu. Kwa hiyo, naomba uzingatie muda wako.

Nilimwita Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, wakati huo wajiandae Mheshimiwa Saashisha Elinikiyo Mafuwe, Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mheshimiwa Zaytun Seif Swai na wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami nichangie Wizara hii ya Maliasili na Utalii. Nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa namna anavyotafuta fursa za utalii na kuongeza utalii katika nchi yetu.

Hongera sana Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yako, Naibu Waziri kwa kazi ambazo mnafanya kwa ajili ya kuhakikisha kwamba Wizara hii inaendelea kuwa salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo machache sana ambayo nataka nichangie leo. Mheshimiwa Waziri ulichokifanya Tarime sasa ni muda muafaka wa kuja kufanya vilevile kuwasikiliza wananchi wa Busega na wananchi wa Magu. Tuna Pori la Sayaka, umefanya kitu kikubwa sana pale Tarime, namna ulivyowasikiliza wananchi kwa kweli uliwapa faraja kubwa sana. Leo wananchi wa Busega na Magu wanataka waje wakusikilize, uwasikilize katika Pori la Sayaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Busega kwa maana ya Kata ya Nyaluhande kuna Kijiji kinaitwa Nyaluhande, Mamkala pamoja na Mwagindi. Vijiji hivi vilikuwa vinanufaika na sehemu ya eneo ambalo sasa limetafsirika kuwa ni pori. Wameendelea kulitumia zaidi ya miaka 40, wamelima zaidi ya miaka 40 maeneo yale, lakini sasa wamekuja kunyang'anywa na kuyafanya mapori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina tatizo na pori, na tunatamani na tuko tayari sisi wananchi wa Busega kufanya uhifadhi, kuhakikisha kwamba, mapori yanalindwa na hili pori lilindwe. Hata hivyo, kuna eneo la mita 840 wananchi wetu wamekuwa wakilihitaji siku zote, wamekuwa wakilitumia katika kazi ya kilimo, lakini sasa hawawezi kulitumia. Hivi karibuni viongozi wanawaambia limeni kwa mwaka huu, mwakani msilime, ufugaji nao umekuwa shida, wakipeleka mifugo wanakamatwa, wanataifishwa na wengine kuuzwa. Sasa ni wakati muafaka Mheshimiwa mchengerwa uje sasa uwasikilize wananchi wa jimbo la Busega na Magu, ili tuweze kujadili tatizo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi hapa nilikuwa nasikiliza hotuba ya Mheshimiwa Waziri katika suala zima la migogoro. Amezungumza pia kwamba migogoro inaongezeka kwa sababu pia wananchi wameongezeka. Nikawa najiuliza swali la kawaida kabisa, ni lini wananchi watapungua? Jibu unapata, hapana, hawatapungua kwa sababu tunaongezeka kila siku. Ukiangalia hata Sensa ya 2012, tulikuwa wananchi milioni 44, Sensa ya 2022 tuko milioni 61.7. Maana yake ni kwamba tumeongezeka kuwa watu 35 katika 1,000. Nini

maana yake? kila mwaka wanaongezeka asilimia asilimia tatu. Sasa asilimia tatu ya milioni 61.7 maana yake katika miaka inayofuata kila mwaka watakuwa wanaongezeka watu milioni moja na laki nane. Sasa watu milioni moja na laki nane kwa miaka kumi ijayo tunategemea wataongezeka kuanzia milioni 15 mpaka milioni 20. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini maana yake? Mwaka 2032 tunategemea kuwa na watu milioni 75 mpaka milioni 80. Hii ni hesabu ya kawaida, haihitaji nguvu nyingi, inafahamika kulingana na sensa tuliyonayo na *birth rate* ya asilimia tatu ambayo imeonekana katika sensa ya mwaka 2022. Sasa mje na mpango kwa sababu watu hawatapungua. Njooni na mpango wa nini kifanyike kupunguza migogoro? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama itakuwa watu wanavyoongezeka na migogoro inaongezeka, maana yake wataongezeka 2023, 2024, na hata migogoro itaongezeka. Ni lazima sasa mje na mpango, ni kwa namna gani watu wataongezeka, lakini migogoro ipungue. Hiyo ndiyo mjenayo ili mweze kuona namna ya kutatua. Mkae Wizara ya Maliasili, Wizara ya Ardhi, Wizara ya TAMISEMI, mje na mpango wa pamoja ili mweze kutusaidia kuhakikisha kwamba wananchi wetu waweze kupata nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kuzungumza hapa ni suala la tembo na viboko. Sasa hivi limejitokeza la fisi, hususan katika moja ya kata huko Wilayani kwangu. Sasa ni wakati muafaka wa kuvuna baadhi ya viboko ili wananchi wetu waweze kupata nafuu, pale Jimboni Busega watu wamekufa, mwaka 2022 zaidi ya watu watatu wamekufa kwa sababu ya viboko. Ni wakati muafaka sasa mje mwavune ili wananchi wawe na amani katika yale mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inatakiwa kufanya *research*. Mfanye tu *reseach* kwa nini hili? Moja ya majibu mtakayoyapata ni kwamba wamezaliana sana. Watu tunaongezeka na wanyama wanazaliana. Sasa ifike muafaka wanyama tuwapunguze kwa sababu si hatujawatolea uzazi, kwa hiyo, tutakapowapunguza, wachache

wataendelea kuzaliana. Kwa hiyo, watakapokuwa wanazaliana, wengine tunawapunguza. Tusipofanya hivyo, maana yake tatizo litaendelea kuwa kubwa, watu watakufa, watu watauawa na pia migogoro itaongezeka. Ni lazima pia baadhi ya wanyama kwa mfano tembo na viboko tuone namna ya kuwapunguza ili tuweze kuwa na tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nataka kuchangia hapa ni juu ya watalii na matumizi ya Uwanja wa Ndege wa Mwanza. Ukiangalia katika hali ya kawaida kutoka pale Mwanza kwenda Serengeti kwa maana ya lile geti ambalo liko pale Lamadi, ni kilometa chache, nafikiri ni kilometa 120. Sasa hapo ni karibu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni lazima tuwekeze katika Uwanja wa Ndege wa Mwanza ili watalii wengine waanze sasa kushukia pia Mwanza ili nasi huku upande wa Kanda ya Ziwa tuweze kupata watalii. Watalii wataingilia huku kwenye geti la Serengeti ambalo liko Lamadi na wananchi wangu wa Lamadi na wenyewe watapata vipato kutokana na watalii watakaopita maeneo haya.nini maana yake? Watu watajenga hoteli, watapata ajira ambayo itatokana na watalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ndugu yangu hapa Mheshimiwa Boniventura Kiswaga na wenyewe watajenga pale hoteli. Kwa ndugu yangu Mheshimiwa Mabula, hapa katikati nao watakuwa na hoteli pale. Hii itasaidia sana watalii wetu sasa kuongeza kipato katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine la mwisho, limezungumzwa hapa suala la Nyatwali. Kuna wananchi wangu ambao…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana kwa kuweza kutii muda. Nilimwita Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Wizara hii. Kwanza namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya na uzima. Pia nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri anayofanya kwenye Wizara hii yeye pamoja na Naibu Waziri. Mko vizuri, chapeni kazi, Mheshimiwa Rais amewaamini na sisi wenzenu tunawaombea mweze kutimiza matarajio ya wananchi na matarajio ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro ambaye ni mhifadhi pia kwenye eneo letu, anatusaidia sana kutunza mazingira pale. Huyu mtu bingwa, Nurdin Babu tunamshukuru sana. Nampongeza Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya, mtu bingwa, Amiri Mkalipa, kwa kazi kubwa anayoifanya pale Hai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba niseme hapa kidogo, namshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kubuni na kuja na *Royal Tour,* imebadilisha maisha yetu kwa kiwango kikubwa. Nami nitasema kwa sababu, kama ni mnufaika namba moja, wote mnakumbuka Mheshimiwa Rais alipotoka huko alishukia pale Hai, Uwanja wetu wa *KIA*. Sasa nataka niwaeleze mambo tunayojifunza na yaliyopatikana kutokana na filamu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2021 watalii waliokuwa wanashuka pale *KIA* walikuwa ni 354,000, hiyo ni mwaka 2021. Leo mwezi Aprili, watalii ambao wanashuka pale Uwanja wa *KIA* uliopo Jimbo la Hai ni 728,000. Hayo ni mabadiliko makubwa sana, lakini ndege zinapishana. Leo unaambiwa *KLM* wanatua pale mara sita kwa wiki na ndege nyingine zinaendelea kuja. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi hii kubwa aliyoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia na wewe Waziri nikushukuru, wananchi wa Hai wanasema ahsante. Nimepiga kelele hapa kuhusu *CSR,* nimeambiwa tayari mmetupelekea fedha pale Shule ya Mure

iliyoko Nuni kwa ajili ya kufanya ukarabati wa majengo, Shule ya Mkoeshoo iliyoko Mkuu, lakini shule ya Kiarasa iliyoko kule Sawe, Shule ya Mkweseko na shule iliyoko kule Foo, lakini pia pale Lukani mnafanya Mradi wa gesi. Tunawashukuru sana kwa kusikia maombi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishauri. Nimekuwa nikisema hapa, tunazungumza utalii, tunazungumza Mlima Kilimanjaro, namwomba sana Waziri, natamani kuona huku ameweka fedha kwa ajili ya kupanda miti Kilimanjaro. Hii mnayosema wanaleta wadau, wanaleta wanapanda, lakini hakuna *mechanism* ya kuitunza. Hata sisi tunapanda sana miti kule, lakini *mechanism* ya kuhakikisha miti hii inapona, haipo. Hizi idadi unazozitaja kwenye hotuba zako Mheshimiwa Waziri, tukienda kukagua iliyopandwa na iliyopona ni vitu viwili tofauti. Kwa hiyo, naombe kwa kweli kwenye bajeti yako utakapokuja kuhitumisha hapa, utuambie bajeti uliyoipanga ya kupanda miti na kuhakikisha miti hiyo inapona. Nakuomba sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni sambamba na lile la vibali. Niliuliza swali hapa jana, miti inakatwa kwa kiwango kikubwa sana. Ni kweli zipo zile kamati zinazohusika na utoaji kwa mwongozo ule wa mwaka 2017, lakini Wenyeviti hawashirikishwi. Ile barua inayoandikwa ya anayeomba kibali anapitisha kwa Mtendaji wa Kijiji, anapitisha, inaenda kwa Mkuu wa Wilaya anakaa na timu yake, inarudi. Ninachoshauri, *Ward DC* wote, Diwani na viongozi wote washiriki kwenye maombi yale, ikirudi Mkutano Mkuu wa Kijiji ushiriki. Tumeona mazingira yanavyoharibika. Nimesema pale Uswaa miti inakatwa, Bonde lile la Weruweru miti imekwisha. Naomba sana hili ulichukulie kwa umakini wake mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba tuimarishe mifumo ya watalii wanaopanda Mlima Kilimanjaro. Moja, nimekuomba kufungua ile barabara mpya. Nadhani Mheshimiwa Waziri umenielewa na umesema timu yako ikafungue barabara ile tuwe na barabara nyingi, lakini kuna jambo, watalii wanaopanda Mlima Kilimanjaro isiwe ni adhabu, iwe ni watu wanaenda kwenye furaha. Naomba mageti yote mkubali kutolewe vibali, watu wajenge hoteli ili mtu anayetaka

kupanda mlima, akichoka apumzike, aendelee na safari kuliko ilivyo sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kumekuwa na malalamiko kwa wale wanaopandisha mlima. Sasa hivi wametangaziwa kuanzia mwezi wa Saba kwamba kila mtalii anayepanda lazima afanye *booking* kwa siku saba, kitu ambacho siyo sawa. Watu walishafanya *booking* kwa siku tano. Kingine ambacho kinafanyika, mtalii akifanya *booking* kwa siku sita, ikatokea hapo katikati ameumwa akashindwa kuendelea na safari, akija ku-*resume* tena anaongezewa siku. Kwa hiyo, *burden* inabaki kwa wale wapandisha mlima. Naomba sana na hili ukatazame, linarudisha nyuma maendeleo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa ninaloliomba, watalii wanapanda Mlima Kilimanjaro, umesikia hapa hakuna Mbunge wa Kilimanjaro anayezungumza kuhusu mgogoro, tunaishi vizuri na watu wa *KINAPA*. Kwa nini? Kwa sababu, tunaendanao na *CSR* mmetuletea, lakini vijana wa Hai hawapati kazi hizi Mheshimiwa Waziri. Kampuni ya Utalii inatoka Arusha inakuja na watu wake, tumeshasema hapa, naomba na wewe utusaidie kusimamia hili. Vijana wa Hai wako tayari kufanya kazi hii na tumeshatengeneza umoja wetu, tumetengeneza kikundi, kama wanaopandisha mlima ni watu saba, basi waje na watu watatu, wanne wachukuliwe pale Hai ili vijana wapate kazi. Hii ni kuongeza *sense of ownership,* hili tunalizungumza mara kwa mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikwambie leo, Wilaya ya Hai ina vivutio vingi, nami nakukaribisha, usije kwa haraka haraka. Kwanza ukija Wilaya ya Hai unakuja kujifunza namna ya kuondoa migogoro maeneo mengine, maana pale hatuna migogoro. Pili, ukija kuna vivutio vingi, njoo ukae hata siku tatu. Pale tuna daraja linaitwa Daraja la Mungu, halipo sehemu nyingine, liko Hai. Tuna maporomoko ya maji kule Kihori, Mshara, Mpeseko, na tuna kituo chetu cha maji ya tofauti. Nmekuwa nakitangaza mara kwa mara, nawe Mheshimiwa Waziri ufike pale. Tuna samaki wanafanya *massage,* maji mazuri yako pale Chemka, lakini watu wanaanza kukigombania. Watu wa *Arusha Tech* ambao wanajenga chuo pale nao wanakitaka, watu wa Pangani nao wanakitaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeongea na Mheshimiwa Mabula hapa, Waziri wa Ardhi ameshanikubalia. Lile eneo litengwe liwe la Halmashauri ya Wilaya ya Hai ili tukusanye mapato pale na tukitunze kwa sababu ni cha kwetu na bahati mbaya sana ni eneo letu la kimila, haliwezi kuchukuliwa na watu wa maeneo mengine. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri aweze kusimamia jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, mimi nishauri jambo, kwenye hii migogoro inayozungumzwa hapa, Waziri umeingia kwenye hii Wizara. Huko ulikotoka, umefanya vizuri sana, hebu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Ahsante sana Mheshimiwa Saashisha Elinikiyo Mafuwe kwa mchango wako.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Anna Richard Lupembe.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Naomba nimshukuru Mungu ambaye ametupa uzima na uhai saa hizi tuko hapa tukiwatumikia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti. Naomba nimpongeze Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa ambayo ameifanya kwa ajili ya utalii. Tumeona jitihada kubwa amefanya kupitia *Royal Tour,* tumeona kazi kubwa sana, tumeona watalii wakija katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Waziri pamoja na watendaji kazi wake wote, Katibu Mkuu na wote wanaowasimamia katika Wizara hii. Kwanza kabisa, naomba niseme ndani ya Jimbo langu la Nsimbo, Mbuga ya Katavi ndiyo ilipo. Hii mbuga haitangazwi kabisa. Sasa Rais katuonesha mfano, kaonesha ubunifu, lakini

ninamuamini Waziri wetu Mheshimiwa Mchengerwa, atafanya ubunifu ili Mbuga yetu ya Katavi iweze kutangazwa kwa sababu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwanja wa ndege Katavi upo, ndege zinafika, barabara kutoka kwenye uwanja wa ndege mpaka kwenye eneo letu la mbuga ni ya lami. Sasa sidhani kama kuna kitu ambacho kinaweza kushinidikana kufanya jitihada za kuhamasisha ili mbuga yetu iweze kutangazwa ili watalii waweze kufika Katavi kwa sababu, mazingira tayari yameshakuwa mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kijiji chetu cha Stalike kinapakana kabisa na Mbuga ya Katavi. Kuna mto ambao umetenganisha; naomba nimshukuru sana Kamishna Mwakilema, tumeongenaye amekubali kwenda kuongea na wananchi. Tatizo ni moja tu, wale wananchi toka mwaka 1974 katika ule mto, huko kijijini kabisa wanavua Samaki, lakini leo tumewazuia kabisa kuvua Samaki, nao ndiyo kipato chao cha uchumi. Sasa na Kata ya Stalike ndiyo inayoathirika kwa wanyama wakali. Wakulima wa Kata ya Stalike, wakilima mazao yao yote yanaliwa na tembo, wanaofanya vurugu katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani ni jambo la busara tu, sasa hivi twende tukakae tukaongee na wananchi wa Kata ya Stalike ili tuelewane. Kama ni kujengewa mabwawa, basi wajengewe mabwawa, kuliko kuacha na kuwazuia kabisa ili wasiweze kufanya shughuli zozote za kibiashara na kiuchumi katika Mto ule wa Stalike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni *TAWA*. Kuna msitu wa *Ugara Game Reserve* na Msitu wa *Msimu Game Reserve*. Wananchi walikuwa wanaenda mle ndani katika hayo maeneo kuvuna asali na wameweka mizinga yao ya asali, lakini leo *TAWA* wamewazuia kuingia kuvuna asali na vilevile wanawa-*charge* pesa. Akiingia na baiskeli analipa shilingi 10,000, akiingia na pikipiki analipa shilingi 30,000, wakiingia na gari wanalipa shilingi 50,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii misitu tumeikuta na hizi *games* tumezikuta, kama wananchi wa Ugalla wao katika *Game Reserve* ya Ugalla walikuwa wanaishi, ni maisha yao walikuwa wanaishi, ndiyo

makazi yao. Wanafanya mila zao za jadi, leo tumewakuta tunawazuia wasifanye mambo yao ya jadi na mila zao. Vilevile kila akiingia atoe shilingi 10,000, akiingia na pikipiki shilingi 30,000. Najua Kamishna wa *TAWA,* Ndg. Nyanda ni msikivu. Ninavyoongea ananisikia, naomba twende tukakae na wananchi tuweze kukubaliananao ili waweze kupunguziwa ghasia hii ambayo wanaipata sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni *TFS,* wenzangu wengi wameongea. Nimi jimbo langu limezungukwa na misitu, lakini *TFS* ndiyo wanaolinda misitu na wananchi wanachotaka ni kitu kidogo tu, wanataka tuwape elimu, tuwashirikishe, tuwaoneshe mipaka kuliko kuwapiga na kuwa-fyekea mazao yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Deus amesema hapa, wananchi wanalima. Sasa hivi *TFS* wametulia kimya. Saa hizi wametulia. Mvua zikianza kunyesha, wananchi wanalima, wanawatizama, mazao yakishakamilika ndiyo kipindi sasa cha kwenda kufyeka mazao yao na kuwanyanyasa na kuwapiga. Ni dhambi kubwa sana. Kwa nini tusiwaelimishe? Kwa nini tusikaenao kitako tukawaambia hapa ni mipaka yetu, hapa msiingie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge tupo, watushirikishe, twenenao wakaongee na hao wananchi kuliko jinsi wanavyofanya. Wananchi wanateseka mpaka wanapata hasira na Serikali yao. Mheshimiwa Waziri tunajua wewe ni msikivu, tumekuona jitihada zako, kwa kipindi kifupi hiki tumeona kazi kubwa, miezi mitatu ulivyokabidhiwa Wizara tumeona jitihada zako. Tunakuomba Mheshimiwa Waziri, pita katika Mikoa yako yote yenye hifadhi ili uweze kuongea na wananchi. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Lupembe.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie moja tu, kuna…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, tunakushukuru kwa mchango wako…

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kidogo tu…

**MWENYEKITI:** …muda wako umekwisha.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kuunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Ninamwita Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, wakati huo Mheshimiwa Zaytun Seif Swai na Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq wanajiandaa.

**MHE. DANIEL B. SILLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye Wizara yetu hii ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi kubwa anayoifanya katika sekta mbalimbali hapa nchini pamoja na sekta yetu hii ya maliasili na utalii. Lakini niwapongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu nzima, kwa kazi kubwa na dhamira nzuri mliyo nayo katika kuiboresha sekta hii ya maliasili na utalii hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Rais, kwenye hili suala la *The Royal Tour,* limekuwa na mafanikio makubwa katika nchi yetu. Na moja kubwa ni kuitangaza nchi yetu kimataifa, la pili kuongeza idadi ya watalii hapa nchini na la tatu ni kuongeza fedha za kigeni katika uchumi wa Taifa letu. Kwa hiyo ni pongezi kubwa sana kwa Mheshimiwa Rais kwa kazi hii kubwa iliyofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Ilani yetu ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2025 pamoja na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26) yako malengo ambayo tulijiwekea. Moja ni idadi ya watalii kufikia milioni tano kwa mwaka; la

pili, mchango wa sekta hii ya utalii kuwa asilimia 15.5 kwenye Pato la Taifa; tatu sekta hii kuchangia asilimia 27 ya mapato yote ya kigeni. Ili kuyafikia malengo haya lazima kazi kubwa ifanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na la kwanza mimi napendekeza, ni kuongeza vitanda kwa ajili ya watalii. Katika eneo hili ni kushirikisha sekta binafsi. Kwa taarifa ya mwaka 2022, Tanzania tuna vitanda 132,684 lakini nchi jirani ya Kenya ina vitanda 1,200,000. Kwa hiyo kuna kazi ya kufanya katika eneo hili kuongeza vitanda kwa kushirikisha sekta binafsi, kujenga hoteli za nyota mbalimbali ili kuhakikisha kwamba tuna vitanda vya kutosha kwa ajili ya watalii wanafika katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili katika eneo hili ni kuboresha miundombinu yetu kwenye masuala mazima ya utalii. Jambo la tatu ni kuboresha huduma *(customer care)* kwa watalii wetu. Jambo la nne utakumbuka wakati tulivyogawa fedha za UVIKO-19 sekta hii ya utalii tuliipa bilioni 90.2. Kazi ilifanyika nzuri sana na Kamati yangu ya Bajeti ilipata ziara katika maeneo mbalimbali, tumeona mafanikio makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa napendekeza kwenye dirisha hili la *ECF* ambalo lilikuwa na nia ya kupunguza matatizo ya urari wa malipo kwa nchi zetu basi Serikali itenge fedha pia kwa sekta hii ya maliasili na utalii ili kuboresha sekta nzima ya utalii ambayo inachangia katika uchumi wetu vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuendeleza na kumaliza migogoro mbalimbali kati ya hifadhi na maeneo yetu mbalimbali hapa nchini. Katika eneo hili niendelee kuipongeza Serikali kwa sababu kazi kubwa imefanyika. Iko timu ya mawaziri nane ambayo imezunguka katika nchi yetu, wamefanya kazi kubwa, tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna baadhi ya maeneo yetu bado kuna migogoro. Nitatoa mfano wa Jimbo langu la Babati Vijijini; kuna Vijiji nane ambavyo vinapakaa na Hifadhi nzuri sana ya

Tarangire; Vijiji vya Gedabung', Ayamango, Gedamar, Mwada, Sarame, Sangaiwe na Vilimavitatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona kuna dhamira nzuri sana ya Mheshimiwa Waziri ya kumaliza migogoro hii. Tumesikia hotuba yake, ameongea masuala mazuri sana. Mheshimiwa Waziri, twende kama timu pamoja, liko jukumu la kwangu kama Mbunge na wananchi wangu, liko jukumu la Serikali, twende kwa pamoja tukamalize miigogoro hii ya muda mrefu ili kuwe na uhusiano wa ujirani mwema kati ya hifadhi na wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua Mheshimiwa Waziri umejipanga vizuri, nami nakuhakikishia kabisa ntakuunga mkono katika suala zima la kumaliza migogoro katika maeneo haya yote ya Babati Vijijini ili wananchi waendelee kuwa salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni eneo la kifuta jasho wananchi wanapoharibiwa mazao na wanyama wakali. Tunaipongeza Serikali kwanza kwa kuwakumbuka wananchi, walau hata kwa hicho kidogo wanachokipata. Lakini kifuta jasho kinachelewa, hakiji kwa wakati. Kwa hiyo tuombe sana Serikali basi kile kifuta jasho kije kwa wakati lakini pia walau kiakisi ule uhalisia wa uharibifu uliofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana katika eneo hili kuwe na tathmini ya uhakika ili wananchi wapate walau kifuta jasho kitakachosaidia familia zao na kisaidie uchumi katika maeneo hayo. Pia viwango vifanyiwe mapitio, ni vya muda mrefu. Kwa hiyo niishauri Wizara iangalie namna ya kupitia viwango hivi vya fidia kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *otherwise* nashukuru sana kwa kupata nafasi hii, na mimi naiunga mkono hoja hii kabisa, na Mheshimiwa Waziri nakutakia kila la heri katika mafanikio yako. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Daniel Baran Sillo. Nilimwita Mheshimiwa Zaytun Seif Swai aweze kuchangia.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa na mimi basi niweze kuchangia na kutoa ushauri wangu kwenye sekta hii muhimu ya Maliasi na Utalii, sekta ambayo ni muhimu sana kwa nchi yetu Tanzania, lakini pia kwa Mkoa wangu wa Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta hii ni muhimu sana kwa kutuingizia fedha za kigeni. Tumeona zaidi ya asilimia 25 ya fedha za kigeni zinatokana na sekta hii lakini pia asilimia 17 ya Pato la Taifa inachagiwa na sekta hii muhimu ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile inachangia kwa kaisi kikubwa ajira kwa Watanzania. Na mpaka sasa tumeona ajira za moja kwa moja na ajira zisizo rasmi takribani milioni 1.6 za Watanzania wameajiriwa kwenye sekta hii muhimu. Utaona kabisa mnyororo wa sekta hii ya utalii ni mrefu sana na unagusa sekta mbalimbali kama za usafirishaji, kilimo na nyingine. Sekta hii inachangia pia kukuza sekta mbalimbali kama nilivyozitaja, kwa hiyo ni muhimu sana Serikali ikatilia mkazi kwenye sekta hii ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyojua sasa hivi kwenye uchumi wa mataifa kuna changamoto kubwa za fedha za kigeni, na Tanzania pia tuna changamoto hiyo ikiwemo upatikanaji wa dola. Lakini Serikali ikiweza kutilia mkazo kwenye sekta hii muhimu ya utalii itaweza kutatua changamoto hii kwa kiasi kikubwa. Naamini kabisa tukiweza kuilea na kuiendeleza sekta hii hata kwenye uchangiaji wa dola tunaweza tukafikisha takriban asilimia 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba nimpongeze sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuweza kuendelea kutangaza sekta hii ya utalii kimataifa. Lakini naiomba Wizara iweze kufanya kazi zaidi ili basi iendane na kasi hii ya Mheshimiwa Rais wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuondokane na utalii wa kimazoea, twende sasa kwenye utalii wa kimkakati. Tukiweza kufanya hivi, tutaweza kushirikisha sekta binafsi ili tuweze kushirikiana nao katika

ujenzi wa miundombinu mbalimbali, lakini vilevile hususan kwenye ujenzi wa hoteli zenye hadhi ya kitaifa ya kulaza wageni wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa hivi nchi yetu tuna vyumba 122,532 tu, lakini ukiangalia nchi jirani wana vyumba zaidi ya milioni mbili. Ukiangalia pia nchi nyingine ambazo zimeendelea kwenye sekta hii kama Seychelles, Mauritius na hata iwe nchi jirani ya Kenya hawakuanza tu hivihivi, waliondokana kwenye utalii wa mazoea, wakaenda kwenye utalii wa kimkakati. Walianzisha programu mahususi, programu za kimkakati kwa ajili ya kuendeleza hoteli nchini mwao. *Strategic Hotel Investment Programmes* lazima zianzishwe ili tuweze kuondokana na changamoto hii. Kwa hiyo ushauri wangu kwenye eneo hili la hoteli, hata sisi itabidi tuanzishe fedha mahsusi na za kimkakati ili basi tuweze kuondokana na changamoto hii ya hoteli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ninalotaka kuchangia jioni ya leo ni kuhusiana na kodi na tozo sumbufu kwenye sekta hii ya utali. Kwanza kabisa nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa tamko lake la kusamehe kodi kwa wafanyabiashara wetu ambazo zimezidi miaka mitano. Na nitumie fursa hii kwa niaba ya wafanyabiashara wa Mkoa wa Arusha kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa tamko lake hili. Sasa, niombe mamlaka husika zote ziweze kufuata maagizo haya ili basi wafanyabiashara wetu wasiwe na usumbufu kwenye biashara zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwenye sekta hii ya utalii utaona kwamba kuna tozo mbalimbali ambazo ni kero sana kwa wafanyabiashara wetu ambao wanahusika moja kwa moja na biashara hii ya utalii. Ukiangalia biashara zile mpya zote, kijana leo anahitimu shule akitaja kujiajiri kwenye sekta hii ya utalii ni lazima alipie leseni dola 50 ili aweze kufanya kazi za u-*tour guide*. Mbona kazi nyingine hazitakiwi kukatiwa leseni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba sana Wizara iangalie kodi zote na tozo mbalimbali ambao ni kero kwa wafanyabiashara wetu ili waweze kwenda vizuri na kuendeleza sekta hii muhimu ya utalii. Na ikiwezekana, naomba biashara zote zile mpya, wafanyabiashara wale wapya wanaotaka kuingia kwenye sekta hii

wapewe angalau likizo ya miezi mitatu mpaka pale biashara zao zitakapokuwa ndipo waweze kutozwa tozo hizi. Tukiweza kufanya hili tutaongeza ajira lakini vilevile tutaongeza wigo wa kodi nchini kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ninaloomba kuongelea jioni ya leo ni kuhusiana na kupanua wigo wa mazao ya utalii na kutangaza pia vivutio vile ambavyo hatuna mazoea navyo. Ukiangalia kwenye sekta hii takriban asilimia 80 tumejikita kwenye utalii wa wanyamapori, na hii ni changamoto kubwa sana ya sekta hii ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tumebarikiwa vivivutio vingi zikiwemo fukwe, mito, milima na utalii wa kiutamaduni. Ukisoma hata hotuba hapa ya Mheshimiwa Waziri, pamoja na maoni ya Kamati, hauoni vipaumbele vya kwenye vivutio vingine kama milima. Tuna mlima mrefu Mlima Kilimanjrao lakini vilevile katika Mkoa wangu wa Arusha kuna Mlima Meru ambao ni namba mbili Tanzania, lakini wa nane Afrika, lakini sijaona jitihada ya Serikali kabisa kwenye kuutangaza mlima huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukianza kutangaza vivutio hivi vingine, tutaweza kuongeza idadi ya watalii, na tutaongeza idadi ya siku watalii wanazokaa hapa nchini. Kwa sababu wakishatoka mbugani kule watakuja hapa watapanda mlima, watatembea kwenye mito, na tukiongeza idadi ya siku ambazo mtalii anakaa nchini, basi tunaweza tukaongeza pia Pato letu la Taifa, lakini na ajira pia kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho ninaloomba kuongelea ni kuhusiana na Chuo chetu cha Taifa cha Utalii. Kwanza kabisa niishukuru Serikali, nimeona kwenye bajeti mmetenga fedha kwa ajili ya kaunzisha tawi la Chuo cha Utalii katika Mkoa wangu wa Arusha; hilo ni jambo jema kwa sababu itawapa fursa vijana wengi wa Mkoa wa Arusha na maeneo jirani yote katika kupata mafunzo ya Utalii na ukarimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hatujaweza kutumia chuo hiki kwa ufanisi. Bado tuna changamoto kubwa ya utoaji wa huduma bora za

utalii pamoja na ukarimu hapa nchini. Katika kipindi hiki ambacho tunategemea watalii waongezeke hadi zaidi ya milioni tano kama mlivyosema kwenye hotuba yenu, nashauri tutumie chuo hiki kwa ufanisi ili tuweze kupata wahitimu wenye ubora wa kimataifa wa kuweza kuhudumia wageni wetu. Nishauri pia, kama mlivyofungua tawi katika Mkoa wa Arusha, basi katika maeneo yote ambayo yana vivutio muweze kufungua matawi ili kuweza kuendeleza vijana wetu waweze kupata elimu ya huduma ya kimataifa kwa ajili ya kuwahudumia watalii wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKI:** Ahsante sana Mheshimiwa Zaytun Seif Swai kwa mchango wako. Mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa ni Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa nami niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumpongeza sana Mhifadhi namba moja, Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye ana dhamira ya dhati kabisa ya kuhakikisha kwamba sekta ya utalii inaipatia pato la uhakika nchi yetu; hongera sana kwa Mheshimiwa Rais. Tumeona kabisa kwamba ile Filamu yake ya *Royal Tour* imesaidia kuiweka Tanzania katika ramani ya dunia na hivyo kubainisha baadhi ya vivutio ambavyo viko nchini mwetu. Kwa hiyo nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi hii nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, naomba pia nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, watendaji wote na taasisi zote za Wizara hii kwa kuandaa hotuba nzuri ambayo imesheheni taarifa mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba nizungumzie kuhusiana na suala zima la biashara ya uwindaji wa kitalii. Biashara hii ilishamiri sana miaka ya 2008 hadi 2009, kwamba Idara ya Wanyamapori iliweza kupata hadi jumla ya shilingi bilioni 60 kwa mwaka wakati biashara hii ilipokuwa ikifanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa masikitiko makubwa sana, kuanzia mwaka 2013 hadi 2014, biashara hii ya uwindaji wa kitalii ilipungua na hatimaye ilikuwa ikipatikana kama bilioni 20 kwa mwaka, hapa ilisuasua kidogo. Lakini niendelee kuipongeza sana *TAWA* kwa kazi ambayo imekuwa ikiifanya, kwamba sasa hivi wamejitahidi tena kuweza kuoneza pato kwa biashara ya uwindaji wa kitalii kwa shilingi bilioni 60. Hii ni hatua nzuri lakini bado mimi natamani sana kwa kile kipindi cha mpito tungeweza tukafika hatua kubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi bahati nzuri nilishawahi kuwa Mkuu wa Wilaya ya Manyoni, na kule kulikuwa kuna vitalu ambavyo vilikuwa kwa ajili ya uwindaji wa kitalii; kwa hiyo walikuwa wanakuja wageni wengi sana katika kipindi kile, na hivyo kutuletea pato la Kitaifa. Lakini pia katika yale maeneo yanayozunguka pale walikuwa wanafaidika sana wale wananchi kwa kuweza kuongeza kipato chao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, katika yale maeneo ya kule maporini, unaweza ukashangaa kwa sababu ndege zilikuwa zinakuja, wageni walikuwa wanakuja, watu mbalimbali walikuwa wanakuja kwa ajili ya kuwinda, na hata nakumbuka ilishawahi kutokea Rais wa Panama alishawahi kuja na binti yake kwa ajili ya utalii na *delegation* kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi naomba niendelee kuishauri Serikali kwamba Wizara ione umuhimu wa kuiongezea bajeti *TAWA* ili waweze kuweka mipango yao vizuri ili waweze kujitanua zaidi katika kuweza kugawa hivi vitalu vya utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kubwa, niendelee kuipongeza *TAWA* kwa sababu wameweza kutumia mfumo wa kielektroniki katika kusimamia ugawaji wa vitalu vile vya utalii; hii ni hatua kubwa. Kwa hiyo natamani wapatikane wataalamu wengi zaidi waweze kusaidia

ukagwaji wa vitalu hivi ili mwisho wa siku tuweze kupata faida kubwa sana. Kwa hiyo naipongeza sana *TAWA* kwa hatua nzuri ambayo wameifikia. Naamini kwamba kama tutakwenda hivi vizuri basi tunaweza tukapata fedha zaidi ya bilioni 120 na kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu mwingine ni kwamba inabidi pia *TAWA* ibuni njia nyinginezo za mapato, kama vile utalii wa picha. Mfano ile *Game Reserve* ya Maswa ni nzuri kwa ajili ya utalii wa picha, kwa hiyo kama wataona huu ushauri unafaa basi waweze kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri pia hii Taasisi ya *TAWA* yale maeneo mengine waweze kufanya tathmini ya kina ili shirika liweze kuyatumia maeneo hayo kwa aina nyingine ya utalii badala ya kutegemea utalii wa uwindaji tu. Natambua kwamba kuna baadhi ya mataifa makubwa ambayo yamekuwa yakifanya kampeni hasi dhidi ya uwindaji wa kitalii, lakini hii ni miongoni mwa mbinu moja wapo katika utalii ambayo inaweza kulileteа pato kubwa sana Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninataka kulizungumzia ni vivutio vinginevyo. Kuna baadhi ya vivutio ambavyo inabidi viendelezwe. Tumeona kabisa kwamba tumejikita zaidi kwa wanyamapori na mambo mengine kidogo, lakini pia sisi tuna makabila mengi sana hapa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tuna makabila zaidi ya 120, tuna mila na desturi zetu; kwa nini pia tusiwekeze kwenye utalii wa makabila ili wale watalii watakapokuja wanakuja waweze pia kuona makabila yetu, mila zao na desturi wanafanya nini? Tuna makabila tofauti; tuna Wamasai, tuna Wagogo, tuna Wanyamwezi, tuna Wasukuma, tuna Waha, Wamakonde, Wangoni na makabila mengi. Kama tukiweza kuonesha zile mila zao na desturi, wote hawa mimi naamini kabisa kwamba watalii hawa wataweza kwenda wakitoka kule mbugani wataweza kuona hizi mila na desturi. Labda na sisi tupeleke watu wetu, waende Ethiopia na Afrika Kusini ambako wenzetu kule wameweza kufanikiwa sana kwenye hili suala zima la mila na desturi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri utafiti ufanyike, kwamba kwa nini asilimia 20 ya watalii ambao wanatembelea katika vivutio vyetu hurudi tena kwa mara ya pili. Kwa sababu tunatamani kwamba kama wamefurahia ile hali waliyoikuta katika mbuga zetu lakini pengine kama tukaweka kwenye suala la malikale, lakini pia tukaweka labda kwenye suala la makabila, na mengineyo mengi, watalii hawa watakuwa na hamu kwamba akitoka inawezekana kabisa akakaa zile siku alizoziweka kati ya 10 au 15, kumbe ana sababu ya kwenda maeneo mengi zaidi akaongeza zile siku za kuweza kukaa hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi ninashauri kwamba basi ufanyike utafiti wa kina kujua, je, ni vivutio vipi ambavyo vitaweza kuwasaidia hawa watalii waweze kurudi tena, isiwe mara moja tu, iwe mara mbili, mara tatu, mara nne, hata mara kumi? Na ikiwezekana waende wakawaambie wenzao ili waweze kufika na kuweza kufanya huo utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua muda si rafiki sana, mimi naomba nitumie fursa hii kukushukuru sana kwa kunipa fursa, naunga mkono hoja na ninaamini kabisa kwa jinsi hali ilivyo Tanzania itaweza kufikia zaidi ya watalii milioni tano, hata milioni 10 au milioni 15 kama katika nchi nyingine zozote duniani ambazo zimeweza kufaidika na utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba niunge mkono hoja. Ahsante sana kwa kunipa fursa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa *session* yetu ya leo. Kwa wale ambao hawakupata fursa ya kuchangia na walikuwa wameorodheshwa tutawapa kipaumbele Jumatatu. Kwa hiyo naahirisha Shughuli za Bunge mpaka Jumatatu, Saa 03.00 Asubuhi.

*(Saa 1.40 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jamatatu, Tarehe 5 Juni, 2023, Saa Tatu Asubuhi)*